Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 27 Juni, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU (K.n.y. MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO) - MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:**

Maoni ya Kamati ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2005/2006.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA (K.n.y. MOHAMMED JUMA KHATIB) - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA UJENZI:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2005/2006.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 138

**Kitengo cha Maafa**

**MHE. TALALA B. MBISE** aliuliza:-

(a) Je, Kitengo cha Maafa hugawiwa wastani wa kiasi gani cha fedha katika Bajeti (kuondoa mishahara) kila mwaka tangu kianzishwe?

(b) Je, ni matukio mangapi yameshatokea nchini ambayo yanaweza kuitwa maafa na kati ya hayo ni yapi ambayo Kitengo cha Maafa kingeweza kumudu kiuwezo na kulingana na Bajeti inayotengwa kwa ajili ya kitengo hicho?

(c) Je, Serikali itafikiria kuanzisha Mfuko au Bima ya Maafa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMED SEIF KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Talala Bana Mbise, Mbunge wa Arumeru Mashariki, lenye sehemu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Kitengo cha kuratibu na kuhudumia matukio ya maafa nchini, hutengewa fedha katika Bajeti ya Serikali wastani wa sh. 70m/= hadi 100m/= katika kasma ya Matumizi mengineyo. Aidha, fedha zaidi, kwa viwango maalum hutolewa pia wakati wa matukio ya dharura yanapotokea. Kwa utaratibu huo, mwaka 2002/2003, Kitengo cha Maafa chini ya Idara ya Maafa katika Ofisi ya Waziri Mkuu kilipatiwa zaidi ya sh. 500m/= na mwaka 2003/2004, pia zilitolewa z aidi ya sh. 1.5bn/=.

(b) Mheshimiwa Spika, maafa ni mlolongo wa matukio ya asili au yanayosababishwa na binadamu ambayo huharibu mfumo wa jamii kiuchumi, kwa viwango ambavyo jamii husika hushindwa kukabiliana nayo kwa kutumia rasilimali zao wenyewe. Matokeo yake jamii hiyo huhitaji misaada toka ngazi ya juu au msaada wa nje. Baadhi ya matukio yaliyokwishatokea na yanayoweza kuitwa maafa ni kama vie kuzama kwa meli ya *M.V. Bukoba* mwaka 1996, Ukame katika Mikoa karibu yote nchini mwaka 1996/1997 uliosababisha upungufu wa chakula kwa watu zaidi ya milioni 2.9. Vile vile maafa ya mlipuko wa bomu katika Ubalozi wa Marekani Dar es Salaam mwaka 1998, Mvua za *El-nino* zilizoharibu miundombinu hususan barabara, madaraja na kadhalika mwaka 1998, ajali ya Kivuko katika Mto Kilombero na ajali ya treni –Dodoma mwaka 2002. Katika matukio yote hayo Serikali ilitoa msaada mkubwa ikiwa ni pamoja na kutoa kifuta machozi kwa waathirika, walioumia na waliofiwa na ndugu zao.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali haina mpango wa kuanzisha bima ya maafa kwa sasa, kwa sababu ni ghali sana kulipa fidia ya madhara ya maafa. Kuhusu Mfuko wa Maafa, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu hutoa fedha kugharamia na kukabiliana na maafa mbalimbala kila yanapotokea.

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza na namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake. Kwa kuwa Arumeru Mashariki kufuatana na mvua zilizonyesha walipata matatizo makubwa kwenye Kata za King’ori, Maroroni na Mbughuni na tukapeleka maombi na taarifa hizo kati ya mwezi wa Tatu na wa Nne kwenye Wizara hii kutoa taarifa na

kuomba msaada na tukaambiwa kwamba haiwezekani. Je, majibu haya yalitoka na kama yalitoka yalipelekwa wapi na msaada unaweza kupatikana kwa njia yoyote?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, tuna utaratibu wa kudumu wa kushughulikia upungufu wa chakula mahali popote unapotokea hapa nchini. Kama katika eneo hilo kumetokea upungufu, basi wataalam wetu huenda katika eneo hilo kufanya makisio ya mahitaji ya chakula na kitapatikana wakati utakapofika. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge asubiri tu hili suala linashughulikiwa kwa pamoja kati ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Kilimo na Chakula.

**MHE. ABDULKARIM E.H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Nilitaka kuuliza moto ni maafa au sio maafa unapotokea katika jamii ya maeneo ambapo nyumba zaidi ya tano au sita zinaungua na watu kupoteza sehemu za kukaa pamoja na vifaa vyao? Mafia ulitokea moto……

**SPIKA:** Hapana ulitaka kujua tu kama moto ni maafa au sio maafa. (*Kicheko*)

Waziri jibu swali hilo.

**MHE. ABDULKARIM E.H. SHAH:** Inatosha. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMED SEIF KHATIB):** Mheshimiwa Spika, katika majibu yangu ya msingi nimetoa mifano mingi sana ya kuonyesha maafa ambayo yamekwishatokea nchini kwetu. Moto unategemea ukubwa wa moto wenyewe, kama nyumba tatu au nne si maafa hayo, ni ajali ndogo tu.

Na. 139

**Masoko ya Kariakoo**

**MHE. JUMANNE H. NGULI** aliuliza:-

Kwa kuwa Masoko ya Kariakoo wakati yalipojengwa yaliweza kutosheleza mahitaji ya wateja wake na kulingana na kuongezeka kwa wafanyabiashara na hakuna nafasi ya kupanua soko hilo:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa ni busara sasa kujenga upya sehemu ya masoko isiyo ya ghorofa na iwe na sehemu ya chini ili kupata nafasi zaidi kwa bidhaa na mazao zaidi kupokelewa?

(b) Kwa kuwa, suala la usafi katika soko hilo ni tatizo kwa sababu ya nafasi kuwa ndogo: Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati wa kurekebisha hali hiyo kwa kuweka miundombinu ya majitaka na taka ngumu ili soko hilo liwe la kisasa zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jumanne Hamisi Nguli, Mbunge wa Singida Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Shirika la Masoko ya Kariakoo liliundwa kwa Sheria ya Bunge Na. 36 ya Mwaka 1974 na kuanza shughuli zake mwezi Desemba, 1975. Madhumuni makubwa ya kuanzishwa kwa Shirika hili yalikuwa yafuatayo:-

- Kusimamia na kuendesha Soko Kuu la Kariakoo pamoja na masoko mengine yatakayokuwa chini ya usimamizi wa Shirika. Kwa sasa yapo masoko madogo katika meneo ya Buguruni, Tandale, Tandika na Ilala ambayo yanaendeshwa na Halmashauri za Manispaa husika.

- Kujenga masoko mengine mapya katika Jiji la Dar es Salaam na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Masoko hayo.

(a) Mheshimiwa Spika, kutokana na ongezeko la idadi ya watu nakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge wa kujenga upya sehemu ya masoko isiyo ya ghorofa ili kupata nafasi zaidi kwa bidhaa na mazao zaidi kupokelewa. Hata hivyo, kwa sasa Shirika la Masoko la Kariakoo lina mpango wa kujenga soko lingine katika eneo la Tabata ambapo tayari eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 5,725 limepatikana. Eneo hili ambalo lilikuwa ni makazi ya watu limepata kibali toka kwa Waziri wa Ardhi kubadilishwa kuwa eneo la biashara. Shirika linaandaa michoro ya soko hilo na itakapokamilika zabuni ya ujenzi itatangazwa. Vile vile Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ina kiwanja katika eneo la Mbezi Luisi ambapo soko jipya la jumla litajengwa ili kupunguza msongamano katika soko la Kariakoo na kupunguza taka zinazozalishwa katika soko hilo. Aidha, yako masoko ya kisasa ya Makumbusho na *Stereo* yaliyojengwa na iliyokuwa Tume ya Jiji.

(b) Mheshimiwa Spika, miundombinu ya majitaka katika soko hili imeunganishwa na mfereji mkubwa wa majitaka (*Main Sewer*) wa Jiji na hivyo haileti matatizo katika suala la majitaka. Kwa upande wa taka ngumu, Shirika linazalisha tani 15 hadi tani 20 kwa siku. Pamoja na wingi wa taka hizi, Shirika limechukua hatua ya kubinafsisha kazi ya usafi na linamudu kutoa huduma hii.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza kero ya msongamano katika soko hili, Halmashauri za Manispaa za Ilala, Kinondoni na Temeke zinatakiwa kuboresha miundombinu katika masoko mengine yaliyopo Dar es Salaam ili wateja na wafanyabiashara wapate huduma ambazo wanazipata toka soko la Kariakoo.

**MHE. HAMISI J. NGULI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Aidha, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa madhumuni ya masoko ya Kariakoo yalitazamiwa kupokea mazao ya kilimo kutoka Mikoa mbalimbali pamoja na bidhaa zingine, lakini kwa sasa hivi tunaona wafanyabiashara wadogo wadogo wakisongamana pale kwa kuuza bidhaa ndogo ndogo.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba ni vizuri kuwaondoa hawa wafanyabiashara wadogo wadogo ili kulipa soko hilo nafasi ya kuendelea na madhumuni yake yaliyokuwa yametazamiwa?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na yeye kwamba wafanyabiashara ndogo ndogo wanasababisha msongamano ambao kwa kweli sio wa lazima, ndio maana Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam inajitahidi kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam mara kwa mara kufanya zoezi la kuwaondoa vijana hawa kuwapeleka katika maeneo waliyotengewa kama vile Mchikichikini, Ilala. Lakini kama tunavyofahamu sote, vijana hawa huondoka baada ya siku mbili, tatu hurudi na zoezi huendelea tena. Lakini nafikiri njia bora ni hii ambayo Halmashauri ya Jiji wameamua kutenga eneo la Mbezi Luisi kujenga soko sasa la jumla ili kupunguza msongamano usiokuwa na sababu katika soko la Kariakoo. (*Makofi*)

Na. 140

**Ufujaji wa Fedha za Miradi ya Halmashauri**

**MHE. EDSON M. HALINGA** aliuliza:-

Kwa kuwa wafujaji wa fedha za miradi ya Halmashauri za Wilaya ni watumishi na watendaji wa Halmashauri hizo na sio Madiwani:-

(a) Je, Serikali inakubaliana nami juu ya mtazamo huo?

(b) Je, Serikali iko tayari sasa kuhakikisha kuwa wahusika wanachukuliwa hatua pamoja na kufilisiwa ili fedha hizo zitumike katika kukamilisha miradi iliyokwamishwa?

(c) Je, Serikali inaweza kulieleza Bunge ni Wilaya zipi kwa majina zilizokithiri katika ufujaji huo na hatua zilizochukuliwa dhidi ya wahusika?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji ni mjumuiko wa Waheshimiwa Madiwani pamoja na watumishi na watendaji. Hivyo basi ni jukumu lao kuhakikisha kuwa ufujaji wa fedha hautokei. Pale Halmashauri inapohisi kuna ufujaji wa fedha ni

wajibu wake kufuata taratibu muafaka za kubaini na kuchukua hatua zinazotakiwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu. Kufuja pesa za umma ni kosa la jinai, hivyo tendo hilo linapaswa kutolewa taarifa Polisi. Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edson Halinga, Mbunge wa Mbozi Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba wafujaji wa fedha za miradi ya Halmashauri ni watendaji pekee. Yako matukio ya ubadhirifu wa fedha za Halmashauri ambayo yamehusisha Madiwani pekee, Madiwani pamoja na watendaji na wakati mwingine watendaji peke yao. Suala la ubadhirifu wa fedha za umma lifikishwa Mahakamani, Mahakama hutoa adhabu kulingana sheria zilizopo. Mahakama haizuiliwi kuagiza pia mali za mshtakiwa zifilisiwe kama itaona inafaa kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Mheshimiwa Spika, mifano hai ni pamoja na tukio la Manispaa ya Dodoma miaka ya nyuma ambapo wajumbe wa Kamati ya Fedha ya Halmashauri ya Manispaa walihusika na ubadhirifu wa fedha na hatua za kinidhamu zikachukuliwa dhidi yao. Aidha, kuvunjwa kwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam mwaka 1996 pamoja na mambo mengine ilikuwa ni ubadhirifu wa fedha katika Halmashauri hiyo. Kwa hivi sasa baadhi ya watumishi katika Halmashauri 28 wamefunguliwa mashtaka kwa ubadhirifu wa fedha za miradi na mashtaka yanaendelea. Hivyo, hatuwezi kuzitaja Halmashauri ambazo zimekithiri kwa ubadhirifu wa fedha kwa vile itakuwa ni kutoa hukumu wakati Mahakama kama chombo chenye mamlaka haya haijafikia uamuzi huo.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Mheshimiwa Waziri anaweza kukubali kwamba utoaji wa zabuni uliwaondoa Madiwani kushiriki ni sababu moja inayofanya ufujaji wa hela za miradi kuwa mkubwa katika nchi hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, wakaguzi wa ndani wapo chini ya Mkurugenzi, hivi haoni kwamba hali hii inawafanya wakaguzi hao wasiwe na mamlaka ya kumdhibiti Mkurugenzi kwa matumizi mabaya ya Halmashauri hizo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, kuondoshwa kwa Madiwani katika vikao vya zabuni ni njia bora ya Waheshimiwa Madiwani kusimamia utendaji pale jambo linapoharibika. Kama Waheshimiwa Madiwani wakihusishwa moja kwa moja kwenye vikao vya zabuni Halmashauri inakosa mtu wa kusimamia kwa sababu wasimamizi wenyewe wamegeuka kuwa watendaji. (*Makofi*)

Pili, wakaguzi si wasimamizi wa mahesabu. Wakaguzi wanakagua taratibu za kihasibu kama zimefuatwa, wasimamizi ni Kamati ya Fedha ya Waheshimiwa Madiwani na nasema haya kwa sababu baadhi ya Halmashauri 28 baada ya Kamati ya Fedha kugundua kwamba kuna uharibifu umefanyika wamewapeleka watendaji wao Mahakamani na hivi sasa kuna kesi hizi za Halmashauri 28 ambazo ziko Mahakamani. Waliosimamia kufikisha masuala hayo Mahakamani ni Waheshimiwa Madiwani wenyewe. Kwa hiyo, ninaomba Madiwani wengine katika Halmashauri zilizobaki

waige mfano wa Halmashauri hizi 28 ili kuweza kulinda fedha zetu kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu.

**MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Katika jibu lake lile la kwanza la kuwaondoa Madiwani wakati mwanzoni ndio walikuwa wanahusika, leo hali ya barabara ambazo zimekuwa na tenda zilizopitishwa na watu ambao hawawajibiki na hawapigiwi kura, haoni kwamba inazidi kuleta matatizo kwa Madiwani na inaweza kusababisha Madiwani wengi kushindwa kwa sababu barabara zilizotengewa pesa zile na kuweka hizo tenda huwa mbaya zaidi kuliko walivyokuwa wakisimamia Madiwani wenyewe? Naomba jibu. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, kwa kweli ukiangalia kwa makini kama sisi Waheshimiwa Madiwani tungekuwepo kwenye Kamati za Zabuni basi kushindwa kungekuwa kukubwa zaidi kuliko ilivyo sasa kwa sababu zifuatazo:-

**WABUNGE FULANI:** Aaa, aaa.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, Kamati ya Fedha ndio inaamua kila kitu na kuwaachia watendaji watangaze zabuni na zabuni zinapotangazwa kunakuwa na vigezo vinavyokubalika kwa mujibu wa kanuni, taratibu na sheria za Halmashauri zetu. Kwa hiyo, inapotangazwa ile tenda kama Kamati ya Fedha ikiona kuwa taratibu zimekiukwa, pale pale Kamati ya Fedha ina uwezo wa kuzuia na kutangaza upya zabuni ile. Kwa hiyo, mimi nasema kuwepo kwetu nje kunatusaidia sana katika kupata heshima kwa wale ambao wametuchagua maana tuna uwezo wa kusimamia zaidi shughuli hizi. (*Makofi*)

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa mara nyingi huu usimamizi wa Madiwani unakuja baada ya tendo kuwa limetendeka na pesa nyingi zimepotea. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kama wenye mali wenyewe ambao ndio Madiwani wangeshughulika na suala hili la zabuni isingewezekana kabisa kutokea wizi ambao unatokea hivi sasa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Malizia kujibu Mheshimiwa Naibu Waziri ingawa sio Wizara yako hii lakini naona unajitahidi. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, kwanza sio kweli kwamba Madiwani ambao ndio wenye mali wanasimamia katika hatua za mwisho. Sisi Madiwani tunaanza kusimamia mwanzoni kwa sababu kabla kikao cha tenda hakijakaa ni Kamati inayohusika ndio inayopanga mradi upi utekelezwe wapi. Baada ya kuamua hivyo Kamati hiyo ya Wataalam inakaa kutangaza zabuni, lakini bado usimamizi wake ni wa

sisi Madiwani. Mimi narudia kusema kama nilivyokuwa najibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Halimenshi Mayonga kwamba, kuwepo kwetu nje ya Kamati za Zabuni kunatujengea heshima na kunatuokoa katika mambo mengi ambayo kwa kweli yangeweza kututumbukiza mahali pabaya nyakati za uchaguzi. *(Makofi)*

Na. 141

**Ugonjwa wa Malaria na Matende**

**MHE. RUTH B. MSAFIRI (K.n.y. MHE. IRENEUS N. NGWATURA** aliuliza:-

Kwa kuwa inaonyesha kuwa sehemu za miinuko au milima kama ilivyo kwa Nyanda za Juu Kusini hususan maeneo ya Mbeya, Iringa, Ruvuma na Kaskazini Mashariki ikiwemo Mikoa ya Kilimanjaro, Tanga na Arusha hayakuwa na mbu na hivyo wakazi wa sehemu hizo hawakusumbuliwa na ugonjwa hatari wa *malaria* na kwa kuwa miaka ya hivi karibuni kasi ya ongezeko la mbu kwenye sehemu hizo hasa kwenye msongamano wa wakazi ni kubwa na hivyo husababisha milipuko ya magonjwa ya Malaria na Matende:-

(a) Je, ni sababu gani zimesababisha janga hilo?

(b) Kwa kuwa kinga ni bora kuliko tiba. Je, Serikali imejiandaa vipi kudhibiti hali hiyo ambayo inazidi kuwa mbaya kila mwaka?

(c) Je, upo ushahidi wowote unaothibitisha hisia za baadhi ya watu kuwa mbu hawawezi kuhimili maeneo ya baridi?

**WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ireneus Ndunguru Ngwatura, Mbunge wa Mbinga Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa na matukio ya ugonjwa wa malaria katika maeneo ambayo hapo awali yalieleweka kuwa hayana malaria hususan maeneo ya milimani ikiwemo maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja.

Kuenea kwa malaria kunahusiana na kuwepo kwa mvua, miinuko ya ardhi chini ya mita 2000 kutoka usawa wa bahari, hali ya joto kati ya nyuzi joto 20 hadi 30 sentigredi na hali ya unyevunyevu hewani *(relative humidity*) kwa asilimia sitini. Maeneo ambayo huwa na sifa hizo ndio ambayo kwa kawaida yamekuwa na tatizo la ueneaji wa ugonjwa wa malaria karibu wakati wote kwa mwaka.Sababu kubwa iliyopelekea maeneo ya milimani na mengineyo kukumbwa na tatizo la malaria ni mabadiliko ya hali ya joto duniani (*Global Warming*) na vile vile uharibifu wa mazingira unaofanywa na wananchi katika maeneo husika. Mabadiliko haya yamesababisha maeneo haya kufikia kiasi cha joto ambacho kinawezesha mbu wa malaria kuzaliana na hivyo kueneza malaria.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria inayo mikakati mbalimbali kukabiliana na ugonjwa wa malaria nchini. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha tiba sahihi ya malaria;
(ii) Kutoa tiba ya tahadhari kwa akinamama wajawazito;
(iii) Kudhibiti mbu hasa kwa kuhimiza matumizi ya vyandarua vilivyotiwa dawa; na

(iv) Kudhibiti milipuko ya malaria katika maeneo yaliyo katika hatari ya kupatwa na milipuko.

Mheshimiwa Spika, katika kuipa kipaumbele kinga dhidi ya malaria Wizara yangu kwa kushirikiana na asasi mbalimbali na Halmashauri za Wilaya imekuwa ikiwahamasisha wananchi juu ya matumizi ya vyandarua hasa vilivyotiwa dawa na vile vile usafi wa mazingira katika mazingira yanayowazunguka. Aidha, Serikali imezindua mpango maalum wa matumizi ya vyandarua unaoitwa HATI PUNGUZO kwa akinamama wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Vyote hivi ni katika jitihada za kujikinga na malaria.

(c) Kama nilivyoeleza katika kipengele (a), ili mbu aweze kueneza vimelea vya malaria katika eneo husika, panahitajika hali ya joto kati ya wastani wa nyuzi joto 20 hadi 30 sentigredi, hali hiyo ndiyo inayojitokeza katika maeneo ya milima kutokana na ongezeko la joto duniani.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa afya bora ni mtaji na mtaji huu unashambuliwa sana na mbu anayeeneza malaria kama majibu yalivyotolewa katika swali la msingi. Katika bajeti iliyopitishwa vyandarua havikupunguzwa bei, sasa je, Serikali itakuwa na utaratibu wa kupunguza bei za vyandarua hivi nchini kwa ajili sio ya akinamama tu ila kwa ajili ya Watanzania wote ili kuweza kujikinga na hali ambayo imejitokeza ya mbu sasa kuwa nchi nzima badala ya maeneo machache ambayo zamani mbu walikuwepo? (*Makofi*)

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kukubaliana naye kwa kauli kwamba afya bora ni mtaji. Ningependa kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba, utaratibu wa HATI PUNGUZO ni kwa akinamama wajawazito na watoto walio chini ya umri wa miaka mitano. Kwa kawaida inategemeana na saizi ya chandarua, vyandarua vinaanzia sh. 3,000/= mpaka sh. 5,000/=. Sasa kwa akinamama wajawazito na kwa watoto wachanga wanapewa hati punguzo ya sh. 2,750/=. Kama ni chandarua cha sh. 3,000/= yule mama mjamzito anatakiwa kulipa tu sh. 50/=, lakini vyandarua vyote havitozwi kodi ya *VAT*, kwa hiyo bei zake ni rahisi. Kwa hiyo, kila Mtanzania anaweza kununua chandarua ambacho bei yake ni rahisi isipokuwa kwa akinamama wajawazito na watoto wachanga urahisi unazidi. (*Makofi*)

**MHE. JANETH B. KAHAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa hivi karibuni Ifaraka kulikuwa na utafiti ambao ulifanywa na Bwana Kija na Waholanzi na Waswiz kuhusu udhibiti wa malaria wakitumia nguo nyeusi na fangasi: Je, Wizara ya Afya mpaka hivi sasa ina mpango gani wa kufuatilia suala hili na kusaidia ili tuweze kudhibiti malaria?

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, katika udhibiti wa malaria suala la kudhibiti mbu wenyewe ni la msingi. Kwa hiyo Wizara kupitia NIMR na vituo vyake vya utafiti vimekuwa vikifanya utafiti kutafuta namna bora ya kuua viluwiluwi vya mbu ili mbu wasitotolewe au namna bora ya kuwaua mbu. Sasa huu utafiti uliofanyika tumepata taarifa zake kwa mara ya kwanza, sasa tunafanya majaribio katika sehemu kubwa zaidi, inatoka kwenye majaribio inakwenda kufanya shughuli hiyo katika maeneo makubwa na ikithibitika kwamba njia hiyo ni bora zaidi basi tutatumia zote vyandarua na namna ya kuua mbu. Ieleweke kwamba haturuhusiwi kutumia *DDT* katika maeneo ambayo yana unyevunyevu kwa nje, *DDT* tunatumia kwa ndani kama inawezekana watu kupata dawa hizi za kunyunyizia kwa ndani.

Lakini utafiti huu uliogunduliwa kule Ifakara unatumia viatilifu vinavyotokana na viumbe asili na hii tunadhani ni kitu kikubwa sana kilichovumbuliwa na Watanzania na mara utafiti huo utakapothibitika ili uweze kutumia katika maeneo makubwa ya kufanya shughuli hii tutaieneza na tutawambia Watanzania na inawezekana hivyo viatilifu vitengenezwe ili wananchi waweze kuvipata kwa urahisi, lakini kwa sasa zile hatua zilikuwa ni za mwanzo.

Na. 142

**Madhara ya Sigara kwa Wanadamu**

**MHE. RAYNALD A. MROPE (K.n.y. MHE. MARIA D. WATONDOHA)** aliuliza:-

Kwa kuwa sigara inaleta madhara katika afya ya binadamu licha ya kuwa Tumbaku inaendelea kulimwa kama zao la biashara:-

(a) Je, Serikali haoni kuwa kusimamia uzalishaji wa zao la Tumbaku kunaongeza ushawishi kwa wananchi kupenda kuendelea kuvuta sigara licha ya madhara yake?

(b) Kwa kuwa katika baadhi ya maeneo ya Tanzania, Tumbaku husokotwa na kuvutwa, aidha wengine wanabwia. Je, Tumbaku hiyo inayotumika hivyo ina madhara gani kwa mtumiaji?

**WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Watondoha, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali inasimamia uzalishaji wa zao la Tumbaku; hata hivyo usimamizi wa uzalishaji wa zao hili na kuongezeka kwa ushawishi wa utumiaji wa Tumbaku miongoni mwa wananchi havina uhusiano wa moja kwa moja. Ushawishi mkubwa wa utumiaji wa bidhaa za tumbaku hufanywa nawafanyabiashara, hususan wale wenye viwanda vinavyosindika tumbaku, kwa lengo la kupata watumiaji wengi wa sigara,kukuza biashara yao na kujipatia faida.

Matangazo mbalimbali yanalenga kushawishi wananchi na hasa vijana kuanza ama kuendelea kutumia bidhaa za tumbaku. Hata hivyo, kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula na Shirika la Afya Ulimwenguni *(WHO)* Wizara yangu na Serikali kwa ujumla ina azma ya kuanzisha zao mbadala ili wakulima wa tumbaku waweze kupata fedha za kuendesha maisha yao badala ya kutegemea zao la tumbaku pekee.

(b) Mheshimiwa Spika, uchunguzi wa kitaalam uliofanywa na Shirika la Viwango Tanzania unaonyesha kuwa sigara zinazosindikwa viwandani hapa nchini zina aina kuu tatu za kemikali zenye madhara makubwa kwa afya ya binadamu. Aina za kemikali hizo ni:-

1. Lami *(Tar);*
2. Nikotini *(Nicotine);* na
3. Kaboni *monoxide (Carbon Monoxide).*

Mheshimiwa Spika, bidhaa nyingine za tumbaku ambazo hazijasindikwa viwandani kama vile ugoro na msokoto na kadhalika zina kiwango kikubwa cha kemikali ukilinganisha na bidhaa za tumbaku zilizosindikwa na kwa hiyo matumizi ya bidhaa hizi yanaweza kusababisha madhara mengi kwa afya ya binadamu. Tumbaku inayotumika kwa kuvutwa au kubwia inaweza kusababisha madhara yafuatayo:-

- Saratani ya koo, ulimi, mapafu, kizazi hasa kwa akinamama, ngozi na viungo vingine.
- Nywele kunyonyoka.
- Mtoto wa jicho.
- Kukunjamana kwa ngozi.
- Kutosikia vizuri.
- Meno kuoza.
- Mapafu kushindwa kufanya kazi vizuri.
- Mifupa kuwa laini.
- Maradhi ya moyo.
- Vidonda vya tumbo.
- Kupungua kwa nguvu za kiume.
- Ukurutu.
- Kuziba mishipa midogo ya damu.

Mheshimiwa Spika, madhara mengine yanatokana na matumizi ya Tumbaku ni pamoja na kupoteza fedha ambayo ingeweza kutumika kwa mahitaji muhimu kwa maendeleo familia. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Raynald Mrope, atafuatiwa na Mheshimiwa *Brother. (Kicheko)*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri wa Afya. Ningependa kuuliza kwamba kwa hivi sasa katika Jiji la Dar es Salaam matangazo ya sigara yapo kwa wingi sana na kutangaza huko kunaleta madhara kwa watoto na watu mbalimbali. Je, kwa nini Serikali kwa hivi sasa haisemi kwamba matangazo ya biashara ya sigara yanapigwa marufuku moja kwa moja katika sehemu zote, barabarani na kwenye mabaa na katika sehemu nyingine zote za starehe?

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba matangazo hayo yapo. Lakini Sheria tuliyokuwa tumeipitisha tulisema kwamba hata yakiwepo kuwe na tahadhari basi kule chini ya kila tangazo tena tumewambia waongeze tahadhari hiyo inasema uvutaji wa sigara ni hatari kwa afya yako. Tumewambia tangazo liwe ndogo lakini lile neno la tahadari liwe kubwa zaidi.

Lakini Serikali inaelekea katika kupiga marufuku matangazo ni mpaka hapo tutakaporidhia Mkataba wa Kimataifa ambao ulipitishwa na Shirika la Afya Dunia juu ya Tumbaku. Kwa hiyo, sisi wanachama tulikwishatia saini lakini inabidi sasa tulilete hapa Bungeni na mara litakapopitishwa hapa Bungeni basi tutachukua pia yote yaliyokubaliwa Kimataifa ili tuyaingize katika sheria yetu. *(Makofi)*

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Tumbaku ni uchumi na kwa kuwa wavutaji wa sigara wengi hatuugui malaria na *actually* Tumbaku ni *Anti – Malaria* hata ukisoma kwenye historia yake huko *South America*. Sasa naomba kuuliza. Je, kwa kuwa hata wale ambao hawavuti sigara nao wanakufa wakati mwingine na kansa hili analielezaje? Ahsante. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Tumbaku ni uchumi na ndiyo maana mimi katika jibu langu la msingi nimesema hivi kwamba kulima Tumbaku hakuhusiani na kuvuta sigara na mimi ninajua wakulima wengi wa tumbaku wala havuti kabisa. Marekani ni wakulima wakubwa vilevile wa Tumbaku lakini wana sheria kali za kuvuta tumbaku. Kwa sababu hii ni biashara, sisi tunalima tufanye biashara. Lakini nimesema itafika wakati ambapo dunia nzima itakubaliana kwamba tuwape wakulima zao mbadala ili kuondokana na zao la Tumbaku. Sisi tutakuwa watu wa ajabu tukisema tupige marufuku zao la Tumbaku wakati dunia nzima inalima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tunajaribu kuwambia watu wasivute sigara. Lakini utafiti kwamba eti anayevuta sigara hapati malaria. Sijui ningemuuliza Mheshimiwa

Mbunge katika Ubunge wake wote katika kipindi hiki hajaugua malaria, sina hakika kama hajaugua malaria. Lakini haina uthibitisho wa kimaabara. Hatuwezi kusema kwamba Tumbaku ni *Anti Malaria* na nisingependa kabisa wananchi waamini jambo hili kwa sababu litaleta athari sana katika maisha yao. *(Makofi)*

Na. 143

**Mikoa Inayohifadhi Wakimbizi**

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO (K.n.y. MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna migogoro ya kiusalama inayojitokeza sasa katika mipaka ya nchi yetu, hususan katika Mikoa inayowahifadhi wakimbizi;

Je, Serikali haioni kwamba itakuwa ni jambo jema na la busara kutazama upya na kuandaa mipango ya kuwahifadhi wakimbizi kwenye Mikoa ya katikati ya nchi ama Mikoa ambayo haipakani na nchi wanamotoka wakimbizi hao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wakati mwingine pamejitokeza matatizo ya kiusalama katika mipaka ya nchi yetu kutokana na kuwepo kwa wakimbizi katika Mikoa ya Kagera, Kigoma na Rukwa, inayopakana na nchi jirani zenye migorogoro ya kivita kama Burundi, Rwanda na *Congo (DRC)* ambako wananchi wake wanalazimika kukimbilia katika nchi yetu.

Katika kudhibiti hali hiyo, Serikali imeweka ulinzi imara katika mipaka yetu kupitia Jeshi la Wananchi. Vilevile Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Wakimbizi Duniani *(UNCHR)* imeweka utaratibu wa kudhibiti ulinzi na usalama ndani ya eneo ya makambi ya wakimbizi na maeneo yanayozunguka makambi hayo katika Mikoa ya Kigoma na Kagera. Chini ya utaratibu huo wa ulinzi, unaoitwa *Security Package*, Serikali yetu inatakiwa na tayari imeshaweka kikosi maalumu cha Jeshi la Polisi kulinda usalama katika maeneo yenye wakimbizi na *UNHCR* hutoa vitendea kazi, hasa magari na vifaa vya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kuhifadhi wakimbizi ni la muda, sio la kudumu, na suluhisho lake ni kwa wakimbizi kurejea makwao punde amani inaporejea katika nchi zao. Hivi sasa amani imerejea Burundi kwa kiwango kikubwa na zoezi la kuwarejesha makwao wakimbizi wa Burundi linaendelea. Vivyo hivyo amani imeanza kurejea *Congo (DRC),* na mazungumzo yameanza baina yetu, Serikali ya Kongo *DRC* na *UNHCR* tukijadili kuhusu taratibu za kuwarejesha kwao wakimbizi wa *Congo DRC.*

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa juhudi za Serikali zimeelekezwa katika kuwarejesha makwao wakimbizi. Hivyo Serikali haioni umuhimu wa kuwahamishia wakimbizi hao kutoka katika Mikoa hiyo ya mpakani na kuwaleta katika Mikoa ya katikati ya nchi. Badala yake Serikali inachukua hatua za kuwarejesha makwao wakimbizi wote.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa imedhihirika mara kwa mara kwamba baadhi ya Mashirika kama *UNHCR* na watumishi wake wamekuwa badala ya kusaidia wakimbizi kurudi makwao, wanasaidia kuchochea wakimbizi kutorudi makwao na kwa kuwa Tanzania imekuwa ikibeba mzigo mkubwa sana wa wakimbizi hao kutoka nchi jirani. Je, nini msimamo wa Serikali kuhusiana na Mashirika hayo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la awali kwamba zile nchi ambazo zina wakimbizi hapa kwetu amani imeanza kurejea na wakimbizi wameanza kurudi makwao. Mpaka sasa wakimbizi wa Burundi tayari wameisharudi kwao 1,82,000 na hao wamerudi kwa msaada mkubwa wa *UNHCR.* Kwa hiyo, Shirika hilo linasaidiana na sisi katika zoezi la kuwarejesha makwao na tunashirikiana vizuri kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, Sasa ni kweli ndani ya Mashirika kama haya kunatokea wakorofi wachache si Shirika lote ila wakorofi wachache wanatokea ambao wanajaribu kuzuiazuia na kushusha nguvu za kurejesha makimbizi makwao na inapotokea hali hiyo Maafisa kama hao tunawafukuza hapa nchini na mwaka juzi tumemfukuza Afisa mmoja hapa nchini kwa kosa kama hili. Lakini kwa ujumla wake kama Shirika *UNHCR* tunashirikiana nao vizuri.

Na. 144

**Ununuzi wa Magari ya Polisi**

**MHE. ABDALLAH KHAMIS FERUZI (K.n.y. MHE. KHAMISI AWESU ABOUD)** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Mkutano wa Bajeti wa mwaka 2004/2005 Serikali ilitoa kauli kuwa itanunua magari 17 kwa ajili ya matumizi ya Jeshi la Polisi nchini na kwa kuwa Serikali haijatoa taarifa juu ya kununuliwa kwa magari hayo:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya ununuzi wa magari hayo?

(b) Kwa kuwa nchi yetu ina vituo vingi vya Polisi na kila kituo kinahitaji gari kwa ajili ya matumizi ya kazi zao kikiwemo Kituo cha Polisi Mkoani Pemba. Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ununuzi wa magari hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khamisi Awesu Aboud , Mbunge wa Mkanyageni, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa katika Mkutano wa Bajeti wa Mwaka 2004/2005 Serikali ilitoa kauli kuwa itanunua magari ya Polisi 215 na siyo 17 kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge. Mpango wa kununua magari hayo umekamilika na yatapatikana wakati wowote kuanzia sasa.

Aidha, kutokana na ukubwa wa nchi yetu, na uhaba mkubwa wa magari katika Jeshi la Polisi, magari hayo yaani 215 hayatakidhi mahitaji yote ya Jeshi la Polisi. Hata hivyo jitihada zitafanywa katika usambazaji ili kila Wilaya pamoja na Wilaya za Pemba zipate gari zima ya kufanyia kazi.

Vilevile katika Bajeti ya mwaka ujao wa fedha 2005/2006 ambayo tutaiwasilisha katika wiki mbili zijazo vilevile mle ndani tumeomba kununua magari mengine ya Polisi ili kuzidi kuliongezea uwezo Jeshi la Polisi katika kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

**MHE. FRANK G. MAGHOBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa Serikali sasa imeagiza magari na karibu yatagawiwa. Je, Serikali ina mpango gani kwa kugawa magari kwenye Mikoa ambayo ina wakimbizi wengi kwa ajili ya kuweka usalama zaidi katika Mikoa hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, hayo magari ambayo tutaanza kugawa hivi karibuni tunazingatia Mikoa na Wilaya zote zikiwemo Wilaya zenye wakimbizi na Wilaya zenye wakimbizi kwa kawaida zinapata migao miwili kwa sababu wana tatizo maalum kwa kawaida wanapata migao miwili.

Mgao wa kwanza ni hayo magari yanatoka katika Wizara yetu, lakini mgao wa pili ni yale magari ambayo yanatolewa na *UNHCR*. *UNHCR* wakitoa magari yanakwenda kwenye maeneo ya wakimbizi tu. Kwa hiyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge kwa jumla na Mheshimiwa Mbunge wa Ngara naona anasikiliza kwa makini kabisa ni kwamba wao watapata mgao wa Wizara na mgao wa *UNHCR* uko pale pale. *(Makofi)*

**SPIKA:** Bado nina maswali matatu ya msingi, kwa hiyo naendelea na maswali kwa Wizara ya Maji na Maendeleo na Mifugo.

Na. 145

**Majisafi ya Kunywa – Mji wa Maganzo**

**MHE. PAUL N. MAKOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa Maji katika Mji wa Maganzo kwenye Kata ya Songwa yana *floride* nyingi na kusababisha wakazi wa eneo hilo kupata shida ya maji ya kunywa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia upatikanaji wa Maji safi ya kunywa katika sehemu hizo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Makolo, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mwaka 2002 Wizara ilifanya uchunguzi wa awali na upembuzi yakinifu wa mradi wa maji utakaohudumia Mji wa Maganzo. Uchunguzi huo ulipendekeza kwamba maji ya bomba kwa ajili ya Mji wa Maganzo yanaweza kupatikana kutoka mabwawa ya Nhumbu na Songwa yanayomilikiwa na Kampuni ya Uchimbaji Madini ya Mwadui.

Wizara yangu iliishauri Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kufanya mazungumzo na kampuni hiyo ili kupata chanzo cha uhakika cha maji kwa Mji wa Maganzo. Mazungumzo hayo bado yanaendelea na punde yatakapokamilika Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga itafanya upembuzi yakinifu wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, wakati juhudi hizo zinaendelea, naishauri Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu kukasimia na kuomba fedha za kupanua na kukarabati mtandao wa mabomba uliopo kwa sasa kutoka Programu ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini inayotekelezwa katika Wilaya zote za Mkoa wa Shinyanga chini ya Msaada wa Serikali ya Uholanzi.

**MHE. PAUL N. MAKOLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa katika Mji huo wananchi walishachimba kisima cha maji kwa gharama kubwa tu na mtambo ukapelekwa. Lakini Maafisa wa Maji wakazuia utumiaji wa maji hayo kwamba yana madhara.

Je, isingekuwa hasa ni vizuri Mheshimiwa Naibu Waziri akaruhusu mtambo ukawekwa ili maji hayo yakaweza kutumika angalau kwa kufulia nguo na pengine kwa kuoga kwa wananchi wa eneo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo ilizuia kuweka pampu katika kisima kile kwa sababu kiwango cha *fluoride* kilikuwa kimezidi kile cha Kimataifa ambacho ni miligramu 8 katika kila lita moja. Maji yale kama yangetumika yangeweza kuleta madhara makubwa ya meno lakini vilevile kupinda viungo vya mwili.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa kushirikiana na watafiti wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kitivo vha Uhandisi na Wizara ya Afya, Kitengo cha Meno wanafanya utafiti wa namna ya kupunguza kiwango cha f*luoride* na inaonekana kwamba jambo hilo litafanikiwa kutokana na utafiti huo.

Mheshimiwa Spika, ninafurahi kusema kwamba hata wataalam wa Kijapan baada ya kuona maendeleo ya utafiti huo sasa wanatarajia kujenga mitambo ya majaribio ya teknolojia hiyo na tutaanza na Wilaya ya Hanang, Igunga, Manyoni na Singida Vijijini. Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Mbunge asione kwamba kuzuiwa kwa kuwekwa pampu ile ni ukatili kwa watu wa Maganzo.

Lakini ni kujaribu tu kuokoa maisha yao maana si kweli kwamba kuna mtu atazuia maji hayo yasitumike kwa matumizi ya binadamu wakayatumia kwa kufulia tu itakuwa ni ulinzi ngumu sana katika jambo hilo. *(Makofi)*

Na. 146

**Shirika la Bima la Taifa**

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliuliza:-

Kwa kuwa yapo malalamiko mengi toka kwa walimu ya kutolipwa Bima zao kutoka Shirika la Bima la Taifa hasa baada ya Bima zao kuiva:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwalipa walimu hao fedha ambazo ni haki yao ya kimkataba na Shirika hilo?

(b) Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya hali ya kifedha kwa Shirika hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA FEDHA)** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, naomba nitoe maelezo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba walimu pamoja na wateja wengine wa Bima wamekuwa wakilalamika kwa kutolipwa kwa wakati mafao yao ya Bima kutoka Shirika la Bima la Taifa. Sababu kubwa iliyopelekea Shirika kushindwa kulipa madai hayo kwa wakati, ni tatizo la ukwasi unaolikabili Shirika hilo hali ambayo imesababisha usumbufu mkubwa kwa wateja wanaolidai mafao yaliyoiva. Hata hivyo, Shirika limekuwa likijitahidi kulipa madai kidogo kidogo kwa kutumia mapato yake yanayotokana na ada za bima pamoja na vitega uchumi.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mwailugula Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kuhusu malipo ya bima za walimu zilizoiva, Serikali kwa kuzingatia kuwa Shirika la Bima lipo katika hatua za ubinafsishaji, imelitaka Shirika kuchukua hatua mbalimbali za kuliwezesha kupata fedha za kulipa madai haya. Hatua hizo ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(a) Kuuza baadhi ya rasilimali za Shirika ili kupata fedha za kulipa madai. Hadi sasa shilingi milioni 300 zimekwishapatikana kulipia madai hayo.

(b) Kutoa maelekezo kwa Tume ya Rais ya Kubinafsisha Mashirika *PSRC* kuuza hisa za *NIC* inazomiliki katika mradi wa jengo kubwa sana la *Ubungo Plaza,* ambapo inategemewa kiasi cha mabilioni kadhaa ya fedha zitapatikana hivi punde.

(c) Kutoa kibali kwa Shirika la kutumia fedha za gawio litokanalo na hisa za Serikali katika Kampuni ya *Africare Insurance*. Tunategemea kupata gawio la takriban shilingi milioni 12 kwa mwaka huu wa 2005.

Kufuatia hatua hizi, na pia kwa kutumia mapato yake mengine, Shirika limekwishafanya malipo kwa walimu ya jumla ya shilingi bilioni 1.457 kati ya madai ya shilingi bilioni 6.158 yaliyoiva kwa kipindi cha kuanzia Januari hadi Oktoba 2004. Shirika litaendelea kulipa madai haya katika mwaka huu wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haioni ulazima wa kutumia fedha za walipa kodi kulipa madai yaliyoiva kwa sababu Shirika lina uwezo wa kuyalipa kwa kuuza mali zake na hata biashara yake.

Hivi sasa Serikali inaangalia namna ya kuikopesha *NIC* fedha kiasi ili kuharakisha ulipaji wa madai yaliyopo. Serikali inaona umuhimu wa kuharakisha

ubinafsishaji wa Shirika hilo ili kulipa madeni yote yaliyopo na yatakayojitokeza. Kazi hii inahitaji uangalifu mkubwa ili wateja wasipoteze haki zao.

**MHE. BENSON M. MPYESYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa kuwacheleweshea walimu hao malipo ya Bima ni kuvunja Mkataba. Je, sasa Serikali itakuwa tayari kuwalipa walimu hao pamoja na riba kwamba wamecheleweshewa kama kanuni za fedha zinavyohitaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara zote, endelea kujibu swali la nyongeza. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA FEDHA):** Mheshimiwa Spika**,** ni kweli kwamba kuwacheleweshea wateja kuwalipa bima zao ambazo zimeishaiva ni kwenda kinyume na Mkataba. Lakini Mkataba wao vilevile hauzungumzii kwamba fedha ikicheleweshwa basi walipwe na riba. Kwa hiyo, wataendelea kulipwa kutokana na Mkataba ule unavyosema. *(Makofi)*

Na. 147

**Misaada kutoka kwa Wafadhili**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA (K.n.y. MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI)** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi rafiki wa Tanzania pamoja na Mashirika ya Kimataifa yanatoa misaada mingi kwa nchi yetu ya Tanzania na misaada hiyo hupelekwa katika Mikoa mbalimbali:-

(a) Je, Mkoa wa Ruvuma umepewa kiasi gani cha misaada hiyo au umefadhiliwa na nchi ngapi tangu tupate uhuru?

(b) Je, kama ile dhana kuwa anayefadhili anachagua Mkoa au eneo atakalofadhili na Serikali ikakubaliana na dhana hiyo. Je, Serikali haioni kuwa nchi itakuwa na maeneo fulani yenye maendeleo mazuri na yale maeneo yasiyofadhiliwa yataendelea kubakia maskini. Serikali inasema nini sasa juu ya hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA FEDHA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Simon Mbilinyi, Mbunge wa Peramiho, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tangu tupate uhuru Mkoa wa Ruvuma kama ilivyo kwa Mikoa mengine, umekuwa ukipata misaada ya aina mbalimbali kwa utaratibu wa Kitaifa kwa wakati husika. Si rahisi kufahamu kwa sasa kiasi cha fedha cha misaada hiyo kwa kila Mkoa kwa sababu Serikali haina utaratibu wa kuweka takwimu za ufadhili Kimkoa.

Hata hivyo, taarifa tulizonazo ni kwamba, Mkoa wa Ruvuma umeshapata ufadhilli wa miradi mbalimbali inayofikia kiasi cha shilingi bilioni 40.7 kutoka nchi wahisani na taasisi za kifedha za Kimataifa ambazo ni pamoja na Austria, Ubeligiji, Uingereza, Jumuiya ya Ulaya, Iran, Italia, Japan, Kuwait, Uholanzi, Hispania, Sweden, Marekani na Mfuko wa Elimu na Watoto wa Umoja wa Mataifa *(UNICEF).* Miradi iliyo husika ni ya sekta za kilimo hasa mahindi na kahawa, barabara, elimu, afya na kadhalika.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu ya Bajeti, Serikali sasa inahimiza wafadhili kugharamia miradi kwa maelekezo ya Serikali, siyo ya kwao, kama ilivyokuwa huko nyuma. Aidha, Serikali sasa inaelekeza fedha Mikoani kwa msingi wa fomula iliyoamuliwa kitaalam na si vinginevyo.

Aidha, Mkoa wa Ruvuma unaendelea kufaidika na ufadhili wa miradi mikubwa mfano wa umeme kutoka Makambako na Njombe, wa barabara na miradi mingine ya *Mtwara Corridor*, wa huduma mbalimbali kwa wakulima, wa Elimu ya Msingi (MEM) Sekondari (MES) *TASAF* na kadhalika.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Prof. Simon Mbilinyi na wana Ruvuma kwa ujumla wasiwe na wasiwasi kuwa wanabaguliwa na kuachwa maskini kuliko Mikoa mingine Tanzania.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa maendeleo huendana na wakati na wakati huleta aina ya maendeleo husika katika kila eneo. Na kwa kuwa katika kuchangia hoja ya Waziri wa Fedha, Mkoa wa Ruvuma ili kujiletea maendeleo umekuwa ukililia sana ujenzi wa daraja la Monkulu ili kuweza kuvuka kuingia Msumbiji kuleta maendeleo. Je, Mheshimiwa Waziri wa Fedha yuko tayari sasa kuwasaidia wananchi wa Mkoa wa Ruvuma kujenga hoja ya maendeleo ya ujenzi wa daraja hilo ili kuwavutia wafadhili kuongeza kiasi cha fedha katika mkoa huo na kuuletea mkoa huo maendeleo?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ujenzi wa daraja linalozungumzwa na Mheshimiwa Mbunge uko kwenye hatua nzuri sana.

Katika Bajeti ya mwaka huu ya Wizara ya Ujenzi zimetengwa shilingi bilioni 4.5. Lakini pia katika Bajeti ya Serikali ya Msumbiji wamekwishapitisha na kutenga Dola za Kimarekani milioni 4.5 ambazo ni sawa sawa na shilingi bilioni 4.5. (*Makofi)*

Kwa hiyo katika Bajeti ya mwaka huu wote katika nchi mbili kuna shilingi bilioni 9. Kwa hiyo, huu ni uhakika wa wazi kabisa kwamba ujenzi wa daraja hili utaanza. Lakini pia *consultant* ambaye ni Kampuni ya *Norconsult* pamoja na Kampuni zingine kutoka Tanzania na Msumbiji mkataba umekwishatiwa saini kwa ajili ya kuanza kufanya *design* na kwenye mwezi Septemba tunategemea jiwe la msingi litawekwa kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo muhimu linalounganisha nchi hizi mbili. (*Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha na maswali vile vile yamejibiwa yote.

Kuna tangazo moja tu la kikao cha Kamati. Ni Kamati ya Mambo ya Nje. Mheshimiwa Dr. Shija, Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje anaomba Wajumbe wake wakutane leo tarehe 27 Juni, 2005 katika chumba Na. 231 kuanzia saa 4.30 asubuhi hii.

Waheshimiwa Wabunge, hapo ndiyo mwisho wa matangazo. Katibu endelea na *Order Paper.*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2005/2006

### Wizara ya Ujenzi

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabla sijaaanza kuzungumza chochote ningeiomba niombe radhi sana sauti yangu zi nzuri sana kwa leo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha wa 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Miundombinu kwa ushirikiano iliotoa kwa Wizara yangu katika kipindi cha miaka mitano ambayo tumefanya kazi pamoja. Kamati hii imesaidia sana Wizara ya Ujenzi kutekeleza majukumu yake kwa kutoa ushauri na maelekezo, na hivyo nafurahi kusema kwamba Wajumbe wa Kamati ya Miundo Mbinu wamechangia kikamilifu katika mafanikio yote yaliyopatikana katika Sekta ya Ujenzi katika kipindi cha kuanzia Novemba 2000 hadi leo.

**Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, Mbunge wa Hanang, kwa hotuba yake katika Bunge hili la Bajeti ambayo pamoja na mambo mengine imefafanua mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu na kutoa upeo wa majukumu ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi katika kipindi kijacho.**

**Aidha, nawapongeza Waziri wa Fedha Mheshimiwa Basil P. Mramba na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda kwa hotuba zao ambazo zimeweka wazi sera, hali ya uchumi wetu, malengo na mikakati ya utekelezaji wa mipango ya Serikali katika kipindi cha mwaka 2005/2006. (*Makofi)***

**Mheshimiwa Spika, katika miezi kumi na moja iliyopita, tumepoteza Wabunge wenzetu watano ambao waliaga dunia. Wabunge hao ni Hayati Mheshimiwa Yete Simtemule Mwalyego aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini,**

**Hayati Mheshimiwa Theodos James Kasapila aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki, Hayati Mheshimiwa Frank Michael Mussati aliyekuwa Mbunge wa Kasulu Mashariki, Hayati Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria aliyekuwa Mbunge wa Rahaleo na Hayati Mheshimiwa Abubakar Towegale Kiwanga aliyekuwa Mbunge wa Kilombero. Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu hawa mahali pema peponi.*(Amin)***

Mheshimiwa Spika, dira ya Wizara ya Ujenzi ni kuendeleza Sekta ya Ujenzi ili iwe endelevu, yenye ufanisi na inayotoa huduma bora na nafuu katika mazingira ya

ushindani ili kuchochea na kuleta ufanisi katika maendeleo ya jamii na kiuchumi, na hivyo kuchangia kikamilifu katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

Aidha, katika kuendeleza Sekta ya Ujenzi, ili kutumia kikamilifu faida ya Kijiografia *(geographical location)* iliyonayo Tanzania katika kuziunganisha nchi kadhaa tunazopakana nazo na Bandari za Dar es Salaam, Tanga, Mwanza, Kigoma, Bukoba, Mtwara, Mbambabay, Kasanga na Itungi, Wizara ya Ujenzi inaendelea kutekeleza ukarabati na ujenzi wa Barabara Kuu kwa kiwango cha lami katika Kanda Kuu Tisa za Usafirishaji kwa kadri hali ya uchumi wetu na bajeti inavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko ya kiutendaji yaliyotokea katika sekta ya ujenzi chini ya *Public Service Reform Programme,* majukumu ya utendaji ya Barabara na Majengo yamehamishiwa kwa Wakala wa Barabara *(TANROADS)* na Wakala wa Majengo *(TANZANIA BUILDING AGENCY - TBA)* na Wizara imebakiwa na majukumu ya msingi yafuatayo:

- Kuandaa Sera, kubuni Mikakati na kupanga Mipango inayolenga katika ukuzaji, uimarishaji na uendelezaji wa sekta ya ujenzi nchini.

- Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ujenzi kwa kuzingatia mikakati iliyowekwa.

- Kusimamia uendeshaji wa shughuli za Bodi ya Mfuko wa Barabara, Wakala wa Barabara, Wakala wa Majengo pamoja na Wakala nyingine zinazotarajiwa kuundwa chini ya Wizara kama vile Wakala wa Ufundi na Umeme *(Tanzania Electrical, Mechanical and Electronics Services Agency* - *TEMESA)* na Wakala wa Bohari Kuu ya Serikali (*Government Stores Agency – GSA).*

- Kuratibu shughuli za Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi ambazo ni Baraza la Taifa la Ujenzi na Bodi za Usajili wa Makandarasi, Wahandisi, Wasanifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi na Usimamizi wa Vifaa.

- Kutafuta fedha za kugharamia matengenezo na miradi ya barabara, madaraja, vivuko na ujenzi wa nyumba.

- Kuandaa na kusimamia Viwango vya ubora wa kazi za Ujenzi, Ukarabati pamoja na Matengenezo ya barabara; ujenzi wa Nyumba na Majengo ya Serikali.

- Kusimamia Ununuzi, Utunzaji, Usambazaji Vifaa na upatikanaji wa Huduma mbalimbali kwa ajili ya shughuli za Serikali.

- Kusimamia shughuli za Usalama wa Barabara *(Road Safety*) na kudhibiti uzito wa magari (*Overloading Control).*

- Kusimamia viwango vya ubora na shughuli za Ununuzi, Ukarabati na Matengenezo ya magari, viyoyozi na vifaa vya elektroniki; kuendesha Vivuko na ukodishaji wa magari, mitambo ya kokoto na mitambo ya barabara ambavyo ni mali ya Serikali.

- Kusimamia Maendeleo ya Watumishi wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha majukumu yaliyotajwa hapo juu Wizara imejiwekea mikakati ifuatayo:-

- Katika kupunguza tatizo la kuwa tegemezi kwa Wahisani na kuongeza kasi ya ujenzi wa barabara nchini, Wizara imeanza utekelezaji wa Mpango Maalum wa kujenga Barabara Kuu kwa kutumia fedha za ndani kuanzia mwaka 2001/2002. Aidha, daraja la Umoja kati ya Tanzania na Msumbiji linajengwa kwa fedha zetu wenyewe toka Tanzania na Msumbiji. *(Makofi)*

- Kutafuta vyanzo zaidi vya fedha za Mfuko wa Barabara ili kukidhi mahitaji ya matengenezo ya mtandao wa barabara zetu.

- Kukarabati na kujenga Barabara Kuu kwa kufuata Kanda Kuu za Usafirishaji na Barabara za Mikoa na za Wilaya ambazo ni muhimu kwa huduma za usafirishaji wa mazao ya kilimo na huduma nyingine muhimu za kitaifa. *(Makofi)*

- Kuwaondoa waliojenga katika maeneo ya hifadhi ya barabara na kuwaelimisha wananchi ili waweze kutambua mipaka ya maeneo ya barabara *(road reserve)* na pia kuweka alama za kuonyesha mipaka ya maeneo ya hifadhi ya barabara.

- Kuweka mazingira mazuri ya upatikanaji wa zana za ujenzi kwa kuimarisha karakana za Serikali na kuhamasisha watu binafsi kuanzisha kampuni za kukodisha mitambo.

- Kutoa mafunzo kwa Wahandisi Washauri na Makandarasi wa Kizalendo ili wasimamie na kutekeleza vizuri mikataba ya ujenzi na matengenezo ya barabara na majengo.

- Kuendeleza teknolojia ya nguvu kazi ili kuwapa uwezo wananchi wengi zaidi kushiriki katika kazi za matengenezo ya barabara katika maeneo yao bila kulazimika kusubiri msaada kutoka Serikalini.

- Kuimarisha uwezo wa kiutendaji wa Wakala, Bodi na Taasisi zilizo chini ya Wizara ili ziweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

- Kuendesha mafunzo kwa Wafanyakazi wa Wizara ili kuwajengea uwezo zaidi wa kufanya kazi.

- Kusimamia kwa makini Sheria ya magari kutozidisha *uzito (Axle Load Control)* na shughuli za matumizi salama ya barabara *(Road Safety).*
- Kuimarisha uwajibikaji na uwazi katika utendaji kazi ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi na kudhibiti vitendo vya rushwa.

- Kukaribisha sekta binafsi kushiriki katika ujenzi wa miradi ya barabara na majengo ya Serikali.

- Kuimarisha huduma za vivuko nchini kwa kununua vivuko vipya na kuvifanyia ukarabati vivuko vilivyopo sasa.

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu kwamba hili ni Bunge la mwisho lilochaguliwa chini ya Serikali ya Awamu ya Tatu ya Chama cha Mapinduzi (CCM) iliyoingia madarakani mwezi Novemba mwaka 1995. Katika kipindi cha miaka kumi cha Serikali ya Awamu ya Tatu (1995 – 2005), Wizara yangu imeendelea kuimarisha mtandao wa barabara nchini kwa kuweka mkazo katika ujenzi na ukarabati wa Barabara Kuu, Barabara za Mikoa na Madaraja kwa lengo la kuhakikisha usafiri na usafirishaji wa kuaminika na nafuu nchini.

- Sambamba na ujenzi na ukarabati wa barabara, Wizara vile vile imekuwa ikiendelea na kazi za matengenezo katika Barabara zote Kuu na za Mikoa nchini kwa lengo la kutunza rasilimali kubwa iliyowekezwa kwenye ujenzi na ukarabati wa barabara hizo na hivyo kulipunguzia Taifa gharama kubwa zinazoambatana na kazi hizo. *(Makofi)*

Aidha, katika kipindi hiki cha miaka kumi (1995 – 2005), Wizara ya Ujenzi imepata mafanikio makubwa kama yanavyodhihirika katika:

- Kubuni na kuanza kutekeleza Mradi Maalum wa Ujenzi wa Barabara Kuu kwa kiwango cha lami kwa kutumia fedha zetu wenyewe. Jumla ya kilometa 826 zinajengwa kwa gharama ya Dola za Kimarekani 375.0 milioni;

- Kuboreka kwa mtandao wa Barabara Kuu na za Mikoa pamoja na Madaraja nchini kutokana na kuimarika kwa usimamizi na kuongezeka kwa bajeti ya matengenezo ya barabara toka Mfuko wa Barabara toka shilingi Bilioni 16.0 mwaka 1995/96 hadi shilingi Bilioni 45.788 mwaka 2004/2005 na shilingi Bilioni 50.077 mwaka 2005/2006;

- Kuimarisha juhudi za kulinda maeneo ya Hifadhi ya Barabara kwa kuweka mawe ya mipaka kwa kila mradi mpya;

- Kupungua kwa tatizo la kuzidisha uzito wa magari katika barabara zetu kutoka kiwango cha asilimia 40 (40%) hadi chini ya asilimia 7 (7%) ilipofika mwishoni mwa mwaka 2004;

- Maendeleo mazuri ya zoezi la kuwauzia watumishi wa Serikali na wa Mashirika ya Umma Nyumba za kuishi na ujenzi wa Nyumba zaidi za Serikali;

- Kuimarika na kuongezeka kwa huduma za Vivuko nchini;

- Usajili wa magari ya Miradi/Serikali kwa namba za Serikali;

- Kuongezeka kwa uwazi na ubora wa kusimamia mikataba na hivyo kupunguza tatizo la rushwa;

- Kuongezeka kwa Ushiriki wa Wanawake na Matumizi ya Nguvukazi katika kazi za barabara;

- Kufanikisha mageuzi ya mifumo ya utendaji katika Wizara kama inavyodhihirika kupitia utendaji mzuri unaoonekana katika Wakala, Mashirika na Taasisi zinazosimamiwa na Wizara ya Ujenzi;

- Kusainiwa kwa Mkataba wa Maelewamo kuhusiana na Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara kati ya Serikali za Tanzania, Msumbiji, Malawi na Zambia;

- Kusainiwa kwa makubaliano kuhusu ujenzi wa daraja la Umoja kati ya Tanzania na Msumbiji, na kuanza kwa utekelezaji wa mradi huu;

- Kuandaa Sera ya Taifa ya Ujenzi iliyoidhinishwa na Serikali mwaka 2003.

**Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka kumi ya Serikali ya Awamu ya Tatu, Wizara ya Ujenzi imeendelea kutekeleza miradi ya ukarabati na ujenzi mpya wa Barabara Kuu katika mfumo wa kanda kuu za usafirishaji *(Trunk Roads Transport Corridors*). Utaratibu huu una lengo la kuhakikisha kwamba barabara zote za kila ukanda zinapitika na kutoa mtiririko wa usafiri wenye uhakika kati ya kanda moja na nyingine na kuiwezesha Tanzania kutumia kwa ukamilifu faida ya Kijiografia iliyonayo katika kuziunganisha nchi kadhaa tunazopakana nazo (*landlocked countries*) na Bandari za Dar es Salaam, Tanga, Mwanza, Kigoma, Bukoba, Itungi, Kasanga, Mbambabay na Mtwara. (*Makofi)***

**Miradi ya ukarabati na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami na madaraja iliyokamilika katika kipindi cha kuanzia Novemba 1995**

Mheshimiwa Spika, kutokana na utekelezaji wa Mpango wa Mabadiliko ya Uendeshaji Kazi Serikalini, Wizara ya Ujenzi tangu mwaka 1995 – 2005 imekuwa mstari wa mbele katika kutekeleza mabadiliko haya. Kutokana na mabadiliko haya Wakala mbili za Serikali, zimeundwa kama ifuatavyo:

• Wakala wa Barabara (*Tanzania National Roads Agency - TANROADS)***:** Wakala wa Barabara ulianzishwa mwaka 2000 kwa Sheria ya Mfuko wa Barabara Na. 2 ya mwaka 1998 na Sheria Na. 30 ya mwaka 1997 ya Wakala za Serikali. Wakala wa Barabara unahusika na kazi za matengenezo na ukarabati wa Barabara Kuu na za Mikoa (*Trunk and Regional Roads*). Tangu kuanzishwa kwake, Wakala umetekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

•Wakala wa Majengo *(Tanzania Buildings Agency (TBA):* Wakala wa Majengo ulianzishwa mwezi Mei mwaka 2002 chini ya Sheria Na. 30 ya mwaka 1997 ya Wakala za Serikali. Lengo la kuanzisha Wakala huu ni kuwezesha kuwa na nyumba bora zaidi za kuishi watumishi wa Serikali wakiwa kazini na baada ya kustaafu kwa kujenga nyumba na kuwakopesha; kujenga majengo ya Serikali kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na kuyatunza; na pia kutoa huduma za ushauri wa kitalaam kuhusiana na majengo. Hadi sasa Wakala umewauzia watumishi wa umma nyumba 7,672. Aidha, Wakala umekamilisha ujenzi wa nyumba mpya 158 maeneo ya Mbweni na Ubungo mkoa wa Dar es Salaam, nyumba 3 mkoa wa Arusha na nyumba 10 mkoa wa Dodoma. Wakala unaendelea na ujenzi wa nyumba mpya kubwa 300 na nyingine ndogo 300 katika Manispaa ya Dodoma, nyumba kubwa 91 na ndogo 91 mkoa wa Dar es Salaam na nyumba kubwa 38 na ndogo 38 katika mikoa mingine 19 ya Tanzania Bara. Wakala pia unaendelea na ujenzi wa nyumba za gharama nafuu 10 (Singida), 10 (Manyara) na 7 (Kagera).

Hivyo Wakala wa Majengo unaendelea na ujenzi wa nyumba 885 baada ya kukamilisha ujenzi wa nyumba 171.

Aidha, Wizara iko katika hatua za mwisho za kuanzisha Wakala wa Ufundi na Umeme *(Tanzania Electrical, Mechanical and Electronics Services Agency (TEMESA)* ambao unatarajiwa kuanza kazi zake rasmi mwaka huu wa 2005. Hatua za kuanzisha Wakala wa Bohari Kuu pia zimeanza.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza Sekta ya Ujenzi, Serikali katika kipindi cha 1995 – 2005 imeunda Bodi mbali mbali ili kusaidia kusimamia, kudhibiti na kuhamasisha shughuli za ujenzi nchini. Bodi zilizoundwa ni:-

- Bodi ya Usajili wa Wahandisi *(Engineers Registration Board*) iliyoanzishwa kwa Sheria Na. 15 ya mwaka 1997.

- Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (*Architects and Quantity Surveyors Registration Board)* iliyoanzishwa kwa Sheria Na. 16 ya mwaka 1997.

- Bodi ya Usajili wa Makandarasi *(Contractors Registration Board*) iliyoanzishwa chini ya Sheria Na. 17 ya mwaka 1997.

- Bodi ya Mfuko wa Barabara *(Roads Fund Board*) iliyoanzishwa chini ya Sheria ya *Roads Tolls (Amendment) No. 2 Act* ya mwaka 1998.

**Aidha, Bodi ya Taifa ya Usimamizi wa Vifaa ambayo imekuwepo tangu kabla ya Serikali ya Awamu ya Tatu, chini ya Sheria Na. 9 ya mwaka 1981, nayo imeendela na utekelezaji wa majukumu yake.**

Mheshimiwa Spika**,** Wizara yangu inasimamia na kuratibu usajili wa Wahandisi, Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi, Wataalamu wa fani ya Ununuzi na Ugavi na Makandarasi ili kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma hizo. Tangu ilipoundwa, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi iliweza kuhakiki orodha ya wataalamu na sifa zao. Katika zoezi hili Bodi iliweza kubaini kwamba kuna wataalamu waliosajiliwa bila kuwa na sifa zinazotakiwa. Baada ya uhakiki huu, Bodi imetengeneza orodha mpya ya wataalam na imeweza kusajili wataalam 291 wenye sifa na makampuni ya ushauri 128. Aidha, Bodi inaendelea na mikakati ya kuwaendeleza wataalamu na makampuni ya ushauri yaliyokosa sifa ili nayo yaweze kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria Na. 16 ya mwaka 1997.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usajili wa Wahandisi na Makandarasi, Bodi ya Usajili wa Wahandisi imeweza kusajili Wahandisi 6,026 wa ndani na wa kigeni na kusajili kampuni za ushauri wa kihandisi 115. Bodi pia imewafutia usajili Wahandisi 221 na kampuni za ushauri wa kihandisi 5 kutokana na makosa mbali mbali. Aidha, Bodi ya Usajili wa Makandarasi imeweza kusajili jumla ya makandarasi 3,730 na imewafutia usajili makandarasi 1,666 kutokana na kushindwa kutimiza masharti ya sheria ikiwa ni pamoja na utendaji mbaya. Bodi pia imeanzisha Mfuko wa Kusaidia Makandarasi ambao hadi sasa una kiasi cha shilingi milioni 891 na una wanachama 335.

Vilevile, katika kipindi cha kuanzia Novemba 1995 hadi sasa, Bodi ya Taifa ya Usimamizi wa Vifaa imeendesha Mitihani ya kitaaluma kwa watahiniwa wapatao 46,046 katika ngazi mbalimbali na kati ya hao watahiniwa 12,682 walifaulu mitihani yao. Bodi pia imeweza kusajili Wataalamu wa fani ya Ununuzi na Ugavi wapatao 1,694.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Miaka Kumi ya Awamu ya Tatu, Wizara ya Ujenzi imeendelea kutengeneza na kukarabati vivuko vyote nchini ili kuviweka katika hali ya kutoa huduma ya kuaminika na salama. Boti mbili za uokoaji zimenunuliwa na zitatumika katika Vivuko vya Magogoni Dar es Salaam na Kigongo – Busisi mkoani Mwanza. Aidha, Serikali imenunua vivuko vipya vya Kilombero na Bugolora – Ukara katika mikoa ya Morogoro na Mwanza. Vivuko hivyo vimepunguza kero kubwa ya usafiri iliyokuwa inawakabili wananchi wa maeneo hayo. Serikali pia imenunua toka *TAMOFA* kivuko cha Kilambo kinachohudumia Tanzania na Msumbiji katika mto Ruvuma eneo la Kilambo mkoani Mtwara. Aidha, taratibu za ununuzi wa kivuko kipya cha Kigongo – Busisi kitakachotumika mkoani Mwanza zimekamilika na kitawasili hapa nchini na kuanza kutumika mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika**,** katika kudhibiti matumizi mabaya ya vyombo vya Umma, Wizara yangu ilianzisha zoezi maalum la kuandikisha magari, pikipiki na mitambo ya Serikali na miradi inayofadhiliwa na Wahisani kwa namba za Umma. Tangu zoezi hili lianze mwaka 2002 jumla ya magari 12,311, pikipiki 5,400 na mitambo 464 vimesajiliwa.

Mheshimiwa Spika, ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2000 iliainisha maeneo kadhaa ambayo Wizara yangu imekuwa ikiyatekeleza katika kipindi cha mwaka 2000 – 2005. Maeneo haya ni yale yanayohusiana na ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara, madaraja na nyumba za Serikali. Wizara yangu imeendelea kuimarisha mtandao wa barabara nchini kwa kuweka mkazo katika ujenzi na ukarabati kwa kiwango cha lami na changarawe wa Barabara Kuu, Barabara za Mikoa na madaraja kwa lengo la kuhakikisha usafiri na usafirishaji wa kuaminika na nafuu nchini.

Aidha, katika kipindi hiki kumekuwa na ongezeko la mtandao unaopata matengenezo mwaka hadi mwaka pamoja na viwango vya ubora wa kazi za matengenezo ya Barabara Kuu na zile za Mikoa. Hali hii inatokana na kuongezeka kwa makusanyo ya Mfuko wa Barabara na kuwepo kwa mfumo mzuri wa usimamizi unaofanywa na Wakala wa Barabara *(TANROADS)* pamoja na Bodi ya Mfuko wa Barabara.

**Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki Wizara yangu imekamilisha miradi ya ukarabati na ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilomita 755.37 katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Miradi ya barabara iliyokamilika kuanzia 2000 – 2005 ni Dar es Salaam – Mlandizi (km. 58.4), barabara ya Kawawa mjini Dar es Salaam (km. 7.5), Wazo Hill-Bagamoyo (km. 43), Njenga-Masaninga (km. 11), barabara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (km. 5.2), barabara ziendazo kwenye hoteli za kitalii katika Pwani ya Jangwani na Kunduchi Mkoani Dar es Salaam (km. 14), Dar es Salaam-Mkuranga (km. 60), barabara ya *KCMC-Mweka* Mkoani Kilimanjaro (km. 9), barabara ya lami kwenye Bonde la Mto Rufiji (km. 13.9), Makuyuni-Ngorongoro (km. 77), barabara za Jiji la Mwanza/Mwanza-Nyanguge/Mwanza mjini-Uwanja wa Ndege (km. 58) na barabara ya *TANZAM* sehemu ya Mlima wa Kitonga (km. 7.64), barabara ya Kyabakari-Butiama (km. 12) na barabara ya *Nyegezi-St. Augustine Campus* (km. 4). Barabara nyingine zilizokamilika ni Halali-Ilembula Mkoani Iringa (km. 5.2), Mutukula-Muhutwe-Kagoma (km 136), Msamvu-Morogoro mjini (km. 2.5), Chalinze-Morogoro-Melela (km. 129), *Monduli Jct-TMA* -Monduli (km. 14), Somanga-Masaninga (km. 33) na barabara ya Kigamboni-Mjimwema (km. 2). Aidha, barabara nyingine ndogondogo zenye urefu wa kilomita 53.37 zimekamilika kujengwa katika mikoa mbalimbali. Pia miradi ya Shelui-Nzega (km. 108) na Songwe-Tunduma (km. 70) iko katika hatua za mwisho kukamilika kujengwa.**

**Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imejenga madaraja katika barabara mbalimbali nchini ili kuimarisha usafiri na uchukuzi kwa njia ya barabara. Ujenzi wa Daraja la Mkapa katika Mto Rufiji umekamilika na daraja hilo lilizinduliwa rasmi na Rais Benjamini William Mkapa mwezi Agosti 2003. Aidha, madaraja 11 katika barabara ya Tanga – Horohoro, madaraja 5 katika barabara ya Tunduma – Sumbawanga, madaraja 7 katika barabara ya *TANZAM,* daraja la Mto Matandu, madaraja ya Mpiji (Pwani), Kyabakoba (Kagera), Ruanda, Sasawala na Ndongosi (Ruvuma) yamekamilika. Aidha, daraja la chuma *(Bailey Bridge)* katika mto Malagarasi nalo limekamilika.**

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia kwa Wakala wa Majengo inasimamia uuzaji na ujenzi wa nyumba mpya za Serikali na watumishi wa umma. Wakala wa Majengo umekwisha wauzia Watumishi wa Umma nyumba 7,672 kuanzia mwaka 2002 hadi sasa. Aidha, Wakala ulikwishakamilisha ujenzi wa nyumba 171 na ujenzi wa nyumba nyingine 885 uko katika hatua mbalimbali katika mikoa yote Tanzania Bara. Kati ya hizo, nyumba 429 ni nyumba kubwa na 456 ni nyumba ndogo.

**Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuhusisha Sekta Binafsi katika ujenzi wa barabara na madaraja. Wizara yangu inaandaa mwongozo wa kuelekeza sekta binafsi jinsi ya kushiriki katika ujenzi wa barabara na madaraja. Aidha, Wizara imeainisha miradi ya barabara na madaraja itakayoweza kutekelezwa na wawekezaji binafsi. Miradi hiyo ni pamoja na Daraja la Kigamboni, Barabara ya Bagamoyo – Saadani – Tanga (km. 204), Barabara ya Mtwara – Masasi – Songea – Mbambay (km. 833) na Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora – Ipole – Mpanda – Kigoma.**

Mheshimiwa Spika, chini ya mradi wa *EAC Road Network Project,* Wizara yangu inaendelea kushirikiana na Nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki *(EAC)* katika kutekeleza miradi ya barabara iliyokubaliwa katika Mkutano wa mwaka 1998 pamoja na miradi mipya ambayo ilikubaliwa iongezwe kwenye mtandao wa miradi ya barabara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Mkutano wa mashauriano kati ya Wahisani na Nchi Wanachama wa Jumuia ya Afrika Mashariki uliofanyika mwezi Aprili, 2003. Mkutano mwingine kati ya nchi zetu za Jumuiya ya Afrika Mashariki na wahisani utafanyika mwaka huu wa 2005 ili kufanya mapitio ya maendeleo ya mradi huu.

Mheshimiwa Spika, Serikali za Tanzania, Msumbiji, Malawi pamoja na Zambia zimetia saini Mkataba wa Maelewano kuhusu Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara mnamo tarehe 15/12/2004. Aidha, Maandalizi ya ujenzi wa Daraja la Umoja yamefikia hatua nzuri ambapo Serikali ya Tanzania na Serikali ya Msumbiji zimetia saini makubaliano kuhusu ujenzi wa daraja hili mnamo tarehe 07/01/2005. Mkataba wa Mshauri wa Usanifu wa awali, kuandaa nyaraka za zabuni za ujenzi na Usimamizi wa kazi za ujenzi ulisainiwa tarehe 02/06/2005 na ujenzi wa daraja unatarajiwa kuanza rasmi katika mwaka huu wa 2005/2006.

Kuhusu Barabara ya Mtwara – Masasi – Songea – *Mbamba Bay,* kazi ya upembuzi yakinifu *(Feasibility Study)* imekamilika. Matokeo yake ni kuwa barabara hii inakidhi vigezo vya kujengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, katika mwaka wa 2005/2006 kazi za usanifu wa kina na maandalizi ya nyaraka za zabuni kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Masasi-Songea-Mbambabay kwa kiwango cha lami zitakamilishwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kufanya majadiliano na wawekezaji wa mradi wa uzalishaji umeme kwa kutumia makaa ya mawe ya Mchuchuma – Katewaka kwa lengo la kuhakikisha kuwa mradi utakapotekelezwa utakuwa na manufaa kwa uchumi wa nchi, hususan sekta ya umeme. Aidha, Serikali imewaelekeza *NDC* na Wizara

ya Nishati na Madini kufanya majadiliano na wawekezaji ili kuharakisha utekelezaji wa mradi huu muhimu.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Mei, 2005 ulifanyika mkutano jijini Dar es Salaam uliojumuisha nchi zinazotekeleza Mkakati wa Maendeleo ya Kikanda *(Spatial Development Initiative).* Nchi zilizowakilishwa ni Msumbiji, Afrika ya Kusini, Zambia, Kenya, Rwanda, Malawi, Namibia, Angola na Tanzania. Kimsingi, mkutano ulisisitiza umuhimu wa kanda za maendeleo. Mkutano huu umesaidia sana kuutangaza Mpango wa Maendeleo na miradi iliyomo katika Ukanda wa Mtwara kwa wawekezaji wa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu katika kipindi cha miaka kumi ya Serikali ya Awamu ya Tatu imefanikisha mambo mengi. Mafanikio haya yote yamepatikana kutokana na uongozi wa pamoja ndani ya Wizara na taasisi zake. Aidha, amani, utulivu wa kisiasa, umoja wa kitaifa na mshikamano uliopo chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni hazina kubwa katika kupatikana kwa mafanikio haya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo kuhusu Dira, Majukumu ya Wizara, Mikakati ya Utekelezaji, Muhtasari wa Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu (1995 – 2005), Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2000 pamoja na Ushirikiano wa Kikanda, naomba sasa nielezee kwa undani zaidi kuhusu utekelezaji wa malengo na majukumu ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka 2004/05, pamoja na mipango ya mwaka 2005/06.

Mheshimiwa Spika**,** katika mwaka huu wa fedha Wizara ilitarajia kukusanya jumla ya shilingi 3,109,483,490.00 kutokana na vianzio vyake mbali mbali. Idara zinazokusanya mapato ni Ufundi na Umeme, Bohari Kuu na Utawala. Hadi kufikia mwezi Mei 2005, jumla ya shilingi 2,633,406,341.00 zilikuwa zimekwisha kusanywa sawa na asilimia 85 ya malengo yaliyowekwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/05, Wizara ya Ujenzi imetengewa jumla ya shilingi 62,099,569,100.00 fedha za hapa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Fedha hizi zinajumuisha fedha za Mfuko wa Barabara shilingi 50,010,100,000.00 na fedha za Mishahara na Matumizi Mengineyo shilingi 12,089,469,100.00.

Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Mei, 2005 jumla ya shilingi 9,876,817,910.00 zilikuwa zimetumika ambazo ni sawa na asilimia 82 ya fedha zote zilizotengwa. Mfuko wa Barabara katika kipindi hiki ulipokea jumla ya shilingi 45,061,096,723.00 ambazo ni sawa na asilimia 90 ya bajeti na kuzigawa kwa watumiaji.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa matengenezo ya Barabara Kuu kwa mwaka 2004/2005 jumla ya kilomita 2,630.1 za lami na kilomita 2,466.0 za changarawe zilipangwa kufanyiwa matengenezo ya kawaida kwa gharama ya shilingi 6,561.105 milioni kutoka Mfuko wa Barabara. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Machi, jumla ya

kilomita 3,543.9 zilifanyiwa matengenezo ya kawaida na jumla ya shilingi 3,514.220 milioni zilitumika kwa kazi hiyo.

Kuhusu matengenezo ya muda maalum (*Periodic Maintenance*), jumla ya kilomita 289.3 zilipangwa kufanyiwa matengenezo kwa gharama ya shilingi 9,793.8 milioni kutoka Mfuko wa Barabara. Hadi mwishoni mwa mwezi Machi 2005, kilomita 212.4 zilikuwa zimefanyiwa matengenezo ya muda maalum kwa gharama ya shilingi 5,475.992 milioni.

Aidha, jumla ya shilingi 1,056.345 milioni kutoka Mfuko wa Barabara zilipangwa kutumika kwa ajili ya kufanya matengenezo ya dharura katika barabara kuu na za mikoa. Mpaka kufikia mwishoni mwa mwezi Machi 2005, kilometa 105.6 na madaraja 16 yalikuwa yamefanyiwa matengenezo kwa gharama ya shilingi 504.807 milioni.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizopangwa ni kufanya matengenezo ya sehemu korofi kilomita 38.4 za barabara kuu kwa gharama ya shilingi 1,041.140 milioni. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Machi 2005, jumla ya kilomita 33.9 zilikuwa zimefanyiwa matengenezo kwa gharama ya shilingi 667.469 milioni kutoka Mfuko wa Barabara.

Pia jumla ya kilometa 78 za barabara kuu zilipangwa kufanyiwa matengenezo yaliyoahirishwa (*Backlog Maintenance)* kwa gharama ya shilingi 142.909 milioni kutoka Mfuko wa Barabara. Hadi mwishoni mwa mwezi Machi 2005, kilomita 19 zilikuwa zimefanyiwa matengenezo kwa gharama ya shilingi 36.682 milioni.

Kwa upande wa madaraja jumla ya shilingi 401.666 milioni kutoka Mfuko wa Barabara zilipangwa kutumika kwa ajili ya kuyafanyia matengenezo ya kawaida (*Preventive Maintenance)* madaraja na makalvati yapatayo 819 katika barabara kuu. Aidha, zaidi ya madaraja 48 yalipangwa kufanyiwa matengenezo makubwa (*major repair*) kwa gharama ya Shilingi 1,483.515 milioni.

Mpaka kufikia mwishoni mwa mwezi Machi 2005, madaraja na makalvati yapatayo 539 yalikuwa yamefanyiwa matengenezo ya kawaida kwa gharama ya shilingi 209.259 milioni. Aidha madaraja yapatayo 46 yalifanyiwa matengenezo makubwa kwa gharama ya shilingi 861.866 milioni.

Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusisha ukarabati na matengenezo ya barabara kuu katika kanda nne za usafirishaji zenye urefu wa kilomita 2,643 zilizoharibiwa na mvua za *El-Nino* mwaka 1997/98. Kazi zinazofanywa kwenye barabara hizo ni pamoja na ukarabati/matengenezo ya madaraja madogo na makalvati, kutengeneza tuta la barabara na kuweka changarawe kwenye sehemu zilizoharibika katika kanda hizo. Urefu halisi unaohusika na ukarabati/matengenezo haya kwenye kanda zote nne ni kilomita 845.

Mradi huu unafadhiliwa kwa pamoja kati ya Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* na Serikali ya Tanzania kwa gharama ya US $ 14.56 sawa na shilingi bilioni 14.56

ambapo *ABD* inatoa shilingi bilioni 13.06 na Serikali ya Tanzania inachangia kiasi cha shilingi bilioni 1.48 kutoka katika Mfuko wa Barabara.

Mgawanyo wa Kandarasi katika mradi huu na hali ya utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:

- Kandarasi Na. 1 ni ya Kanda ya Ziwa (Mikoa ya Mwanza na Mara – km. 128) yenye thamani ya shilingi bilioni 1.7 bila kodi. Mkandarasi wa mradi huu ameshakamilisha barabara ya *Nyamuswa-Ikoma Gate* na Usagara-Katoro kwa kiwango cha changarawe na Nyanguge-Musoma kuziba viraka na kuweka tabaka nyepesi ya lami.

- Kandarasi Na. 2 ni ya Kanda ya Kati-Magharibi (Mikoa ya Tabora, Rukwa na Singida – km. 325) yenye thamani ya shilingi bilioni 2.878. Mkandarasi wa mradi huu anaendelea na matengenezo ya barabara za

- Tabora-Nzega, Tabora-Ipole-Koga, Ipole-Rungwa, Manyoni-Rungwa na Mpanda-Koga kwa kiwango cha changarawe.

- Kandarasi Na. 3 ni ya Kanda ya Kusini (Mikoa ya Iringa, Ruvuma na Mtwara – km. 203) yenye thamani ya shilingi bilioni 1.816 bila kodi. Mkandarasi wa mradi huu amekamilisha matengenezo ya barabara ya Songea-Masasi na Itoni-Manda kwa kiwango cha changarawe na anaendelea na matengenezo ya barabara ya *Songea - Mbamba Bay.*
- **Kandarasi Na. 4 ni ya Kanda ya Magharibi (Mikoa ya Kigoma na Rukwa – km. 189) yenye thamani ya shilingi bilioni 1.566 bila kodi. Mkandarasi wa Mradi huu amekamilisha matengenezo ya barabara za Mwandiga-Manyovu, Mpanda-Uvinza-Kanyani na Sumbawanga-Kasesya kwa kiwango cha changarawe.**

Mheshimiwa Spika, jumla ya kilomita 261.5 za lami na kilomita 6,806.7 za changarawe za barabara za Mikoa zilipangwa kufanyiwa matengenezo ya kawaida kwa gharama ya shilingi 5,247.778 milioni kutoka Mfuko wa Barabara. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Machi, jumla ya kilomita 4,206.6 zilifanyiwa matengenezo na jumla ya shilingi 2,571.500 milioni zilitumika kwa kazi hiyo.

Kwa upande wa matengenezo ya muda maalum jumla ya kilomita 373.7 za barabara za mkoa zilipangwa kufanyiwa matengenezo kwa gharama ya shilingi 8,654.3 milioni kutoka Mfuko wa Barabara. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Machi 2005, kilomita 297.8 zilikuwa zimefanyiwa matengenezo kwa gharama ya shilingi 4,112.779 milioni. Aidha, jumla ya kilomita 157.2 zilipangwa kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo sehemu korofi katika Barabara za Mikoa kwa gharama ya Shilingi 2,742.26 milioni. Hadi mwishoni mwa mwezi Machi 2005, jumla ya kilomita 118.8 zilikuwa zimefanyiwa matengenezo kwa jumla ya shilingi 1,095.372 milioni kutoka Mfuko wa Barabara.

Kuhusu matengenezo ya madaraja, jumla ya shilingi 292.189 milioni kutoka Mfuko wa Barabara zilipangwa kutumika kwa ajili ya kuyafanyia matengenezo ya kawaida *(Preventive Maintenance*) madaraja na makalvati yapatayo 760. Aidha, zaidi ya madaraja 65 yalipangwa kufanyiwa matengenezo makubwa (*major repair*) kwa gharama ya shilingi 1,413.082 milioni. Mpaka kufikia mwishoni mwa mwezi Machi 2005, madaraja na makalvati yapatayo 469 yalikuwa yamefanyiwa matengenezo ya kawaida kwa gharama ya shilingi 292.189 milioni. Pia madaraja yapatayo 58 yalifanyiwa matengenezo makubwa kwa gharama ya shillingi 1,413.083 milioni. Jumla ya kilometa 232.2 za barabara za mikoa zilipangwa kufanyiwa matengenezo yaliyoahirishwa (*Backlog Maintenance*) kwa gharama ya shilingi 146.712 milioni za ndani. Hadi mwishoni mwa mwezi Machi 2005, kilomita 27.2 zilikuwa zimefanyiwa matengenezo kwa gharama ya shilingi 28.720 milioni kutoka Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Spika, Wahisani mbalimbali wanashiriki katika miradi ya matengenezo ya barabara za mikoa kama ifuatavyo:

(a) Mkoa wa Ruvuma: Kazi zilizokuwa zinaendelea katika Barabara za Mkoa kwa mwaka 2004/2005 ni za matengenezo yalioharishwa *(backlog maintenance)* yenye urefu wa kilomita 45 katika barabara ya Mtwara Pachani - Lingusenguse na matengenezo ya kawaida *(routine maintenance*) kwenye barabara ya *Mbamba Bay* - Liuli na barabara ya Lumecha - Kitanda yenye urefu wa kilometa 62.5.

Kazi zinazoendelea katika Barabara Kuu ni pamoja na matengenezo yaliyoahirishwa (kilometa 82.3) kwenye barabara ya Songea – Tunduru na matengenezo ya kawaida yenye urefu wa kilomita 317.8 katika barabara ya Songea – Tunduru na Songea Makambako.

Matengenezo ya barabara yanaendelea pia katika barabara za Mbinga – Ngumbo, Songea – Mitomoni, Kilosa – Chiwindi na Azimio – Lukumbule zenye jumla ya urefu wa kilomita 120.

(b) Mkoa wa Iringa: Kazi zilizokuwa zinazoendelea kwa mwaka 2004/2005 ni pamoja na matengenezo yaliyoahirishwa kilomita 57 kwenye barabara kuu ya Itoni – Ludewa na kilomita 60.5 katika barabara za Mikoa za Njombe-Makete-Kitulo (km 25), Mkiu-Madaba (km 15.5) na Ndulimo-Nkeenja Kitulo-Mfumbi (km 20). Aidha, matengenezo ya kawaida kilometa 15.5 yalikuwa yanaendelea katika barabara ya Mkoa ya Njombe-Makete-Kitulo (km 25).

**Mheshimiwa Spika, *DANIDA* wanafadhili matengenezo yaliyoahirishwa ya Barabara za Mikoa katika mkoa wa Iringa. Mpaka mwishoni mwa mwezi Machi, 2005 kazi katika barabara tatu zenye urefu wa kilometa 119.4 na thamani ya shilingi 1,702.088 milioni zilikuwa zimekamilika na kazi katika barabara tatu zenye urefu wa kilomita 55.9 na thamani ya shilingi 1,693.246 milioni zilikuwa kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji. Barabara zilizokamilika ni Iringa-Pawaga (km. 46), Iringa-Msembe (km. 27.4) na Ihemi-Ihimbo (km. 46). Barabara ambazo utekelezaji ulikuwa unaendelea ni**

Iringa-Pawaga *(package III – km. 22.2),* Iringa –Msembe (package 1a – km. 8.7) na Mbalamaziwa-Kwatwanga (km 25). Kutokana na kasi nzuri ya manunuzi ya kazi za barabara mwaka huu wa fedha, hadi kufikia mwisho wa mwezi Machi 2005, asilimia 81 ya fedha za bajeti ilikuwa imekwisha fanyiwa manunuzi ambayo yana thamani ya shilingi 37,297 milioni. Kazi hizi zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ambapo baadhi zinaendelea na nyingine zimeshakamilika. Ifikapo mwisho wa Juni 2005, manunuzi yote ya kazi yatakuwa yamekamilika kwa fedha iliyobakia kwenye bajeti.

Mheshimiwa Spika**,** katika mwaka wa fedha 2004/2005 Wizara ya Ujenzi ilitengewa jumla ya shilingi milioni 219,130.00 kwa Miradi ya Maendeleo ambapo shilingi milioni 89,606.60 zilikuwa fedha za hapa na shilingi milioni 129,623.40 zilikuwa fedha za kigeni zilizotokana na michango ya wahisani mbalimbali. Kati ya fedha za hapa shilingi milioni 5,087.60 zilikuwa fedha za Mfuko wa Barabara na shilingi milioni 84,519.00 zilikuwa fedha za Maendeleo kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali.

Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Mei 2005, shilingi milioni 84,518.00 sawa na 100% ya fedha zote za Maendeleo kutoka HAZINA na shilingi milioni 4,439 sawa na 87% ya fedha za Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mwaka 2004/2005 zilikwishatolewa

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Idara na Taasisi nyingine zilizo chini ya Wizara kwa mwaka 2004/2005 ni kama ulivyofafanuliwa katika maelezo ya Idara/Taasisi husika katika aya za 41 hadi 87 za hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imepata mafanikio mengi katika utekelezaji kama ilivyofafanuliwa katika taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2004/2005 (aya za 26 -36). Aidha, mafanikio mengine yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:-

(a) Kukamilika na kufunguliwa kwa Barabara na Madaraja yafuatayo:-

- Madaraja 7 katika barabara ya Tanga – Horohoro tarehe 7 Julai , 2004;
- Madaraja 11 katika barabara ya Tunduma – Sumbawanga na madaraja 5 katika barabara ya *TANZAM* tarehe 14/07/2004
- Kuzinduliwa kwa Kivuko cha Ukara tarehe 06/08/2004;
- Barabara za Jiji la Mwanza (km. 58) tarehe 10/11/2004;
- Barabara ya Kagoma-Muhutwe (km. 24) tarehe 11/11/ 2004;

- Barabara ya Mutukula – Muhutwe (km. 112) tarehe 12/11/2004;

- Barabara ya Makuyuni – Ngorongoro (km. 77) tarehe 14/02/2005;

- Barabara ya Somanga – Masaninga (km. 33) na daraja la Mto Matandu tarehe 24/03/2005;

- Barabara ya Chalinze–Melela (km 129) tarehe 02/04/2005;

- Kuzinduliwa kwa Kivuko cha Ilagala tarehe 09/04/2005; na

- Kuzinduliwa kwa boti la uokoaji – Kigamboni Dar es Salaam tarehe 03/06/2005.

Aidha, miradi ifuatayo iko katika hatua za mwisho kufunguliwa rasmi, ama kukamilika.

- Barabara ya Shelui-Nzega (km. 108)

- Barabara ya Kyabakari-Butiama (km. 12);

- Barabara ya Songwe-Tunduma (km. 70);

- Daraja la Mpiji.

(b) Kuweka Mawe ya Msingi/Kusaini Mikataba kwa Ajili ya Ujenzi wa Barabara Zifuatazo:-

- Barabara ya Geita-Buzirayombo-Kyamiorwa (km. 220);

- Barabara ya Tarakea – Rongai - Kamwanga (km. 32);

- Ukarabati wa barabara ya Morogoro-Dodoma (km. 256);

- Ujenzi wa barabara ya Singida-Shelui (km. 110);

- Ununuzi wa Kivuko cha Kigongo-Busisi; na (c) Kuanza/Kukamilisha Maandalizi ya Miradi ya Barabara Zifuatazo:

•Upembuzi Yakinifu/Usanifu wa awali**:** Zabuni za upembuzi yakinifu, usanifu wa awali na *Environmental/Social Impact Assessment* kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami kwa barabara ya Dodoma-Iringa (km. 267) zimeitishwa tarehe 01/06/2005. Aidha, mkataba wa upembuzi yakinifu wa barabara ya Sumbawanga-Kigoma na Kigoma-Nyakanazi (km. 866) umesainiwa Juni, 2005. Pia, mkataba wa upembuzi yakinifu, usanifu wa awali, kuandaa nyaraka za zabuni na usimamizi wa ujenzi wa daraja la Umoja umesainiwa tarehe 02/06/2005.

•Usanifu wa Kina/Nyaraka za Zabuni za Ujenzi: Mikataba ya usanifu kwa kiwango cha lami imesainiwa mwezi Juni 2005 kwa miradi ya Kigoma-Uvinza/Kaliua-Tabora (km. 151); Makutano-*Fort Ikoma (km.* 140) na Bwanga-Biharamulo (km. 69). Mikataba ya usanifu na kuandaa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi/ukarabati kwa kiwango cha lami barabara za Msimba - Mto Ruaha – Ikokoto - Mafinga (km. 167); Tunduma-Sumbawanga (km. 230); Singida-Babati-Minjingu (km. 223); Same-Mkumbara-Korogwe (km. 165); Dodoma-Babati (km. 261) na Tanga-Horohoro (km. 65) inatarajiwa kusainiwa mnamo mwezi Julai, 2005.

Aidha, usanifu na uandaaji wa nyaraka za zabuni umefanywa na kukamilika kwa mradi wa Kagoma-Lusahunga (km. 154) na kufuatiwa na uitishwaji wa zabuni kwa mara ya pili mwezi Machi 2005 baada ya zile zilizoitishwa kwa mara ya kwanza Aprili 2004 kufutwa kutokana na bei zake kuwa ghali sana. Zabuni mpya zimerudishwa tarehe 15/6/2005 na uchambuzi unaendelea ili kuteua mkandarasi wa ujenzi. Usanifu na uandaaji wa nyaraka za zabuni umekamilika pia katika barabara ya Mbeya-Makongolosi (km. 115) ambao utafuatiwa na kuitisha zabuni za ujenzi kwa kiwango cha lami mwaka wa fedha wa 2005/06.Vilevile, baada ya upembuzi yakinifu wa barabara ya Masasi-Songea-Mbambabay (km. 649**)** kukamilika, fedha kwa ajili ya usanifu wa kina na kuandaa nyaraka za zabuni za ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami zimetengwa katika bajeti ya 2005/2006.

(d) Kukamilika kwa maandalizi ya kuanzisha Wakala wa Huduma za Ufundi na Umeme *(TEMESA):*

Maandalizi ya kuanzisha Wakala wa Ufundi na Umeme yako katika hatua za mwisho na unatarajiwa kuanza kazi zake rasmi kuanzia mwaka huu wa 2005.

(e) Kupungua kwa Tatizo la Kuzidisha Uzito wa Magari katika Barabara zetu:

Kutokana na jitihada za kubadili kanuni Na. 114(i)p ya Sheria Na. 30 ya mwaka 1973 ya Usalama Barabarani, pamoja na juhudi za kudhibiti uzidishaji uzito kwa kujenga vituo vipya vya mizani na kununua mizani inayohamishika, pamoja na kuwaelimisha wadau wote wanaohusika na uagizaji na usafirishaji wa mizigo, tatizo la kuzidisha uzito wa magari katika barabara zetu limeendelea kupungua ambapo mpaka sasa magari yanayozidisha uzito ni chini ya 7% ya magari yote yanayopimwa ikilinganishwa na 40% mwaka 2000.

(f) Kuendelea Kujenga na Kuwauzia Nyumba Watumishi wa Umma: Wakala wa Nyumba umekwisha wauzia Watumishi wa Umma nyumba 7,672 kuanzia mwaka 2002 hadi sasa. Aidha, Wakala ulikwishakamilisha ujenzi wa nyumba 171 na ujenzi wa nyumba nyingine 885 uko katika hatua mbalimbali katika mikoa yote Tanzania Bara.

(g) Daraja la Kigamboni: *NSSF* wamekwishamteua Mhandisi Mshauri ambaye anafanya upembuzi yakinifu pamoja na kuandaa mapendekezo *(Proposal*) ya kujenga daraja hili kwa kutumia wawekezaji. Kwa mujibu wa makubaliano kati ya NSSF na Wizara yangu, NSSF watawasilisha Serikalini mapendekezo yao ya mpango wa kujenga daraja hili ifikapo mwishoni mwa mwezi Juni 2005.

(h) Kusainiwa kwa Mikataba ya Maelewano Kuhusu Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara na Daraja la Umoja: Maelezo kuhusu mafanikio yaliyofikiwa ni kama nilivyofafanua katika aya ya 22 ya Hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, wakati wa utekelezaji wa kazi zilizopangwa kwa mwaka 2004/2005 Wizara yangu ilikabiliwa na matatizo/changamoto zifuatazo:

- Taifa kutokuwa na uwezo wa kifedha kulinganisha na mahitaji halisi ya miradi ya maendeleo.

- Uhaba pamoja na uduni wa mitambo ya kuwawezesha makandarasi wazalendo kumudu utekelezaji wa kazi za barabara.

- Ujenzi usio halali katika maeneo ya hifadhi ya barabara (*Road Reserve*). Wananchi wengi wamekuwa wakijenga katika maeneo ya hifadhi ya barabara hivyo kusababisha usumbufu mkubwa wakati wa matengenezo na ujenzi wa barabara kwa ujumla.

- Wizi wa alama na samani zingine za barabarani. Baadhi ya watu wamekuwa waking'oa alama na samani nyingine za barabarani. Ukosefu wa alama na samani hizi kimekuwa ni chanzo na kichocheo kikubwa cha kuwepo kwa ajali nyingi nchini.

- Uwezo mdogo wa baadhi ya makandarasi katika kutekeleza kazi za barabara hivyo kuchelewesha ukamilishwaji wa miradi.

- Baadhi ya wahisani kuwa na urasimu mrefu na kuchelewa kutoa fedha kufuatana na ratiba iliyowekwa hivyo kuchelewesha miradi kuanza ama kuchelewesha malipo kwa makandarasi kwa muda uliokubaliwa katika mikataba.

- Utaratibu mrefu wa kutoa zabuni (hasa kwa miradi ya Wahisani) umekuwa ukichelewesha kuanza kwa utekelezaji wa baadhi ya miradi.

- Uwezo duni wa sekta binafsi katika ujenzi na matengenezo ya barabara.

Mheshimiwa Spika, malengo ya mwaka wa 2005/06 ni kuzifanyia matengenezo Barabara Kuu na Barabara za Mikoa zenye urefu wa kilomita 28,473.5 na madaraja

2,167. Fedha zilizopangwa kutumika ni shilingi milioni 82,457.025 ambapo shilingi milioni 50,077.852 ni za Mfuko wa Barabara, shilingi milioni 4,952 ni kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na shilingi milioni 27,427.173 ni fedha za wahisani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006 Wizara yangu imetengewa jumla ya shilingi 271,067,333,900 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 141,538,833,900 ni fedha za hapa na shilingi 129,528,500,000 ni fedha za kigeni. Aidha wizara imetengewa shilingi 5,564,205,787 fedha za Mfuko wa Barabara kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2005/2006. Kwa hiyo jumla ya fedha za hapa zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2005/06 ni shilingi 147,103,039,687. Mgawanyo wa fedha za ndani kwa mwaka 2005/06 umezingatia sana kuelekeza rasilimali katika miradi inayoendelea hasa Mradi Maalumu wa Ujenzi wa Barabara Kuu.

Mheshimiwa Spika, lengo la mradi huu ni kusimamia shughuli za kudhibiti uzito wa magari yanayotumia barabara zetu, kutafiti vyanzo vya ajali na kuchukua hatua mbalimbali za kupunguza ajali. Taifa limekuwa likipoteza watu wengi na kutumia fedha nyingi kwa ajili ya kutibu majeruhi watokanao na ajali pamoja na kukarabati magari yaliyoharibika kutokana na ajali. Pia uharibifu wa barabara utokanao na uzidishaji uzito, husababisha barabara zetu kuharibika haraka na kwa hiyo kuhitaji fedha zaidi za kuzitunza na kuzikarabati mapema kabla ya muda wake uliokadiriwa wakati wa usanifu. Wizara yangu inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kudhibiti ongezeko la ajali hizi na uzidishaji uzito katika barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, tayari Wizara ya Ujenzi imechukua hatua kadhaa zinazolenga kuwa na mifumo bora ya ukaguzi wa magari, utoaji leseni kwa madereva; ujenzi wa barabara salama; kubadilisha tabia ya watumiaji barabara kwa kuwapa elimu ya usalama barabarani na athari zitokanazo na uzidishaji uzito na kudhibiti uzito wa magari makubwa. Katika mwaka 2004/05, kazi zilizofanyika ni kama ifuatavyo

- Wizara kupitia Kitengo cha Usalama Barabarani iliendelea kuwaelemisha Wananchi juu ya utumiaji salama wa barabara zetu kupitia vyombo mbalimbali vya habari, vipeperushi pamoja na kushiriki Wiki ya Nenda kwa Usalama iliyofanyika Songea, Septemba 2004.

- Wizara imekamilisha ujenzi wa mzani wa Mikese. Aidha, Wizara imeanza maandalizi ya ujenzi wa mizani mingine maeneo ya Mpemba (Tunduma), Nangurukuru na Mingoyo mkoani Lindi.

- Wizara kupitia Wakala wa Barabara imeendelea kutumia mizani iliyopo, isiyohamishika na inayohamishika kudhibiti uzito wa magari katika barabara zetu.

- Wizara iliendesha kozi ya wiki moja kwa Askari wa Usalama Barabarani na Wahandisi juu ya uwekaji wa takwimu za ajali kwenye kompyuta na uchambuzi wake.

- Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya elimu Tanzania, imefanya mapitio ya mitaala ya somo la usalama mashuleni na kufanya marekebisho muhimu. Pia imeandaa miongozo ya kujifunza na kufundisha somo hili shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006 kazi zifuatazo zimepangwa kufanyika:

- Kufanya mapitio ya sheria na kanuni mbalimbali zinazohusu sheria ya barabara na kutoa mapendekezo ya marekebisho yanayolenga kuboresha usalama barabarani na udhibiti wa uzito. Baadhi ya sheria hizo ni sheria za alama za barabarani, udhibiti wa uzidishaji uzito na ukaguzi wa magari.

- Kukamilisha mapitio ya Kanuni za Njia (*Highway Code*), mwongozo wa kujifunza udereva (*Learners' Drivers Manual*) na Mwongozo wa Ukaguzi wa Magari (*Vehicle Inspectors Manual*). Pia Mwongozo wa Alama za Barabarani *(Traffic Device Control Manual)* utakamilishwa.

- Kuendelea kuwaelemisha Wananchi juu ya utumiaji salama wa barabara zetu kupitia vyombo mbalimbali vya habari pamoja na kushiriki Wiki ya Nenda kwa Usalama.

- Kuendelea na ujenzi wa mzani wa kisasa katika eneo la Mpemba (Tunduma) na kukamilisha maandalizi ya kujenga mizani mingine maeneo ya Nangurukuru, Mingoyo mkoani Lindi na mwigine mkoani Dodoma. Mizani hii itajengwa sambamba na ujenzi wa barabara unaoendelea kati ya Nangurukuru – Mingoyo na Dodoma - Manyoni.

- Kuendelea kudhibiti uzito wa magari katika barabara zetu kwa kutumia mizani iliyopo isiyohamishika na inayohamishika.

- Kununua Kompyuta zaidi kwa ajili ya kuweka kumbukumbu za ajali za barabarani.

**Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005 Wizara yangu iliendelea kuratibu matumizi ya nguvu kazi katika kazi za barabara ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo. Hadi kufika mwishoni mwa mwezi Machi, 2005 kazi zifuatazo zilikuwa zimefanyika:**

- **Uzinduzi wa Programu ya *Taking Labour Based Technology (LBT) to Scale* mwezi Oktoba, 2004:**

**Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ilizindua mpango maalum wa kuinua matumizi ya teknolojia ya nguvu kazi nchini ujulikanayo kama *"Taking Labour Based Technology (LBT) to***

***Scale*". Mpango huu utatekelezwa kwa ushirikiano wa Serikali na wadau wengine k.m. mashirika ya wafadhili na sekta binafsi. Mpango huu umeshaanza kutekelezwa na mawasiliano yanaendelea na wadau mbalimbali ili kupata msaada wa uendeshaji ambao ni wa miaka minne.**

- **Kutoa mafunzo ya usimamizi wa kazi za matengenezo ya barabara kwa kutumia teknolojia ya nguvukazi kwa mafundi stadi 60 kutoka Halmashauri mbalimbali.**

- **Kufuatilia utekelezaji wa maazimio yaliyowekwa kwenye mkutano wa kimataifa wa wadau wa teknolojia ya nguvukazi uliofanyika mwezi Oktoba, 2003 mjini Arusha.**

- **Kufanya tathmini ya mahitaji halisi ya mafunzo ya teknolojia ya nguvu kazi kwenye kazi za barabara katika Halmashauri za Wilaya, Manispaa, Miji na Jiji, pia taasisi nyingine zikiwemo sekta binafsi na Wakala wa Barabara.**
- **Kusambaza vitabu vya miongozo na maelekezo ya kitaam matumizi ya teknolojia ya nguvu kazi katika kazi za barabara katika Halmashauri mbali mbali.**

**Mheshimiwa Spika, kazi zilizopagwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2005/2006 ni pamoja na:-**

- **Kuimarisha kitengo cha *Labour Based Technology Unit (LBTU)* ili kiweze kusimamia utekelezaji wa mpango wa *"Taking Labour Based Technology (LBT) to Scale";***

- **Maandalizi ya kuundwa sera ya kitaifa ya matumizi ya teknolojia ya nguvu kazi katika kazi mbalimbali za miundombinu ili kushirikisha wananchi waishio vijijini na mijini katika kazi hizo kama njia mojawapo ya kuwapatia ajira ili kuondoa umaskini;**

- **Kukiendeleza kituo cha utunzaji habari *(Documentation Center*) zihusuzo teknolojia ya nguvukazi ili kiweze kuwa chanzo cha usambazaji habari zihusuzo Teknolojia ya nguvu kazi. Pia kituo hiki kitapatiwa tovuti yake itakayounganishwa na vituo vingine vya maktaba nchini kama *T2 Centre,* na kadhalika.;**

- **Kubadilisha mfumo wa uendeshaji wa chuo cha *ATTI* uwe wa kujitegemea *(Semi – Autonomous*) kwa kuandaa mtaala mpya na kukiandikisha katika Baraza la Taifa la Ufundi *(NACTE)* ili kiweze kutoa mafunzo yanayotambuliwa kitaifa na kimataifa;**

- **Kuimairisha elimu ya matumizi ya teknolojia ya nguvu kazi kwa njia ya utafiti; na**

**• Kuandaa mpango wa mafunzo kwa wadau wa teknolojia ya nguvu kazi ili waweze kuandaa mipango yao na bajeti ya kazi zinazotumia teknolojia ya nguvu kazi ikiwa ni pamoja na kuandaa ripoti na kusimamia kazi hizo kikamilifu.**

**Mheshimiwa Spika, Wizara yangu katika mwaka 2004/05 imetekeleza majukumu yafuatayo:-**

**• Kutayarisha Hadidu za Rejea kwa ajili ya kumpata Mtaalam Mshauri (Consultant) atakayefanya tathmini ya shughuli za ushirikishwaji wanawake katika kazi za ujenzi.**

**• Kuendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo Waratibu wa Mikoa wa Ushirikishwaji wa Wanawake katika kazi za barabara kutoka Mikoa ya Mtwara, Rukwa, Kilimanjaro, Dodoma, Kagera, Iringa, Pwani, Mbeya, Singida na Tabora.**

**• Kufuatilia utekelezaji wa mpango wa ushirikishwaji wa wanawake katika mikoa.**

**• Kuandikisha kampuni tatu za nguvu kazi katika Mkoa wa Kilimanjaro katika daraja la saba zinazomilikiwa na wanawake ambapo kila kampuni ilipata kazi ya kufyeka nyasi kando kando ya barabara na hivyo kutoa ajira kwa wananchi waishio kandokando ya barabara wakiwemo wanawake.**

**• Kuendesha Semina ya uhamasishaji wanawake kushiriki katika kazi za barabara katika Mkoa wa Pwani kwa lengo la kuelimisha taratibu za kushiriki katika kazi pamoja na kuanzisha makampuni.**

**Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/06 kazi zilizopangwa ni pamoja na:-**

**•Kuhamasisha na kuendeleza vikundi vya wanawake vinavyofanya kazi za barabara kufikia ngazi ya kujiandikisha daraja la saba la nguvu kazi au zaidi.**

**• Kufanya semina ya tathmini kwa walimu waliopatiwa mafunzo na mbinu mbalimbali za kuhamasisha wasichana kusoma masomo ya Sayansi.**

**• Kuandaa vielimishaji na makala mbalimbali za kuelimisha jamii, wadau, vikundi mbalimbali katika sekta ya ujenzi kuhusu ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za barabara.**

**• Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mpango wa ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za barabara kwenye Mikoa na miradi mbalimbali ya barabara.**

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi ina majukumu ya kusimamia Sera ya Ununuzi, Utunzaji na Usambazaji wa Vifaa na Upatikanaji wa Huduma na kazi mbalimbali kwa ajili ya shughuli za Serikali. Aidha, Wizara inasimamia taratibu za

ugomboaji na usafirishaji wa shehena za Serikali na shughuli za uendeshaji wa Bohari Kuu ya Serikali.

Majukumu haya yaliyotajwa yanalenga katika kupunguza matumizi ya Serikali kwa kuhakikisha kunakuwepo mfumo thabiti wa utendaji wa kazi za ugavi unaolenga katika matumizi bora ya fedha za umma hasa ikizingatiwa kuwa kati ya asilimia 60 hadi 70 ya matumizi ya Serikali hutumika katika ununuzi wa vifaa, kazi na huduma. Serikali pia hutumia fedha nyingi katika kugomboa shehena zake kutoka nje ya nchi zinazoletwa kupitia bandari, viwanja vya ndege na mipakani.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/05, Wizara yangu imeweza kutekeleza yafuatayo:

- Kuboresha huduma za ununuzi, utunzaji na uuzaji wa vifaa vya Serikali. Wizara imejenga ghala moja katika Mkoa wa Pwani na imeendelea na ukarabati wa maghala na ofisi za Dar Es Salaam na Mikoa ya Mara, Singida, Tanga, Morogoro na Kigoma ili kuweka mazingira mazuri na kuhifadhi kwa usalama vifaa vya Serikali vinavyonunuliwa.

- Kuimarisha huduma za usambazaji wa vifaa vya Serikali kwa kununua magari makubwa mapya mawili ya mizigo na kukarabati magari mengine makubwa ya mizigo yapatayo 11.

- Kuendelea na zoezi la kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa Watumishi wa Ugavi ili wafanye kazi zao kwa ufanisi. Jumla ya watumishi 34 wanaendelea na masomo katika vyuo mbalimbali.

- Kuimarisha shughuli za Wakala wa Ugomboaji na Usafirishaji wa shehena za Serikali.

- Kuongeza usimamizi na ukaguzi wa vifaa na huduma kwa mikoa yote kwa kutembelea na kukagua vituo hivyo.

Mheshimiwa Spika, malengo ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka 2005/2006 ni:-

- Kuhakikisha kwamba taratibu za uanzishaji wa Wakala wa Bohari Kuu ya Serikali zinaendelea.

- Kuendelea na zoezi la kuandaa orodha ya viwango vya vifaa ambavyo vinatumika Serikalini kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali

- Kutoa mafunzo kwa Watumishi wa Ugavi Serikalini kuhusu sheria, kanuni na taratibu kama zilivyoainishwa na Sheria ya Ununuzi ya Umma ya mwaka 2004.

- Kuanzisha Bohari ya Mkoa wa Manyara kwa kuanza ujenzi wa maghala na ofisi.

- Kuhakikisha kwamba Watumishi wa Ugavi Serikalini wanaendelea kupewa mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika taaluma yao ili wafanye kazi zao kwa upeo mkubwa na ufanisi.

- Kuimarisha shughuli za Kitengo cha Wakala wa Ugomboaji na Usafirishaji wa Shehena za Serikali kwa kukiongezea vitendea kazi ili kiweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa gharama nafuu.

- Kuongeza vitendea kazi ikiwa ni pamoja na kununua magari ya kusambaza vifaa mikoani.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Ufundi na Umeme inashughulika na kazi za kutathmini, kusajili, kukodisha na kufanya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo ya Serikali; uendeshaji wa Vivuko, uendeshaji wa mitambo ya kokoto; ushauri na usimamizi wa miradi ya umeme, usimikaji na matengenezo ya mitambo ya umeme na mabarafu pamoja na matengenezo ya vifaa vya Elektroniki.

**Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/05 utekelezaji wa malengo ulikuwa kama ifuatavyo:**

- **Kukamilisha ukarabati wa Kivuko cha Kyanyabasa Mkoani Kagera.**
- **Kukamilisha ukarabati wa kivuko kilichokuwa kinamilikiwa na Kampuni ya Mafuta ya *TPDC (ex-TPDC)* na kukihamisha kutoka Rufiji kwenda Kigoma (Ilagala).**

- **Kukamilika kwa ununuzi wa Boti 2 za uokoaji (*Rescue Boats)* kwa ajili ya Kivuko cha Kigamboni na Kigongo-Busisi, Mwanza. Boti ya Kivuko cha Kigamboni ilizinduliwa tarehe 03/06/2005.**

- **Kukamilika kwa maandalizi ya ununuzi wa Kivuko kipya cha Kigongo-Busisi ambapo mkandarasi ameshapatikana na mkataba ulisainiwa mwezi Aprili, 2005. Baada ya muda wa miezi 14 tangu kusainiwa kwa mkataba kivuko kitakuwa tayari kutumika.**

- **Ununuzi wa vifaa vya kujiokolea majini *(Life Saving Equipment)* kama *life jackets* za watu wazima 335 na za watoto 345 ili kuhakikisha usalama wa watumiaji wa vivuko nchini.**

- **Kukamilika kwa ununuzi na ufungaji wa mashine za kukatia tiketi (*Ticket Vending Machines)* katika Kivuko cha Magogoni ili kurahisisha ukataji wa Tikiti na kusaidia kudhibiti mapato ya Serikali.**

- **Kukamilika kwa ununuzi wa Kivuko cha Kilambo kilichokuwa kinamilikiwa na *TAMOFA*.**

- **Kusajili magari 1,641, pikipiki 147 na mtambo 1 na hivyo kufanya jumla ya vifaa vyote vilivyosajiliwa kwa mwaka 2004/2005 kufikia 1,789. Aidha, tangu zoezi hili la kusajili magari, pikipiki, na mitambo kwa namba za umma lianze mwaka 2002, jumla ya magari 12,311, pikipiki 5,400 na mitambo 464 imesajiliwa kwa namba za umma na kufanya jumla ya vifaa vyote vilivyosajiliwa hadi sasa kuwa 18,175.**

**Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006 kazi za kiutendaji za Idara ya Ufundi na Umeme zitafanywa na Wakala wa Serikali utakaojulikana kama *TEMESA (Tanzania Electrical, Mechanical and Electronics Services Agency). TEMESA* inaundwa chini ya Sheria ya Wakala *(Executive Agencies Act No. 30)* ya mwaka 1997. Idara ya Ufundi na Umeme sasa itakuwa inashughulika na uandaaji wa Sera, kuweka viwango vya ubora wa kazi za ufundi na umeme na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wakala *(TEMESA)*.**

**Katika mwaka wa fedha wa 2005/2006 Idara hii inalenga kutekeleza yafuatayo:**

- **Kuratibu uanzishwaji wa Wakala wa Ufundi na Umeme *(TEMESA)*.**

- **Kusajili magari 1,750, pikipiki 1,300 na mitambo 150.**

- **Kutathmini magari yapatayo 1,668 na pikipiki zipatazo 1,080 kwa matumizi mbalimbali ya Serikali.**

- **Kukamilisha upatikanaji wa Kivuko cha Kigongo-Busisi mkoani Mwanza.**

- **Ununuzi wa Kivuko kipya cha Ruhuhu chenye uwezo wa tani 50. Kivuko hiki kitakuwa kiungo cha wilaya mbili za Ludewa mkoani Iringa na Mbinga mkoani Ruvuma.**

- **Kusimamia mradi wa ukarabati wa vivuko vitano vya *Mv. Kigamboni (DSM), Mv. Rufiji (Pwani), Mv. Kilombero (Morogoro), Mv. Pangani (Tanga) na Mv. Sengerema (Mwanza).***

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Barabara *(TANROADS)* ilianzishwa rasmi tarehe 1 Julai, 2000 kwa mujibu wa Sheria ya Wakala za Serikali (*Executive Agencies Act No. 30 of 1997*) na Sheria ya Mfuko wa Barabara – *Road Tolls (Amendment) No. 2 Act*, 1998.

*TANROADS* imechukua jukumu la ukarabati na matengenezo ya Barabara Kuu na za Mikoa zenye jumla ya kilomita 35,000 kazi zilizokuwa zikifanywa moja kwa moja na Wizara ya Ujenzi. Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa kazi hizi kwa kipindi cha

2004/2005 yametolewa katika aya za 29 - 34 za hotuba hii. Aidha, mpango wa matengenezo ya barabara 2005/2006 ambao utatekelezwa na *TANROADS* umefafanuliwa katika aya ya 39.

Mheshimiwa Spika, katika miaka mitano ya utendaji wake, *TANROADS* imeweza kuweka mifumo ya kisasa ya Menejimenti na Mawasiliano katika ngazi zote za Makao Makuu na Mikoa ili kuweza kukabili majukumu yake katika karne hii ya Sayansi na Teknolojia. Matokeo ya juhudi hizo yanadhihirishwa na kuboreka kwa hali ya barabara na nidhamu katika matumizi ya fedha. Aidha, Wakala umeongeza kasi ya kutumia Wakandarasi na kupunguza kutumia mfumo wa kufanya kazi kwa kutumia vikosi vyake *(Force Accounts).*

Katika kupunguza muda wa manunuzi na kusimamia mikataba kwa ufanisi, Wakala wa Barabara umerekebisha mfumo wa kutoa mikataba ambapo mikataba ya kati ya miezi 3 hadi mwaka 1 imeanza kutolewa. Kwa kuwa kazi za matengenezo zinafanywa na Makandarasi Wazalendo kwa zaidi ya asilimia 90, manufaa kadhaa yamepatikana katika uchumi ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha wananchi kwa asilimia kubwa katika kufanya matengenezo ambapo fedha inayopatikana inawanufaisha wananchi wengi wanaojihusisha na kazi za barabara. Hii inapunguza kasi ya umaskini na kutoa ajira kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kupitia *TANROADS* inaendelea kusimamia kwa makini masuala yafuatayo:

- Utunzaji wa Alama na Samani za Barabara:Wizara inaendelea kuwaelimisha wenye magari kuwa waangalifu ili wasizigonge alama za barabarani. Aidha, wananchi wanaendelea kuelimishwa juu ya kulinda na kutunza alama za barabarani ili kuepusha ajali za mara kwa mara zinazosababishwa na ukosefu wa alama za barabarani.

- Usalama Barabarani:Wizara inalo jukumu kubwa la kuwaelimisha madereva na wenye magari kuwa mwendo wa kasi ni kichocheo kikubwa cha ajali. Pamoja na kuhakikisha kunakuwepo na alama za tahadhari barabarani, ukaguzi wa mwendo wa magari na ubora wa magari vinatakiwa kufanyika mara kwa mara.

- Udhibiti wa Uzito wa Magari:Ili kuhakikisha kuwa barabara zetu zinaendelea kudumu kwa muda mrefu, Wizara yangu itaendelea kuboresha shughuli ya upimaji wa uzito wa magari kwa kununua mizani mpya na kujenga vituo vipya vya mizani katika

barabara zetu zinazokamilika kujengwa na kuwaelimisha wasafirishaji na wadau wengine ili kuhakikisha magari yanazingatia sheria na taratibu zilizowekwa.

- Hifadhi ya barabara *(Road Reserve):* Wizara yangu inaendelea kusimamia kwa makini Sheria ya Hifadhi ya Barabara Na. 167 ya mwaka 1967. Katika Sheria hii, eneo la hifadhi ya barabara limebainishwa kuwa katika Barabara zote Kuu na Barabara za Mikoa ni futi 75 (Mita 22.86) kila upande kutoka katikati ya barabara; Barabara za Wilaya eneo la hifadhi ya barabara ni futi 33 (Mita 10.058) kila upande kutoka katikati ya barabara. Aidha, katika barabara ya Dar es Salaam – Morogoro, eneo la hifadhi ya barabara limeainishwa kama ifuatavyo:-

*(i) United Nations Road hadi Maili 6.22 (km. 9.95) – Futi 75 (Mita 22.86).*

*(ii) Maili 6.22 (km. 9.95) hadi Maili 10.02 (km. 16.03) – Futi 300 (Mita 91.44).*

*(iii) Maili 10.02 (km. 16.03) hadi Maili 23.12 (km. 39.99) – Futi 400 (Mita 121.92).*

*(iv) Maili 23.12 (km. 39.99) hadi Maili 43.12 (km. 68.99) - Futi 75 (Mita 22.86).*

*(v) Maili 43.12 (km. 68.99) hadi Maili 44.12 (km. 70.59) (Daraja la Ruvu) – Futi 300 (Mita 91.44).*

*(vi) Sehemu iliyobaki hadi Morogoro – Futi 75 (Mita 22.86).*

Katika kipindi cha mwaka 2004/05, Wizara imekuwa ikiendesha zoezi la kuhakikisha kuwa eneo la hifadhi ya barabara linaangaliwa na kulindwa kwa kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kuheshimu maeneo ya hifadhi ya barabara kupitia vyombo mbali mbali vya habari vikiwemo Magazeti, Radio na Televisheni**.**

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Majengo, (*Tanzania Buildings Agency – TBA)* ulianzishwa mwezi Mei mwaka 2002 kwa mujibu wa Sheria Namba 30 ya mwaka 1997 kwa madhumuni ya kutunza nyumba na majengo ya Serikali, kutekeleza utaratibu wa kujenga na kuwauzia Watumishi wa Serikali nyumba za kuishi kutokana na fedha zinazolipwa na Watumishi waliouziwa nyumba, kutoa huduma za ushauri (*Consultancy Services*) wa ujenzi wa nyumba na majengo na kuhakikisha kuwa majengo ya Serikali yanajengwa na kutunzwa kwa kuzingatia viwango (*Standards*) vilivyokubalika.

Katika mwaka 2004/2005, Wakala ulipanga kufanya kazi zifuatazo:-

- Kuzifanyia ukarabati nyumba za Serikali 59 na kufanya matengenezo ya kawaida kwenye nyumba 188 katika mikoa yote ya Tanzania Bara.

- Ukusanyaji wa Mapato kutokana na nyumba zilizouzwa kwa watumishi wa Umma shilingi 8,617 milioni.

- Kujenga nyumba 129 za daraja la ‘A’. Nyumba 91 (zinazojumuisha nyumba kubwa 91 na nyumba ndogo 91) zitajengwa Dar es Salaam na nyumba 38 (zinazojumuisha nyumba kubwa 38 na nyumba ndogo 38) zitajengwa mikoani.

- Kujenga nyumba 10 za gharama nafuu Mkoani Singida.

- Kukamilisha ujenzi wa nyumba kubwa 300 na ndogo 300 Dodoma.

- Kukamilisha ujenzi wa nyumba 10 Mkoani Manyara.

- Ujenzi wa Makao Makuu ya Wakala katika Mtaa wa Sokoine.

- Utafutaji wa viwanja kwa ajili ya ujenzi wa nyumba.

Hadi Mei, 2005, utekelezaji ulikuwa kama ifuatavyo:

- Nyumba za Serikali 43 zilifanyiwa ukarabati na nyumba 132 zilifanyiwa matengenezo ya kawaida katika mikoa yote ya Tanzania Bara.

- Ukusanyaji wa mapato kutokana na nyumba zilizouzwa kwa watumishi wa Umma ulifikia shilingi 6,899 milioni ambayo ni sawa na asilimia 80 ya lengo la mwaka.
- Ujenzi wa nyumba 91 (nyumba kubwa 91 na nyumba ndogo 91) za daraja la ‘A’ ulianza Dar es Salaam. Aidha, ujenzi wa nyumba 38 (nyumba kubwa 38 na nyumba ndogo 38) ulianza mikoani. Mradi huu unaendelea vizuri na nyumba zote zitakamilika mwaka huu wa 2005.

- Ujenzi wa nyumba 10 za gharama nafuu Mkoani Singida, 10 katika mkoa wa Manyara na nyumba 7 katika Mkoa wa Kagera unaendelea vizuri. Ujenzi utakamilika mwaka huu wa 2005.

- Ujenzi wa nyumba kubwa 300 na ndogo 300 Mkoani Dodoma unaendelea ambapo nyumba zote zimekwishaezekwa. Ujenzi utakamilika mwaka huu wa 2005.

- Ujenzi wa Makao Makuu ya Wakala katika Mtaa wa Sokoine umekamilika na kinachoendelea sasa ni uwekaji wa samani ili ofisi zianze kutumika.

- TBA imeweza kupata jumla ya viwanja 171 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/06 Wakala umepanga kutekeleza yafuatayo:

- Kukusanya jumla ya shilingi 11,426 milioni kutokana na uuzaji wa nyumba kwa watumishi wa Umma.

- Ujenzi wa majengo 3 ya ghorofa hapa Dar es Salaam.

- Ujenzi wa nyumba 226 mikoani.

- Kukamilisha miradi inayoendelea ya ujenzi wa nyumba kubwa 300 na nyumba ndogo 300 Dodoma, nyumba 10 za gharama nafuu Mkoani Manyara, 10 Mkoani Singida na nyumba 7 Mkoani Kagera. Aidha, ujenzi wa nyumba kubwa 38 na nyumba ndogo 38 mikoani, ujenzi wa nyumba kubwa 91 na nyumba ndogo 91 Dar es Salaam pamoja na uwekaji samani wa makao Makuu ya Wakala vitakamilishwa.
- Ujenzi wa nyumba 100 za watumishi katika Mikoa yote Tanzania Bara kwa gharama ya shilingi 2,628,000,000.

- Kuendelea na matengenezo ya kawaida ya nyumba za Serikali 80 kwa gharama ya shilingi 119,948,030.00 pamoja na kuzifanyia ukarabati nyumba 39 kwa shilingi 500,577,678.

- Kufanya upembuzi yakinifu wa miradi mitatu kwa ajili ya kuingia ubia.

- Ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya Wakala katika mji wa Babati Mkoani wa Manyara.

- Kuhifadhi jengo moja la kihistoria Mkoani Lindi.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mfuko wa Barabara ilianzishwa chini ya Sheria ya *Roads Tolls (Amendment) No. 2 Act, 1998.* Kuanzishwa huko kulikuwa ni sehemu ya marekebisho yanayoendelea katika sekta ya barabara. Marekebisho hayo yalibuniwa kwa madhumuni ya kuimarisha upatikanaji na matumizi mazuri ya fedha za matengenezo na ukarabati wa Barabara Kuu, Barabara za Mikoa na barabara zinazosimamiwa na Serikali za Mitaa. Vyanzo vya mapato ya Mfuko wa Barabara ni pamoja na ushuru wa barabara unaotozwa katika petroli na dizeli, ushuru wa magari ya kigeni mipakani, ada za leseni za magari mazito na faini ya magari yaliyozidisha uzito.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mfuko wa Barabara ilizinduliwa rasmi mwezi Agosti, 1999 na kupewa pamoja na mambo mengine majukumu makuu yafuatayo:

- Kumshauri Waziri wa Ujenzi kuhusu vyanzo vipya vya mapato kwa ajili ya Mfuko na kurekebisha taratibu za kukusanya tozo za barabara kwa nia ya kuhakikisha kwamba zinapatikana fedha za kutosha kwa muda unaofaa kwa ajili ya matengenezo ya barabara.

- Kumshauri Waziri wa Ujenzi kuhusu taratibu za mgawanyo wa fedha za mfuko kwa watumiaji mbalimbali.

- Kuhakikisha tozo za barabara zinakusanywa kikamilifu na kuwekwa kwenye akaunti ya Mfuko.
- Kugawa fedha za Mfuko kwa taasisi zinazoshughulikia matengenezo ya barabara na kufuatilia matumizi yake kuona kama zinatumika kwa mujibu wa sheria iliyoanzisha Mfuko.

Mafanikio ya Bodi tangu kuanzishwa ni kama ifuatavyo:

- Kumekuwa na ongezeko la makusanyo ya mapato ya Mfuko wa Barabara. Makusanyo yameongezeka kutoka Shs. 47.252 bilioni mwaka 2000/01 hadi kufikia Shs. 67.342 bilioni mwaka 2003/04. Katika mwaka wa fedha wa 2004/05 makusanyo ya Mfuko wa Barabara yanatarajiwa kuwa Shs. 73.414 bilioni. Jedwali lifuatalo hapa chini linaonyesha mafanikio hayo:

**MAKUSANYO YA MAPATO MWAKA 2000/2001 – 2004/2005**

| Mwaka wa Fedha | Makadirio yao Makusanyo | Makusanyo Halisi |
|---|---|---|
| 2000/2001 | 41,396,000,000 | 47,252,000,000 |
| 2001/2002 | 50,788,000,000 | 52,881,000,000 |
| 2002/2003 | 64,684,000,000 | 59,390,000,000 |
| 2003/2004 | 64,510,000,000 | 67,342,000,000 |
| 2004/2005 | 73,414,000,000 | 67,538,725,585* |

* *Haya ni makusanyo hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Mei, 2005.*

Makusanyo ya fedha katika kipindi hiki yaligawanywa kwa Taasisi za Utekelezaji kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo:-

*TANROADS:* 2000/2001 - 25,632; 2001/2002 - 31,390; 2002/2003 - 41,648; 2003/2004 - 40,206; 2004/2005 - 39,948.

TAMISEMI: 2000/2001 - 10,847; 2001/2002 - 15,240; 2003/2004 - 19,302; 2003/2004 - 19,146; 2004/2005 - 19,023.

UJENZI: 2000/2001 - 2,928; 2001/2002 - 3,488; 2002/2003 - 4,449; 2003/2004 - 4,467; 2004/2005 - 4,439.

BODI YA MFUKO WA BARABARA 2000/2001 - 624; 2001/2002 - 620; 2002/2003 - 674; 2003/2004 - 691; 2004/2005 - 640.
JUMLA: 2000/2001 - 40,031; 2001/2002 - 50,738; 2002/2003 - 66,073; 2003/2004 - 64,510; 2004/2005 - 64,050.*

*** Mgawanyo wa fedha hizi ni hadi kufikia mwezi Mei, 2005.*

- Hali kadhalika, kutokana na utaratibu wa kuingia mikataba ya utendaji kazi (*Performance Agreements*) kati ya Bodi ya Mfuko wa Barabara na Wizara/Taasisi za Utekelezaji, ni dhahiri kuwa sasa fedha zinaelekezwa katika kazi za barabara zilizopangwa na hivyo kuimarisha udhibiti wa matumizi ya fedha za Mfuko.

- Bodi imeandaa taratibu za ukaguzi wa matumizi ya fedha za Mfuko kwa kutembelea kazi za matengenezo ya barabara, na kwa kushirikiana na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, Bodi imekuwa ikiendesha ukaguzi wa vitabu vya fedha na ubora wa kazi ili kuhakikisha kwamba fedha zinatumika vizuri.

- Bodi imeandaa mapendekezo ya kuongeza vyanzo vya mapato ya Mfuko wa Barabara kwa lengo la kuongeza fedha za matengenezo ya barabara nchini. Mapendekezo haya yanaendelea kufanyiwa kazi na Serikali.

- Bodi imechapisha Majarida yanayotoa miongozo juu ya matumizi ya fedha za Mfuko na kugawiwa kwa wadau mbalimbali.

- Bodi ilifanya utafiti wa kupanua wigo wa Mfuko wa Barabara kwa ajili ya matumizi endelevu ya barabara. Mapendekezo ya utafiti huu yatafanyiwa kazi ili yaweze kuimarisha mapato ya Mfuko wa Barabara kwa lengo la kukidhi mahitaji makubwa ya fedha za matengenezo ya barabara nchini.

Mheshimiwa Spika, uzoefu wa Wizara ya Ujenzi katika kipindi hiki kifupi umeonyesha kuwa Sera ya kuanzisha Mfuko Maalum kwa ajili ya maendeleo ya barabara ni sahihi na uthibitisho wa hili ni hali ya barabara zetu kuendelea kuboreka mwaka hadi mwaka. Kazi kubwa ambayo imefanyika katika matengenezo ya barabara imetokana na upatikanaji wa fedha kutoka mfuko huo ambao hautegemei fedha kutoka kwa wafadhili.

Katika mwaka 2005/2006, Bodi ya Mfuko wa Barabara inatarajia kukusanya jumla ya shilingi 80,413 milioni. Kati ya fedha hizi shilingi 76,487 milioni zitatokana na tozo ya mafuta, shilingi 2, 136 milioni zitatokana na faini za kuzidisha uzito, shilingi 1,600 milioni zitatokana na tozo ya magari ya kigeni mipakani na shilingi 190 milioni zitatokana na ada za leseni za magari makubwa.

**Bodi inatarajia kugawa fedha hizi (shilingi 80,413 milioni), kwa *TANROADS* shilingi 50,078 milioni, TAMISEMI shilingi 23,847 milioni, Wizara ya Ujenzi shilingi 5,564 milioni na Bodi ya Mfuko wa Barabara shilingi 924 milioni.**

Mheshimiwa Spika, bodi ya Usajili wa Wahandisi ilianzishwa na Serikali kwa Sheria ya Bunge Na. 15 ya mwaka 1997 na imepewa majukumu ya kusimamia mienendo na shughuli za kihandisi zinazofanywa na wahandisi pamoja na kampuni za ushauri wa kihandisi nchini. Chini ya Sheria hii ni kosa kwa mtu au kampuni yoyote kufanya kazi za kihandisi bila kusajiliwa. Vile vile ni kosa kutumia huduma za kihandisi kutoka kwa mtu au kampuni isiyosajiliwa na Bodi.

Katika kutekeleza majukumu yake, Bodi inafanya kazi ya kusajili wahandisi wa kada na fani zote, kuratibu mienendo na shughuli za kihandisi, kuwaendeleza wahandisi kitaaluma ikiwa ni pamoja na kusimamia programu ya mafunzo ya vitendo kwa wahandisi wahitimu, kujenga uwezo wa wahandisi na kampuni za ushauri wa kihandisi na kuandaa warsha, kongamano na mashauriano yanayohusu shughuli za kihandisi.

**Jukumu kubwa la Bodi ni kulinda maslahi ya Taifa na watumiaji wa huduma za kihandisi kwa kuhakikisha kuwa shughuli zote za kihandisi zinafanywa na wahandisi wenye sifa za utaalamu, uwezo na uzoefu vilivyothibitishwa kwa kusajiliwa na Bodi; au makampuni ya ushauri wa kihandisi yenye utaalamu, uwezo na uzoefu vilivyothibitishwa kwa kusajiliwa na Bodi.**

**Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Mei 2005 Bodi imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:**

- **Kusajili Wahandisi 509 hivyo kufanya idadi ya Wahandisi wote waliosajiliwa tangu Bodi ianzishwe kufikia 6,026.**

- **Kusajili kampuni za Ushauri 15 hivyo kufanya idadi ya makampuni ya ushauri yaliyosajiliwa kufikia 115.**
- **Kukamilisha maandalizi ya utekelezaji wa utaratibu wa mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma kwa wahandisi wote ili kuwafanya wahandisi kwenda sambamba na mabadiliko ya kisayansi na kiteknolojia na hivyo kuwafanya wahandisi waendelee kufanya shughuli zao za kihandisi kwa ufanisi, na kumudu ushindani unaoletwa na utandawazi.**

- **Kutembelea mikoa 10 na kukagua shughuli za kihandisi pamoja na maendeleo ya wahandisi wahitimu wanaofanya mafunzo ya vitendo.**

- **Kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo ya vitendo kwa wahandisi wahitimu. Bodi ilisimamia mafunzo ya wahandisi wahitimu 275. Kati ya wahandisi hao 54 wametoka Halmashauri za Serikali ya Mitaa 23 wametoka Wizara nyingine na taasisi mbalimbali za Serikali.**

- **Kusherehekea Siku ya Wahandisi 2005 *(Annual Engineers' Day, 2005)* ambayo madhumuni yake, pamoja na mambo mengine, ni kuwatambua wahandisi na makampuni ya kihandisi waliotoa michango mikubwa katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini. Utaratibu huu unalenga kuwahamasisha wahandisi kuwa wabunifu daima na hivyo kuharakisha maendeleo ya taifa. Bodi ilitumia muda huo pia kufanya majadiliano ya kitaaluma ambayo mada yake kuu ilikuwa "Dira ya Maendeleo 2025: Michango ya Wahandisi katika Kupunguza Umaskini". siku ya kilele cha sherehe ya Siku ya Wahandisi 2005, jumla ya wahandisi 18 walitambuliwa kutokana na michango yao mbalimbali ya kihandisi.**

- **Kutembelea Mradi Maalum wa ujenzi wa barabara itakayounganisha mikoa ya Ziwa na ile ya Kusini ili kuhakikisha kuwa wahandisi wa kigeni walioajiriwa katika mradi huu wamesajiliwa na Bodi.**

- **Kuandaa majadiliano ya kitaaluma yaliyowakutanisha wahandisi washauri nchini ambayo mada yake kuu ilikuwa Michango ya Wahandisi wa Tanzania katika Uzalishaji Mali.**
- **Kuandaa mitihani ya kitaaluma pamoja na masomo ya wiki 10 kwa ajili ya maandalizi ya mitihani hiyo.**

- **Kuendesha mihadhara ya kitaaluma mitatu na warsha tatu kwa wahandisi wataalamu wanaosimamia mafunzo ya vitendo kwa wahandisi wahitimu.**

- **Kuchapisha majarida mawili ya *ERB Engineers Newsbrief.***

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006 Bodi imepanga kufanya yafuatayo:

- Kusajili Wahandisi 620 na kampuni za Ushauri wa kihandisi 20.

- Kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo ya vitendo kwa wahandisi wahitimu 405. Idadi hii ni pamoja na wahandisi wahitimu 275 wanaoendelea na mafunzo.

- Kuendelea kufanya ukaguzi wa shughuli za kihandisi nchini ili hatimaye shughuli zote za kihandisi ziwe zinafanywa na wahandisi waliosajiliwa kwa kufuata maadili ya utendaji kazi za kihandisi katika mikoa yote nchini.

- Kuendelea kuwashawishi wahandisi wataalamu ili waanzishe kampuni za ushauri wa kihandisi mikoani na hivyo kusogeza huduma hii muhimu karibu na watumiaji.

- Kuandaa mitihani ya kitaaluma pamoja na masomo ya maandalizi kwa mitihani hiyo.

- Kuandaa kozi fupi fupi tatu na mihadhara ya kitaaluma sita.

- Kuandaa sherehe ya Siku ya Wahandisi 2006.

- Kutembelea wahandisi wote walio katika mafunzo ya vitendo ili kukagua maendeleo yao.

- Kusimamia mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma kwa wahandisi wote.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Taifa ya Usimamizi wa Vifaa ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 9 ya mwaka 1981 kwa lengo la kukuza na kuendeleza taaluma ya Ugavi. Majukumu ya Bodi ni kama ifuatavyo:-

- Kukuza, kusimamia na kuratibu mafunzo na Elimu inayohusu fani ya Ununuzi na Ugavi.

- Kuendesha mitihani na kutunuku vyeti, Stashada na Shahada katika fani ya Ununuzi na Ugavi.

- Kutoa na kusimamia mwongozo na utendaji kazi wa taaluma ya Ununuzi na Ugavi.

- Kutoa, kuhamasisha, kuendeleza, kuratibu na kuboresha mfumo wa taratibu za Ununuzi na Ugavi.

- Kusimamia na kuongoza shughuli za semina, mikutano na kongamano kuhusiana na fani ya Ununuzi na Ugavi.

- Kusajili na kusimamia mienendo ya wana Taaluma wa Ununuzi na Ugavi ili wafuate maadili ya taaluma.

- Kutoa na kusimamia mihutasari ya mafunzo ya taaluma.

- Kuchapisha majarida yanayohusu shughuli za Bodi na za taaluma kwa ujumla.

- Kuratibu ubora wa mafunzo ya Ununuzi na Ugavi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/05 Bodi imetekeleza yafuatayo:

- Usajili wa wataalamu: Bodi ilisajili wataalamu 85 na kufanya idadi ya wanataaluma waliosajiliwa hadi sasa kufikia 1,694 katika ngazi mbalimbali.

- Mitihani ya Taaluma: Bodi imetahini jumla ya wataalamu 1,924 na kati ya hao 656 sawa na asilimia 34 wamefaulu. Toka Bodi ianze mwaka 1982 imetahini watahiniwa 46,046 na kati yao watahiniwa 12,682 sawa na 27.5% wamefaulu. Idadi hii inajumuisha pia watahiniwa kutoka Zanzibar na Pemba.

- Mafunzo endelevu: Bodi imetoa mafunzo endelevu *(Continued Professional Development)* kwa njia ya warsha, semina na Kongamano. Jumla ya semina na warsha 15 ziliendeshwa zikihusu Sheria mpya za ununuzi, ugavi, utunzaji bora wa vifaa na kadhalika. Washiriki walikuwa watendaji wa ngazi mbalimbali kwenye Serikali Kuu, Wilaya, Miji, Manispaa, Taasisi za Umma na binafsi.

- Bodi pia iliendesha kongamano la kitaaluma la mwaka na semina nne (4) ndani ya Wizara na Asasi za Serikali zilizohusu *Public Procurement.* Aidha Bodi iliendesha Semina kwa Kamati ya Miundo mbinu ya Bunge kuhusu NBMM na sheria Na.9 ya mwaka 1981, chimbuko la fani ya Ugavi na Sheria za Ununuzi na Ugavi.

- Ushauri wa Kitaalamu: Bodi imendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kwenye fani ya Ununuzi na Ugavi katika Serikali na Asasi zake ikiwa ni pamoja na marekebisho ya Sheria Na. 3 ya Ununuzi ya mwaka 2001

- Ushirikiano na Taasisi za Kimataifa: Bodi imeendeleza azma ya kushirikiana na taasisi zilizopo nje ya nchi kwa lengo la kupata mbinu bora za ununuzi na ugavi. Aidha, Bodi imeanzisha mahusiano na *Administrative Staff College of India (ASCI).*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo Bodi ilikabiliwa na changamoto/matatizo yafuatayo wakati wa utekelezaji wa majukumu yake:

- Uhaba wa fedha za kuendeshea Bodi: Bodi imekumbwa na ufinyu wa bajeti hasa baada ya shughuli zake kupanuka. Ada wanayolipa watahiniwa na wanataaluma haiwezi kutosheleza kuiendesha Bodi. Bodi imepitia upya ada hizi kwa lengo la kuziboresha.

- Ukosefu wa ajira: Wahitimu wengi hawapati ajira kutokana na fani kuvamiwa na wasio wanataaluma. Kazi nyingi za ununuzi na ugavi zinafanywa na wasiosajiliwa kwa mujibu wa sheria Na.9 ya mwaka 1981. Hivyo Wizara imeandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria Na. 9 ya mwaka 1981 ili Bodi ipewe nguvu ya kisheria kuwachukulia hatua waajiri wanaoajiri Maofisa Ugavi wasio na fani ya ununuzi kufanya kazi za ununuzi na utunzaji vifaa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/06, Bodi imejiwekea malengo yafuatayo:-

•Kusimamia kwa ukamilifu mpango maalumu wa mafunzo endelevu ili kuinua uwezo wa wanataaluma ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi, hasa kwenye mazingira ya sasa ya soko huru lenye ushindani na mbinu mpya za ununuzi.

•Kuboresha mafunzo ili kuweza kuongeza kiwango cha wanaofaulu mitihani toka wastani wa 34% kwa mwaka hadi 40%.

•Kuhamasisha wananchi na watendaji wakuu wa Serikali na Asasi zake kuhusu umuhimu wa fani hii kwenye kujenga uchumi wa nchi. Lengo ni kuweza kupata utendaji bora kwenye kazi na pia wanataaluma wengi wachukue mafunzo haya.

•Kutoa ushauri kwa Serikali juu ya Sera za Ununuzi na Usimamizi Bora wa Vifaa kwa kusaidia kuandaa mfumo wa maadili wa wanataluma wa Ununuzi na Ugavi.

•Kuandaa mbinu na mikakati ya kuongeza vyanzo vya mapato kama vile kuendesha semina na warsha bora na nyingi zaidi, lengo na dhumuni likiwa baada ya miaka mitano kuanzia sasa Bodi ijitegemee na kujiendesha yenyewe.

•Kupanua huduma za Bodi kufika kwenye sehemu ambazo hazijafikiwa, hasa mikoani.

•Kupanua wigo wa mahusiano na ushirikiano baina ya Bodi na taasisi za ugavi kanda ya Afrika Mashariki na kwingineko ulimwenguni kwa lengo la kukuza taaluma na uwezo wa wanataaluma.

• Kuboresha huduma ya maktaba kwa kupata nyenzo na vitabu vya kutosheleza mahitaji ya wanataaluma. •Kutafuta mfadhili/mbia atakayeweza kuipatia Bodi baadhi ya nyenzo muhimu za kufundishia na vifaa vya kisasa vya ofisi au mtandao. Hii itaenda sambamba na kuboresha uwezo, elimu na upeo wa wafanyakazi ili waweze kuongeza tija.

•Kujenga uwezo (*Capacity Building)* wa wataalamu wa ununuzi na ugavi ili waweze kuanzisha kampuni zao za ushauri kwenye taaluma ya ununuzi na ugavi.

Mheshimiwa Spika, bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (*Architects and Quantity Surveyors Registration Board* - *AQSRB)* ilianzishwa

kwa Sheria ya Bunge Na. 16 ya mwaka 1997 kwa lengo la kusajili, kusimamia, kuangalia na kuratibu mwenendo wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi na kampuni za kitaalamu na za ushauri zinazohusiana na fani hizo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/05 Bodi iliweza kufanikisha malengo yake kama ifuatavyo:

•Kusajili jumla ya wataalamu 24 na makampuni ya ushauri 16. Usajili huu unaifanya Bodi kuwa na jumla ya watalaamu waliosajiliwa kuwa 291 na makampuni 128 nchi nzima. Katika kipindi hicho, kampuni 5 za Ubunifu Majenzi na wataalamu 5 walifutiwa usajili. Pia usajili wa wabunifu Majengo 5, mkadiriaji majenzi mmoja na kampuni ya ubunifu majengo ulisitishwa kwa muda kwa kukiuka Sheria Na.16 ya 1997 na sheria ndogo ndogo *(GN No. 168* ya 2000).

•Kuanzisha mafunzo kwa vitendo kwa Wahitimu wa fani za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi *(Enhanced Articled Pupilage Programme).* Mpango huu ulianza rasmi tarehe 10-01-2005. Maombi 103 yalipokelewa lakini kutokana na upungufu wa fedha ni wahitimu 20 waliochaguliwa kuanza.

•Kupanua wigo wa mapato ya Bodi kwa kubuni vyanzo vipya ambavyo ni pamoja na kutoa ada za kushiriki makongamano yaliyotayarishwa na Bodi, kuuza Jarida la Bodi, kuuza fulana zinazotangaza Bodi, kuuza nyaraka mbalimbali zilizotayarishwa na Bodi na faini kwa wakosaji.

• Kutembelea na kufanya ukaguzi katika mikoa 14 ya DSM, Pwani, Iringa, Mbeya, Dodoma, Morogoro, Arusha, Mwanza, Shinyanga, Manyara, Kilimanjaro, Tanga, Mtwara na Lindi.

- Kutayarisha mitihani ya kitaalamu na kutahini watalaamu watarajiwa 48 katika ngazi mbalimbali. Kati ya hao watahiniwa 30 walifaulu.

- Kutayarisha Makongamano 2 ya kutoa Elimu *Endelevu (Continued Professional Development Programme)* kwa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi. Jumla ya walengwa 322 walinufaika na mpango huu.

- Katika juhudi za kuimarisha mawasiliano na kuitangaza Bodi, kwa mara ya kwanza Bodi ilizindua Jarida la *Bodi (The Architect and The Quantity Surveyor Newsletter).* Jarida hili linatoka mara nne kwa mwaka. Aidha, machapisho 18 yalitolewa kwenye magazeti na Televisheni.

- Kuhamasisha Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi kutumia nyaraka zenye viwango sawa kiutendaji *(Standard Documents*) zilizotayarishwa na Bodi. Watalaamu wengi walijitokeza kununua na kutumia nyaraka hizi, na hivyo kurahisisha ukaguzi sehemu za majenzi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya Bodi ilikabiliana na changamoto zifuatazo:-

- Kutokuwepo kwa Sheria ya Majengo ya Kitaifa *(National Building Control Act)* inayoratibu wadau mbalimbali wanaoshiriki katika ujenzi wa majengo. Tatizo hili linakwamisha utekelezaji na usimamizi wa Sheria Na. 16 ya mwaka 1997. Wizara inalifanyia kazi suala la uanzishwaji wa Sheria hii.
- Kuvamiwa kwa fani ya Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi. Mazingira yaliyojengwa yanaendelea kuharibiwa kwa sababu watu wasio Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi wanatayarisha ramani za ubunifu majengo na kukadiriaji gharama za Majenzi.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hizi Bodi itaimarisha ukaguzi wa miradi na kufuatilia kwa karibu zaidi utekelezaji wa miradi mbali ya ujenzi wa majengo ili kuhakikisha kuwa shughuli zote za ubunifu na ujenzi wa majengo unafanywa na wataalamu wenye fani hizo kama sheria zinavyotaka.

Katika mwaka 2005/2006, Bodi inatarajia kutekeleza yafuatayo:

- Kusajili wataalam 35 na wale wenye sifa za kati 67.
- Kusajili kampuni za kitaalamu 22.
- Kuwatahini wataalamu watarajiwa 66.
- Kuendeleza mpango wa mafunzo maalum ya vitendo kwa ajili ya kuwasaidia wahitimu wa taaluma husika ili waweze kusajiliwa kwa mujibu wa sheria. Walengwa 143 wanatarajiwa kujiunga na mafunzo haya.
- Kutembelea na kukagua sehemu 300 za majenzi nchi nzima.
- Bodi itaangalia upya mfumo wa mitihani na mfumo mzima wa usajili kwa lengo la kuimarisha na kuwavutia wataalamu wengi zaidi kujisajili.
- Bodi itaendelea kutangaza shughuli zake kwa wadau kwa kutoa elimu kwa umma kuhusu huduma zitolewazo na bodi na pia kutembelea shule za Sekondari kuhamasisha wanafunzi kupenda na kujiunga na taaluma hizi.
- Kuendelea kutekeleza Mpango Kabambe *(Strategic Action Plan* 2002-2006) wa Bodi hasa maeneo yanayolenga kuweka msingi wa kuimarisha utekelezaji wa Sheria Na.16 ya 1997 na kuimarisha Bodi kimapato.

Mheshimiwa Spika, bodi ya Usajili wa Makandarasi *(Contractors Registration Board (CRB)* ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na.17 ya mwaka 1997. Chini ya Sheria Na. 17 ya 1997 ni kosa la jinai kwa mtu yeyote au kampuni yoyote kufanya kazi za kikandarasi bila kusajiliwa na Bodi. Madhumuni ya kuanzishwa kwa Bodi hii ni kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma za makandarasi katika soko huria. Katika kuendeleza azma hiyo Bodi imepewa majukumu yafuatayo:-

- Kusajili makandarasi wa aina zote;

- Kuratibu shughuli na mwenendo wa makandarasi wote; na

- Kujenga uwezo wa makandarasi wa Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/05, Bodi imetekeleza yafuatayo:

- Usajili wa Makandarasi: Bodi imesajili jumla ya makandarasi mia saba ishirini na wawili (722) wa ndani na nje katika madaraja mbalimbali. Idadi hii inafanya jumla ya makandarasi wote waliosajiliwa na Bodi hadi sasa kufika elfu tatu mia saba na thelathini (3,730) baada ya kutoa wale ambao wamefutwa. Hata hivyo, bado makandarasi wengi waliosajiliwa wako kwenye madaraja madogo ya tano mpaka saba hali inayodhihirisha kuwa makandarasi wengi wana uwezo wa kufanya miradi midogo midogo tu.

- Usimamizi na uratibu wa Shughuli za Makandarasi: Bodi ilikagua jumla ya miradi 759. Ukaguzi huu umebaini kuwepo kwa maendeleo makubwa katika utendaji wa kazi za Makandarasi. Kati ya miradi iliyokaguliwa, miradi 540 sawa na asilimia 71 haikuwa na mapungufu yoyote. Asilimia 29 ya miradi mingine ya kazi iliyokaguliwa ilikuwa na mapungufu kama vile kutokuwa na mkandarasi aliyesajiliwa, kutokuzingatia usalama kazini, kutokuwa na bango na kutokuwa na uzio. Takwimu zinaonyesha kwamba kumekua na ongezeko la kufuata sheria *(compliance)* toka asilimia 52 mwaka 2003/2004 mpaka asilimia 71 mwaka 2004/05. Maeneo yanayoonyesha maendeleo makubwa ni pamoja na kuongezeka kwa matumizi ya vifaa vya usalama vya kujikinga kwa wafanyakazi katika maeneo ya ujenzi na waajiri kutumia Makandarasi waliosajiliwa. Wale waliokiuka sheria walitozwa faini isiyopungua Shilingi milioni tano (5) na wengine kushitakiwa polisi au kufunguliwa kesi mahakamani moja kwa moja.

- Makandarasi Waliofutiwa Usajili: Katika mwaka 2004/2005 jumla ya Makandarasi 351 walifutiwa usajili wao kwa sababu mbalimbali zikiwemo kutokufuata maadili yalioainishwa chini ya Sheria ya Usajili wa Makandarasi na kutokulipa ada zao za mwaka kwa miaka miwili mfululizo. Hii inafanya jumla ya makandarasi waliofutiwa usajili na Bodi toka mwaka 1999 kufikia 1,666.

- Mfuko Maalum wa Kusaidia Makandarasi: Katika mwaka 2004/05 Mfuko huu ulioongezewa fedha kutoka shilingi millioni 716 mpaka shilingi milioni 891 ili kuweza kuhudumia makandarasi wengi zaidi. Aidha, katika mwaka 2004/05 uanachama wa Mfuko huu uliongezeka toka wanachama 215 mpaka 335, na kati ya hao wanachama 252 walifaidika na Mfuko huu.

- Kujenga uwezo wa Makandarasi: Katika mwaka 2004/05 Mpango Endelevu wa Mafunzo ya Makandarasi (Sustainable Structured Training Program) uliendesha jumla ya kozi nane katika mikoa ya Dar es salaam, Kagera, Morogoro, Mtwara, Iringa, Shinyanga na Dodoma. Jumla ya makandarasi 298 walihudhuria mafunzo haya. Hii inafanya jumla ya kozi hizi kufikia 33 toka zilipoanzishwa mwaka 2001, na makandarasi waliopatiwa mafunzo kufikia 1,059.

- Mikutano ya Majadiliano na Waajiri na Wadau: Katika juhudi zake za kuelimisha waajiri juu ya umuhimu wa matumizi ya makandarasi waliosajiliwa, Bodi ilifanya mikutano ya majadiliano na watendaji na madiwani katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Kigoma, Rukwa, Tabora na Shinyanga. Vile vile Bodi ilitembelea jumla ya waajiri 220 katika sekta binafsi na ya umma. Ili kuhamasisha vyombo vya dola katika kusimamia sheria ya Usajili wa Makandarasi, katika kipindi cha mwaka 2003 hadi 2004, Bodi iliendesha mikutamo 3 ya majadiliano na Maafisa waandamizi wa Jeshi la Polisi kutoka mikoa ya Pwani, Dar es salaam na Morogoro, Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga. Mikoa mingine ni Mwanza, Mara, Kagera, Shinyanga na Tabora.

- Aidha katika kipindi hiki Bodi ilifanya marekebisho ya sheria yake ndogo ili kuboresha mazingira katika sekta hii, na kutoa uwezo zaidi wa kuendeleza makandarasi wazalendo. Mabadiliko haya yanahusu:

-Kuongeza thamani ya viwango vya juu vya kazi katika kila daraja la Ukandarasi kwa kuzingatia thamani ya fedha za Tanzania katika soko la dunia.

-Kuweka sifa za chini za nafasi ya Mkurugenzi Mmiliki wa kampuni ya Ukandarasi ili kuhakikisha kwamba biashara ya ukandarasi inafanywa na wenye fani zinazotakiwa.

- Ili kuongeza nafasi za kazi kwa makandarasi wazalendo, Bodi imesajili Makandarasi wageni katika daraja la kwanza peke yake ili kuhakikisha kwamba ni wageni wenye uwezo mkubwa tu ndio wanaoruhusiwa kufanya kazi Tanzania. Aidha Bodi imeweka utaratibu wa Makandarasi kusajili miradi na kupata nembo maalum kwa kila mradi wanaotekeleza ili kuondoa udanganyifu wa watu kununua majina ya makandarasi waliosajiliwa na kufanya kazi kinyume cha sheria. Vilevile hatua hii inalenga katika kuiwezesha Bodi kudhibiti ukiukwaji wa viwango vya kazi kwa kila daraja na kukusanya takwimu zinazotakiwa katika Sekta ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazowakabili makandarasi nchini ni pamoja na:

- Mitaji midogo na masharti magumu ya kupata mikopo ya kufanyia kazi kutoka mabenki na taasisi zingine za fedha.

- Udhaifu wa uendeshaji na usimamizi wa miradi miongoni mwa makandarasi.

- Ukosefu wa vifaa na mitambo ya ujenzi kwa makandarasi wenyewe, hii ni pamoja na kutokuwa na uwezo wa kuimiliki, bei kubwa za kukodisha mitambo na uchache wa sehemu za kuikodisha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/06 Bodi imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

- Kusajili jumla ya makandarasi wapya 767.

- Kufanya ukaguzi wa miradi 850 katika sehemu mbali mbali nchini.

- Kuanza utaratibu wa kusajili miradi yote yenye gharama ya zaidi ya shilingi milioni kumi.

- Kuendesha jumla ya kozi sita katika mikoa ya Shinyanga, Ruvuma, Mbeya, Kilimanjaro na Dar es Salaam chini ya mpango endelevu wa mafunzo ya makandarasi.
- Kuendesha warsha ya kuwafundisha makandarasi jinsi ya kufanya kazi kwa ubia (*Joint Ventures*) ili kuwajengea uwezo wao.

- Kuendesha kozi maalum ya kuwafundisha makandarasi muundo mpya wa manunuzi ya kazi za ujenzi wa Buni- Jenga yaani *'"Design and Build"* kwa lengo la kuwapa makandarasi wazalendo uwezo wa kushindania kazi hizi katika soko huria.

- Kupanua wigo wa Mfuko Maalum wa Kusaidia Makandarasi ili kuongeza idadi ya makandarasi wazalendo watakaofaidika na Mfuko huu kwa kuwahusisha makandarasi wa daraja la nne. Kwa hali hii mfuko huu utaweza kutumika na makandarasi wa kuanzia daraja la nne mpaka la saba.

Mheshimiwa Spika, baraza la Taifa la Ujenzi lilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 20 ya mwaka 1979 likiwa na majukumu makuu ya kusimamia na kuratibu maendeleo ya sekta ya ujenzi nchini na kushauri kuhusu Sera, Mipango na mikakati ya kukuza sekta ya ujenzi ili kutoa mchango wake kikamilifu katika ujenzi na uchumi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005 Baraza lilitekeleza kazi zifuatazo:

- Kwa kushirikiana na wadau wengine Baraza limekamilisha utayarishaji wa Programu ya Utekelezaji wa Sera ya Ujenzi na imeshajadiliwa na kukubalika na wadau na hivi sasa inasubiri kuchapishwa na kusambazwa.

- Kukamilisha maandalizi ya mapendekezo ya marekebisho ya Sheria Na. 20 ya mwaka 1979 iliyounda Baraza la Taifa la Ujenzi. Mapendekezo hayo yanafanyiwa kazi na Serikali kabla ya kuyafikisha Bungeni.

- Baraza liliendelea kufanya majadiliano na Mabenki Binafsi jinsi ya kutunisha mtaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Ujenzi *(CIDF).* Aidha,

majadiliano na Benki ya Dunia kupitia Serikalini yanaendelea kwa ajili hiyo hiyo.

- Ripoti mbili zilikamilishwa na Wataalam Washauri kuhusu utekelezaji wa miradi kwa ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*Public-Private Partnership (PPP).* Aidha, mafunzo juu ya *PPP* kwa washiriki 54 na Warsha kwa ajili ya Mabenki na Taasisi za Fedha zilifanyika pia. Timu maalum ya *PPP* iliandaa mapendekezo kutokana na ripoti hizo mbili ambayo yalijadiliwa na kupitishwa na wadau kwenye ya Warsha tarehe 15 Oktoba, 2004.

- Baraza limeshiriki katika kuandaa mkakati wa ukarabati wa miundo mbinu ya Afya ya Msingi chini ya Wizara ya Afya na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Aidha, Baraza lilitoa mafunzo kuhusu utayarishaji na utoaji wa zabuni, usimamizi wa mikataba, ukadiriaji wa gharama za ujenzi, uratibu wa kazi ya ukarabati, udhibiti wa ubora wa kazi na matumizi ya fedha kwa watendaji 150 kutoka wilaya 40 ambazo ziko kwenye awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi huu.

- Kukamilisha ukaguzi wa kiufundi kwa miradi 12. Pia ukaguzi wa kiufundi wa miradi 15 mingine ulikuwa unaendelea. Miradi hiyo inajumuisha ukarabati wa hospitali na vituo vya afya katika mkoa wa Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na hospitali ya rufaa Muhimbili, ujenzi wa uwanja wa ndege Mbeya, ujenzi wa nyumba na ofisi za Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Ofizi za Bunge Dar es Salaam na miradi ya barabara, maji na umwagiliaji.

- Baraza lilitoa huduma 20 za ushauri wa kiufundi na usuluhishi wa migogoro 5 ulikuwa unaendelea.

- Baraza lilitayarisha machapisho na miongozo kuhusu Sekta ya Ujenzi kama ifuatavyo:-

    - Mwongozo wa vifaa vya ujenzi (*Directory of Construction Materials);*

    - Mkataba wa shughuli za majengo *(Agreement and Schedule of Conditions of Building Contract with Quantities*) toleo la 2004;
    - Jarida la shughuli za ujenzi (*Construction Business Journal).*

Aidha, katika kipindi hiki Baraza lilijishughulisha pia na kazi zifuatazo:-

• Maendeleo ya Sekta ya Ujenzi isiyo Rasmi *(Informal Construction):* Baraza kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*United Nations Development Programme (UNDP)* na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam walikamilisha utafiti kuhusu mifumo ya Sekta ya Ujenzi isiyo Rasmi na matatizo yao kwa Mkoa wa Dar-es-Salaam. Utafiti huu ulifadhiliwa na Serikali ya Japan. Baraza limechukua jukumu la kuendeleza utafiti huu kwa lengo la kutengeneza programu ya utekelezaji wa Sekta ya Ujenzi isiyo rasmi kwani sekta hii inachangia katika pato la taifa na kupunguza umasikini na kwamba hii ni moja ya mikakati ya Sera ya Ujenzi.

• Mradi wa Nyumba kwa Kutumia Mianzi: Baraza kwa kushirikiana na mtandao wa kimataifa wa mianzi na matete *(International Network for Bamboo and Rattan - INBAR)* liliendelea na utekelezaji wa mradi wa uhamasishaji wa ujenzi wa nyumba kwa kutumia mianzi. Mradi huu kwa hivi sasa unatekelezwa katika wilaya za Kyela na Rungwe.

• Utafiti wa Afya na Usalama Kazini katika Miradi ya Ujenzi: Baraza kwa kushirikiana na watafiti kutoka Bodi ya Usajili wa Makandarasi *(CRB),* Wakala wa Barabara *(TANROADS)* na Chama cha Wafanyakazi wa Ujenzi na Migodi *(TAMICO)* lilifanya utafiti wa afya na usalama kazini katika miradi ya Ujenzi. Utafiti huo ulionyesha kuwa sheria za kazi kuhusu afya na usalama kazini katika ujenzi hazitekelezwi kikamilifu; hivyo kuwaweka wafanyakazi wa miradi ya ujenzi katika hatari ya afya zao pamoja na usalama wao.

•Baraza lilishiriki katika maandalizi ya Mkutano wa Kimataifa wa Barabara za Vijijini chini ya "*International Focus Group (IFG) on Rural Roads Engineering*" uliofanyika Arusha, mwezi Machi, 2005 na kuhudhuriwa na washiriki 175 kutoka nchi 28 duniani.

•Baraza lilishiriki katika maandalizi ya Wiki ya Usafirishaji mwezi Oktoba, 2004. Aidha, katika maadhimisho hayo, Baraza liliandaa Warsha ambapo Programu ya Utekelezaji wa Sera ya Ujenzi pamoja na mapendekezo kuhusu uboreshaji wa mazingira ya utekelezaji wa miradi kwa njia ya ubia katika sekta ya umma na sekta binafsi *(Public Private Partnerships* - *(PPPs)* vilijadiliwa kwa kina na wadau mbali mbali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Baraza litaendelea na kazi zifuatazo:

- Kutoa msukumo katika utekelezaji wa Sera ya Ujenzi;
- Kuendeleza jitihada za kutunisha mtaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Ujenzi *(CIDF)* ili uanze kufanya kazi;
- Kupima tija na ubora *(productivity and quality*) wa kazi za ujenzi;
- Kuandaa mazingira mazuri kwa utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa njia ya ubia kati ya Sekta za Umma na Sekta Binafsi;
- Kutoa mafunzo, ushauri, usuluhishi wa migogoro, na ukaguzi wa kiufundi, utayarishaji na uchapishaji wa majarida ya kiufundi, mradi wa ujenzi wa nyumba kwa kutumia mianzi, mradi wa utafiti na meandeleo ya sekta isiyo rasmi;
- Ukusanyaji na uwekaji wa takwimu za shughuli za ujenzi, na kuongoza kamati ya Shirikisho la Barabara Duniani *(PIARC).*

**Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ujenzi Morogoro kilianzishwa kwa madhumuni ya kufundisha Mafundi sanifu, mchundo na wahandisi wa Wizara ya Ujenzi na Halimashauri za wilaya. Aidha, Chuo sasa kinatoa pia mafunzo kwa mafundi sanifu na stadi wanaoshiriki kazi za ujenzi kwenye sekta za umma na binafsi. Katika kipindi cha 2004/2005 Chuo kimetekeleza yafuatayo:**

- **Ukarabati wa karakana pamoja na majengo;**
- **Kufundisha mafundi Sanifu 68 wa fani mbalimbali;**
- **Kufundisha madereva wapya 148;**
- **Kuendesha mafunzo ya mafundi stadi mbalimbali 55; na**
- **Kuendesha mafunzo kwa madereva wa umma – 11.**

**Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006 Chuo kimepanga kutekeleza kazi zifuatazo:**

- **Kufundisha mafundi Sanifu (*technicians*) 80;**
- **Kufundisha madereva mahiri 30;**
- **Kuendesha mafunzo ya mafundi stadi mbalimbali (*artisans*) na wanafunzi wa udereva wa awali 150; na**
- **Kukarabati majengo matatu (bwalo la chakula, na mabweni 2).**

Mheshimiwa Spika, kulingana na Muundo wa Wizara uliopitishwa mwezi Novemba 2002, Wizara yangu inastahili kuwa na watumishi 1,488 katika kada mbali mbali. Watumishi waliopo hadi sasa ni 1,476 ambao ni wale walioko katika Idara, na Vitengo vya Makao Makuu ya Wizara, Mikoani pamoja na Vyuo vya Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005 Wizara imeunda Kamati Maalum ya Ajira kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003, Kanuni Na. 9 (3) ambapo katika Mkutano wake wa kwanza imeajiri watumishi wapya kumi na tano (15) wa kada mbalimbali kwa njia ya uwazi na ushindani. Aidha, ili kuongeza ari ya utendaji kazi watumishi kumi na nane (18) wa kada na ngazi mbalimbali walithibitishwa kazini na watumishi hamsini na tano (55) walipandishwa vyeo.

Pia, iIi kuongeza tija na ubora wa huduma zitolewazo na Wizara kwa Umma, watumishi 434 wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi na 59 mafunzo ya muda mrefu kwa ajili ya kuwaongezea ujuzi katika fani zao. Wizara yangu itaendelea na juhudi za kuwapatia mafunzo zaidi ya kitaaluma wafanyakazi wake katika mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na utekelezaji wa Programu ya Kuboresha Utumishi wa Umma wa mwaka 2000 -2011 katika maeneo ya Usimamizi na Utendaji, Ubadilishaji na Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi na Programu ya Wakala Tendaji za Serikali. Katika kutekeleza Programu hii, Wizara imeanza kutumia utaratibu mpya wa upimaji wa utendaji kazi wa watumishi kwa uwazi *(Open Performance Review and Appraisal System (OPRAS)* ambapo watumishi hupandishwa vyeo na kupewa nyongeza za mishahara baada ya kupimwa na kuonekana wamefikia malengo ya kazi waliyowekewa. Aidha, Watendaji Wakuu na Maafisa Wafawidhi wameandaa Mikataba ya Kazi (*Performance Agreements*) kati yao na wasimamizi wao wa kazi. Halikadhalika, katika hatua nyingine ya kuboresha utendaji kazi, Wizara inatarajia kushirikisha Sekta Binafsi katika utoaji huduma za Ulinzi na Usafi katika baadhi ya Ofisi za Makao Makuu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kazi nzuri inayofanywa na wafanyakazi wa Wizara ya Ujenzi, kwa mara ya kwanza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amewatunukia vyeti vya Wafanyakazi Bora na zawadi jumla ya Wahandisi 15 wa Wizara ya Ujenzi katika Sherehe za Sikukuu ya Wafanyakazi zilizofanyika mjini Songea mnamo tarehe 01/05/2005. Wafanyakazi hawa walikuwa ni wawakilishi tu wa wafanyakazi wengine wengi wa Wizara wanaofanya kazi nzuri ya kuboresha miundombinu ya barabara na kutoa huduma nyingine katika sekta ya ujenzi. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais pamoja na Shirikisho la Jumuia ya Wafanyakazi kwa heshima kubwa waliyotupa Wizara ya Ujenzi. Wizara yangu imefarijika sana kwa jinsi mchango wa Wahandisi hawa ulivyotambuliwa katika ngazi ya Kitaifa na tutaendelea kuhakikisha kuwa juhudi za wafanyakazi bora wa Wizara zinaendelea kuthaminiwa mwaka hadi mwaka ili kuwaongezea ari na moyo wa kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la rushwa nchini limekuwa ni ajenda muhimu katika vikao vya kiutendaji katika ngazi mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2004/2005, Wizara imechukua hatua mbalimbali za kiutawala ili kupambana na rushwa. Hatua hizo ni pamoja na:

- Kuanzisha na kuendeleza matumizi ya mizani za magari inayotumia mfumo wa Kompyuta huko Kibaha (Pwani), Mwenda Kulima (Shinyanga) na Mikumi (Morogoro) na pia kuongeza idadi ya mizani za magari inayobebeka kutoka kumi na nne (14) hadi kumi na nane (18) kwa ajili ya udhibiti wa Uzito wa Ekseli.
- Katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara itapitia upya Mkakati wa Kuzuia Rushwa uliopitishwa mwaka 2000 kwa lengo la kuuboresha kwa kushirikisha Idara zote na Wakala zilizo chini ya Wizara.

- Kufuatilia taarifa na malalamiko yanayoelekezwa dhidi ya watendaji wa Wizara kupitia kwenye magazeti, redio, mikutano na barua na kuyafanyia kazi ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za nidhamu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005 Wizara imeendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya kudhibiti UKIMWI kwa kutumia mbinu mbalimbali kama vile kuendesha warsha kwa ajili ya kuhamasisha watumishi juu ya athari za UKIMWI na uwepo wa madawa ya kurefusha maisha. Aidha, Wizara kwa kutumia fedha za Mradi wa UKIMWI katika mwaka 2005/2006 itaendelea kutekeleza Mpango Mkakati *(Strategic Plan)* ya kupambana na UKIMWI, kuandaa mwongozo wa Sera ya UKIMWI *(HIV/AIDS Policy Guidelines)* sehemu ya kazi utakaotumika kama mwongozo wa kuendesha shughuli za UKIMWI pamoja na kutoa huduma kwa waathirika wa UKIMWI na kuanzisha sehemu maalum katika Wizara kwa ajili ya kutoa huduma ya ushauri nasaha na huduma ya kwanza kwa watumishi watakaokuwa na maradhi yanayoambatana na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi inatarajia kukusanya jumla ya shilingi 489,949,794.00 kutokana na vianzio vyake mbalimbali. Idara zinazokusanya mapato ni Utawala, Ugavi na Huduma pamoja na Ufundi na Umeme. Kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya *retention* kwa Idara za Ufundi na Umeme na Ugavi na Huduma kwa mwaka 2005/2006 ni shilingi 455,912,000.00. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/06 Wizara ya Ujenzi imetengewa jumla ya shilingi 73,763,984,600.00 fedha za hapa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Fedha hizi zinajumuisha:-

- Mfuko wa Barabara – Sh. 56,566,482,200.00;
- Mishahara ya Wizara - Sh. 2,338,250,600.00;
- Mishahara ya Taasisi zilizo chini ya Wizara - Sh. 4,919,985,700.00;
- Ruzuku kwa Taasisi zilizo chini ya Wizara - Sh. 3,964,085,400.00;
- *Retention* - Sh. 455,912,000.00;
- Matumizi Mengineyo kwa Wizara - Sh. 5,519,268,700.00.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006 Wizara imetengewa jumla ya shilingi 271,067,333,900.00 kwa ajili ya miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 141,538,834,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 129,528,500,000.00 ni fedha za nje. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maelezo niliyoyatoa kuhusu kazi ambazo Wizara yangu imezifanya katika mwaka 2004/2005 na zile zinazokusudiwa kutekelezwa katika mwaka 2005/2006 ndio msingi na kielelezo cha majukumu ya wizara yangu.

Utekelezaji wa majukumu haya katika kipindi kilichopita umeonyesha mafanikio mazuri katika suala zima la ujenzi na uimarishaji wa barabara, majengo na nyumba za Serikali, huduma za vivuko na shughuli zinazoratibiwa na Bodi zilizoko chini ya Wizara, ingawaje bado kuna kazi kubwa mbele yetu.

Kinachotutia faraja ni kule kuonekana kwa barabara nzuri katika mikoa mbalimbali nchini na kushamiri kwa shughuli za kiuchumi kutokana na mchango mkubwa wa barabara katika maeneo hayo. Tunatoa wito kwa wawekezaji wa aina zote wawekeze rasilimali zao katika maeneo mbali mbali ili rasilimali kubwa tuliyoiwekeza katika barabara iweze kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya wananchi na Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, sina budi kukiri kuwa katika utekelezaji wa majukumu yetu tumepata ushirikiano mkubwa toka pande mbalimbali ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge, wawakilishi wa wahisani wetu na wananchi kwa ujumla.

Kubwa zaidi ni msaada na maelekezo kutoka kwa viongozi wetu wa Kitaifa ambao umesaidia sana kuimarisha utendaji wetu. Hali hii inatupa moyo wa kuendelea kujituma kwa nia moja ili tufanikishe yale yote tunayotarajiwa kufanya.

**Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wote, nikielekeza shukrani maalum kwa Kamati ya Bunge ya Miundo Mbinu chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Prof. Henry Mgombelo, Mbunge wa Tabora Mjini, kwa kukamilisha kazi ya kupitia, kujadili na kutoa ushauri kuhusu Bajeti ya Wizara yangu na hatimaye kuidhinisha Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya mwaka 2005/2006.**

**Wizara yangu itaendelea kuzingatia ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati katika Bajeti hii. Aidha, Wizara yangu itaendelea kuyafanyia kazi maelekezo yote yatakayotolewa na Bunge lako Tukufu wakati wa kujadili Bajeti hii.**

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeelezea hapo awali, Wizara yangu inatekeleza malengo yake kwa kushirikiana na Wahisani. Napenda nitumie fursa hii kuzishukuru Serikali za nchi za Denmark, Finland, Japan, Norway, Saudi Arabia na Switzerland ambazo kwa kiasi kikubwa zimeendelea kuisaidia sekta ya Ujenzi.

Pia nayashukuru mashirika ya kimataifa ya *IDA, ADB, EU,* Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait na *OPEC, BADEA* na *Nordic Development Fund (NDF)* kwa kuendelea kusaidia sekta hii.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kuwashukuru viongozi wa ngazi mbalimbali katika Wizara ya Ujenzi ambao ni Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha (Mb), Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini, Katibu Mkuu Eng. John Kijazi, Wenyeviti wa Bodi za *RFB, NCC, CRB, ERB, AQSRB* na *NBMM.*

Aidha, nawashukuru Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Taasisi na Wakala zote zilizo chini ya Wizara yangu pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara kwa kuonyesha utendaji mzuri wa kazi na uwajibikaji. Miaka mitano ambayo tumefanya kazi pamoja imekuwa ya mafanikio makubwa. Nawashukuru sana. (*Makofi)*

Vile vile napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Uchaguzi la Biharamulo Mashariki kwa ushirikiano walionipa katika kipindi hiki na kwa kunivumilia pale niliposhindwa kuwa nao kutokana na majukumu mengine ya kitaifa yaliyonikabili. Kwa pamoja ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ya mwaka 2005/06, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Bajeti ya jumla ya Shilingi 344,831,318,500 ambapo kati ya hizo, Shilingi 215,302,818,500 ni za hapa na Shilingi 129,528,500,000 ni za nje. *(Makofi)*

- Fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi 73,763,984,600/=.

- Fedha za Maendeleo shilingi 141,538,833,900/=.

**Fedha za Nje Zinajumuisha:**

- Shilingi 129,528,500,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ya Barabara Kuu na za Mikoa pamoja na Vivuko.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA;** Waheshimiwa Wabunge hoja imetolewa na imeungwa mkono, sasa namwita Makamu Mwenyekiti wa Kamati za Miundombinu ili aweze kutoa maoni ya Kamati yake.

**MHE: HENRY D. SHEKIFFU- MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa, Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 88 (11) ya Bunge Toleo la 2004 napenda kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya

Miundombinu kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Ujenzi katika mwaka uliopita 2004/2005 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa maoni ya Kamati yangu ningependa kutumia fursa hii kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wajumbe wote wa Kamati yangu kutoa pole na rambirambi kwa familia na wananchi wate wa Jimbo la Kilombero, kwa msiba wa kuondokewa na Mbunge wao Mheshimiwa Abu Towagale Kiwanga aliyefariki dunia tarehe 2 Juni, 2005. Aidha tunatoa pole kwa familia na wananchi wa Mkoa wa Rukwa, kwa kuondokewa na Mbunge wao, Mheshimiwa Margareth J. Bwana aliyefariki dunia tarehe 23 Juni, 2005, Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu hao mahala peme peponi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Miundombinu imeundwa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 103 B (1) ya Toleo la 2004 na ningependa kuwatambua wajumbe kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Prof. Henry R. Mgombelo, Mbunge ambaye ni Mwenyekiti, Mheshimiwa Henry D. Shekiffu - Makamu Mwenyekiti; Mheshimia Lydia T. Boma - Mjumbe, Mheshimiwa Zamda S. Bozzen Mbunge - Mjumbe, Mheshimiwa Dr. Batilda S. Burian - Mjumbe, Mheshimiwa Robert J. Buzuka -Mjumbe, Mheshimiwa Bakari S. Faki - Mjumbe, Mheshimiwa Abdallah K. Feruzi - Mjumbe, Mheshimiwa

Wengine ni Dr. Amani W. Kabourou - Mjumbe, Mheshimiwa Ally A. Karavina, - Mjumbe, Mheshimiwa Mohammed J. Khatib - Mjumbe, Mheshimiwa Dr. Thadeus M. Luoga - Mjumbe, Mheshimiwa Danhi B. Makanga, - Mjumbe, Mheshimiwa Ibrahimu W. Marwa - Mjumbe, Mheshimiwa Zubeir A. Maulid - Mjumbe, Mheshimiwa Mohammed H. Missanga Mjumbe, Mheshimiwa Dr. James A. Msekela - Mjumbe, Mheshimiwa James P. Musalika - Mjumbe- Mheshimiwa Prof. Daimon M. Mwaga - Mjumbe, Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila - Mjumbe, Mheshimiwa Karim S. Othman - Mjumbe, Mheshimiwa Sijamini M. Shaame - Mjumbe , Mheshimiwa Maria D. Watondoha - Mjumbe.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu iliridhishwa na maandalizi na mawasilisho yaliyofanywa na Wizara ya Ujenzi kuhusu mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa kipindi cha mwaka 2004/2005, pamoja na mafanikio na matatizo yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa mpango wa mwaka jana. Kamati iliridhishwa na mawasilisho kuhusu Mpango na Makadirio ya Bajeti ya mwaka 2005/2006. Pamoja na hayo, Wizara ilitoa maelezo kuhusu kazi zilizopangwa kufanyika katika kipindi hicho na maombi ya fedha kwa kazi hizo.

Mheshimiwa Spika**,** napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa John J. P. Magufuli, Mbunge. Waziri wa Ujenzi, Naibu wake Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha Mbunge pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Ndugu John Kijazi pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa utelezaji wa Bajeti ya mwaka 2004/2005 pamoja na maandalizi ya mpango wa makadirio ya Bajeti ya mwaka 2005/2006

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa ushauri na maoni ya Kamati, naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara ya Ujenzi kwa juhudi walizionyesha katika kutekeleza takribani maoni na mapendekezo yote ya Kamati kwa mwaka 2004/2005. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuboresha mtandao wa barabara muhimu kwa lengo la kutimiza sera ya MKUKUTA; ujenzi wa nyumba za gharama nafuu kwa wafanyakazi wa Serikali; kulinda hifadhi za barabara pamoja na kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kuheshimu maeneo ya hifadhi ya barabara; kuanzisha mpango wa mafunzo ya kujiendeleza kwa Wahandisi na Wataalam wa fani za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majengo; kuhamasisha Makandarasi wa ndani ili waweze kuingia katika ushindani wa ununuzi wa zabuni mbalimbali za ujenzi zinazotangazwa na serikali na kadharika. Kamati inaishauri Wizara iendelee kuufanyia kazi ushauri na maagizo ya Kamati ambayo bado hayajapata ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika,utekelezaji wa malengo ya Wizara kwa mwaka 2004/2005, kama alivyoeleza Waziri taarifa iliyotolewa na Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa John P. Magufuli kuhusu utekelezaji wa mipango ya Wizara kwa Mwaka 2004/2005 ilionyesha kuwa katika kipindi hicho Wizara ilipata mafanikio na changamoto zifuatazo:-

Wizara imefanikiwa kufungua barabara na madaraja katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Kwa mfano Barabara ya Tanga – Horohoro, barabara Mtukula – Muhutwe, Makuyuni – Ngorongoro, Somanga – Masaninga na Chalinze – Melela. Barabara za Jiji la Mwanza, Kigoma – Muhutwe na miradi mingine ambayo iko katika hatua za mwisho kukamilika.

Aidha, Wizara imekamilisha ufunguzi wa Kivuko cha Ukara pamoja na madaraja matano katika barabara ya Tunduma – Sumbawanga na Saba katika barabara ya *TANZAM,* na kuweka mawe ya msingi kwa ajili ya ujenzi wa barabara zingine.

Kukamilika kwa maandalizi ya Ujenzi wa Daraja la Umoja litakalohusisha Nchi mbili yaani Tanzania na Msumbiji.

Kukamilisha maandalizi ya Wakala wa Huduma za Ufundi na Umeme yaani *TEMESA*.

Kupunguza tatizo la kuzidisha uzito wa magari barabarani.

Kujenga na kuwauzia nyumba watumishi wa umma sehemu mbali mbali nchini.

Mhandisi Mshauri amekwisha kuteuliwa na *NSSF* kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na kuandaa mapendekezo ya kujenga Daraja la Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, changamoto, naomba nitumie fursa hii pia kuainisha matatizo yaliyoathiri utekelezaji wa mipango ya Wizara kwa kipindi kilichopita kama ifuatavyo:-

haya yalielezwa na Waziri lakini pengine kutaja machache, Ufinyu wa bajeti ya Serikali katika Wizara ikilinganishwa na mahitaji halisi ya miradi ya kimaendeleo iliyo chini ya Wizara.

Uhaba pamoja na uduni wa mitambo ya kuwawezesha makandarasi wazalendo kumudu utekelezaji wa kazi za barabara na ukosefu wa fedha hivyo kuchelewesha ukamilishaji wa kazi kwa wakati.

Ujenzi holela katika maeneo ya hifadhi ya barabara pamoja na wizi wa alama na samani mbalimbali za barabarani.

Urasimu kutoka kwa baadhi ya wahisani katika kutoa fedha za miradi japo kulikuwa na mwaka huo walisema kwamba kulikuwa na hali nzuri kidogo ya kupokea hela.

Uwezo duni wa sekta binafsi katika ujenzi na matengenezo ya barabara.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka wa fedha wa 2005/2006 katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara itatekeleza malengo yake kwa kuzingatia mkakati wa Sera ya MKUKUTA; kukuza uchumi na kupunguza umaskini, kuongeza ubora wa maisha na hali ya kijamii nchini pamoja na kuimarisha utawala bora wa kisheria. Aidha Wizara imepanga kwa mwaka wa fedha 2005/2006 kufanyia matengenezo Barabara Kuu mbalimbali na za Mikoa zenye jumla ya urefu wa kilomita 26,803.9 na madaraja 2,166.

Wizara inalenga pia kukusanya jumla ya mapato ya shilingi 489,949,794 kutokana na vyombo vyake mbalimbali na Idara zinazokusanya maduhuli za Utawala, Ugavi na Huduma, Ufundi na Umeme.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Pamoja na Wizara kuwa na mpango mzuri kwa mwaka 2005/2006, naomba sasa nitoe maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa Wizara na kwa Serikali kwa ujumla kama ifuatavyo:-

Kwanza, Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi kwa kutoa fursa kwa wajumbe kutembelea miradi ya Wizara hii. Serikali iendelee kutenga fedha za kutosha ili Kamati za Bunge ziweze kukagua miradi na kujionea hali halisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namba mbili, katika kutembelea miradi ya ujenzi wa barabara imejitokeza kuwa makandarasi kadhaa wako nyuma ya muda ulio katika mikataba, kama vile Dodoma – Manyoni, Manyoni – Singida. Pia vile vile Nangurukuru hadi Lindi - Mingoyo Kamati inashauri sababu zinazopelekea kuchelewa huko ziainishwe na ufumbuzi upatikane. Kamati inaishauri Wizara ifuatilie kwa karibu maendeleo ya ujenzi wa barabara zote ili kuhakikisha kuwa miradi hiyo inakamilishwa kwa wakati kulingana na mikataba na makubaliano yaliyowekwa.

Aidha Sheria ya Mfuko wa Barabara, *RFB* irekebishwe ili iweze kuhudumia pia ujenzi na maendeleo ya reli na bandari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namba tatu, uwiano kati ya makandarasi wa nje ambao ni asilimia 3 na makandarasi wa ndani ambao ni asilimia 97 haulingani na kazi za ujenzi wanazopewa makandarasi wa nje kwa asilimia 80 na wandani kwa asilimia 20 tu kwa makandarasi wazalendo. Kamati inashauri kuwa sheria ya manunuzi ya Serikali ibadilishwe ili kutoa kipaumbele kwa makandarasi na washauri wazalendo wenye uwezo na kuandaliwa mikakati maalumu ya kuwawezesha makandarasi wazalendo na wenye sifa kupewa kazi kuliko ilivyosasa.

Mheshimiwa Spika, namba nne, Kamati inashauri kuwa zoezi zima la ugawaji wa nyumba za Serikali liangaliwe kwa makini ili kupunguza kasoro zilizopo. Serikali iweke bayana vigezo vinavyotumika katika uuzaji wa nyumba hizo. Aidha orodha ya watumishi waliouziwa nyumba ikiwa ni pamoja na maeneo waliyouziwa iwekwe wazi katika zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika ni vema Serikali ikaanzisha benki ya nyumba ili watumishi na Watanzania wengine wenye uwezo wa kuridhia na kutekeleza masharti yatakayowekwa waweze kukopeshwa fedha za kujengea nyumba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kwamba katika nyumba za Serikali zinazojengwa zijengwe vizuri, ziwe na uzio, maeneo ya majengo yasionekane kama makambi ikiwezekana zijengwe ghorofa, *flats* ili kuwezesha matumizi mazuri ya ardhi pamoja na usambazaji rahisi wa huduma za jamii hususani maji, umeme, masoko pamoja na shule.(*Makofi*)

Kwa kuwa Kitengo cha Wakala wa Majengo (*TBA*) hakina vyanzo vingine vya mapato, Kamati inashauri Kitengo hicho kibuni vyanzo vingine vya mapato badala ya kutegemea nyumba pekee.

Kwa kutumia mpango wa Jenga – Endesha – Kabidhi (*Build – Operate - Transfer*), ni vema Serikali ikajaribu kuanda utaratibu huo kujenga nyumba nyingi zaidi Dodoma ambako ndiko Makao Makuu ya nchi.

Kwa vile barabara nyingi zinahitajika kujengwa na vile vile Serikali haina fedha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuutangaza mpango wa *BOT* na ule wa *BOOT* kwa uwazi zaidi baada ya kutunga sera. Aidha Kamati inashauri kuwa mfumo wa *Build-Design* kwa ujenzi wa barabara uangaliwe upya kwa maana ya kuuboresha ili barabara nyingine zijengwe kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Spika, pendekezo namba kumi, Kamati inashauri kuwa barabara ya Shirati ijengwe sambamba na barabara nyinginezo zinazokwenda kwenye maziwa na bahari ili kuboresha huduma za usafiri katika eneo hilo.Pendekezo la 11, Kamati inapendekeza kuwa barabara ya Manyoni – Itigi – Kigwa – Tabora – Kigoma ipewe kipaumbele. daraja la Mto Malagalasi lijengwe na kuitwa jina la Rais wa Awamu ya Nne. Aidha Kamati inaipongeza Serikali kwa kukamilika kwa taratibu za kuanza kwa

ujenzi wa Daraja la Umoja yaani *Unity Bridge* ambalo ni kiungo kati ya nchi za Tanzania na Msumbiji.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namba 12 ushauri, Serikali ifanye jitihada ili daraja la Mto Ruvu lijengwe upya na daraja mbadala lipatikane wakati wa ujenzi ili huduma ya usafiri kupitia daraja hilo usikwame. Hii ni hofu tu kwamba daraja la Ruvu linaonekana kuwa na kasoro ndiyo maana limewekewa mapipa. Serikali inatahadharishwa kuchukua hatua za tahadhari. Ushauri namba 13, Serikali itoe kupaumbele katika ujenzi wa barabara kwa mikoa ambayo haina barabara zinazopitika badala ya kuendeleza barabara ambazo tayari ni nzuri na zinapitika kama vile barabara ya Chalinze-Segera. Fedha zinazopatikana zigawanywe sawa kwa Mikoa yote ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ushauri namba 14, Serikali ifanye kila jitihada kuweza kukamilisha miradi yake ya maendeleo kama Mtwara *Development Corridor* na kufungua barabara za Mikoa na zile zinazounganisha Tanzania na nchi jirani. Hii itawezesha bandari zetu kupata mizigo ya kutosha na kutoa huduma nyinginezo kwa mizigo na abiria ndani na nje ya nchi. Kamati hii ina maana ya kwamba tuchukuwe nafasi ya Tanzania, *geographical position* ya Tanzania kwa *advantage* ya maendeleo na uchumi wa nchi yetu (*Makofi*)

Serikali ifanye utafiti wa kutosha kuhusu raslimali zilizopo Mikoa ya kusini, kama vile mradi wa Makaa ya Mawe-Mchuchuma, Gesi ya Songosongo na Mnazi-*Bay* ili kuinua uchumi wa wananchi. Aidha Kamati inashauri Serikali kufanya jitihada kuendeleza miundombinu iliyopo Mikoa ya Kusini li kuwezesha matumizi ya raslimali zilizoko huko. Hii imesisitizwa kwa sababu Wizara ya Ujenzi ndiyo inayosimamia Mtwara *Corridor* kwa hiyo inaombwa izingatie hilo.*( Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri namba 16, Kamati inaipongeza Serikali kwa ujenzi wa madaraja ya barabara ya Tunduma - Sumbawanga kwani itafungua na kuongeza tija katika uchumi wa kijiografia. Kamati inashauri barabara hii iwekewe lami hadi Kasanga. Kamati inasisitiza Barabara ya Sumbawanga - Matai - Kasanga na Matai - Kisesya ziwekewe lami ili kufungua uchumi wa Tanzania na nchi za Zambia, *DRC* na Burundi na pia kwa manufaa ya wananchi wa mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, pawepo na Wakala wa Barabara yaani *TANROADS* katika Halmashauri zetu ili ubora wa barabara zinazojengwa ziweze kukidhi viwango vinavyotakiwa. Aidha *TANROADS* wakabidhiwe jukumu la kushughulikia barabara zilizoko kwenye Halmashauri kutokana na uzoefu waliouonyesha wa kuzitunza na kuziboresha barabara hizo kuliko zilivyo sasa.Kuhusu suala la Halmashauri kukosa Wahandisi waliosajiliwa na *ERB*; Kamati inahimiza Serikali kulipatia ufumbuzi wa haraka suala hili maana fedha nyingi zinapelekwa kwenye Halmashauri. Hii ina maana hawa watu wa ERB kuna Sheria inayopaswa kuwaandikisha Wahandisi, walioko Wilayani kwa sasa wengi hawajaandikishwa.

Mheshimiwa Spika, ushauri namba 19, Mikutano ya Bodi za Mifuko ya barabara, ifanywe wakati Wabunge hawako Bungeni ili kutoa fursa ya wao pia kushiriki.

Aidha Bodi za mikoa zinazohusika na barabara zihimizwe kuweza kufanya ukaguzi yaani *physical inspection* wa mara kwa mara katika barabara zinazoendelea kujengwa ili kuwa chachu ya Makandarasi husika kumaliza kazi zao kwa muda uliopangwa. Pendekezo na ushauri namba 20, suala la Mizani ya Kibaha litafutiwe ufumbuzi wa kudumu kwani imekuwa ni kero kwa wasafiri na magari ya mizigo. Adha hii ndio imekuwa kichocheo cha rushwa katika eneo hilo

Mheshimiwa Spika, ushauri namba 21, kuhusu suala la kukwama kwa kibali cha Boti ziendezo kasi yaani *Lake Fast Ferries* kupelekwa katika Ziwa Victoria, Kamati inaishauri Serikali kuwa yawepo mawasiliano kati ya Wizara ya Ujenzi na Wawekezaji hao ili ufumbuzi upatikane kwa manufaa ya Wananchi na taifa bila kuathiri miundombinu iliyopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa mwaka 2005/2006. Baada ya mawasilisho ya Wizara ya Ujenzi kuhusu mpango wa makadirio ya Bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka 2005/2006, kwa niaba ya Bunge lako tukufu, Kamati yangu ilipitia na kujadili kwa kina taarifa hizo. Ninaliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kukubali kupitisha kiasi kilichoombwa cha shilingi 344,831,318,500/- kati ya hizo shilingi 73,763,984,600/- ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi 271,067,333,900/- ni fedha za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hitimisho: Kwa mara nyingine tena napenda kukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii, vile vile kumshukuru Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Naibu wake Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi Ndugu John Kijazi pamoja na Wataalam wote wa Wizara ya Ujenzi kwa ushirikiano mzuri. Mawasiliano na ushirikiano uliokuwepo kati ya Wizara hii na Kamati yangu umetuwezesha kutembelea kama nilivyosema maeneo mbali mbali. Ziara hizo zimesaidia Wajumbe wa Kamati kujionea hali halisi ya matumizi ya fedha za Serikali na kuweza kuishauri Serikali ipasavyo. Aidha, ziara hizo zimewezesha Wanakamati kuijadili Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2005/2006 na kuandaa taarifa hii kwa umakini zaidi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii pia kumshukuru Makamu Mwenyekiti ambaye ndiye anayesoma taarifa hii kwa ushauri na busara zake zilizoweza kumsaidia kuiongoza Kamati. Naomba pia niwashukuru kwa namna ya pekee Wajumbe wenzangu kwa mchango wao mkubwa wa kupitia na kuchambua mpango wa makadirio ya Bajeti ya Wizara hii kwa umakini na uadilifu mkubwa, hivyo kufanya kazi yangu kama mwenyekiti kuwa rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii pia kumshukuru kwa dhati Katibu wa Bunge Ndugu Damian S.L. Foka na wewe mwenyewe Spika na Makatibu wake wasaidizi katika Kamati hii ambao ni Ndugu Justina M. Shauri na Ndugu Bisile M. Dickson pamoja na wafanyakazi wengine wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuhudumia Kamati ipasavyo katika hatua zote za maandalizi ya taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu naomba kuwasilisha, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Kabla sijamwita Msemaji wa Upinzani naona orodha ndiyo kwanza inakamilika kuchapwa, haijawekwa kwenye ubao, lakini bora niwataje ili kama wako kwenye chai waweze kurejea ndani ya Ukumbi. Wasemaji wa mwanzo mwanzo watakuwa ni mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Ndaboine, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Joel Bendera na Mheshimiwa Mrope. Hao ndio wa mwanzo mwanzo, wajiandae.

Sasa namwita Msemaji wa kambi ya Upinzani kwa Wizara hii atoe maoni ya kambi hiyo. *(Makofi)*

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA (K.n.y. MHE. MOHAMED JUMA KHATIBU – MSEMAJI WA UPINZANI WIZARA YA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maoni kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa Fedha wa 2005/2006 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5), (b) na (c), toleo la 2004.

Kadhalika, naomba niungane na Wabunge wenzangu kuwapa pole familia na wananchi wa Jimbo la Kilombero kwa kufiwa na Mbunge wao Mheshimiwa Hayati Abu Kiwanga pamoja na familia na wananchi wa Rukwa kwa kufiwa na Mbunge wao wa Viti Maalum Mheshimiwa Hayati Margareth Bwana. Mungu aziweke roho zao Marehemu hawa mahali pema peponi, ameni. Mheshimiwa Spika, naomba nitumie pia wasaa huu kumpongeza kiongozi wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Wilfred M. Lwakatare (Mbunge) na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed (Mbunge) Msemaji Mkuu wa Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Grace Kiwelu (Mbunge) Msemaji Mkuu wa Tawala za Mikoa na Mheshimiwa Thomas Ngawaiya (Mbunge) Msemaji Mkuu wa Kilimo na Chakula kwa hotuba zao nzito, za kina na ambazo kimsingi zilitulia, zilizowaonyesha Watanzania kuwapa matumaini mapya ya maisha yao pindi wakiuchagua Upinzani kushika madaraka ya nchi mwezi Oktoba mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sera ya Ujenzi na Uuzaji wa Nyumba za Serikali: Pamoja na hoja nzuri na za kuvutia na takwimu lukuki zenye lengo la kuitetea sera ya kuuza nyumba za serikali, bado sera hiyo haikubaliki kwa wananchi walio wengi. Sera hii ina mikanganyo mingi na ni jambo la busara kwa Serikali kuelewa kwamba si umbumbumbu unaofanywa na wananchi kuipinga sera hiyo. Ni wazi kwamba sera hii inapendelea kundi dogo la watanzania kwa gharama za walio wengi, na inatoa nafasi kwa watu wachache sana kupata mwanya wa kujitajirisha kwa migongo ya watanzania walio wengi. Kwa mfano, nyumba kubwa ya Serikali iliyoko katika kiwanja kikubwa eneo zuri la Dar es Salaam, yaweza kununuliwa kwa bei ndogo ya shilingi milioni 30. Anayenunua naye anaweza kuiuza kabisa kwa mtu mwingine nyumba hiyo hiyo kwa shilingi milioni 300. Je, kama huko si kujitajirisha kwa watu wachache ni nini?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani itakapopata ridhaa ya Watanzania hapo Oktoba mwaka huu kuongoza nchi hii, inatarajia kufanya yafuatayo:-

Moja, nyumba zitajengwa kwa muundo tofauti kabisa ilivyo sasa ambapo zinaonekana kama makambi ya wakimbizi. Sisi tutajenga nyumba zenye kuonyesha thamani yake mbele ya macho ya watu ili kuharakisha manunuzi.

Mbili, nyumba zitajengwa kwa bei nafuu ili zilingane na kipato halisi cha mtanzania, tofauti na ilivyo sasa.

Tatu, nyumba zitajengwa katika mikoa na miji yote kwani lengo ni kwa watanzania wote na hasa watumishi wa Umma ili kuondoa tatizo la makazi.

Nne, badala ya kusisitiza suala la kuwajengea watumishi nyumba, pia mkazo na mipango madhubuti itawekwa katika kuwakopesha watumishi fedha au kuwadhamini kwa Kampuni za ujenzi ili wajengewe nyumba watakazozipenda wenyewe..

Tano, mikopo ya nyumba itatolewa kwa watanzania wa kada zote, yaani wafanyakazi, wakulima na wafanyabiashara kwani wote wanastahili kupewa haki hiyo na kwa kuwa Serikali ni ya wote. Kitu cha kuangalia hapa ni namna gani kutimiza masharti ya mikataba itakayowekwa kwa ajili ya kuwakopesha nyumba au mikopo ya fedha.

Mheshimiwa Spika, si miiko ya Serikali kupitia mashirika yake kama *NHC*, *NSSF, PPF, LAPF* na kadhalika. Kujenga nyumba kwa ajili ya kuuza. Lakini si sahihi sana kwa serikali kuibuka na zoezi la ghafla la kuuza karibu nyumba zake zote kwa kukwepa kuzikarabati, kuzijenga upya, au kuzipendezesha. Mathalan, Askari wa JWTZ, Polisi, JKT, Magereza na kadhalika. Ni sehemu ya watumishi wa umma. Zipo nyumba nyingi chakavu na nzima karibu katika makambi yote ya watumishi wa vyombo vya dola.

Je, hao nao wakidai wauziwe nyumba wanazoishi makambini mwao hali itakuwaje? Je, chini ya sera hiyo nani atasema hao hawastahili kuuziwa nyumba? Aidha, kuhusu nyumba nyingi za walimu, wakufunzi, na wahadhiri katika shule zetu, vyuo vya kati na vyuo Vikuu, Je, nao Serikali itawakubalia wakidai kuuziwa nyumba wanazoishi ndani ya maeneo ya shule na vyuo?

Vipi kuhusu madaktari na watumishi wengine wanaoishi ndani ya maeneo ya Hospitali Kuu ya Muhimbili? Je, wao si ruksa kununua nyumba wanazoishi ndani ya eneo hilo? Na je, kama watazinunua hatima ya Taasisi hizo baadaye ni nini? *(Makofi)*

Ni ukweli usiopingika kwamba sera hiyo ni ya utata mtupu, wapinzani tukichukua nchi tutaiangalia upya sera hii na kama siyo kuitupilia mbali. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kupuuzwa kwa Barabara za Vijijini. Pamoja na majibu matamu na hotuba nzuri za kuwapa watanzania matumaini ya kusafiri kwa teksi kutoka Mtwara hadi Bukoba, bado asilimia 80 ya watanzania wanaoishi vijijini wanasota na kuhangaika kufikisha mazao yao kwenye masoko.

Serikali inahangaika sana kuiboresha miji kwa lami nzuri lakini bado inashindwa hata kutengeneza kilomita tano tu za barabara ya vumbi kati ya kijiji na kijiji, na kati ya vijiji na barabara kuu. Kupuuza miundombinu muhimu vijijini kama barabara, umeme n.k. kunachochea kundi kubwa la vijana kuhamia mjini kwani kukosekana vitu hivyo huko ni kichocheo cha umaskini na ufukara

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi ambazo zimefanyika bado Tanzania ina tatizo kubwa la mawasiliano ya ardhini yaani usafiri na usafirishaji. Sehemu kubwa ya mtandao wa barabara uko katika hali mbaya sana. Baada ya zaidi miaka ya 43 ya Uhuru kwa mfano mtu anayetaka kwenda mikoa ya Kanda ya Ziwa kwa usafiri wa Basi kutokea Dar es Salaam, inakuwa ni nafuu kwake kupitia nchi za jirani za Kenya na Uganda. *(Makofi)*

Aidha ubovu wa barabara zetu umesababisha magari ya abiria kusafiri mchana kwa kuhofia majambazi na ajali. Hatua hii inaathiri kwa kiasi kikubwa mafanikio ya kiuchumi ukilinganisha na wenzetu wanaofanya kazi usiku na mchana. Pamoja na umaskini wetu uliokithiri, ikifika saa nne usiku kila mmoja analazimika kupumzika, atake asitake.

Kambi ya Upinzani tukichukua Serikali Oktoba mwaka huu, utaratibu huu tutauondoa mara moja. Tutaimarisha barabara zetu pamoja na suala zima la Ulinzi na Usalama barabarani, ili wale ambao wameshafaulu na sasa wanatembea, basi sisi tufikie hatua ya kukimbia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa barabara bora za vijijini ni sababu kubwa ya umaskini uliokithiri. Hata Serikali ikija na mi-KUKUTA hamsini na mi-KURABITA mia moja, ikiwa barabara za vijijini hazitaimarishwa umaskini utazidi kujichimbia vijijini, kwa sababu mtizamo wa Serikali ni ule ule wa kikoloni wa barabara safi mjini, walioko vijijini "watajiju". Ni mtizamo huu potofu ndiyo umesababisha hata sisi waheshimiwa wabunge kupendelea kujenga nyumba zetu katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, Arusha n.k. kwa kukimbia kujenga nyumba hizo katika Vijiji ambavyo mara nyingi huwa havifikiki.

Mheshimiwa Spika, kazi duni za ukandarasi: Pamoja na juhudi za kishindo za Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, bado wapo makandarasi wababaishaji wanaomudu kupata kazi za Serikali zenye thamani ya mabilioni kwa namna ya ajabu! Kupasiana kazi *(sub-contracting)* kumejitokeza kuwa ni kikwazo cha ubora wa kazi. Watu wengi wanajiuliza; hivi hii *Konoike* ya sasa inayofanya kazi barabara ya Dodoma – Manyoni kwa kusuasua, ndiyo ile ile ya miaka ya tisini iliyokuwa na ufanisi wa kutisha jijini Dar es Salaam? Kama ni *Konoike* nyingine ni ya "kiaina" Je, inamudu vipi kupata kandarasi za mabilioni ya shilingi?

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada nyingi ambazo Mheshimiwa Waziri Magufuli na wenzake wanazojaribu kuzifanya kurekebisha tatizo la barabara zetu, lakini bado sababu kubwa zinazofanya mambo yasiende ipasavyo ni rushwa, ubadhirifu na kutojali wanyonge.

Serikali kila mwaka inakusanya zaidi ya bilioni 66 kama ushuru na barabara unaotozwa kwenye kila lita moja ya mafuta. Fedha hizi kama zimesimamiwa vizuri tunaamini zinatosha kujenga umbali wa wastani wa kilomita 436 wa barabara imara na za kisasa kwa mwaka mmoja. Kwa kipindi cha miaka 10 kungekuwepo na uwezekano wa kujenga barabara zenye umbali wa kilomita 4,360.

Kwa bahati nzuri katika kipindi cha miaka mitano iliyopita Serikali imeingia kichwa kichwa katika suala zima la kuweka mtandao mzuri wa barabara nchini. Hata hivyo, kama ilivyo kawaida ya mtu aliyevamia jambo, kuna ushahidi mkubwa kwa barabara nyingi zilizojengwa katika uharaka haraka huu hazina ubora unao takiwa. Kwa mfano barabara ya lami kati ya Misungwi hadi Mwanza tayari imeharibika. Aidha, baadhi ya Miradi inatelekezwa na Makandarasi baada ya kushindwa kuhimili vitendo vya rushwa na ufisadi.

Mheshimiwa Spika, kuna utitiri mkubwa wa makampuni ya ujenzi kutoka Jamhuri ya Watu wa China na makampuni hayo yanazo kandarasi tamu tamu na kubwa kubwa za Serikali. Yawezekana yapo mahusiano ya miaka mingi ya "Kikomredi" Kati ya China na Tanzania na hilo si tatizo. Jambo muhimu hapa ni kujua kwamba China ya sasa ni tofauti kabisa na ile China ya Mao Tse Dong. China ya sasa ni China inayoinukia katika uchumi wa kibepari na rafu zote zinazoendana na ubepari unaokimbilia kwenye ubeberu inautambua.

Kuna umuhimu mkubwa sana kuyafuatilia makampuni haya ya ujenzi ili kuijua siri inayoyafanya yarundikane hapa Tanzania na yazoe kandarasi mbalimbali katika Serikali ya Tanzania. Kama siri yao ipo katika kuchapa kazi kiubora tutayasifu na tutayaiga, lakini kama kuna sehemu yamekuwa yakicheza rafu ili "kujinyooshea mambo" basi ni lazima tutafutane.

Aidha, utaratibu unaotumika na Makampuni haya kuleta hata wabeba karai na waweka mafuta kwenye magari kutoka nchini kwao ukomeshwe mara moja. Ni vyema tukaelezwa vibali vya kufanyia kazi za namna hii wanapewa na mamlaka gani. Na pia tujiulize hivi hawa watanzania wazawa watapata ajira hizo wapi, na kama hakuna ajira, wakale wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Upinzani uingiapo madarakani tunakusudia kufanya mawasilino ya barabara kuwa ni moja ya masuala ambayo yatapewa kipaumbele maalum kwa kuzingatia yafuatayo:-

Moja, ni maeneo ambayo Serikali ya Upinzani itaruhusu misamaha ya kodi kamilifu. Tutahakikisha ushuru wote wa barabara unaelekezwa kwenye ujenzi na uimarishaji wa barabara zenyewe.

Mbili, ili kuongeza ajira kwa vijana tutaimarisha na kusaidia uundwaji vikosi vya kutunza barabara katika maeneo ya vijiji ambamo barabara zinapita na vitakuwa vinalipwa na kupewa mafunzo.

Tatu, asilimia 50 ya fedha za ushuru wa barabara zitaelekezwa kwenye ujenzi wa barabara za vijijini. Aidha, ndani ya miaka mitano, tutahakikisha baadhi ya maeneo ambayo hivi sasa yanatumia vivuko yatakuwa na madaraja ya uhakika. Kwa maeneo yatakayo kuwa na vivuko, uvushaji katika vivuko hivyo utakuwa bila malipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Taa za Barabarani na Vibanda vya Abiria: Pamoja na uchache wa taa za barabarani, taa hizi zimekuwa zinagongwa kila mara. Ni bahati mbaya kwamba wanaozigonga huwa hakuna hatua kali za kisheria zinazochukuliwa dhidi yao, lakini pia urejeshwaji wa taa hizo ama huchelewa sana au haupo kabisa na Wizara bado haijashituka.

Mheshimiwa Spika, Vibanda karibu vyote vya kusubiria abiria wa mabasi vimegongwa na magari kandoni mwa barabara kuu za mji wa Dar es Salaam, na hasa barabara ya Morogoro na sasa hivi kuna wimbi kubwa la kugongwa kingo za madaraja katika barabara hiyo.

Hadi sasa hakuna anayejali kuvitengeneza upya vibanda hivyo na wala kutengeneza upya kingo za barabara zilizogongwa. Kuwaadhibu waliohusika daima si rahisi kwa serikali ambapo tayari wakosaji huwa wamemalizana" na askari wa trafiki kwa vijisenti vya aibu kama 2000/-, 5000/- au "Buku"

Mheshimiwa Spika, wakati barabara na madaraja vinaharibiwa kwa uzembe wa madereva, walevi, wezi na wahalifu wengine na kwa sababu ni mali zenye thamani ya mabilioni ya shilingi, ni vyema na hivyo tunashauri kuwa Wizara ya Ujenzi ishirikiane na Wizara ya Mambo ya Ndani kuwabana ipasavyo wale wote ambao wanaohusika na uharibifu huo.

Mheshimiwa Spika, Alama za Barabarani: Kufuatia ujio wa alama mpya za Kimataifa za barabarani kwa nchi zote za *SADC*, Mtanzania anatakiwa kuziweka kichwani na kuzitumia karibu alama mia moja za barabarani. Mpita njia ya watembea kwa miguu aliyejichokea kwa kutembeza mitaani mashati mawili ya mitumba kutwa nzima ili agange njaa, hana muda wa kuzijua alama mpya za barabarani, na kimsingi anasubiri kugongwa tu na dereva wa daladala ambaye naye kachoka kuhangaika kutimiza hesabu za tajiri, na kichwa chake hakina muda wa kujifunza alama mpya haraka haraka. Yeye gari anaendesha kwa mazoea na huweza kupata ajali ishirini kabla hata ya kuzijua hizo alama mpya na kama hatakufa kwa ajali hizo.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko makubwa yanayosababisha kubadili mazoea ya muda mrefu yanahitaji kufanywa_taratibu na kwa makini. Pamoja na sababu zozote zile nzuri za kutumia alama hizo mpya, matayarisho mengi yalitakiwa na yanatakiwa yafanywe kwanza kabla ya chochote kile kufanyika.

Mafunzo ya kutosha kupitia kampeni za elimu kwa umma, na kadhalika yalihitajika. Yanahitajika katika kuzifanya alama hizo zianze kueleweka kwa wananchi.

Alama hizo mpya za barabarani ni sehemu ya suala zima la utandawazi kupitia uchumi wa kikanda na ushirikiano wa kiuchumi wa kieneo.

Ni vyema basi, maaskari wetu wa barabarani wakajihusisha na suala la kuwaelekeza na kuwafunza madereva na watembea kwa miguu badala ya kujihusisha zaidi na shughuli za kuwapiga bao au kuwatisha katika kutengeneza mazingira ya kuwatoa chochote.

Mheshimiwa Spika, Huduma ya Vivuko: Zimekuwepo juhudu nzuri zenye lengo la kupunguza tatizo la vivuko katika maeneo mbalimbali ya Tanzania. Hata hivyo, bado vivuko vya kuaminika na vyenye vifaa vyote vya tahadhari si vya kutosha. Ukosefu wa vipuri na matengenezo ya mara kwa mara yenye lengo la kuzuia kuliko kuponya, bado ni tatizo kubwa. Vivuko vilivyopo katika eneo la Kivukoni *Ferry* Dar es Salaam sasa vina umri mkubwa na vimezeeka na kama si kuelekea kuzeeka. Aidha, Vivuko vilivyopo vinaweza kufanyiwa matengenezo makubwa na kuwekwa *Standby* kusaidia usafiri pindi inapojitokeza haja.

Ninachukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kuchukua hatua ya kununua Vivuko vipya na kuvisambaza katika maeneo mbali mbali nchini kupunguza tatizo la usafiri. Ni vyema basi hatua za ziada zichukuliwe kuwapatia vivuko wananchi katika sehemu nyingine ambazo bado vivuko havijapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kero katika Mizani ya Barabara Kuu: Pamoja na panga pangua na fukuza fukuza za watumishi hapa na pale katika mizani, bado lipo tatizo la kukosekana uharaka jambo ambalo husababisha msongamano mkubwa wa magari, kwa mfano Kibaha na wakati fulani Mikumi katika barabara ya Dar - Mbeya Magari yaliyozidisha mizigo hufanikiwa kupita wakati fulani bila faini yoyote na yamekuwepo madai ya "kitu kidogo" kutolewa kwa maafisa husika waliopo katika mizani hizo. *PCB* inapaswa kufuatilia vitendo vya Maofisa hawa na kujiridhisha kuwa mali wanazojilundikia wanazipata kutokana na mapato ya halali ya mishahara na posho. Panapotoa moshi bila shaka pana moto.

Hata hivyo katika hili tunampongeza Waziri wa Ujenzi kwa kulivalia njuga, bali anahitaji msaada mkubwa wa kuungwa mkono kwa dhati kabisa na wasaidizi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu njia moja muhimu ya kutunza barabara ni kudhibiti uzito wa mizigo inayobebwa na magari, ni jambo la lazima kuwepo kwa watu safi kimaadili, wenye motisha safi ya kufanya kazi, wenye uwezo wa kufanya kazi haraka na kwa umakini, walio na ubunifu na wasiohitajika kusimamiwa.

Barabara bora ni silaha muhimu katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika taifa letu. Watu wanaohujumu barabara kwa namna moja au nyingine ni maadui wa maendeleo ya watanzania na ni muhimu washughulikiwe ipasavyo. Mali nyeti za

taifa si tu Mlima Kilimanjaro au migodi ya dhahabu au Benki Kuu au Ikulu peke yake, bali pia ni pamoja na barabara na madaraja.

Mheshimiwa Spika, Mtandao Wa Barabara: Barabara zetu nyingi kongwe zilibuniwa katika namna iliyotarajiwa kusaidia ufanisi na malengo ya kiuchumi wa kikoloni. Nyingi kati ya barabara hizo zinaunganisha maeneo yaliyo na kilimo cha kibiashara cha mazao asilia, migodi, viwanda pamoja na bandari na mifumo ya reli.

Baada ya Uhuru hali haikubadilika sana, barabara zinaendelea kuheshimu matakwa ya uchumi wenye mwelekeo wa kiukoloni mambo leo.

Mikataba ya Lome kufuatia utaratibu wa *EEC-ACP* na baadae *EC& EU-ACP* iliendelea kuunga mkono kiufadhili barabara zinazopeleka mazao ghafi bandarini na kusambaza bidhaa za viwandani kutoka katika nchi zilizoendelea.

Mheshimiwa Spika, changamoto kwa Kambi ya Upinzani tuingiapo madarakani baada ya kupata ridhaa ya watanzania ni kwamba barabara zote ziendazo kwa wakulima vijijini ni lazima ziwekwe katika hali nzuri ya kurahisisha mizunguko ya bidhaa zitokazo mashambani, pembejeo na bidhaa zingine ziendazo mashambani. Azma ya kufanya kilimo kuwa ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu ni lazima isimamiwe ipasavyo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hitimisho: Nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Chonga kwa kunikubalia niwe mtumishi wao kwa nafasi hii ya ubunge hadi hivi sasa.

Aidha ninatoa pongezi na shukrani kwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani pamoja na Kamati nzima ya Uongozi katika kusimamia na kuratibu majukumu ya Wizara vivuli hapa Bungeni, na kuendesha shughuli zote kwa mshikamano wa hali ya juu na kwa kusikilizana kwa njia ya kupanga mambo kwa kushirikishana.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Waziri Magufuli na Naibu wake pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa ushirikiano mkubwa niliopata kutoka kwao katika kipindi chote nikiwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani. Wameifanya kazi yangu kuwa nyepesi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza na mimi niweze kuchangia kidogo Hotuba ya Waziri wa Ujenzi. Lakini kabla sijafanya hivyo naomba na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole na rambirambi kwa familia ndugu na jamaa wa aliyekuwa Mbunge wa Kilombero Marehemu Abu Kiwanga. Pia nataka nitumie nafasi hii kutoa pole hizo hizo kwa aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana. Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, pia nitumie nafasi hii kutoa pongezi na pongezi za kwanza ziende kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ambaye ameteuliwa na Chama cha Mapinduzi kugombea nafasi ya Urais katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nampongeza sana. *(Makofi)*

Pia nimpongeze Mgombea Mwenza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa kuwa Mgombea Mwenza wa Urais katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pongezi za mwisho lakini siyo kwa umuhimu ziende kwa Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Amani Abeid Karume, ambaye pia ameteuliwa kugombea nafasi ya Urais wa Zanzibar. Wote nawatakia ushindi wa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maneno hayo ya utangulizi na mimi naomba nichangie kidogo maeneo machache ya hotuba ya Waziri wa Ujenzi. Kwanza nianze kwa kutoa pongezi kwa Waziri mwenyewe kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kufanya ya kutengeneza barabara katika nchi nzima. Nampongeza pia na Naibu wake, Katibu Mkuu na watendaji wake wote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo naomba sasa nichangie maeneo machache ya barabara. Mimi nitazichangia barabara chache tu. Kwanza labda nianze na maombi, ninayo maombi matatu kwa Waziri wa Ujenzi. Ombi la kwanza linahusu barabara ya kutoka Kondoa hadi Oluboloti yenye urefu wa kilometa 82. Napenda niishukuru Serikali imetoa fedha za kutengeneza sehemu ya barabara hiyo kwa kilometa 32 kutoka Kondoa hadi Dalai kwa kiwango cha changarawe. Sehemu ya barabara ile sasa hivi ni nzuri sana na usafiri umekuwa mzuri sana kutoka Kondoa hadi Dalai ambako ni kilometa 32. *(Makofi)*

Lakini kama nilivyosema kwamba barabara hiyo ina kilometa 82 kwa hiyo, kuna sehemu ya barabara ambayo imeachwa kutoka Dalai hadi Mlijochini ama Oluboloti kwa sasa ambayo barabara hii ni mbaya sana lakini haikufanyiwa matengenezo ama imeachwa. Lengo la kutengeneza barabara ni kufika mwisho, sasa ukiishia katikati hiyo barabara itakuwa haina faida.

Mimi naomba Waziri aangalie katika Bajeti yake aweze kutupa fedha. Hapa naweza kupendekeza kwamba tumefutiwa madeni mengi, sasa zile fedha ambazo ilikuwa zilipe madeni basi tuelekeze katika barabara hizi ambazo hazijatengewa fedha. Nimejaribu kuangalia programu zake za matengenezo ya barabara sikuona fedha yoyote hata senti tano, isipokuwa nimeona shilingi milioni 9 zimetengwa kwa kurekebisha barabara yaani sehemu ya daraja fulani katika barabara hiyo. Lakini barabara yenyewe haina hata senti tano. Sasa kwa kuwa sasa hivi barabara hiyo, haipitiki kwa kweli ombi langu mtusaidie kutafuta fedha za haraka kuweza kurekebisha hiyo barabara. Hiyo barabara ni mbaya sana hilo ni ombi la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi la pili linahusu barabara ya Kondoa-Kwamtoro - Mpendo. Hapa naomba nitoe maelezo machache ya utangulizi kabla sijatoa ombi langu. Maelezo ni kwamba hii barabara niliyoitaja ilikuwa ikihudumiwa na Ofisi ya *RAS* kabla ya kuanzishwa huu utaratibu wa wakala wa barabara Mikoani. Lakini baada ya

kuanzishwa utaratibu wa wakala wa barabara Mikoani, hii barabara imetelekezwa ama imeachwa, haikuchukuliwa na Wizara kama ilivyokuwa huko awali na ikadaiwa kwamba hiyo ni barabara ya Halmashauri. Lakini si kweli huko nyuma barabara hii ilikuwa inahudumiwa na Mkoa kwa hiyo, ni barabara ya Mkoa. Sasa sababu ya kutekelezwa mimi sielewi.

Sasa naomba wataalam wa Wizara hii waangalie kumbukumbu zao hii barabara ilikuwa chini ya *RAS* kwa maana hiyo ilikuwa ni barabara ya Mkoa kwa hiyo, sioni sababu ya kuitekelekeza. Naomba Waziri pamoja na Katibu Mkuu na wataalam wake warejee kumbukumbu zilizokuwepo huko nyuma kabla ya uanzishwaji wa wakala wa barabara ili barabara hii iweze kuchukuliwa na ihudumiwe na Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niseme kwamba barabara hii kwa sababu ilikuwa ni ya Mkoa naomba basi ichukuliwe kwa kweli sisi hatuna uwezo wa kuweza kuhudumia. Kwa hiyo, ombi langu ni kwamba tunaomba barabara hii ichukuliwe. Bodi ya Barabara ya Mkoa ilikwishapendekeza na mapendekezo yamekwishapelekwa Wizarani. Sasa nasisitiza hili ombi lililotolewa na Bodi ya Barabara ya Dodoma basi lizingatiwe na litekelezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi la tatu ambalo napenda nitoe katika Wizara hii naomba nisaidiwe, linahusu daraja la Munguri. Daraja la Munguri liko katika barabara hiyo hiyo ambayo nimekwishaizungumza ya kutoka Kondoa- Kwamtoro - Mpendo. Hapa naomba nieleze maelezo mafupi kwamba daraja hili lilikuwa ndiyo linahudumiwa barabara hiyo. Lakini wakati wa mvua za *El-nino,* daraja hili lilichukuliwa na maji. Baada ya kuchukuliwa na maji barabara hii ilikuwa haina daraja hili la Munguri. Hiyo imekuwa ni kero kubwa sana hasa kwa Tarafa ya Kwamtoro ambayo ndiyo inatumia barabara hii kwa ajili ya mawasiliano na ndiyo barabara pekee ambayo inatumika kwa mawasiliano kati ya Makao Makuu ya Wilaya na Tarafa ya Kwamtoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jitihada zimefanyika na Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa kutafuta wafadhili mbalimbali wa kusaidia kurejesha hilo daraja. Hapa napenda nitambue Shirika *SNV* ambalo limetoa fedha shilingi 120 milioni kwa kuona umuhimu wa hii barabara ilitoa ili tuweze kuanza ujenzi wa daraja hilo.

Napenda nishukuru kwa niaba ya wapiga kura na wananchi wa Wilaya ya Kondoa, kwa kuona umuhimu wa daraja hilo na kutoa fedha hiyo. Pia napenda niishukuru Wizara ya TAMISEMI nayo imechangia shilingi 60 milioni. Kwa hiyo, naishukuru pia na yenyewe nayo ilitambua umuhimu wa barabara hiyo. Pia niishukuru Halmashauri yangu ya Wilaya ya Kondoa, nayo imejibana sana na ikatoa shilingi milioni 60. Kwa hiyo, jumla yake tumepata shilingi milioni 240 kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo. Lakini gharama ya daraja ni shilingi milioni 340 tumepungukiwa na shilingi milioni 100. Kwa heshima zote naomba Wizara ya Ujenzi itusaidie shilingi milioni 100 tukamilishe kulipa deni la daraja hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana mkandarasi ambaye amejenga daraja hilo, amejenga daraja imara sana na sasa limekamilika. Lakini sasa tumekabiliwa na deni la shilingi milioni 100.

Mheshimiwa Waziri, amekuwa akisaidia miradi mingi sana katika nchi yetu. Sisi hajawahi kutusaidia Wilaya ya Kondoa, nafikiri sasa ndiyo zamu yake ya kutusaidia kwa kweli, tunaomba sana, vinginevyo tutapelekwa Mahakamani kwa sababu hili daraja limekwishakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maombi hayo sasa niende kwenye eneo la mwisho kabisa la kuchangia nalo linahusu barabara ya kutoka Iringa - Dodoma - Kondoa - Minjingu. Sitaki kurudia kueleza umuhimu wa barabara hii kwa sababu mwaka jana nilieleza umuhimu wa barabara hii kwa kirefu. Pia mwaka jana katika mchango wangu nilibainisha kwamba Serikali ilikuwa ikiahidi kwamba itajenga barabara hii kwa kiwango cha lami kwa muda wa miaka kumi na tano sasa.

Napenda warejee kwenye hotuba za Mawaziri wote waliopita tangu mwaka 1990/1991 bajeti hizo ukirejea sasa ni miaka 15, kila siku ama kila mwaka neno linalotumiwa ni upembuzi yakinifu. Sasa mimi nashangaa hii barabara upembuzi yakinifu utachukua muda gani na ujenzi utaanza lini? Sina sababu ya kusema kwamba upembuzi yakinifu siyo muhimu, hapa ninachohoji ni kwamba itachukua muda gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kwamba hata mwaka jana barabara hii ilitengewa shilingi milioni 2410. Nilitegemea kuona wataalam, sijui upembuzi yakinifu unafanyika mezani ama kule barabarani sina uhakika. Lakini nilitegemea kwamba kazi zingeanza kuonekana kwenye *site* ya barabara sikuona kitu zaidi ya alama za X kwenye nyumba kando kando ya hiyo barabara nimeziona hizi. Lakini zaidi ya hapo sikuona kitu chochote kilichofanyika. Sijui hiyo alama X ni sehemu ya upembuzi yakinifu, sina uhakika. Lakini pia mwaka huu barabara hii imetengewa shilingi kama milioni 2800 na kitu hivi. Lakini maelezo ni yale ya miaka 15 iliyopita upembuzi yakinifu. Mimi naomba sana kwa heshima zote basi upembuzi yakinifu uishe mwaka huu mwakani tuanze ujenzi wa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nimeangalia programu ya matengenezo ya barabara inaonekana imepangwa kama kweli upembuzi utaishia miaka 17 kwa hiyo, hiyo barabara itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami kuanzia mwaka 2007/2008. Mimi nafikiri kule ni mbali sana. Naomba upembuzi yakinifu uishe mwaka huu wa fedha 2005/2006 ili mwaka 2006/2007 basi tuanze ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Naomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho nakumbusha tena kwamba tumesamehewa madeni mengi na wafadhili mbalimbali, natambua kwamba siyo fedha tunapewa, tunaachiwa fedha ambazo tulitakiwa tulipe madeni basi tuelekeze huko kwa sababu hii barabara haina pesa tuelekeze hizo pesa ambazo tumesamehewa ziende kwenye barabara hii tuweze kujenga kwa kiwango cha lami. Naomba sana tufanye hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba baada ya mchango huu mfupi nikushukuru tena na natamka kwamba naunga mkono hotuba ya Waziri wa Ujenzi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuongea Bungeni hapa kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kutoa salaam zangu za rambirambi kwa familia na ndugu wa Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga, pamoja na Marehemu jirani yangu, rafiki yangu Mheshimiwa Margareth Bwana, Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wizara ya Ujenzi, kwa jinsi ilivyojitahidi na ikaweza kutuletea kivuko cha Ilagara. Itakumbukwa kwamba mara nyingi nilikuwa nikimwomba Waziri, atupatie kivuko hiki kwa sababu kivuko tulichokuwa nacho kilikuwa na matatizo na kingeweza kuleta hatari kwa wananchi wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kivuko hiki kitakuwa ni changamoto kwa wananchi wa Kigoma hasa wa sehemu za Kusini kusudi waweze kusafirisha mazao yao yaweze kufika Kigoma na baadaye yaweze kufika katika sehemu nyingine za nchi ya Tanzania. Ni imani yangu kwamba baada ya kutupatia hiki kivuko barabara ya Ilagara Kalya itatengenezwa haraka iwezekanavyo kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais wetu Benjamin William Mkapa. Barabara hii ni barabara pekee ambayo inaweza kuwafikia wananchi wa Kigoma Kusini kwa sababu mara nyingi usafiri wa kwenda ni usafiri wa boti ambao siyo wa uhakika na ni hatari kwa wananchi wa Kigoma. Lakini barabara hii inapaswa itengenezwe kwa kiwango cha changarawe kama lami kwa sababu udongo wake ni tifutifu na haiwezi kupitika wakati wa masika. *(Makofi)*

Vile vile barabara hii inapaswa isaidiwe na barabara zinazokwenda katika Vijiji vya Sigunga pamoja na sehemu nyingine ambazo hazina barabara za Vijijini. Sehemu za Sigunga na sehemu ambapo hakuna barabara kabisa, unaweza ukashangaa watoto wanaotoka sehemu zile walikuja Kigoma mara moja ni watoto hawajawahi kuona gari hata mara moja. Inatisha sana, watoto hawajawahi kuona magari. Kuna mtoto wa miaka saba ambaye anasema boti inatembea barabarani, inashangaza sana. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali kwa kuwa inatambua kwamba Mkoa wa Kigoma hauna umeme, kwa kuwa hauna umeme hakuna viwanda, kwa hiyo, Halmashauri haina fedha za kutosha kuweza kutengeneza barabara za vijijini. Ni dhahiri kabisa kwa hiyo, Serikali isaidie kutengeneza barabara za vijijini, kusudi wananchi waweze kusafirisha mazao yao yaweze kufika Kigoma. Tumesema ni sehemu ambayo hatuna matatizo ya njaa tuna ardhi ambayo ina rutuba ya kutosha shida ni usafiri. Kwa hiyo, tunaomba Serikali itengeneze barabara za vijijini wananchi waweze kusafirisha mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikizungumzia Sigunga kuna sehemu inaitwa Kajeje sehemu ya Ilagara huko vile vile nako hakuna barabara. Angekuwepo Mheshimiwa Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi, angekuwa shahidi yangu. Kule hata shule hakuna kwa sababu walimu wanashindwa kusafiri kwenda kule, wanatembea kwa miguu kwa saa 12

kuna shule ina walimu wawili. Hivyo bila shule hatuwezi kutegemea maendeleo katika Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba vile vile nizungumzie barabara ya Mwandiga-Manyovu. Katika hotuba yake Waziri amesema kwamba barabara hii imekamilika, naomba nimhakikishie Waziri kwamba barabara hii haijakamilika, barabara kutoka Njiapanda kwenda Mwandiga penyewe ina mashimo mengi sana zaidi ya 100. Barabara hii wamei-*nickname* barabara ya Mayonga. Barabara ya kutoka Njiapanda Kigoma kwenda mpaka hapo Mwandiga wameiita barabara ya Kabourou kwa sababu hiyo imetengenezwa kwa kiwango cha lami.

Naomba Waziri, aitengeneze barabara ya Mayonga kwa sababu ameshahakikisha hapa kwamba barabara ya Mayonga imeshatengenezwa kumbe barabara ilitengenezwa lakini si ipasavyo ni sehemu moja tu ya Mlima Kasagamba ndiyo imetengenezwa vizuri. Lakini mimi mwenyewe pamoja na gari langu la *four wheel drive* nimekwama kutoka shule ya Nyarubanda kwenda Mukigo wakati wa masika, barabara hiyo ikiwa imeisha lakini ina mashimo, tumeshindwa kutoka tumekaa pale kwa muda wa nusu saa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, umedanganywa barabara hii inahitaji ukarabati mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ambayo ni kero kwa mji wa Kigoma, kama nilivyosema hatuna viwanda, hatuna kipato ni barabara ya kutoka Kigoma Mjini - *Railway Station* kwenda Ujiji. Barabara hii imetengenezwa kidogo mpaka pale sokoni, lakini kutoka sokoni Mwanga kwenda Ujiji imejaa mashimo na ikumbukwe kwamba hii barabara ndiyo inaleta wageni wote kutoka *airport* wanasema ni barabara ya Halmashauri lakini mimi nashindwa kuelewa. Barabara ya *TANROAD* inapaswa iunganishwe Mkoa na Mkoa, sasa hii barabara kwa nini haiunganishi Mkoa wa Kigoma na Makao Makuu ya Kigoma, inaishia njiapanda tu. Naomba Waziri atusaidie katika kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami ambayo ina uhakika kutoka Kigoma Mjini mpaka kwenda Ujiji. *(Makofi)*

Vile vile kuna barabara ya kwenda *airport* kutokea Mwanga kupitia Katubuka nayo ni mbaya sana haipitiki na ndiyo njia fupi inayokwenda *airport.* Barabara hii inahitaji msaada wa Serikali, tunaomba nayo itengenezwe. Vile vile tunahitaji barabara kutoka Kagunga kwenda Kigoma na kutoka Kagunga kwenda Kalinzi Makao Makuu ya Tarafa. Wananchi wa Kagunga wako mpakani na Burundi na mara nyingi wamevamiwa na majambazi kutoka Burundi, hawana mahali pa kukimbilia isipokuwa kwa kutumia boti ambazo haziaminiki. Kwa hiyo, barabara inahitajika kutoka Kagunga kwenda Kigoma Mjini na kutoka Kagunga kwenda Kalinzi Makao Makuu ya Tarafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile tunahitaji barabara ya Kigoma-Tabora ipitike. Mheshimiwa Waziri amesema kwamba barabara iko katika hatua za *design* lakini ni barabara ambayo inaunganisha Mkoa wa Kigoma na sehemu nyingine za Tanzania. Ni barabara ambayo ingeweza kupitisha mazao ambayo sasa tumeshapata kivuko kutoka Kusini mwa Kigoma kwenda Tabora na kwenda sehemu nyingine ni barabara fupi. Lakini sehemu ya Mto Malagarasi pale kwenye daraja ni sehemu ambayo haipitiki wakati

wote, ni sehemu hiyo ambayo inaunganisha Nguruka na Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya. Kwa hiyo, wananchi wa Nguruka wanalazimika wakati wote kupita kwa njia ya treni ambayo na yenyewe haina uhakika.

Mheshimiwa Spika, tunaomba hii barabara itengenezwe haraka iwezekanavyo. Kabla haijawekwa kiwango cha lami tunaomba angalau iwekwe changarawe kusudi wakati wa masika, wakati ambapo mvua ni nyingi na kwa sababu ina utelezi mwingi barabara hii iweze kupitika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kigoma sehemu ya Nyamtukuza kule Kibondo ni barabara ya *TANROAD.* Hii barabara ni barabara korofi na mara nyingi inapotengenezwa wanavuka sehemu ambazo ni korofi na wanatengeneza sehemu ambazo siyo korofi kwa hiyo, inakuwa haipitiki wakati wote. Madiwani wameomba kwamba angalau nao washirikishwe katika kutengeneza hii barabara waweze kusaidia kwa sababu wenyewe ndiyo wanajua sehemu korofi. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iangalie kwa macho mawili barabara hii ya Nyamtukuza, Kibondo kusudi nayo iweze kupitika wakati wote ni barabara ya *TANROAD. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matatizo ya barabara katika Mkoa wa Kigoma ni makubwa mno. Barabara karibu zote za vijijini hazipitiki. Walimu wameshindwa kwenda kufundisha katika sehemu zile ambazo barabara hazipitiki na kwa sababu mara nyingi wanapaswa waje Kigoma Mjini kuchukua mishahara yao, wanashindwa kupata mishahara. Kwa hiyo, wanatoa visingizio vya aina nyingi, wanashindwa kwenda kufundisha katika hizo sehemu ambazo hazina barabara. Tunaomba Serikali iupe kipaumbele Mkoa wa Kigoma kusudi wananchi nao waweze kuonja matunda ya Uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara kuu inayotoka Kigoma kwenda mpaka Njiapanda Rusaunga, barabara hii inahitaji matengenezo ya mara kwa mara. Ingawa ni barabara ambayo imeahidiwa kutengenezwa kwa kiwango cha lami, lakini inahitaji matengenezo ya mara kwa mara. Mara nyingi magari yanakwama njiani kwa sababu barabara ina udongo tifutifu, haipitiki wakati wote, kwa hiyo, ni vizuri zaidi ikatengenezwa. Wananchi wanakwama. Ni barabara mojawapo ambayo wananchi wanatokea Mkoa wa Kigoma kwenda sehemu nyingine wanaweza kukimbilia ni barabara ambayo kunakuwa na majambazi wakati wote, wananchi wanakuwa na wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukitoka Kigoma sehemu ya Mkuti pale wameteka magari mara tatu kwa sababu ya ubovu wa barabara, lazima ukifika pale utapunguza *speed* na pale kuna kona kwa hiyo, wanakuwa wanakusubiri, wananchi wametekwa mara tatu sehemu ya Mkuti. Kwa hiyo, tunaomba sehemu hiyo ifanyiwe matengenezo hata kabla kiwango cha lami hakijawekwa katika barabara hiyo. Siyo sehemu hiyo tu, hata sehemu kabla hujafika Makele tuna pori. Siku moja nilimkuta Mheshimiwa Beatus Magayane, amekwama pale na magari hayawezi kusimama kwa sababu yanaogopa majambazi. Ni hali mbaya sana, tunaomba hiyo barabara ipewe kipaumbele, isisubiri kwamba itengenezwe kwa kiwango cha lami kwa sababu tuna matatizo makubwa sana, tunahitaji hizi barabara zitengenezwe kusudi wananchi waweze kujiletea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie tena barabara za Kasulu, barabara za Kasulu nazo ni mbaya sana. Kuna barabara inayokwenda Kagera Nkanda, wananchi hawajawahi kuona basi kwa sababu kule barabara ni mbaya sana na ni mbali sana. Kuna barabara inayokwenda Kitanga, Kitanga iko karibu na mpaka wa Burundi na ipo mbali sana na Kasulu, kule wananchi wanalima sana mhogo na wananiomba sana kwamba wanakosa soko kwa sababu ya ukosefu wa barabara. Kutokana hali hiyo, wananchi wanapaswa kusafirisha mhogo wao kwenda Kibondo na huko wanapambana na ushuru wa Halmashauri ya Kibondo, pamoja na ushuru wa Halmashauri ya Kasulu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaomba barabara hii ya kutoka Nyalugusu kwenda Kitanga nayo itupiwe macho pamoja na barabara inayokwenda Kagera Nkanda. Lakini kuna barabara inayokwenda Shunga vile vile nayo ni mbaya sana. Hizi barabara zilizo nyingi unakuta zinaharibika kwa sababu ya magari makubwa yanayopeleka vifaa kwa wakimbizi. Kwa hiyo, sioni kwa nini wasitumiwe haya mashirika ambayo yanasaidia wakimbizi kuzitengeneza hizi barabara za Kigoma kwa sababu wenyewe wanashiriki sana katika kuziharibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hotuba ya Waziri wa Ujenzi, lakini naomba autupie macho ya huruma Mkoa wa Kigoma. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia hoja hii. Awali ya yote naomba kuungana na ndugu wa Marehemu, waliofiwa na Wabunge wenzetu, namwomba Mwenyezi Mungu ajalie makaburi ya Marehemu Wabunge wenzetu yawe mapana, watembelewe na malaika watakaowasemeza maneno mazuri, awajalie kuwa miongoni mwa watu wema watakaoingia katika pepo yake. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Lakini pamoja na kuunga mkono hoja hii nilikuwa na mambo machache ya kumwomba Mheshimiwa Waziri. Jambo la kwanza sisi katika *Road Board* tulizungumza juu ya daraja la Mkata kwamba wakati wowote ule linaweza likavunjika na likivunjika litaharibu mawasiliano kati ya Morogoro na Kilosa pamoja na sehemu nyingine za Wilaya ya Kilosa. Majibu tuliyoyapata ilikuwa ni kwamba hoja zimepelekwa Wizarani na leo naona katika mapendekezo hapa sikuona matengenezo ya daraja la Mkata. Lakini vile vile lipo daraja la Kitete ambalo *TANROAD Manager* mwenyewe alikiri katika kikao chetu kwamba haliko katika sura nzuri na litafanyiwa utaratibu wa matengenezo. Lakini humu ndani sikuona. Kwa kuwa yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri alisema leo sauti yake siyo kali kama ilivyo desturi kwa sababu na mafua inawezekana kwa sababu hizo sikumsikia alivyokuwa anazungumzia juu ya barabara hizi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo sikumsikia safari hii kulizungumzia labda kwa sababu sauti yake ina mafua, ni juu ya barabara ya kutoka Korogwe-Handeni-Mziha-Turiani-Mvomero-Magole-Dumila-Madudu-Itete-Msowero-Rudewa-Kimamba-Kilosa hadi unafika Magomeni na kwenda Mikumi. *(Makofi)*

Hoja ya umuhimu wa barabara hii nina hakika Mheshimiwa Waziri anakumbuka, nilianza kuizungumzia hoja ya barabara hii tangu wakati yeye akiwa Naibu Waziri wa Wizara hii. Kwa hiyo, anajua kabisa umuhimu wa barabara hii. Leo kwa sababu sauti yake siyo kali sana kama ilivyokuwa desturi yake kwa sababu ana mafua sikumsikia akiizungumzia na wala sioni iko katika hatua gani katika ujenzi. Nitashukuru sana atakapokuwa anajibu hoja atusaidie kutueleza kwa fedha zilizopangwa mwaka jana ambazo zilikuwepo kwenye bajeti ya mwaka jana zilifanya kazi gani. Je, sasa kazi hiyo ndiyo basi au ndiyo inaendelea na kama inaendelea kwa utaratibu upi?

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine kubwa inayofanywa na Wizara hii ni ya ujenzi wa barabara ya kutoka Morogoro kuja Dodoma, inapendeza. Namwomba Mheshimiwa Waziri na jambo hili nilishamwomba Meneja wa *TANROAD* hawa Makandarasi wanaojenga barabara hii wanaishi na wananchi, wanavijiji wanaoishi kandokando ya barabara hii. Kwa mfano, Maguha pale ni karibu sana na kambi yao ya ujenzi wa barabara hii. Kuna tatizo kubwa la maji la ujenzi wa bwawa, kama mkandarasi wa barabara hii katapila likienda na kuzuia tu pale maji yanabaki pale na watu wanakuwa hawana shida ya maji kwa muda wote.

Kadhalika Magubike, kuna kazi ndogo sana ya *caterpillar work,* jambo ambalo inachukua muda usiozidi saa mbili au tatu na kuna kazi ndogo sana ya kiwanja. Hiyo ni *grader work* haichukui hata muda wa saa mbili, saa tatu. Hoja hii nilimzungumzia Meneja wa *TANROAD,* lakini Meneja wa *TANROAD* niliona alikuwa na kigugumizi. Kwa kuwa leo mwenyewe baba mwenye nyumba upo niliona nilitaje jambo hili kwako ili kusudi utusaidie, maana kama unavyojua Mheshimiwa Waziri likishatengenezwa bwawa pale, bwawa likitengenezeka, pamoja na wananchi kunufaika, lakini ndiyo itajulikana Mbunge nimesema. Kadhalika kiwanja kikitengenezeka pale, kazi ikifanyika itakuwa Mbunge wao nimeleta ombi hili kwako.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri John Magufuli, ndugu yangu, mwanangu, nakuomba sana kwa hili wasialiana na hawa Makandarasi wafumbe macho, wafanya ile kazi kwa muda kidogo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo nasema naunga mkono hoja hii mia kwa mia kwa sababu kazi ya Wizara hii ni kazi ambayo ni ya kupigiwa mfano katika mafanikio ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono sana hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye hoja hii ya Waziri wa Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kufanya hivyo naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa pole kwa wananchi wa Sumbawanga kwa kifo cha ghafla cha Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Margareth Bwana, namwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, kwenye hoja hii ya Wizara ya Ujenzi nisingelazimika sana kuzungumza, kwa sababu nilizungumza kwa kirefu wakati wa Bajeti ya Serikali. Lakini kwa sababu Waziri wa Fedha, aliniambia kwamba tujenge hoja kuhusu barabara kutoka Babati kwenda Orkesimeti,Wilaya ya Simanjiro na Kiteto, kwa kuwa alinielekeza kwa Waziri wa Ujenzi nataka kusema kwamba hoja ilikwishajengwa na nataka nieleze namna hiyo ilivyojengwa.

Mheshimiwa Spika, hoja hii imejengwa kwanza kabisa kutokana na uamuzi wa Mheshimiwa Rais katika kuugawa Mkoa uliokuwa wa Arusha na naomba ninukuu maneno ya Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais alisema hivi, "Ndugu wananchi, pingamizi nyingi zilizotolewa zilihusu namna ya kuugawa Mkoa wa Arusha kuwa Mikoa miwili. Watoa pingamizi wote wamepongeza uamuzi wa Serikali kuugawa Mkoa wa Arusha. Lakini hawakuafiki makusudio yangu juu ya namna ya kuugawa Mkoa huo. Wapo waliopinga kuimega sehemu ya Wilaya ya Monduli na kuihamishia Wilaya ya Babati. Lakini wapo waliopinga Wilaya ya Simanjiro kuwekwa katika Mkoa mpya wa Manyara, wapo waliopinga Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara kuwa Babati."

Mheshimiwa Spika, akaendelea kusema hivi katika hoja ya pili, "Hoja ya matatizo ya wananchi wa upande wa Mashariki wa Wilaya ya Simanjiro kufika Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara imezingatiwa. Hivyo nimeamua ijengwe barabara ya kudumu kutoka Okesimeti hadi Babati." Sehemu ya kwanza mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, akaendelea kusema, "Serikali itatoa kipaumbele kwa Mkoa mpya wa Manyara pamoja na Wilaya ya Simanjiro katika kuzipatia huduma na miundombinu muhimu. Hii itasaidia kuondoa hofu za wanaopinga Wilaya hii kuwa katika Mkoa wa Manyara ambao ni mpya." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, hoja ilikwishajengwa kwamba Rais amekwishasema atajenga, ameamua kujenga barabara ya kudumu kutoka Okesimeti hadi Babati. Ukisema barabara ya kudumu maana yake kwa kweli unazungumzia barabara kuu.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ilijengwa na Wizara ya Ujenzi yenyewe baada ya kupewa kazi hiyo na Mheshimiwa Rais kwa kufanya usanifu na upembuzi yakinifu kwa barabara hiyo ambayo hatimaye ilionekana walau kuweza kuunganisha kwenye barabara inayotoka Kibaya kwenda Okesimeti barabara ya karibu kilometa 250 ingeweza kusaidia kuondoa tatizo hilo kutoka Babati mpaka inapounganishwa na hiyo barabara inayotoka Kibaya kwenda Okesimeti.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hoja tayari imekwishajengwa na usanifu ulianza na kazi ikamalizika. Hoja ya tatu ilijengwa katika kikao cha ushauri cha Mkoa wa Manyara ambapo taarifa ilitolewa kwamba baada ya upembuzi yakinifu Mhandisi Mshauri ameeleza kwamba barabara hiyo itahitaji bilioni 9. Lakini Kikao cha Mkoa tuliona kwamba Serikali pengine isingeweza kutoa hizo fedha kwa mara moja katika kufungua barabara hii muhimu. Tukaomba hoja ipelekwe Serikalini ili barabara hii iwekwe kwenye mpango maalum wa kujenga barabara kama ilivyo barabara hizi za Dodoma kwenda Manyoni mpaka Mwanza iwekwe kwenye mpango maalum.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu katika mipango ya kawaida barabara hii haiwezi kujengwa na tukasema walau basi kwa hatua ya kwanza nusu ya fedha hizo zitolewe katika huo mpango maalum bilioni 4. Nina hakika mipango yote hii imewasilishwa Wizara ya Ujenzi kupitia *TANROAD,* nina hakika hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hoja ilikwishajengwa kwamba barabara gharama yake ni bilioni 9 na inahitaji fedha walau katika awamu ya kwanza bilioni 4, hata hivyo Serikali haikuweza. Hoja hii nadhani kwa mujibu wa maelezo ya Waziri wa Fedha haikufika sawasawa kwake, ndicho alichokisema kwamba tujenge hoja. Lakini Wizara ya Ujenzi katika hatua ya kwanza ilianza na kutengeneza kilometa 17 ambazo kwa sasa ndizo zinaendelea kutengenezwa kutoka Babati eneo la Singe kwenda Kijiji kinachoitwa Gedimar eneo la Kata ya Galapo kilometa 17 kwa sasa zipo chini ya hayo matengenezo.

Mheshimiwa Spika, nilipoona kwamba katika vitabu imewekwa kilometa 10 na fedha kidogo sana imetengwa kuendeleza tena barabara hiyo, nikaona kwa *speed* hiyo kufika kilometa 250 itakuwa tatizo kubwa sana na kwamba hoja ya wale waliokuwa wanapinga Wilaya ya Simanjiro kuwa katika Mkoa mpya wa Manyara basi itakuwa na mantiki kama Serikali haiwezi kufungua barabara hii kwa sababu kwa sasa hakuna mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilieleza hapa wakati nazungumzia kwenye Bajeti kwamba inabidi utafute barabara upite kwenye Paliiro ndio uende kwenye Wilaya hizi zingine. Kwa hiyo, kama tunataka kweli kuhakikisha kwamba Mkoa huu mpya unaunganishwa na kwa hoja ambayo Mheshimiwa Rais mwenyewe ameisema kwamba Mkoa huu utapewa sasa kipaumbele kwa huduma na miundombinu basi ni vyema barabara hii ikawekwa kwenye mpango maalum na kwa sababu sasa tumesamehewa madeni kiasi cha fedha ambazo ukiangalia kwenye vitabu kwenye bajeti ya Serikali ilitengwa zaidi ya bilioni 500 na kitu. Kwa hiyo, nina hakika walau kwenye bilioni 300 lazima zitakuwepo katika mpango huu mzima ambao tungeweza sasa kuhakikisha kwamba barabara hii inawekwa kwenye huu mpango maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka kuweka hiyo hoja kwamba hoja imekwishajengwa na Mkoa ulikwishamaliza kazi yake na naomba Wizara ya Ujenzi basi ikae na Wizara ya Fedha kujenga hoja hii ili barabara hii iwekwe kwenye mpango maalum, wakati niliponong'ona na Waziri wa Ujenzi hapa asubuhi, walau Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake nimeona amefikiria kidogo japo siyo katika huo mpango maalum ambao pengine atanieleza kwamba sasa ana mpango gani baada ya hoja hii kukamilika, walau nishukuru na kumpongeza, ameongeza kile kiasi ambacho nilisema ni kidogo na nikiona kwa ujumla wake kwenye vitabu inaweza kufika karibu milioni 500 japo milioni 500 ukijenga barabara kwa kiwango cha changarawe kwa kiwango cha karibu kilometa moja kwa milioni 15 au mpaka 20 nadhani bado kilometa zitakuwa chache pengine kwenye 20 na kitu tu bado. Kwa hiyo, bado sana Makao Makuu yatakuwa mbali sana na Wilaya hizo mbili. Lakini namshukuru kwa kiwango hicho ambacho kimeongezwa kwa kiasi hicho.

Mheshimiwa Spika, la kwanza nilitaka niseme hilo ambalo ndilo jambo kubwa katika kuunganisha huu Mkoa wa Manyara na Wilaya zake. Kuhusu miundombinu kwenye Mji, Makao Makuu ya Mkoa wa Babati nataka nitumie nafasi hii, nashukuru Wizara ya Ujenzi kwamba walau tuliomba lile vumbi linalotimka pale Mjini Babati basi lipungue kwamba sasa zimejengwa kilometa karibu nne sasa za lami. Kwa hiyo, walau tuna kaulimi wa lami si mbaya sana lakini ni ndogo sana. Kwa hiyo, napongeza juhudi za Serikali katika kuona hilo katika kuendelea kuimarisha miundombinu katika Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Spika, vile vile kwa sababu barabara hii inayotoka Babati kwenda Okesimeti na Kibaya ni mpya. Barabara hii kwa vyovyote vile wale wanaopitiwa kwenye barabara hii watahitaji fidia. Kwa hiyo, ni vyema Serikali kwa kweli ikaharakisha kuwalipa wale ambao imewapitia kwa sababu zipo nyumba ambazo sasa zimezingirwa katika maeneo haya haya ambayo yanafanyiwa matengenezo ya kilometa 17.

Mheshimiwa Spika, sipendi kuongeza mengine ila Mheshimiwa Paschal Degera, amelizungumzia suala la barabara ambayo kwa kweli ni barabara muhimu sana kwenye historia ya nchi yetu na katika Afrika barabara hii ambayo inaitwa *The North Great Road* kutoka sehemu inayotoka Minjingu kwenda mpaka Iringa. *(Makofi)*

Naomba kusisitiza tu kwamba sasa tumekwishaona upembuzi yakinifu kwa muda mwingi sana. Katika miaka ya 1980 alikuwepo Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mustafa Nyang'anyi, wakati ule barabara hii ilifanyiwa upembuzi yakinifu na kama nakumbuka vizuri nadhani ilikuwa Serikali ya Italia. Lakini barabara ile baadaye ilipindapinda na hatimaye ikaachwa na ni barabara hiyo hiyo ya upembuzi yakinifu.

Kwa hiyo, barabara hii ina historia kubwa sana na kipande hiki ndicho kipande pekee katika Afrika barabara ambayo inatoka Cairo mpaka huko *Capetown* ni kipande ambacho hakina lami. Kwa hiyo, inapunguza sifa ya Tanzania na barabara hii kwa kweli ingeweza kusaidia katika kuongeza shughuli za utalii katika ukanda huu wote wa Afrika. Ingeweza kuunganisha Makao yetu Makuu hapa Dodoma na Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yaani Arusha. Kwa hiyo, tunaomba jambo hilo lisisitizwe na tawi lake kubwa barabara vile vile ni kutoka Minjingu, Babati kwenda Singida. Nimeona fedha zilizotengwa hapa kwenye hatua ya upembuzi yakinifu ni zaidi kidogo si mbaya. Lakini tunaomba juhudi hizi ziongezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapounganisha barabara ya karibu Mikoa mitatu, minne, kwa kweli unaunganisha nchi, siyo Mikoa hadi Mikoa tunaunganisha nchi. Kwa hiyo, ni vizuri sana jambo hilo likaangaliwa sana. Barabara hii ya katikati imesahauliwa kwa muda mrefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka niseme hayo na kwa hayo basi, nakushukuru na naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi ya kuchangia kwenye hoja hii ya hotuba ya Waziri wa Ujenzi ambayo ni muhimu sana. Kwanza kabla sijachangia na mimi naomba nitoe rambirambi zangu kwa kifo cha Mheshimiwa Margareth Bwana, Mbunge mwenzetu. Naomba roho ya marehemu ikae mahali pema Peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, kabla sijachangia naomba nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Waziri wa Ujenzi pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu pamoja na wataalam wake kwa jinsi ambavyo wanafanya kazi nzuri kwenye Wizara hii. Mimi nawapongeza kwa dhati sana. Kwa sababu kazi wanayoifanya inaonekana iko wazi. Ukisoma hiki kitabu kimesheheni masuala yote ya msingi na utekelezaji wa shughuli ambazo kwa kweli ni za msingi na za muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukizungumzia barabara ni kwamba umezungumzia mishipa ya mwili wa binadamu kwa sababu barabara ndiyo kiungo kinachofanya shughuli zote katika kuimarisha uchumi wa nchi yetu. Kwa hiyo, nawapongeza kwa dhati kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitoe pongezi za dhati kabisa na za kipekee kwa niaba ya wananchi wa Korogwe na wamenituma niseme hilo, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Katibu Mkuu na viongozi wote wa Wizara kwa kazi nzuri wametufanyia pale Korogwe, wale ambao wanajua Korogwe pana kilometa mbili na nusu lami kutoka *Old Korogwe* kwenda *Railway Station* kutoka *Korogwe Girls* kwenda *Railway Station* pana lami ya kilometa mbili na nusu. Mji ule ulikuwa unakufa maana ukizungumza Korogwe ni *Old Korogwe* lakini leo umefufuka kwa sababu pana lami. Naomba niipongeze Wizara kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nakuomba kabla hujamaliza muda wako basi angalau upite pale Korogwe unisaidie kufungua ile barabara ili angalau wananchi waone kwamba ni kitu kizuri kimefanyika pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo naomba nipongeze kwa kazi nzuri pia inayofanywa na Meneja wetu wa Mkoa wa Tanga wa *TANROAD,* ndugu yangu Ako, kwa kweli ana ushirikiano mzuri sana na Waheshimiwa Wabunge na anafanya kazi nzuri. Naomba nimpongeze kwa dhati kabisa kwa kazi nzuri ambayo anaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hilo wazi, juzi kulikuwa kuna daraja moja, kuna kijiji kimoja kinaitwa Rwengera, daraja lilikuwa limebomoka, lakini baada ya mawasiliano ya muda mfupi daraja hilo limetengenezwa. Sasa hivi wananchi wanapita bila taabu yoyote. Sikutaka nizungumze mengi lakini naomba nichangie tu mchango wangu kwa machache ambayo nimekuwa nayo, kubwa la kwanza kabisa niungane na Mheshimiwa Shaweji, kwamba Mheshimiwa Waziri kuna barabara ya msingi sana huwa unaizungumza mara kwa mara ni barabara ya kutoka Korogwe-Handeni-Turiani-Mvomero.

Mheshimiwa Spika, inazungumzwa kwa maneno, lakini nadhani ni barabara ambayo ingesaidia sana uchumi na ni barabara pia ambayo ingeweza kuokoa kama

barabara inatokea tatizo kwenye Mto Wami huku basi barabara ile ingeweza kuokoa usafiri na ni barabara ya kiuchumi na ingetusaidia sana. Kwa sababu inapita, inaambaa ambaa kwenye Mlima huku na kuna mazao mengi sana. Naomba ifikiriwe katika utaratibu ili iweze kutengenezwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo naomba nilizungumze ni kwamba katika Kikao chetu cha *Road Board* ya Mkoa wa Tanga, kuna baadhi ya barabara tumezishauri zipandishwe daraja na nadhani si kwa Mkoa wa Tanga tunadhani kwa Mikoa yote. Tumekuwa tukizungumza mara kwa mara hata hapa Bungeni.

Ningeomba Wizara basi ifikirie barabara hizo zipandishwe daraja. Kwa sababu Halmashauri uwezo hawana wa kuzitengeneza na ni barabara ambazo ni muhimu sana zina mazao, zinasaidia sana wananchi. Kwa hiyo, ningependekeza na ningeshauri kwamba zoezi hilo lingefanyika hata kama siyo barabara nyingi, lakini basi zingekuwa zinapunguzwa moja baada ya moja ili angalau ziwe zinatengenezwa kwa ufanisi zaidi.

Kuna barabara ambayo mimi huwa nimekuwa nikiizungumza mara kwa mara ni barabara ya kutoka Korogwe kwenda Magoma-Mashewa, Kwetonge unakwenda mpaka Kizara unatokea Amani, unatokea Muheza. Hiyo ni barabara nzuri na ni barabara ya kiuchumi ina mazao mengi. Tumeipendekeza muda mrefu sana ingeweza kupandishwa daraja. Lakini ni muda mrefu haijashughulikiwa. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri utakapopitia hizi barabara basi usiisahau hiyo kwa sababu ni barabara mojawapo muhimu sana sana katika uchumi wa eneo hasa la Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo naomba nilizungimzie ni kwamba Mji wa Korogwe kama alivyozungumza ndugu yangu Omar Kwaangw', ni Miji ambayo imepata hadhi ya kuwa Miji. Unapokuwa Mji ukiwa na barabara za ajabu ajabu haifanani fanani na kuwa Mji.

Mheshimiwa Spika, nakuomba kwamba katika kufikiria hii Miji ambayo ni mipya kama Babati, Korogwe na Kibaha basi ingepatiwa mafungu maalum ya miundombinu hasa ya barabara ili miji hiyo ifananefanane na Miji inayolingana, kulikoni kuiachia kama ilivyo. Hilo nilikuwa naomba.

Mhehsimiwa Spika, halafu lingine ambalo naomba kwa dhati kabisa nipongeze Wizara hii ule ukurasa wa tisa kazi ambayo wameifanya ukipita kutoka Chalinze kuja mpaka Morogoro wangefanya hivyo miaka yote hili tatizo la watu wanaokaa kwenye hifadhi ya barabara lisingetokea. Kuimarisha juhudi za kulinda maeneo ya hifadhi ya barabara kwa kuweka mawe ya mipaka kwa kila eneo. Ukitoka Chalinze sasa kuja Morogoro unakuta kulia na kushoto eneo lile la barabara limewekwa alama. Hii ingefanyika miaka yote tusingekuwa na taabu ya kuondoa watu sasa. Nawapongeza kwa dhati kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ingefanywa kwa nchi nzima, kwa sababu binadamu mahali ambapo anaambiwa asifanye, anafanya. Sasa unapoweka tangazo ni ishara ya kumkumbusha, Wizara imelikumbuka hilo na wamelifanyia kazi. Kwa kweli

nawapongeza kwa dhati. Basi fanyeni hivyo kwa nchi nzima ili tusipate taabu ya kuwaondoa watu. Nimefarijika sana kwa kitendo hicho ambacho mmekifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo naomba niwapongeze ni kazi yenu nzuri ambayo mmeifanya ya kupunguza tatizo la kuzidisha mizigo ya magari kutoka kiwango cha asilimia 40 mpaka kufikia asilimia 7. Ni kazi kubwa sana imefanyika. Naomba muendelee kwa sababu barabara zetu nyingi zinaharibika kwa sababu hiyo. Kwa sababu mizigo mikubwa na magari yanakuwa na mizigo mikubwa yanaharibu barabara zetu na matokeo baada ya muda barabara inakuwa haipitiki kabisa. Lakini kwa kweli mmejitahidi na mimi naomba muongeze juhudi hiyo kwa barabara zote. Ni suala gumu kwa sababu unaweza mtu akapima kwenye mizani anasogea mbele akifika tena anaongeza mizigo, akifika huko mbele imezidi. Hilo tumelipata mara nyingi na watu wanalalamika lakini kwa kweli ni suala ambalo naomba nilipongeze kwa dhati kabisa kwa jinsi ambavyo mnalishughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo naomba nitoe ushauri ni suala la Makandarasi. Juhudi kubwa inafanywa, lakini fedha nyingi sana zinapotea kwa utengenezaji wa barabara mbovu, makandarasi wanakuwa siyo waaminifu, pale mahali ambapo wanapewa wanaambiwa watengeneze kwa kiwango fulani kunakuwa na udanganyifu. Sasa sijui Wizara itajielekeza vipi katika kutatua tatizo hili lakini hilo nalo ni tatizo. Niombe Wizara ifanye utaratibu wa namna ya kuwabana hawa makandarasi anapopewa *tender* hasa katika Halmashauri zetu tunapata matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, barabara zetu za Halmashauri zinatengenezwa kwa kiwango cha chini sana, mahali ambapo mtu amewekwa anaambiwa aweke changarawe kilometa 5 anaweka kilometa mbili, kinakuwa ni tofauti kabisa na utaratibu. Natoa mfano hai kabisa iko barabara yangu moja ni mpya kabisa inatoka katika Kata ya Kwagunda inakwenda Kijiji cha Ubiri ni juu mlimani. Ni barabara mpya kabisa hiyo, lakini ukiambiwa imetengenezwa na mkandarasi huwezi ukaamini kabisa na wananchi wanalalamika.

Mheshimiwa Spika, niombe tu Wizara yetu hii itusaidie kwa sababu humu ndani mna namna ya kucheki makandarasi muone watu kama hawa hata kama ninyi hamfiki chini huko lakini ninyi ndio wataalam wetu tunaowategemea muweze kusaidia namna gani tunaweza kuwabana makandarasi wa nchi hii ili angalau waweze kututengenezea barabara nzuri. Yako malalamiko mengi sana katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nilikuwa naomba nitoe ushauri ni hizi barabara. Iko barabara ambayo mimi naomba niizungumzie. Ni barabara hizi za Mikoa. Iko barabara yangu ya kutoka Korogwe kwenda Magoma, Magoma kwenda Mashewa, Mashewa mpaka unafika Maramba, Maramba mpaka Mabukwenyi. Tunaingiliana na Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, ni barabara moja hii. Lakini ndiyo uti unaopita katikati ya Jimbo langu la Korogwe Mashariki na inakwenda mpaka eneo la Mkinga. Ni barabara muhimu sana. Lakini ina matatizo makubwa kuna maeneo ambayo mvua zinaponyesha basi hayapitiki.

Naishukuru Wizara kwa dhati kabisa eneo la Forofofo walitoa fedha za makusudi kabisa karibuni milioni 100 na ikatengenezwa. Lakini eneo lile bado ni bovu na zilikuwa

zitengwe milioni zingine 100 katika Kikao cha *Road Board* tuliambiwa hivyo. Lakini mpaka leo bado. Matokeo yake kuna daraja la Songea-Magoma bado halijakwisha na eneo la Foroforo nalo bado lina utata.

Mheshimiwa Spika, ukifika kuna baadhi ya maeneo korofi hayajatengenezwa. Nimwombe tu Mheshimiwa Waziri alioine hilo kwa sababu barabara hiyo ina *cut across* karibuni Kata 18 ukichukua za kwangu mimi pamoja na Kata za Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, inaungana na barabara inayokwenda Mombasa ni barabara muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, hata katika programu ya kuondoa umaskini kulikuwa na minong'ono labda unaweza ukalijibu Mheshimiwa Waziri kwamba hiyo barabara ilikuwa imeingizwa kwenye programu ya kuondoa umaskini iwekwe lami. Sasa sijui imeishia wapi. Lakini ni barabara muhimu kweli kweli ambayo ingeweza lipatiwa uwezo huo.

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu lingine kwamba ziko ahadi ndogo ndogo za kuweka matuta Hale. Hale pale wamekufa watoto zaidi ya 12. Kila mwaka tunapoteza watoto pale, nakumbuka siku moja Mheshimiwa Waziri ulisema kwamba huwezi kuweka matuta tena. Lakini kuna maeneo mengine hayaepukiki, madereva wetu hawa pamoja na kwamba upite *speed 30* wao wanakwenda *speed* wanayoitaka wao. Kwa hiyo, nilikuwa naomba matuta maeneo hayo yawekwe ili angalau kuepusha maisha ya wananchi hao.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii, naipongeza na tuendelee kushusha fedha kwenda vijijini ili barabara za vijiji nazo ziwe nzuri kama ambavyo juhudi zinavyofanyika katika barabara za *trunk roads* na za Mikoa sasa ziende vijijini ili wananchi kule mazao yaweze kupelekwa sokoni na kufika maeneo yanayohusika kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo nashukuru kwa kunipatia nafasi na naunga mkono hoja hii asilimia mia moja. Ahsanteni. *(Makofi)*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nitoe machache kuhusu Wizara yetu hii ya Ujenzi.

Kwanza naomba nitoe pole kwa wenzetu wa Mkoa wa Rukwa pamoja na Musoma kwa kufiwa na kipenzi chetu Mheshimiwa Margreth Bwana, kifo kilichotokea hivi majuzi tu na naomba Mwenyezi Mungu aiweke mahala pema peponi roho ya marehemu. *Amin.*

Pili nataka kutoa pongezi za dhati kabisa, kwa sababu mara kwa mara, nilipokuwa naizungumzia Wizara ya Ujenzi nilikuwa nazungumza kwa sauti ya ukali kidogo, lakini leo nazungumza kwa raha na furaha kubwa na kicheko tu kwamba Wizara hii ndio inayoonyesha mafanikio makubwa ya awamu ya tatu na hasa katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Katika awamu hii ya tatu na kwa mantiki ya askari wa miavuli, basi mfano wa kuigwa wa askari wa mwavuli ambaye ameteremka ardhini ni Mheshimiwa John Pombe Magufuli ambaye yuko ardhini, anaonyesha jinsi anavyotekeleza vitu vyake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapo hapo pia nimpongeze Naibu Waziri Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, ambaye tunaweza kumwita ni mpiga debe wa huyu askari wa miavuli ambaye ameteremka na mwisho Katibu Mkuu *Engineer* wa kutukuka John Kijazi ambaye naye amefanya kazi kubwa ya usimamizi wa shughuli mbalimbali za ujenzi katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mwanzoni kwamba tunajivunia kwamba Ilani ya Uchaguzi ya CCM utekelezaji wake uonekane zaidi kutokana na mafanikio makubwa Wizara ya Ujenzi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wengi wanaonekana wamefanya kazi kubwa katika awamu hii ya tatu kutokana na mafanikio ya Wizara ya Ujenzi. Wakati wa kuchagia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha nilisema mgema tembo ukimsifia sana basi tembo lake linatiwa maji na katika hili ukiangalia Wizara ya Ujenzi, Waziri anajitahidi sana lakini kuna dalili sasa hivi kwamba tembo linatiwa maji na linatiwa maji kutokana na ubadhirifu mkubwa ulioripotiwa na magazeti mbalimbali kutokana na ripoti ya ukaguzi ya Wizara ya Fedha, kwamba tumepoteza kiasi cha shilingi bilioni 560 kutokana na ubadhirifu uliofanywa na watumishi mbalimbali wasio waaminifu, katika programu hii kubwa ya ujenzi wa barabara. Suala hili limeonekana katika ujenzi wa barabara za Mingoyo kuja Nangurupulu, Nangurukulu kwenda mpaka Somanga, imeripotiwa kuwa kuna kiasi kikubwa cha fedha kinaonekana kimepotea. Sasa ningeomba Waziri udhibiti hali hii ili hawa wenye nia mbaya ya kuharibu sifa nzuri Wizara ya Ujenzi wachukuliwe hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, ningependa sasa kuzungumzia juu ya madaraja ambayo kwa bahati mbaya yalikumbwa na mafuriko mwaka 1990 hasa katika maeneo ya kule Kusini. Kwa bahati mbaya kutoka Mnazi Mmoja au Mingoyo kwenda Masasi kuna madaraja karibu tisa yalikuwa yamezolewa na mengi mpaka sasa hivi hayajarudishiwa katika hadhi. Wakati umefika sasa wa kuonyesha kwa dhati ni jinsi gani tutarudisha miundombinu katika Mto wa Nangoo. Kuna hili daraja lilibomolewa na kwa muda mrefu wa miaka zaidi ya kumi halijarudishiwa miundombinu yake naamini katika bajeti yako hii utaangalia jinsi gani sehemu hii inaweza kutengenezwa ili wananchi waweze kupita sawa sawa.

Katika sehemu za Chipite kwa bahati mbaya Serikali imejaribu kufanya ukarabati mkubwa wa bonde lile lakini mimi si *engineer,* makalvati waliyotumia ni madogo madogo na tayari mvua zilizopita zilileta mchanga mwingi kiasi kwamba katika makalavati yale sasa inakuwa vigumu hata mtoto mdogo wa kutambaa hawezi kupita. Sasa kama mtoto mdogo wa kutambaa hawezi kupita pale, je, wakati yanavyoteremka yale mawe na michanga ile mingi si itaziba kabisa.

Kwa hiyo, naomba suala hili uchunguze upya na Mkuu wa *TANROADS* aweze kuangalia vizuri. Sisi tulikuwa tumefikiri kwamba kama kungekuwa na makalvati makubwa, bila shaka yangeweza kupitisha mchanga na takataka nyingine zote, lakini kwa sababu makalvati yale ni madogo yanaleta shida kiasi kwamba baadaye itabidi kujenga daraja upya, hebu angalieni mambo haya.

Mheshimiwa Spika, sasa nikitaka kuja kwenye suala la *Mtwara Corridor*, *Mtwara Corridor* wenzetu wa Wizara ya Ujenzi wamefanya kazi kubwa hasa katika ujenzi wa miundombinu. Kwa hilo sisi tunaotoka mikoa ya Kusini hatuna matatizo yoyote, lakini tulitaka kuonyesha wasiwasi wetu, kwamba inawezekana sasa Wizara ya Ujenzi inazidiwa kazi kwa sababu ya kazi za ujenzi za miundombinu. Tunashauri *Mtwara Corridor* ijengewe *Secretariat* yake ili iweze kuendeleza shughuli zingine. Kwa mfano utalii, utalii baada ya kujenga hizi barabara tulitaka uendelee kwa kasi kubwa, lakini unashindwa kuendelea kwa sababu hakuna mtu wa kusukuma, tungekuwa na *Secretariat* tuna uhakika suala la utalii sasa hivi lingekuwa limeshughulikiwa kikamilifu, tungeona mahoteli makubwa makubwa yanaanza, fukwe zetu zilizoko Mtwara na Lindi zinatumika na kadhalika.

Suala la umwagiliaji pia nalo ni muhimu lakini hakuna yeyote sasa hivi anayelifuatilia kwa sababu hatuna *secretariat* ya aina hiyo, kwa hiyo, kuna haja kubwa ya kuhakikisha kwamba masuala haya yanahakikiwa vizuri. Halafu kuna suala lingine katika *Mtwara Corridor* juu ya matumizi ya *gas* ambayo inachimbuliwa kutoka *Mnazi Bay* lakini *gas* hii ni nyingi kama walivyotuambia wataalamu *gas* itatoka kiasi cha 67.5 za ujazo ambazo sisi tunaweza kutumia kiasi cha 18.3 za ujazo. Sasa kuna kiasi kikubwa cha *gas* ambacho hakitatumika, tungeomba hii *secretariat* ione jinsi gani *gas* hiyo inaweza kutumika katika kutengeneza vitu vya *plastic* na mambo mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naona kuna haja kubwa sana sana ya kuwa na *secretariat* sasa ya kuangalia suala zima la *Mtwara Corridor.*

Mwisho nililotaka kuzungumzia linahusu suala la upembuzi yakinifu katika hotuba yako ukurasa wa 22 umesema kuhusu barabara ya Mtwara-Masasi-Songea-*Mbambabay* upembuzi yakinifu umekamilika na matokeo haya yatatumika katika kuanza kazi za kina za upembuzi yakinifu. Sasa mimi pamoja na wananchi wa kule Kusini tunajiuliza maana yake hasa unataka kufanya nini, hivi ujenzi utaanza lini? Tungependa kuambiwa ujenzi wa barabara hii muhimu utaanza mwezi Oktoba au utaanza mwezi Desemba.

Hii habari ya kusema upembuzi yakinifu, yakinifu mimi nafikiri hii sasa inaanza kuchosha watu wengi, wananchi wengi hawaelewi sasa tunaomba wakati unajibu hebu tupe matumaini kwamba tarehe fulani kazi ya ujenzi wa barabara hii toka Masasi mpaka Songea mpaka *Mbambabay* itaanza tarehe fulani hilo ndilo litakalo tufuraisha na kutupa faraja zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza haya naomba tena kushukuru kwa dhati kwamba nimeweza kuchangia katika hotuba hii muhimu na nawatakia kila la heri huyu askari wa miavuli arudi tena na Naibu wake arudi tena na Katibu Mkuu wake azidi kukomaa katika kuongoza hii Wizara nyeti asante sana. *(Makofi)*

**MHE. EDWARD N. NDEKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika hotuba ya Waziri wa Ujenzi, lakini kabla ya kufanya hivyo naomba niungane na Wabunge wenzangu kutoa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Kigoma Kusini, salaam za rambirambi kufuatia kifo cha Mheshimiwa Margareth

Bwana, Mbunge wa Viti Maalum na pia Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mbunge wa Kilombero, ambao tulikuwa nao na sasa wametutangulia mbele ya haki, naomba Mungu Mwenyezi, mwenye rehema aziweke roho za marehemu hawa mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, napenda kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Naibu wake na wataalamu wote katika Wizara hii kwa kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu hotuba yenye kina ambayo inajieleza kwa uwazi sana katika sekta hii, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ziara aliyoifanya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi mwaka jana Mkoani Kigoma na hususani katika Jimbo la Kigoma Kusini Kata ya Ilagala ilikuwa ni ya aina yake. Mheshimiwa Waziri aliandamana na timu kubwa kabisa ya wataalamu katika Wizara yake akiwemo Mkurugenzi Ndunguru wa Vivuko na Mkurugenzi Kilowoko na Maafisa wengine wa ngazi za juu katika Wizara hiyo, ulikuwa ni ujumbe mzito ambayo ulitoa hamasa kubwa kwetu wananchi wa mkoa wa Kigoma hasa ukanda wa Ziwa Tanganyika na Waziri kwa kufanya hivyo alikuwa anajibu maombi ya mara kwa mara niliyokuwa nimempatia kwamba yeye ndiye aliyekuwa anashika mpini wa kisu cha maendeleo ya mkoa wetu wa Kigoma ukanda wa Ziwa Tanganyika na kwamba yeye bila kuanza Mawaziri wengine wa Utalii, Waziri wa Biashara, Waziri wa Madini na Mawaziri wa Kilimo wasingeweza kufanya kitu kabla ya kutatua tatizo la barabara kwenda ukanda wa Ziwa Tanganyika, na kwa kufanya hivyo aliweza kutoa matamko yaliyotoa matumaini kwa watu wetu wa Kigoma Kusini. Nampongeza sana kwa kuja na ujumbe mzito wa namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono pendekezo lililotolewa na Kamati ya Miundombinu, Kamati ya Miundombinu katika maoni yao kupendekeza kuwa barabara ya Manyoni, Itigi, Kigwa, Tabora na Kigoma ipewe kipaumbele. Nawashukuru sana Kamati hii kwa kutoa tamko hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema nawashukuru kwa sababu barabara hii ni nguzo kuu ya uchumi si kwa Kigoma peke yake au Tabora lakini ni kwa nchi yetu kwa ujumla, kwa sababu barabara hii inaunganisha chumi kuu mbili uchumi katika nchi za maziwa makuu ambao wote tunafahamu kwamba ni eneo ambalo linafursa kubwa za kiuchumi ambao bado haujatumika ya kutosha. Nchi za Maziwa Makuu za Kongo, Burundi, Rwanda na hata Zambia kwa Kaskazini yake, ni Ukanda wenye fursa kubwa za kiuchumi na hata nchi za Magharibi zinaangalia eneo hilo.

Kwa hiyo, barabara hii ambayo inaunganisha nchi yetu na ukanda huo kupitia bandari ya Kigoma na pia barabara hii itaunganisha uchumi mkubwa wa Mashariki, ambao ni Uchina na nchi za Mashariki ya mbali kupitia bandari ya Dar es Salaam. Kwa hiyo, hii ni barabara ya Kimataifa na kwa maana hiyo pendekezo hili nakubaliana nalo kabisa na naomba iangaliwe katika kipaumbele cha hali juu kwa mtazamo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nyongeza kwenye hilo inatokana na kitabu hiki cha Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2004, kitabu hiki ukurasa 175 umeonyesha miji

mbalimbali ya nchi yetu na kuonyesha idadi ya mabasi ya abiria katika miji mbalimbali. Nimejaribu kufanya uchambuzi wa hili jambo nikagundua kwamba mabasi ambayo yako katika miji hii hayafanyi kazi katika miji yenyewe lakini ni mabasi yanayokwenda katika barabara kuu saba ambazo nimeziainisha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ya kwanza, ni Dar es Salaam - Arusha, ambayo ukichukua mabasi yaliyo kwenye miji inayotanda kwenye barabara hii kuna jumla ya mabasi 8,495.

Ya pili, barabara ya Dar es Salaam - Mwanza ambayo ni mabasi 7,885.

Ya tatu, ni barabara ya Dar es Salaam - Kigoma, ambayo kuna mabasi 7,709.

Ya nne, barabara ya Dar es Salaam - Sumbawanga yenye mabasi 7,650, ya tano ni Dar es Salaam - Mbeya mabasi 7,618. ya sita ni Dar es Salaam - Songea 7,219 na ya saba ni Dar es Salaam - Mtwara mabasi 6,640.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hizi njia zote ni dhahiri hiyo ya kwanza Dar es Salaam - Arusha haina tatizo ina njia nzuri, inayofuata Dar es Salaam - Mwanza, Wizara ya Mheshimiwa John Magufuli, iko mbioni kuifanya barabara hiyo iweze kuhudumia uchukuzi katika njia hii.

Mheshimiwa Spika, nyingine ambazo hazina matatizo ni barabara za Dar es Salaam - Mbeya, Dar es Salaam - Songea na Dar es Salaam - Mtwara kwa kazi inayoendelea. Ni barabara mbili tu ambazo zina matatizo, nazo ni Dar es Salaam - Kigoma na Dar es Salaam - Sumbawanga kwa kipande kile cha kutoka Tunduma kwenda hadi Sumbawanga. Hata hivyo, napata faraja kwa hotuba ya Waziri kuonyesha kwamba ile barabara ya Muhutwe hadi Sumbawanga iko katika mipango ya utekelezaji.

Lakini hii barabara ya Dar es Salaam - Kigoma jinsi ilivyoonyeshwa pale bado ina masafa marefu kwa sababu bajeti ya Mheshimiwa Waziri inaonyesha kwamba hadi mwaka 2007/2008 bado itakuwa katika utekelezaji.

Napenda nisisitize hapa kwamba umuhimu wa barabara hiyo ambayo nimeisema, hata ukiacha magari yaliyoko kwenye njia hiyo kama kigezo kimojawapo ambacho waamuzi hutumia kutoa vipaumbele kwa kujenga barabara ambayo ni *traffic.* Kwa kuwa *potential traffic* iliyo katika barabara hii kwa mujibu wa takwimu nilizozionyesha hapa ni kubwa hata kwa kukiangalia Tanzania peke yake na bila kuzungumzia malori au magari ya mizigo, magari ya makotena yanayoweza kutoka Burundi na Kongo. Barabara hiyo ikiwapo fursa kubwa ipo katika barabara hii ya Kigoma - Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nataka nimpongeze Waziri ni pale alipowezesha Mheshimiwa Rais kufanya ziara katika mkoa wetu wa Kigoma. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais alipofanya ziara katika mkoa wa Kigoma hasa kwa shabaha ya kuzindua kivuko cha *MV Ilagala.* Ziara hiyo ilihamasisha wananchi katika Ukanda huo lakini zaidi kilichohamasisha wananchi ni tamko la Mheshimiwa Rais alipoonyesha matarajio yake ya kumpitisha mgombea wa CCM kwenye hiyo barabara ya Simbo-Kalya.

Mheshimwa Spika, baada ya kuangalia fungu la pesa lililoonyeshwa katika kijitabu hiki hotuba ya Waziri nimeona ujenzi wa daraja kwenye mto Rugufu ni shilingi milioni 400 tu pamoja na barabara za kuingia kwenye daraja hilo. Nina wasiwasi kwamba kiwango hicho pengine kinaweza kisitosheleze, kwa hiyo, hapa nilikuwa namwomba Waziri aangalie ni jinsi gani anavyoweza kulifanikisha hilo na ili Mheshimiwa Rais atakapokuja kumnadi mgombea wa CCM aweze kufika angalau kwenye hilo daraja na hivyo kuwa ametimiza ahadi aliyokuwa ameitoa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nimalizie pia kwa kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kwamba alipokuwa Ilagala aligundua kwamba bajeti iliyokuwa imetengwa kwa ajili ya barabara ile Simbo-Ilagala-Kalya ilikuwa ni kidogo sana milioni 38.5. Baada ya kuona kiwango hicho ni kidogo alitoa tamko kwamba anaongeza shilingi milioni 100. Nilitarajia kwa sababu ni tamko la mwaka jana kifungu kisingebaki zile shilingi milioni 38 kwa sababu lile alilitamka mwaka jana alipokuwa amekuja Ilagala.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba zile mia moja zionekane pamoja na lile fungu la awali la shillingi milioni 38, kwa hiyo, napenda Waziri aliangalie hilo ambalo litasaidia katika kuharakisha kasi ya ujenzi wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, nirejee tena katika kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yote ya Wizara hii kwa kazi nzuri wanazozifaya kubadilisha sura ya nchi yetu na niwatakie kila la heri katika ufanisi wa Wizara yao na naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja asante. *(Makofi)*

**MHE. ESTHERINA KILASI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuungana na Waheshimiwa Wabunge kuchangia hoja hii ya Waziri wa Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kutoa rambirambi kwa ndugu, marafiki na wewe mwenyewe Spika, kwa kumpoteza ndugu yetu Mheshimiwa Margareth Bwana, kifo ambacho kimetuletea majonzi makubwa sana. Mheshimiwa Margareth ni Mwalimu, amekuwa mwalimu wa Wabunge wanawake kwa mchango wake mkubwa ambao amekuwa akiutoa hapa Bungeni, Mungu aiweke mahali pema peponi roho ya marehemu Margareth. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli sina mambo mengi sana ya kuchangia katika Wizara hii kwa furaha tu nimeona si vizuri nikakaa bila kuchangia ni vizuri kabisa Wizara hii ya Ujenzi kazi nzuri ambayo wamezifanya kwa kipindi chote hiki cha miaka mitano ambacho tumekuwa nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri na timu yake ya Wizara ya Ujenzi imekuwa ikifanya kazi nafikiri katika mikoa yote sawia, tumegawana kile ambacho tunacho kidogo kuhakikisha kila Mbunge pale anapotoa malalamiko yake anaweza kusikilizwa kwa kiwango kidogo ambacho anacho kwa hiyo, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema timu yake imekuwa ni timu mahsusi kwa sababu hata ukifika pale ofisini kwao afisa yeyote unayemkuta mtendaji yeyote unahoja, una swali kwa kweli unapokelewa vizuri bila tatizo lolote, kwa hiyo, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nilikuwa na maombi machache ya kumwomba Mheshimiwa Waziri kwamba katika yote ambayo ameyafanya Wilaya ya Mbarali kwa kweli tumekuwa na matatizo ya mawasiliano na yeye anafahamu, na barabara kongwe ambayo nimekuwa nikiisema tangu mara ya kwanza tu naingia Bunge hili na si ajabu hata Mbunge aliyepita kabla ya mimi sijaja hii barabara ya Rujewa, Madibila inatokea Mafinga.

Sasa leo nilikuwa naangalia kwenye kitabu sikutaka hata kuchangia nikasema hii rasimu imewekwa katika mpango ule ambao ameshaukamilisha kwa maana ya upembuzi yakinifu umefanyika, kila kitu kimefanyika na kitabu kimeshakamilika. Bajeti hii nilikuwa nategemea kuona mpango maalum kwamba inaanza lini kuwekwa lini kiwango cha lami, sasa baada ya kuona bajeti iliyowekwa ni kiwango kidogo sana na inasemea kutengeneza sehemu korofi. Sasa nilitaka tu Waziri wakati anafanya majumuisho aniambie mpango wa barabara hii ukoje na yeye nafikiri tuko wote naamini wananchi wake watamrudisha na Rais atamuweka kwenye nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vizuri kwa maandishi na kwa mpango mzuri na kwenye rekodi ya *Hansard* ikaonekana kwamba amepanga vipi katika Bajeti hii, je, katika huu utaratibu ambao alikubaliana na sisi wananchi wa Mbarali kabisa ametusikiliza na sisi tuone matunda ya Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kuhakikisha kwamba hii barabara inapata lami, sasa mpango wake ukoje, inaanza mwezi wa ngapi? Na kwa mpango upi? Ili wananchi hotuba yake na wakaona mpango ambao ameupanga waweze kuwatia faraja kwa sababu barabara ni muhimu sana kwa hiyo hilo niliomba kabisa Mheshimiwa Waziri alizingatie.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu pesa hizi zinazoletwa kwa wakala wa barabara watu wa *TANROAD* kwenda mkoani. Kwa kweli zimekuwa na matatizo kiwango cha pesa ni kidogo mnapokaa kwenye vikao Waheshimiwa Wabunge kila mtu anatetea kwenye Jimbo lake barabara itengenezwe tunampa kazi kubwa meneja huyu wa *TANROAD.* Unapangiwa milioni sita barabara ambayo ina kilometa 20, 30 na inahitaji changarawe, kwa hiyo na mkandarasi anapotangazwa ile gharama ya kutangaza mkandarasi na nini milioni sita na nusu unakuta sio hela na akipata hiyo kazi sana sana ataweka tu vifusi kidogo barabara inaambiwa imeshakarabatiwa. Sasa labda ingewekwa taratibu kamili labda mameneja wa *TANROAD* waeleze hali halisi ya barabara hizi za mkoa ambazo pesa yeye anazipokea na kuzisimamia kwamba zina matatizo yapi makubwa ili kila *quarter* inayokuja kule ikaelezwa labda ni milioni 50, milioni 70 itatengeneza barabara hii ili kusudi ukarabati uweze kuonekana na kuleta *impact* ya matengenezo ya barabara hiyo kuliko ile ya kumwaga vifusi au vimchanga shilingi milioni 6 zimekwenda, shilingi milioni 60 zimekwenda, hili ni pendekezo langu.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna ombi la barabara moja ya Mkoa inayotoka Ilongo - Lwiwa - *Usangu Ranch.* Hii *ranch* imebinafsishwa juzi tu na Wizara ya Maji na

Maendeleo ya Mifugo lakini baada ya kugawa vile vipande wale waliopata hiyo nafasi ya kupata hivyo vipande vya *ranch* wanashindwa kufika kuangalia hizo *ranch* ziko sehemu gani kwa sababu barabara ni mbovu. Tangu mwaka 2001 imekuwa ikipata bajeti ya shilingi milioni 12, shilingi milioni 10 kwa hiyo, inakarabatiwa tu kufika kwenye makazi ya watu lakini imeshindwa kufika sehemu hiyo ambayo uwekezaji ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara na Watendaji wake ikibidi basi popote pale wanapoweza kupata fungu wahakikishe kwamba wanaifungua njia hii ili kusudi kuwawezesha wale ambao wamepata nafasi ya kuwekeza kule waweze kuwa na moyo wa kuwekeza ili kusudi lile pori lisiendelee kuwa pori na wale wananchi wanaoishi kando kando ya njia hiyo mpaka kufika kwenye *ranch* hiyo watakuwa wameondokewa na kero hii. Naomba Mheshimiwa Waziri ufanye kila jitihada kuhakikisha kwamba fungu kidogo, ukahamisha hapa na hapa ili barabara ile iweze kufunguka mwaka huu na watu waweze kuwekeza kwenye hiyo *ranch* haraka iwezekanavyo.

Ombi lingine ni hili la barabara za kwenda kwenye Makao Makuu ya Wilaya. Nakumbuka tumekuwa tukisema hapa kwamba barabara kuu kwenda Makao Makuu ya Wilaya ziwe na lami. Sasa Mbarali mara nyingi wanaopita pale, Wilaya yangu iko kando kando ya *Iringa Road* lakini ukisema unaingia Makao Makuu ya Wilaya ya Mbarali lazima uwe kwa kweli umejiandaa kama ulikula chakula ukae kwanza pembeni utulie kwa jinsi kukoto zile zilivyo ni barabara mbaya, ni barabara chafu sana. Kuna siku nilikuwa nawakaribisha Wajumbe wa Kamati ya *PAC,* nikasema jamani tuingie kidogo ni kilometa tano tu kutoka *main road,* ilikuwa ni kazi kuingia na gari la Bunge maana yake tumetumia karibu nusu saa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri katika Mkoa wa Mbeya ni Wilaya yangu imebakia kwa kutokuwa na barabara ya lami, ni kilometa tano kutoka pale Igawa kufika Rujewa na sasa Makao Makuu imesogea kidogo angalau ni kilometa nne. Sasa nimeona wenzangu hapa wakichangia wanasema kwamba aah, tunashukuru kilometa nne zimetengenezwa, Mheshimiwa wa Ileje anasema naye kwake bado lakini tungefikiria Wilaya za Mkoa wa Mbeya sisi kwa kweli tuna hatari, Mawaziri wote ambao wametembelea pale wameona, magari yanaharibika na mtu anaona uvivu kuingia asalimie Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi inakuwa ni tatizo kwa sababu barabara haipitiki.

Naomba mlizingatie hilo kama huo mpango mwingine utachukua muda mrefu lakini angalau hizo kilometa nne zifikiriwe. Naomba hii kwa sababu ni bajeti yako ya mwisho ulitamke hili watu wa Mbarali waone kwa kweli wamefikiriwa na wewe umewazingatia.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nataka kuzungumzia kuhusu makandarasi, tuna tatizo la makandarasi pamoja na pesa zote ambazo zimekuwa zikitolewa huko. Kuna wakati mwingine mimi nafikiria kwamba haiwezekani tukawa na wakandarasi wa kudumu kwenye kila Mikoa wale ambao wana uwezo wa kujenga barabara hizi. Kwa kweli kwa Mkoa wa Mbeya tatizo kubwa ni wakandarasi sijui Mikoa mingine. Mitaji yao ni midogo, kama walipasishwa, hatufahamu kwa sababu wanapopewa kazi hizi kukamilisha au kuanza mradi wenyewe inakuwa ni tatizo mpaka apate hivyo vyombo, a-

*mobilize resources* kuja pale inachukua muda mrefu na unakuta pesa nyingi zinakaa hazitumika kwa sababu ya matatizo ya makandarasi. Sasa labda Wizara ifikirie itafanya nini kuhusu tatizo hili. Kama ni kuwaunganisha, inabidi kuwe na kitu cha kuwapa changamoto ili waweze kuunganika pamoja kwa ajili ya kupata hizi kazi na kufanya kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuchangia kwa upande wa nyumba ambazo zimejengwa. Nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kujenga nyumba hizi za wafanyakazi zikiwepo hizi hapa za Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtu ukitoka mbali unaweza ukasema kule kuna bahari ya maji au nini kwa jinsi zilivyokaa. Sasa kidogo naguswa na hili kama zitabaki hivyo hivyo au zile bati zinapakwa rangi halafu mle ndani angalau kungewekwa mitaa kuliko vile zilivyokaa na wafanyakazi kama watakaa Wizara moja tunayafahamu matatizo ya nyumba na nyumba, ya watoto na watoto. Labda niungane na Kamati ya Miundombinu mpaka mwisho utakuwaje lakini napendekeza hilo kwamba angalau ziwekewe fensi ziweze kuonyesha tofauti na angalau ziwe kwenye mtaa utaunganishaje kule kwenye nyumba mpaka kufika Dodoma Mjini na tunataka hii Dodoma ipendeze? Pia na nyumba ziwe tofauti, za maofisa ziwe kwa *grade* angalau kuliko ramani inafanana kila kitu sijajua mpango ulivyo watapewa watu wa *grade* moja au *grade* tofauti? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nilikuwa na haya ya msisitizo sana sana hizo barabara zangu ambazo nimezitaja za Wilaya ya Mbarali, hii ya kwenda Makao Makuu na hii ya Madibila. Mheshimiwa Waziri nitaomba tu utupe mpango ukoje lakini hii ya lami mpaka Makao Makuu na Wilaya nyinginezo ambazo sijajua Mheshimiwa Gideon Cheyo kama atasimama atasema, naye anaomba vile vile angalau Mbeya na sisi tuwe na barabara za kwenda Makao Makuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tumefikia mwisho wa kipindi cha asubuhi cha kikao cha leo. Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Mwenyekiti Eliachim Simpasa, wote wawili wako safarini nje ya nchi. Kwa hiyo, kwa wiki yote hii nitakuwa napokezana na Mheshimiwa Anne Makinda, katika kuongoza vikao. Kipindi cha mchana mtakuwa na Mheshimiwa Anne Makinda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06.48 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika kipindi hiki cha mchana. Nianze kwa kutoa rambirambi zangu kwa ndugu na jamaa wa Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga na Mheshimiwa Margareth Bwana, ambao ni Wabunge wenzetu ambao Mungu amewachukua siku chache zilizopita. Naomba niwaombee wapumzike kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mchango wangu mdogo katika bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi. Kwanza, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri sana aliyoifanya kwa kipindi chake cha miaka mitano akishirikiana na Mheshimiwa Naibu Waziri. Pia nichukue nafasi hii kumwombea Waziri na Naibu Waziri kwamba Mungu awajalie waweze kurudi tena Bungeni na niwaombe wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Jimbo la Biharamulo Mashariki na wananchi kwa jumla wampe kura nyingi sana Mheshimiwa John Pombe Magufuli ili tumwone katika Bunge lijalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nichangie kwa nguvu zangu zote barabara ya *Great North Road* inayojulikana kama Barabara ya Afrika Mashariki ya zamani. Barabara hii nilishaizungumzia tena kwa upande wa maswali, ni barabara ambayo ilitumika sana zamani kuunganisha Mkoa wa Tanga na Mkoa wa Kilimanjaro. Barabara hii inatokea Mkomazi inapita Bendera inapita Kijiji cha Kihurio, Ndungu inaendelea mpaka Gonja Kisiwani na inatokea Same.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii wakati sisi tukiwa wadogo ilikuwa ni barabara kubwa sana iliyokuwa inachukuwa mabasi yale ya *DMT* yakitoka Dar es Salaam kwenda Nairobi mpaka Kampala. Lakini kwa sababu mimi naishi maeneo haya sasa nizungumze kwamba hii barabara imepoteza wadhifa wa kuitwa barabara, tunapaswa kuiita njia. Barabara hii ina Kata kubwa nne ambazo zinalima mazao ya biashara na chakula. Wananchi wa Kata hizi wanalima mpunga, maharage na mahindi. Lakini naomba nizungumze kwa uchungu mkubwa kwa sababu huku ni kwetu, ndiko nilikozaliwa mimi, barabara hii imezidi kututia umaskini wananchi wa Same Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii sasa hivi hakuna gari zinazotaka kupita huku. Wananchi wanalima mpunga na mahindi lakini hawana mahali pa kuuza mpunga wao wala hawana uwezo wa kufikisha mahindi haya Tanga wala Moshi, wanabaki na mahindi nyumbani kwao. Wananchi hawa hawana uwezo wa kuuziana wenyewe kwa wenyewe kwa sababu wote ni wakulima. Kwa hiyo, barabara hii imewafanya wananchi wa Kata hizi nne pamoja na Kata za Milimani kuwa na umaskini mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba wakati nilipomwuliza swali kuhusu barabara hii aliniahidi kwamba angeandamana na mimi kwenda kuiona barabara hii. Barabara hii ni lazima aione kwa sababu kuona ni kuamini. Hakuweza kuiona kwa kipindi hiki kinachokwisha, sasa mimi naendelea kumwombea arudi ili aje aione barabara hii na aifanyie kazi. Wananchi wamekuwa maskini na sasa nikubali kwamba wanaanza kukata tamaa. Wanakata tamaa kwa sababu umaskini umewazidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie barabara nyingine. Hizi barabara ni barabara ambazo mara chache sana Serikali inafika kuziona. Same kama Wilaya ina wananchi wanaoishi Same tambarare na Same milimani, lakini Wilaya hii wananchi wanaoishi milimani ni zaidi ya asilimia sitini. Wananchi hawa ambao ni zaidi ya asilimia sitini wana hali mbaya zaidi kuliko hata wananchi wa tambarare, wanazo barabara ambazo haziwaunganishi na barabara kuu zilizoko tambarare. Hapa naomba nitoe mfano, Kata ya Mbwambo, Pareni, Vuje, Bombo, Lugulu, Mtii, Hinji, Vunha, Kirangare na Mamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata hizi zina wananchi ambao ni wachapa kazi sana, wanaishi juu ya milima mirefu mno, lakini hakuna barabara. Wananchi hawa wamekuwa kwa muda mrefu zaidi ya miaka ishirini wanatengeneza barabara kwa Msalagambo, wanatumia mikono yao wenyewe. Sasa wamefika mahali hawana uwezo tena wa kuendelea kufanya kazi ile kwa sababu kuna miamba mikubwa, kuna mawe makubwa na hawana uwezo wa kuvunja miamba hii. Niiombe Serikali kwamba iwe na jicho la huruma kwa wananchi wanaoishi milimani kwani nao wanataka watambulike na waonwe lakini Serikali haitembelei wananchi wanaoishi milimani. Hili naliongea kwa uchungu mkubwa kwa sababu wana taabu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano mmoja, asubuhi wanavuna sana ndizi, mahindi na maharage lakini mama wa kijijini kule mlimani ana uwezo kwa siku moja kubeba mkungu mmoja wa ndizi kuupeleka tambarare, mikungu mingine yote inaoza. Kwa hiyo, sasa hivi ni Serikali ndio inachangia katika umaskini wa wananchi wa milimani. Naiomba Serikali kwamba sasa umefika wakati wananchi wa milimani wapewe kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa mfano hai, mwaka 2002, nilipata nafasi ya kuandamana na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenda kutembelea Kata moja ya Same Magharibi, Kata ya Suji. Hii Kata ya Suji ipo mlimani sana, ilituchukua saa tatu kuifikia Kata hii, Kata ya Suji ipo Same Magharibi.

Tulipofika pamoja na Mheshimiwa Rais tukakaribishwa kunywa chai, tulipoingia tu mahali pa chai nakumbuka swali kubwa alilouliza Mheshimiwa Rais ni kwamba hapa tulipo ni kwa nani? Akiwa na maana Mbunge wa pale ni nani? Akajibiwa na Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa hapa ni kwangu. Akamwuliza hizi barabara zimejengwa na nani? Mheshimiwa John Singo, akamjibu tumejenga wenyewe kwa mikono yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchungu alioupata Mheshimiwa Rais alipokuwa anawahutubia wananchi, jambo la kwanza alisema kwamba mmefanya kazi vya kutosha, kuanzia sasa Serikali inachukua nafasi ya kuboresha barabara hii. *(Makofi)*

Sasa hali iliyopo Suji ambayo ilimtia uchungu Mheshimiwa Rais mpaka akatoa tamko hilo ni hali hiyo hiyo ambayo ipo kwenye Kata zaidi ya kumi na tano zilizoko milimani. Sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri ajue kwamba hawa nao wanahitaji jicho la huruma kama lile ambalo Suji walipata kutoka kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ni mtoto wetu maana yake sisi ni Wagogo. Sasa asinifikishe mahali mimi mama yake nikalia ndani ya ukumbi huu, atapata laana. Naomba sana hili jambo nilishalizungumza hapa Bungeni na nikamsihi Waziri tuandamane nafikiri alikaidi lakini sasa aache ukaidi. *(Kicheko/Makofi)*

kitu kingine ambacho ningependa Serikali ijue ni kwamba wananchi wa Same Mashariki na wananchi wa Same Magharibi hawana wimbo mwingine, wimbo wao ni Chama cha Mapinduzi tu. Kwa hiyo, Serikali ya Chama cha Mapinduzi ijue kwamba wananchi hawa wanakiheshimu Chama hiki, nao wawaangalie kwa macho ya huruma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja hii, hoja hizi nilizozungumza ndizo hoja zilizonifanya nisimame. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba nianze kwa kuwapa pole ndugu na jamaa wa Wabunge wenzetu wote waliotutangulia mbele za haki. Nawaombea waondolewe adhabu ya kaburi na moto wa *Jahanam Yaa Rabbi-l-alamiina.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwa ruhusa yako niipongeze Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Serikali ya Awamu ya Tatu kwa kweli imefanya mambo makubwa na mazuri sana hasa katika Jimbo langu, kwanza hatuamini, zahanati zote zimekarabatiwa, shule zote nzuri, maji *JICA* wapo Jimboni sasa hivi, gesi inachimbwa kule Msimbati, simu za mkononi tunaongea, barabara inapanuliwa, *VETA* tumepata yaani nikianza kuhadithia hapa muda wenyewe utakwisha. Hongera sana na tunashukuru kupita kiasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo lakini kuna mjadala unaoendelea Jimboni kwangu sasa hivi ambao haujafikia muafaka. Kundi la kwanza, wanasema bwana wewe safari hii tukusikie unatoa shilingi Bungeni kwa Wizara ya Ujenzi kama haitaeleza maneno ya kupendeza juu ya kuwekwa lami barabara ya Mtwara-Nanyamba-Tandahimba-Newala hadi Masasi. Lakini kiwango cha changarawe barabara ya Mtwara hadi Boda kule kwenye Kivuko cha kwenda Msumbiji, barabara ya Madimba-Kitaya-Mnongodi-Chikwaya, barabara ya Madimba-Msimbati, barabara ya Mpapula-Kitere, barabara ya Hiari-Dihimba-Njengwa-Nanyamba. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi la pili linasema hapana, Serikali ya Awamu ya Tatu kupitia Ujenzi imefanya mambo makubwa sana upande wetu hatutakuwa wastaarabu leo tukiitikisa Wizara hii. Kwa sababu kitendo cha kuonyesha kwamba wanajenga barabara ya Kibiti-Lindi hasa kwa kutuwekea daraja, ustaarabu huu hautaki kutikiswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunateswa, Wandengereko wametutesa sana pale, walikuwa wanasukuma kinyesi na kuchota maji kutupikia chai tunywe, utafanyaje lazima unywe. Walikuwa wanavusha wake zetu wakisema tutawarudieni nyie wanaume. Basi wake zetu wanalala kule na sisi tunalala huku, huna uhakika na mwana amelala lalaje huko, hawa Wandengereko ni watu wabaya kabisa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akinamama na watoto walidhalilika pale, waliuza bangili, saa na vitu vingi kwa sababu ya kupata chakula wakati pantoni inapoharibika pale, ilikuwa inaweza kuharibika wiki au wiki mbili na pia watu wamepoteza maisha. Lakini bwana John Magufuli, amekuwa mkombozi wetu na Mheshimiwa Benjamin Mkapa, haitapendeza ukitoa shilingi katika hili. Isipokuwa uwaombe wapiga kura wa Biharamulo Mashariki wamrudishe Mheshimiwa Magufuli hapa na ninyi wapiga kura wa Biharamulo Mashariki, wananchi wa Mtwara Vijijini wanawaomba kumrudisha Mheshimiwa John Magufuli hapa na kumwomba Mheshimiwa Jakaya Kikwete, *Inshallah* atakuwa Rais, kumrudisha bwana huyu kuwa katika Wizara ya Ujenzi au ngazi ya juu zaidi ikiwezekana. Lakini wakasema sisi tutakurudisha Namkulala ili wewe ukirudi, Mheshimiwa John Magufuli akirudi, mkae mwangalie barabara hizi katika kipindi kijacho mzifanyeje, lakini leo usitoe shilingi kwa ustaarabu aliotufanyia kipindi hiki ila ninyi mrudi, maana yake, muone barabara hii kutia lami, hii changarawe mnafanya fanyaje, mzungumze mapema kabla ya bajeti ya mwaka 2006/2007. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa *group* hili wapo wengi na kwa kuwa maneno yao ni mazuri zaidi, mimi naungana nao, kwa hiyo, leo sitatoa shilingi nakubaliana nao kwamba Mheshimiwa John Magufuli arudi na mimi nirudi *Inshallah* tukutane, tuweke mikakati ya kutengeneza barabara hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu wanayoomba barabara hizi zijengwe mabwana ninyi, barabara hizi ndizo zinazosafirisha korosho, ninyi mnajua. Lakini kingine kizuri zaidi tumepata Manispaa, sisi Mtwara tarehe 1 Julai, 2005 ni Manispaa, tumepanda daraja. Sasa haipendezi unatoka Tandahimba Wilaya ya Mtwara unakwenda kwenye Manispaa na matope. Haipendezi unatoka kwenye Manispaa ya Mtwara unakwenda kwenye Jiji la Dar es Salaam unafika na matope. Unajua ukivaa suti haipendezi kuendesha baiskeli ukainukia hivi. Haipendezi kushangaa shangaa, unauliza ovyo ovyo wakati umevaa suti na tai, kuna mambo fulani ukiwa nayo hayapendezi mambo mengine kufanyika. Ukitoka Manispaa unakwenda kwenye Jiji la Dar es Salaam hutakiwi kufika na matope, unatakiwa ukiweka mkanda nje huko huko Mtwara unaingia Dar es Salaam na mkanda nje, sio tena unakuwa na matope, unabadilisha nguo, mambo gani hayo. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba barabara hizi ziwekwe lami na zingine ziwe katika kiwango cha changarawe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya pili, hii barabara ya Mtwara-Kitaya ni barabara ya ulinzi. Hivi mkiona kuna amani hakuna uhakika kama kutakuwa na amani hivyo hivyo mpaka kiama. Inawezekana hali kubadilika, huwezi kujua mambo yote ya Mungu haya. Mheshimiwa Jakaya Kikwete alikuwa anasema wakati anaomba kura pale, kwamba toa jasho jingi sana wakati wa amani ili utoe damu kidogo sana wakati usio wa amani. Sasa madhali tuna uhusiano vizuri na Msumbiji wakati wa amani basi tutoe jasho jingi sana kwa kuitengeneza barabara ya Mtwara-Kitaya-Mnongodi mpaka kufikia Chikwaya na huku pembezoni Tandahimba-Newala mpaka Masasi ili mambo yakibadilika vijana wetu waweze kutumia barabara hizi katika ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaeleze Waheshimiwa Mawaziri hawa kwamba *deal* la kupata Uwaziri na kukaa kwenye Uwaziri kwa muda mrefu lipo Mtwara kwa kipindi hiki. Kwa ruhusa yako niwape elimu kidogo Mawaziri labda wanaweza kutumia. Unajua kuna majini fulani wanaotawala kwa muda fulani, kuna *Zuhra, Kamal* na *Mustara.* Kuna jini mmoja anatawala mahusiano ya undugu tu na ndio maana unaweza ukaona leo umechoka choka hivi, hutaki kwenda safari, baadaye ukapata habari ya msiba wa ndugu yako. Kumbe ilikuwa kuchoka choka huku ni kwa sababu ya ndugu yangu kufariki, kwa sababu yule jini alikuwa anafanya kazi hiyo bila wewe kujua. Halafu *Zuhra* anafanya kazi ya uhusiano kati ya mume na mke, kuoana, nyumba ndogo, huyu anaitwa *Zuhra. (Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huyu *Zuhra* naye ana nguvu, sasa naomba nitoe mifano ili muelewe. Mimi nimemwolea Waziri wa Fedha, yeye mwenyewe hajui lakini, Mheshimiwa Spika kaniolea mimi dada yangu. Kuna siku nimeuliza swali hapa la barabara hii ya Mtwara-Nanyamba, Naibu Waziri akasema hatuna hela kabisa, akagomba hatuna hela. Yule jini mahaba akamwingia Mheshimiwa Waziri wa Fedha, aliposimama Waziri wa Fedha, alitoa hotuba bila kujua, akasema nani anayesema nchi hii haina fedha, mimi mwenyewe nilikwenda nje kuomba fedha, mamilioni haya, mamilioni haya, akataja na *Mtwara Corridor* bilioni kumi na moja bila kujijua kwamba anampinga Waziri mwenzake, yule ni jini mahaba wa mimi kuoa kwake. Lakini kengele ikalia inamkataza Mheshimiwa Waziri kuendelea, basi jini mahaba akamvaa Spika kwa sababu ni shemeji yetu, akamwambia endelea usijali kengele hiyo, kengele hakuijali ndio hii. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaambia Waheshimiwa Mawaziri *deal* lipo Mtwara. Habari hizi wanajua Wachaga na sisi Wamakonde, maana Wachaga walikaa wakasema Mkapa huyu alivyo huyu anaweza kuwa kifaa hapo baadaye, wakampa dada yao. Nasi tukawajibu kwamba Jakaya Kikwete, anaweza kuwa kifaa baadaye hapo, tukamchomekea dada yetu, tuna akili sisi. Sasa nakuelezeni *deal* lipo Mtwara na Lindi. Mnaweza kupoteza Uwaziri bila kujua, bila kukusudia, lakini huyu jini mahaba anafanya kazi, ukiibugudhi Mtwara na Lindi kwa kipindi hiki utakwenda na maji. Waziri wa Maji amelijua hilo *JICA* wapo Mtwara, Waziri wa TAMISEMI amelijua hilo, juzi ametoa Manispaa.

Kwa hiyo, Mawaziri wote fuateni mlolongo huo huo, Mtwara na Lindi *deal* liko huko, mtakosa Uwaziri bila Rais kujua wala ninyi wenyewe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Assalam Alaykum Warahmatullah Taala Wabarakatu. (Makofi/Kicheko)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hoja hii ya Waziri wa Ujenzi. Kwanza kabisa niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutuma salaam za rambirambi kwa kifo cha Mheshimiwa Margareth Bwana, tunawaombea wenzetu ambao wametutangulia mbele ya haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Naibu Waziri wa Ujenzi, Katibu Mkuu pamoja na wataalam wote wa Wizara hii.

Wanafanya kazi nzuri na tunaiona, tatizo kubwa ni ufinyu wa bajeti. Kwa bajeti ya mwaka 2005/2006, fedha ambazo zimetengwa, fedha za ndani ni bilioni 141 na fedha za nje ni 129 bilioni. Fedha hizi ni kidogo sana kutengeneza barabara zetu, barabara kuu, barabara za Mkoa pamoja na barabara za Wilayani. Kwa hiyo, Wizara ina lengo zuri la kutengeneza barabara katika nchi hii, tatizo ni ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie barabara ya Minjingu-Babati-Dodoma-Iringa. Tumeanza kuzungumzia barabara hii tangu Bunge la Karimjee Dar es Salaam mwaka 1990. Kwa hiyo, kila bajeti bado inafanyiwa usanifu, upembuzi yakinifu.

Sasa upembuzi yakinifu na usanifu zaidi ya miaka kumi na tano, hatuelewi. Kwa watu wa kawaida tu kuwaambia tunafanya upembuzi yakinifu na usanifu miaka kumi na tano, hawakuelewi. Bajeti ya mwaka 2004, fedha zilizotengwa kwa ajili ya usanifu ni shilingi bilioni 2.4 na bajeti ya mwaka 2005/2006, zilitengwa shilingi bilioni 2.8. Kwa miaka miwili bilioni 5.2 za usanifu na upembuzi yakinifu.

Sasa wananchi hawaelewi bilioni tano zitumike kwa upembuzi yakinifu na usanifu. Sasa tunaomba Mheshimiwa Waziri atupe maelezo ya kina katika Bunge hili, ni lini barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami, hatupendi tena kuona mwaka kesho katika bajeti ya 2006/2007, upembuzi yakinifu na usanifu unaendelea, sidhani kama Bunge tutapitisha hiyo bajeti. Tunataka tuone barabara inatengenezwa. Barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu na maendeleo ya nchi yetu na ni fupi, Arusha-Dodoma-Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni barabara ya Mbande-Kongwa-Mpwapwa mpaka Mlali. Mwaka jana Wizara ilinipa matumaini kwamba barabara hii itawekwa kwenye mpango mkubwa wa matengenezo, mpango wa *HIPC,* lakini la kushangaza nimeangalia kwenye bajeti ya mwaka jana ni kilometa 16 tu.

Kwa hiyo, Mbande-Kongwa na barabara hii inaanzia Mbande-Kongwa-Mpwapwa hadi Mlali. Niwapongeze Wizara hii kwa matengenezo ambayo wamefanya katika kilomita 16, sina ugomvi na ndugu zangu wa Kongwa na mimi bahati nzuri nimeolea Kongwa. Wamefanya vizuri kutengeneza eneo lile, lakini barabara haiishii Kongwa, inakwenda mpaka Mpwapwa-Mlali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhandisi wetu wa Mkoa, Meneja wa *TANROADS* anafanya kazi nzuri. Lakini kwa sababu ya ufinyu wa bajeti hatuwezi kumlaumu. Kwa hiyo, naomba maelezo kwamba barabara hii itatengenezwa lini kwa matengenezo makubwa sio kulima na greda tu basi. Barabara hii ina umuhimu wake.

Kwanza, barabara inakwenda Makao Makuu ya Wilaya na Mji wa Mpwapwa na sio Kijiji cha Mpwapwa, Mji wa Mpwapwa. Barabara hii ni muhimu kwa sababu shule kumi na tatu za sekondari za Wilaya ya Mpwapa zinategemea barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Kituo cha Utafiti wa Mifugo ambacho hivi karibuni sherehe ya miaka mia kusherehekea huduma ya mifugo hapa nchini imefanyika katika Kituo cha Utafiti wa Mifugo Mpwapwa, lakini barabara hii ndio inayokwenda maeneo ya umwagiliaji, barabara hii ndio inakwenda mpaka Jimbo la Kibakwe. Kwa hiyo, naomba maelezo, ni lini barabara hii itawekwa kwenye mpango mkubwa wa matengenezo wa *HIPC* sio kulima na greda tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne, juzi niliuliza swali hapa kuhusu matengenezo ya daraja la Godegode. Sasa nilipewa matumaini kwamba Serikali inatafuta fedha. Lakini bado watatupiana Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, Serikali Kuu itasema hapana ni Serikali za Mitaa.

Kwa hiyo, naomba pamoja na matumaini ambayo nimepewa na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa iombe fedha kwa ajili ya matengenezo ya daraja hilo. Daraja hilo ni muhimu kwa sababu linaunganisha Majimbo mawili Jimbo la Mpwapwa na Jimbo la Kibakwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ni hili la uhaba na uduni wa vifaa vyetu vya kutengenezea barabara. Halmashauri zetu zina matatizo makubwa sana ya vifaa vya kutengenezea barabara. Serikali ingeweka mikakati kuhakikisha kwamba kila Halmashauri ya Wilaya inapewa greda moja ili tuondokane na suala ka kutegemea greda moja au mawili katika Mkoa. Najua uwezo wa Serikali ni mdogo lakini hali itakapokuwa nzuri ni vizuri tupate mitambo hii kwa ajili ya kutengeneza barabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile hili sasa ni la kwetu wananchi, barabara nyingi zinaharibika kwa sababu wananchi wanalima karibu na barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sheria zifuatwe, ipo sheria inayozuia kulima karibu na barabara, lazima kuwe na umbali fulani. Kwa hiyo, sheria za kudhibiti suala hilo ni vizuri zifuatwe na wananchi nao pamoja na kulalamika kwamba barabara zinaharibika, lakini wawe waangalifu, wasilime karibu na barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huu, nikushukuru tena na nimpongeze tena Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na wataalam wote na Katibu Mkuu. Katibu Mkuu amewahi kukaa Dodoma na alikuwa Mhandisi wetu wa Mkoa. Kwa hiyo, naomba aniangalie kwa jicho la huruma. Barabara ya kutoka Mbande-Kongwa-Mpwapwa-Mlali anaifahamu vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi jioni hii niweze kuchangia kwenye hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa msiba ambao ulitupata wiki iliyopita wa Ndugu yetu mpendwa Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana na ni juzi tulikuwa kwenye mazishi. Tunaomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenz,i kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya kwa kipindi cha miaka mitano. Lakini ni matumaini yangu mafanikio hayo yote amekuwa akiyapata kutokana na ushirikishwaji ambao amekuwa akiufanya kwa ushirikiano na Watendaji hususan Katibu Mkuu pamoja Watendaji wote walioko chini ya Wizara hii wakishirikiana na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi. Kwa kweli tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitakuwa na mengi ya kuchangia kwa sababu mengi yaliyofanywa ni mazuri. Juzi kulikuwa na swali hapa ambalo alilileta Mheshimiwa Salome Mbatia, nilimwulizia mimi na nikawa na swali la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri alinipongeza wakati akijibu swali kwa jitihada ambazo zimekuwa nikizifanya za kuweza kufuatilia masuala ambayo yalikuwa yanatoka Jimboni kwangu. Alitamka kwamba nilikuwa kero kwenye Wizara yao si kwamba alitamka kwa nia mbaya, hapana ilikuwa kwa nia nzuri tu.

Sasa na mimi kwa kudhihirisha kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri alilitamka neno hilo kwa nia nzuri, basi naomba nichukue nafasi hii kumwomba radhi sana Katibu Mkuu pamoja na Mheshimiwa Waziri kwa usumbufu ambao nilikuwa nikiufanya kwa kipindi chote cha miaka mitano katika kufuatilia masuala ya wananchi. Lakini yote hayo tulikuwa tunagombania fito lakini tulikuwa tunajenga nyumba moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nachukue nafasi hii tena kuwashukuru sana wenzetu katika Wizara hii ya Ujenzi kwa kuweza kufikia muafaka wa kuitengeneza barabara hiyo ya *Kilwa Road*. Wiki iliyopita kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, kwa kweli nilipata simu nyingi sana kutoka Jimboni kwangu hususan Kata zote zinapitiwa na barabara ya *Kilwa Road*. Walikuwa wanapongeza majibu mazuri ya Serikali kwamba tayari zimetengwa fedha nyingi na mwezi Julai, mwaka huu 2005 ujenzi huo utaanza mara moja. Kwa hiyo, nampongeza lakini pia Wizara ya Ujenzi imepongezwa na bado wanaamini kwamba kumbe kugombana kati ya Mbunge wao pamoja na Wizara ya Ujenzi ndiko kumezaa matunda hayo. Kwa kweli tunawashukuru. Naomba mzipokee pongezi hizi kutoka kwa wananchi wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mazuri hayo ambayo yatafanywa kwenye barabara ya *Kilwa Road* tunalo tatizo moja. Baada ya kubomolewa nyumba, wananchi waliokuwa kandokando ya barabara ile bado zipo sehemu ambazo zimeachwa zikisubiri angalau watu waweze kujipanga vizuri na kuangalia ni jinsi gani tutaweza kuwaondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Msikiti ambao uko pale Mtongani na ni Msikiti wa muda mrefu, waumini wa Kiislam hufanya ibada yao pale. Lakini pia inawezekana kule mbele yapo Makanisa, Shule labda na Zahanati. Sasa inapofikia ubomoaji wa aina ile, kwa kweli mimi niishukuru Serikali, huwa haifanyi vile inavyofanya katika nyumba za watu binafsi. Inajaribu kutoa muda angalau waweze kujipanga ni jinsi gani wataweza kuuondoa Msikiti, iwe Kanisa, ama Zahanati ama Shule. Kwa kweli naishukuru Wizara, imetoa nafasi ambayo ni ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza, bado waumini wanaoishi katika maeneo ya Mtoni Mtongani wanaendelea kuutumia Msikiti huo. Lakini bado kazi hii amepewa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Mfuko wa Barabara ambaye ni Mkuu wa Mkoa na yeye ameunda Kamati ya kuweza kuzungumza na wananchi wa maeneo hayo na kuangalia ni wapi wataupeleka Msikiti huo. Mmoja wa Wajumbe wa Kamati hiyo, mimi ni mojawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejitahidi kuweza kuongea na kufikiria tunafanyaje hata kama tungekwenda kwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo na Makazi tukaombe kiwanja kule Twangoma, lakini yale matarajio ya Msikiti kuwepo pale na waumini waliujenga ili uweze kuwasaidia wakazi wa pale, sasa yatakuwa hayapo. Kwa hiyo, kazi iliyopo ni kujitahidi angalau nyumba zilizopo karibu, basi tuweze kuzungumza nao angalau tuweze kutafuta kila njia ya kuwafidia ili waweze kuondoka mahali pale watafute viwanja katika sehemu nyingine ili eneo lile liweze kujengwa Msikiti. Sasa hii ni kazi kubwa, si kazi ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba kwa kuwa sisi tumeshaanza kuzungumza, basi Serikali katika mipango yake ama fedha hizo ambazo tumeambiwa zimetengwa nyingi, basi waweze kufikiria kufidia ama kutusaidia pamoja na nguvu ambazo sisi wenyewe tutajitahidi na waumini wa maeneo yale kutuongezea fedha ili tuweze kununua baadhi ya nyumba na hatimaye Msikiti ule tuuhamishe kama itakuwa ni Kanisa ama Shule ama Zahanati. Hili lilikuwa ni ombi langu kwa kweli, Wizara ya Ujenzi iweze kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala lingine. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwa jitihada zake za kushughulikia pia Vituo vya Mafuta ambavyo viko chini yake. Mimi nimepata bahati kwenye Jimbo langu Kata ya Kurasini kuna Kituo kikubwa cha Mafuta ya magari ya Serikali, kiko pale nyuma ya *BP*. Nimekuwa nikitembelea sana maeneo hayo, juzi wamefanya uboreshaji wa zile mashine za kuuzia mafuta, kwa kweli zimewekwa mashine za kisasa kweli kweli na nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwa kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa utaalamu ukikiangalia Kituo kile cha Mafuta ambacho ni cha Serikali, hususan Wizara kubwa kama ya Ujenzi jinsi kilivyo ukikilinganisha na Vituo vya Mafuta vya watu binafsi. Kwa kweli Kituo kile cha mafuta kinatia aibu. Ninasema kinatia aibu jinsi kilivyokaa, nadhani hata kama tungemwita mtaalam anayetoa vibali vya kuweka Vituo vya Mafuta na yeye atakuwa ni shahidi kwamba kinahitaji kufanyiwa ukarabati wa kutosha kabisa ukiachilia mbali zile mashine ambazo zipo pale. Paa lile limejengwa kwa vyuma, ni imara, lakini yale mabati kwa sababu ni ya muda mrefu, kwa kweli yanavuja. Sasa kama mvua zinanyesha pale na ni Kituo cha Mafuta, usalama wa Kituo kile ni mdogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupitia mchango huu, nilikuwa namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, kabla hajamaliza muda wake kwenye Wizara ya Ujenzi na mimi bado naendelea kumwombea kwa Mwenyezi Mungu katika utawala unaokuja, basi aendelee kuwepo hapo ili amalizie kazi na kwa kweli ajitahidi kukitengeneza Kituo hicho cha Mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hicho tu, toka nimekuwa Mbunge kwa miaka mitano, juzi nimefika kwa mara ya kwanza kwenye Kituo cha Mafuta cha Serikali kilichopo hapa Dodoma, kile ndiyo kibaya kabisa, hata zile mashine zake ni zile za mwaka 1947.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilipenda hili niliseme ili kuisaidia Serikali kwamba kama walikuwa wamesahau, basi waweze kutafuta fedha angalau waweze kukamilisha mazuri yale ambayo wameyafanya katika Kituo kile cha Mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nitumie Wizara ya Ujenzi kuzungumzia habari za Halmashauri yangu. Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ilikuwa ina tatizo kubwa la barabara ambayo inatoka Chang'ombe Polisi kupitia kwenye Hospitali ya Temeke, kupitia Mtaa Sudani kwenda kuunganisha barabara ya Kilwa.

Barabara ile imekuwa ni mbaya kwa muda mrefu na kwa kweli tumetumia fedha nyingi kwa kuikarabati kwa maana ya kuziba viraka. Ilikuwa ukisimama kwenye Kituo cha Sudani, uende tu hivi umesimama, basi utakuta watu wanatukana wanasema hii barabara imekuwa ya Hadija Kusaga ama Hadija kukoboa! Kwa kweli ilikuwa mbaya, ilikuwa inabatizwa majina yangu. Ninamshukuru Mungu kwamba Halmashauri imetenga fedha na sasa hivi barabara ile inatengenezwa angalau kwa kiwango cha lami nyepesi. Kwa hiyo, lile tatizo lililokuwa pale kwa ujumla limekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine, tunayo matatizo katika barabara zetu za Mitaani. Tulikuwa tunapata ugumu sana wa kuzitengeneza kama alivyozungumza Msemaji aliyemaliza, Mheshimiwa George Lubeleje, kwamba suala la kuwa na vyombo vya kufanyia kazi kwenye barabara ni muhimu sana. Sasa tulikuwa na tatizo la greda. Tulikuwa tukihitaji greda mpaka tukakodi kwenye Halmashauri nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuwajulisha wananchi wa Wilaya ya Temeke kwamba sasa Halmashauri yao ya Manispaa ya Temeke imekwishanunua greda lake jipya kabisa ambalo linafanya kazi. Kila Kata tumepanga siku mbili mbili, litakuwa linafanya kazi. Kwa hiyo, lile tatizo la barabara kuwa na mashimo linasaidia sana kupunguza uharibifu wa barabara kwa sababu tutakuwa tunawapangia kila wiki linakaa kwenye Kata moja angalau linaweza kusafisha zile barabara wakati Halmashauri yao inajiandaa kuzitengeneza kwa kiwango kinachostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona niliseme hili kwa sababu mara baada ya Chaguzi za Mitaa, ndiyo tulikuwa tumelinunua greda hilo. Kaja mjanja mmoja, bahati nzuri greda lilikuwa limepangiwa Kata ya Azimio, basi Diwani wa pale alisimama kwenye lile greda akasema mnaona Mitaa mmeipa Vyama hivi, sasa tumenunua greda. Hii ilikuwa ni propaganda ya ajabu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimeona nitumie nafasi hii kuwaeleza wananchi kwamba lile greda lilikuwa siyo la Chama kimoja ambacho mtu mmoja alikuwa anajigamba kwamba greda limenunuliwa na Halmashauri na litatembea katika Kata zote kufanya kazi hiyo. Kinachotakiwa ni kwamba upo wakati unafika Halmashauri inakuwa haina fedha za kutosha, kwa hiyo kwenye Kata wahusika huwa wanaombwa kuchangia fedha kwa ajili ya mafuta. Kwa hiyo, wasiwe na wasiwasi na wala wasifikirie ni Chama kimoja kilileta greda kwa ajili ya kutengeneza barabara mara baada ya Chaguzi za Mitaa, hapana. Ni Serikali ya CCM kupitia Halmashauri yake ndiyo imeweza kufanya mipango hiyo vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi ya kusema, mengi yamefanywa na Wizara ya Ujenzi. Naomba nichukue nafasi hii kuiunga mkono hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MHE. NJELU E.M. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, ningependa nitoe rambirambi zangu kwa kifo cha Mbunge mwenzetu, Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana, kilichotokea wiki iliyopita. Tunamwomba Mwenyezi Mungu ampe mapumziko mema Marehemu. Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John Pombe Magufuli pamoja Naibu Waziri wake na Katibu Mkuu - *Engineer* Kijazi, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika ujenzi wa barabara hapa nchini. Ukisoma katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuna eneo ambapo anaonyesha barabara ambazo zimejengwa na kukamilika. Ni barabara ni nyingi ambazo zinajengwa kwa kipindi kimoja ukilinganisha na historia yetu

ya siku za nyuma katika ujenzi wa barabara. Ni wazi kwamba katika kipindi hiki kumekuwa na mafanikio makubwa kuliko ilivyopata kutokea huko nyuma.

Hizi pongezi ziende kwanza kwa Jemadarimkuu ambaye ni Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa mwenyewe kwa kutilia mkazo suala zima la ujenzi wa barabara kama ndiyo kiungo muhimu au kichocheo muhimu cha kuleta maendeleo katika nchi yetu. Lakini pia kama nilivyosema pale awali, ni shukrani kubwa kwa Viongozi wa Wizara ya Ujenzi wakiongozwa na Mheshimiwa John Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi ningependa nizungumzie ibara ya 37(c), pale kwenye *bullet* inayozungumzia usanifu wa kina na nyaraka za zabuni za ujenzi katika ukurasa wa 38. Katika eneo hilo anaizungumzia pia barabara ya Mbeya-Chunya-Makongorosi Kilometa 115.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda hapa kwanza nianze kwa kushukuru na kupongeza kwa hatua ambayo imefikiwa kwamba barabara hii imefanyiwa *survey* ikakamilika. Imefanyiwa usanifu na kwa taarifa hii ni kwamba umekamilika na kilichobaki ni kutangaza *tender* kwa lengo la ujenzi. Mpaka hapo naipongeza sana Serikali pamoja na Wizara ya Ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mbeya kwenda Chunya mpaka Makongorosi na ndiyo barabara inayoendelea hadi kufika Tabora na Itigi kwetu sisi wakazi wa Wilaya ya Chunya ni barabara muhimu sana na ni barabara ambayo tumekuwa tukiitumia kuwasiliana na Mikoa mingine kwa miaka yote ya kuwepo kwa Wilaya ya Chunya. Ni barabara iliyojengwa tangu miaka ya 1930 nadhani ujenzi ulianza mwaka 1932, 1933, 1934 ndipo barabara hiyo ilipojengwa, lakini hadi leo barabara hiyo haina lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1997 Mheshimiwa Rais alipotembelea Wilaya ya Chunya tukaliwasilisha ombi hilo kwake kwamba barabara hiyo imekuwa ikizungumziwa, lakini bado haijapata kuwekwa kwenye programu za Serikali za kuwekewa lami; wakati ule Mheshimiwa Anna Abdallah alikuwa Waziri wa Ujenzi na Mheshimiwa John Magufuli akiwa Naibu Waziri wake. Mheshimiwa Rais alilipokea hilo na kutuahidi kwamba atalifanyia kazi. Tunashukuru kwamba baadaye lilifanyiwa kazi, barabara hiyo ikaingizwa kwenye programu za Wizara na ndiyo imefikia hapo ambapo leo tunazungumzia juu ya utangazaji wa *tender.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii inatusumbua sana wakati wa mvua, inapita juu ya milima ya Mbeya ambayo ni milima ya *volcano.* Wakati wa mvua barabara inakuwa na utelezi na pia inatitia sana. Kwa hiyo, wakati wa mvua ukiondoka kutoka Mbeya huna uhakika kama utafika Chunya au ukitoka Chunya huna uhakika kama utafika salama Mbeya na kama mvua zinanyesha unaomba usikutane na gari nyingine njiani, mkikutana na gari nyingine, basi mnabaki mnatazamana kwa sababu hakuna wa kumpisha mwenzake kwa kuogopa kwamba ukianza kwenda pembeni kidogo tu unakwenda kuzama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni jambo ambalo tunaiomba Wizara ya Ujenzi kwa kweli waipe umuhimu mkubwa sana na maadam wamefikia mahali ambapo sasa nimekuwa nikisoma hapa wametenga karibu Shilingi bilioni 10 kwa ajili ya barabara hiyo, basi naomba ile hatua iliyobaki ya kutangaza *tender* kwa kweli ifanyike haraka iwezekanavyo ili na sisi tuanze kupata matumaini ya baadaye kuwa na barabara ya uhakika ya kufika Makao Makuu ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hiyo ndiyo tunayoitumia kusafirisha tumbaku. Sisi Wilaya ya Chunya tunalima tumbaku na ni malori makubwa sana yanapita kwenye barabara hiyo kubeba tumbaku. Nashukuru *TANROADS* pale Mkoani Mbeya wanajitahidi sana kuifanyia barabara hiyo matengenezo ya mara kwa mara. Wanafanya kazi nzuri sana na niliwahi kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba kweli ninampongeza, yule *Manager* wa *TANROADS* Mkoani Mbeya kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuhudumia barabara hiyo. Naomba hizo salamu zangu na pongezi mumfikishie yule *Manager* na wataalamu wake kwa kweli wanajitahidi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wanajitahidi kuhakikisha kwamba barabara hyo inapitika, lakini ikifika msimu wa tumbaku kama hivi sasa masoko yanamalizika wanaanza kubeba tumbaku kutoka Chunya kupeleka Morogoro ambako ndiyo Makao Makuu ya hawa wanunuzi wa tumbaku. Yale malori yakianza kupita katika bararabara hiyo ile kazi yote nzuri iliyofanywa na *TANROADS* katika kipindi hicho inaharibika hapo hapo katika kipindi cha miezi mitatu, minne barabara imeshachakaa yote kabisa. Kwa hiyo, kiasi kidogo cha fedha walichopewa huwa kimeishatumika na kwa hiyo wanakuwa hawana fedha nyingine ya kuweza kuendeleza matengenezo hayo. Kwa hiyo, mnabaki mnakuwa na barabara mbaya kwa mwaka mzima tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi wakati ambapo mipango hiyo ya kuweka lami inaendelea, hizo fedha za matengenezo ya kawaida aendelee kuipatia *TANROADS* Mbeya ili hiyo barabara waendelee kuihudumia kwa kasi ile ile ambayo wanaihudumia sasa. Lakini najua wakiwa na fedha, uwezo wa kuihudumia hiyo barabara wanao, wanachokikosa mara nyingi huwa ni fedha. Kwa hiyo, naomba sana Serikali ijaribu kutusaidia katika barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini barabara hiyo kama nilivyoeleza pale awali, ndiyo inayokwenda hadi Itigi hadi Mkiwa kuunganisha na barabara ya kutoka Dodoma kwenda Tabora mpaka Mwanza. Barabara hiyo inatoka Rungwa kwenda mpaka Tabora, sasa wasipotufungulia upande wa pili kutokea Itigi napo hapo tutakuwa tumekwama kwa sababu mizigo mingine inabidi ipelekwe Kaskazini tukaunganishe na reli ya kati ili kuisafirisha ama kwenda Dar es Salaam ama kama inakwenda huko Kaskazini zaidi upande wa Ziwa, basi barabara tunayoitumia ndiyo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishawahi kuzungumza hapa kwamba hii barabara ni muhimu sana katika kuunganisha Kaskazini mwa Tanzania na Kusini mwa Tanzania hasa Kusini Nyanda za Juu, kwa sababu barabara hii ukiunganisha toka Mwanza, Shinyanga, unakuja Singida, unafika Itigi, unaipita Chunya unakwenda Mbeya na ndiyo hiyo

inaendelea mpaka Malawi na baadaye inakwenda mpaka Zambia. Kwa hiyo, ni muhimu sana barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana niliwahi kuzungumza kwenye Kamati yetu, nikasema zamani tulikuwa tunajifunza kwenye masomo, wanatuambia kwamba Wakoloni walikuwa wanajenga barabara zinatoka ndani ya nchi kwenda Pwani. Kwa sababu wao malengo yao yalikuwa ni kubeba bidhaa zetu na maliasili zetu kupeleka kwao Ulaya. Lakini inavyoelekea hadi sasa baada ya miaka 40 ya uhuru bado barabara zetu nyingi tunataka zitoke ndani huku kwenda Pwani. Barabara za kutoka Kaskazini kwenda Kusini bado hazijaanza kupewa umuhimu unaostahili. Tunashukuru juzi juzi hapa barabara ya kutoka Dar es Salaam kwenda Mtwara ndiyo imewekewa umuhimu mkubwa na daraja la Mto Rufiji nalo likajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia sasa ndiyo tukaanza kuona badiliko la barabara badala ya kuelekea Pwani sasa zimeanza hata kuelekea Kusini. Sasa msukumo ule ule ambao umejionyesha katika kujenga barabara ya kutoka Dar es Salaam kwenda Mtwara. Sasa tujenge na barabara hizi za kutoka Kaskazini kwenda Kusini Nyanda za Juu. Hii barabara ya kutoka Itigi-Chunya-Mbeya, basi tuunganishe kwenda hadi Malawi ili wafanyabiashara wanaotoka Kenya kupitia Sirari wakiingia Mwanza wakitaka kwenda Malawi, basi watapita pale Itigi, watapita Chunya, watapita Kyela na wataingia Malawi. Wakitaka kwenda Zambia, basi wataendelea kupita Tunduma na kwenda Zambia na hiyo ndiyo inafanana na barabara nyingine inayotoka Kaskazini kwenda Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ninayoizungumzia ya Mbeya- Chunya hadi Tabora ni moja katika muundo wanaouita *Mid West Corridor* na *Mid West Corridor* ni barabara hii ya Mbeya- Chunya – Rungwa- Tabora halafu Rungwa-Itigi-Mkiwa na barabara ya kutoka Ipole kwenda Mpanda na barabara zote katika *corridor* hiyo hakuna hata moja yenye lami. Kwa hiyo, barabara ambayo labda itakuwa ndiyo ya kwanza kupata lami, ni hii ya kutoka Mbeya kuingia Chunya itakuwa labda ndiyo mwanzo wa barabara hizi kujengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa muda mrefu tumeambiwa barabara ya kutoka Tabora kwenda Ipole nayo ilitakiwa ijengwe kwa lami na wakatuambia kwamba upembuzi ulishafanyika kutoka Itigi mpaka Tabora hadi Ipole. Basi barabara hizi katika ukanda huu zipewe umuhimu kama zinavyopewa umuhimu barabara katika kanda nyingine, nazo zijengwe kwa kiwango cha lami ili nasi tuweze kusukuma mbele maendeleo katika eneo hili. Eneo hili liko nyuma sana kimaendeleo na sababu mojawapo ya kuwa nyuma ni kwa sababu barabara zake ni mbaya na barabara zake ni za udongo, wakati wa mvua malori makubwa hayawezi kupita katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwa hatua hiyo ambayo wameshaifikia ya kumaliza upembuzi na kumaliza usanifu na kumaliza uandaaji wa nyaraka za kutangaza *tender,* basi hatua inayofuata ya kutangaza *tender* ifanyike haraka ili kazi iweze kuanza na hii ndiyo itakayowapa matumaini wananchi wa eneo hili kwamba sasa wanaelekea kupata barabara ya lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sikutaka kuzungumzia kitu kingine chochote, nilitaka nizungumzie hiyo barabara yangu tuipatie lami iwe ya kupitika mwaka mzima tuondokane na adha ya kukwama njiani na kulala njiani na hivyo tuingie katika maendeleo ya kisasa. Mbeya unaweza kufika kwa muda wa saa moja toka Chunya, lakini sasa hivi tunatumia masaa mawili mpaka masaa matatu kwa sababu barabara ni mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda nitumie tena nafasi hii kuipongeza Wizara ya Ujenzi kwa kazi nzuri wanayoifanya na ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi apewe hizo fedha ili na sisi tupate zile Shilingi bilioni 10 kazi iweze kuanza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge kwa kutoa rambirambi zangu kwa ndugu na watoto wa Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana kwa kifo chake na kwamba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema Peponi. Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nichukue nafasi hii katika kuchangia Wizara ya Ujenzi, kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri alizofanya katika kipindi chake chote cha miaka 10 akiwa Waziri Mkuu. Naamini ni Waziri Mkuu ambaye amekuwa ameteuliwa mfululizo na akafanya kazi kwa miaka kumi mfululizo. Kwa hiyo, ni vizuri nimpongeze kwa sababu hiki ndicho kipindi chake cha mwisho. Lakini vilevile nimtakie kila kheri kwa shughuli zake za baadaye yeye na familia yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Naibu Waziri wa Ujenzi, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi kwa kazi nzuri walizofanya katika kipindi chote cha miaka hii kumi. Kazi yao kwa kweli imekuwa ni ushahidi mkubwa na maendeleo makubwa ya uchumi wa nchi hii. Wamejitahidi kuboresha barabara na hasa lile suala la kusimamia barabara za kuunganisha Mikoa kwa Mikoa na vilevile kuzijenga katika kiwango cha lami.

Kwa hiyo, nawapongeza sana. Kwa kweli nimtakie Mheshimiwa John Magufuli kijana wangu pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri wake, Mungu awajalie warudi tena kuwa Wabunge na niwaombe wapigakura wao wawachague tena warudi katika Bunge hili ili waendeleze hii kazi nzuri waliyoifanya ya kujenga barabara za nchi hii. Nina uhakika wakirudi watafanya kazi nzuri zaidi na ikiwezekana basi wapate nafasi nyingine za juu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze kwa kuchangia hotuba ya Wizara ya Ujenzi. Tunashukuru kwamba hotuba iliyotolewa imetuonyesha ni jinsi gani Wizara hii ilivyofanya kazi na jinsi inavyojitahidi kuendelea kusimamia ujenzi wa barabara karibu zote nchini. Tunaomba waendelee hivyo. Nina uhakika katika malalamiko ya

Waheshimiwa Wabunge wengi wameyachukua na wameyafanyia kazi. Nina uhakika na haya tunayoyazungumza watayachukua na Mungu akijalia wakirudi wataendelea kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie juu ya barabara za Mikoa ambazo hutengewa fedha katika Mfuko wa *Road Fund*. Kwa upande wa barabara zetu, Mkoa wa Dodoma pengine niwapongeze au nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake wote kwa jinsi walivyosimamia barabara ambazo nyingi zimejengwa katika hatua ya changarawe. Kwa mfano nichukue barabara inayotoka Njia panda kwenda Itiso ambayo imetengenezwa vizuri pamoja na kwamba haijafikia mwisho, lakini hatua ambayo imefikia ni nzuri.

Barabara ya kutoka Kondoa Mjini kupitia Mondo mpaka Dalai nayo vile vile imetengenezwa vizuri. Vile vile baadhi ya barabara ambazo wamezitengeneza, ombi langu ni kwamba, inaonekana mkandarasi aliyepewa barabara zile amepewa eneo kubwa sana na matokeo yake ni kwamba mkandarasi yule anakwenda pole pole na inawezekana kabisa kwa jinsi anavyokwenda itafika hata kipindi cha mvua bado hajakamilisha kazi yake.

Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri ajitahidi kuwahimiza waweze kukamilisha kazi yao kwa sababu kazi yao inayofanyika ni nzuri sana. Yule mkandarasi anafaa na anafanya kazi nzuri nina uhakika na uhakika huu ni pamoja na usimamizi wa Mhandisi wetu wa Mkoa upande wa *TANROAD* kwa kweli tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Vile vile, nizungumzie juu ya barabara ambazo ziko chini ya Halmashauri. Barabara ambazo nitazitaja, baadhi zilikuwa zimetengenezwa na Mfuko wa *TASAF* na walijitahidi kwa uwezo wao kuzitengeneza barabara hizo. Sasa kwa bahati mbaya kwa sababu hawakuwa na vifaa vya kufanyia kazi, barabara hizo zimekuwa zinaharibika mapema hasa kipindi cha mvua. Barabara hizo ni kama ifuatavyo:-

Kwa mfano barabara ya kutoka hapa Njiapanda ya Chalinze kwenda Mpwapwa vile vile barabara hiyo imetengenezwa, lakini mara nyingi hata ikitengenezwa inakuwa haichukui muda. Kama ni wakati wa mvua, kwa kweli inakuwa ni mavumbi matupu na matokeo yake inaharibika haraka.

Kwa hiyo, tunaomba fedha zinazotolewa na Serikali Kuu kwenda kwenye Halmashauri ambazo asilimia 30 kwa kweli zinakuwa ni ndogo sana na matokeo yake, matengenezo haya yanakuwa hayakidhi uwezo wa kuwezesha kukaa kwa muda bila kuharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile barabara ya kutoka Gulwe – Kibakwe – Kinusi – Ipela; barabara ya kutoka Mnenia – Masange - Kisese mpaka Kikore na kupitia mpaka Bumbuta na kwenda mpaka Kwadelo na kwenda Busi na vile vile barabara ya kutoka Bugiri – Handali - *Mvumi Mission* - Mvumi Makulu; barabara ya kutoka Mpunguzi – Huzi – Manda; barabara ya kutoka Chibelela - Mwitikila mpaka Mpwayungu; barabara ya kutoka Bambala mpaka Chipanga; barabara ya kutoka

Mundemu - Kisima cha Ndege mpaka Makanda, tunaomba Serikali Kuu angalau iziangalie na kuziongezea fedha ziweze kupitika kwa uhakika na kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hizi ni muhimu sana. Kwa mfano nichukue barabara ya kutoka hapa Mpunguzi kwenda Huzi mpaka Manda ni barabara muhimu sana kwa sababu kule wananchi wengi wanalima mahindi, mazao mbalimbali ambayo kwa kweli wanahitaji barabara imara ya kuweza kuleta mazao yao hapa Mjini na kuja kuyauza.

Ukichukua barabara ya kutoka Mnenia – Masange - Kisese mpaka Kikore kwa kweli ile barabara Mheshimiwa Waziri sijui kama alipata hata muda wa kupita huko. Wala huwezi kuamini kwamba hii ni barabara ya kupita gari. Ni barabara ambayo imeshaharibika na hata ukipita kwa gari lako Mheshimiwa Waziri utaionea huruma kwa sababu makorongo yamekuwa ni mengi sana. Naomba kama kuna uwezekano basi mpate muda wakati mwingine kuzipitiapitia pamoja na kwamba Viongozi wetu wa Barabara wa Mkoa wanazijua na wanazifahamu vizuri. Lakini na nyinyi Mawaziri mkiziona itakuwa ni rahisi kuamini kwamba hii barabara kwa kweli inahitaji kusaidiwa. Barabara zote hizi nilizozitaja Mheshimiwa Waziri ni barabara ni muhimu sana kwa sisi watu wa Mkoa wa Dodoma. Kwa kweli zinahitaji msaada mkubwa na zinahitaji fedha nyingi ili ziweze kutengenezwa na kuwa barabara zinazopitika. Hili ni ombi rasmi, nakuomba kijana wangu uziangalie na uziweke katika utaratibu mzuri ambao unaweza ukaona kwamba sasa kuna haja ya kuzitengeneza. Hilo ni ombi naomba uliweke kwa sababu nina uhakika utarudi katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vile vile nizungumzie barabara ambayo kwa kweli safari hii ni vizuri kila mmoja hata kama Waheshimiwa Wabunge hampiti kwenye hiyo barabara naomba muizungumze. Barabara hii ya kutoka Minjingu, Babati, Kondoa, Dodoma - Iringa. Hatuna uhakika ni kwa nini barabara hii kila mara inawekwa pembeni. Huu upembuzi yakinifu ni vipi haukamiliki na hawa wanaopembua sijui wanapembuaje. Kwa nini hawapembui wakaangalia na upembuzi wa wenzao. Ingekuwa wanachukua upembuzi wa wenzao wanasoma. Sasa kila siku wanakuja kupembua tu, kupembua tu.

Mheshimiwa Waziri mimi nakuomba kijana wangu sasa iwe ni mwisho kusema kupembua. Tunataka tusikie maneno ya kujenga barabara hiyo. Miaka zaidi ya 10 sasa tunazungumzia barabara hiyo, inakuwaje? Au mnaionaje barabara hii? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningemwomba Mheshimiwa Waziri kwa kweli ajue hicho ni kilio kikubwa. Barabara hii ndiyo barabara ya kwanza katika nchi hii. Hizi zote zimekuja nyuma. Sasa sijui inakuwaje, barabara za nyuma zinatengenezwa hiyo iliyotangulia bado haijatengenezwa. Wote mmesoma Shule, mkisoma hiyo barabara, sasa inapembuliwa mwisho itabaki yenyewe. Mimi nikuombe sana, hebu safari hii tabia ya kupembua tuache, tufanye kazi ya kujenga hiyo barabara. Ni ombi kubwa ambalo kwa kweli mimi naomba mtusikie kilio chetu wote tunaozungumza juu ya barabara hii. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo lingine la barabara za hapa Dodoma Mjini. Tunajua barabara hizi zinahusu Manispaa ya Dodoma. Lakini nilimsikia juzi Mheshimiwa Waziri wakati anajibu swali alikuwa anasema ametembea nchi za nje nyingi, alikuwa anatafuta fedha za barabara, sasa kutafuta fedha kwa ajili ya Wilaya ya Dodoma Mjini inakuwaje? Kwa sababu barabara hizi kwa kweli nyinyi wote ni mashahidi. Nina uhakika mmejitahidi kutengeneza barabara ambazo mmetengeneza, tunashukuru sana, si kana kwamba tunawabeza, hapana.

Tunawashukuru kwa pale mlipofikia. Lakini kwa sababu huu Mji sasa hivi umeshakuwa ni Mji unaotembelewa na Viongozi wengi, unatembelewa na watu kutoka nchi za nje, kila siku wanakuja kuona Bunge hapa linavyoendelea sasa na zenyewe basi mziangalie. Hebu zitafutieni wafadhili zijengwe vizuri wakipita wajue kwamba kweli hii Dodoma ni Makao Makuu ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapopita na mavumbi yanawasumbua, inakuwa haipendezi. Lakini tunashukuru tu kwa kweli kiwango mlichojitahidi mjitahidi, lakini vile vile tuwaombe mwendelee kujitahidi hasa katika haya mambo matatu niliyoyasema. Mheshimiwa Waziri, naomba sana jitihada zako, jitihada za Wizara yako na sisi kazi yetu ni kusema hapa, maana yake tukishasema tena ndio tumeshamaliza kazi, inabaki kazi kwenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi kwa kweli sikuwa na mambo mengi ya kuchangia, uchungu wangu na maelezo yangu ni hizi barabara nilizozitaja. Ukishanijibu wakati unapomalizia hotuba yako nikajua sasa barabara ya Minjingu Iringa imewekewa fedha, nikajua kwamba barabara hizi nilizozitaja za Vijijini na zenyewe zimewekewa utaratibu mzuri na nitashukuru kusikia kwamba na barabara za Dodoma Mjini nazo zimewekewa utaratibu, kwangu mimi itakuwa ni furaha na kwa kweli hata katika zile maksi ambazo ningeweza nikapunguza angalau nusu, maana yake siwezi kupunguza nzima moja, siwezi kutoa kwako kwa sababu kazi unazozifanya nchi hii za barabara ni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kujenga nyumba kwa ajili ya watumishi ambazo amejenga kwa Mkoa wa Dodoma nyumba 350. Sasa labda hatuna uhakika na bei ambazo zitauzwa hizo nyumba. Ni vizuri tukajua na tunaomba basi bei yake ilingane na kipato cha watu ambao watazinunua nyumba hizo. Maana yake ikiwa tena bei ya juu, bahati mbaya pengine watu ambao watazinunua watapata taabu kuzilipia. Kwa hiyo, hili ni ombi kwa nyumba ambazo mnajenga bei yake angalau ifanane na kipato cha wanaozinunua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niunge mkono hoja hii mia kwa mia na niwatakie kila la kheri Waheshimiwa Wabunge wote wanaporudi Majimboni, basi Mungu awajalie wapate Ubunge warudi tena Bungeni. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. STANLEY H. KOLIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nishukuru kwa kupewa nafasi na pili nijiunge na wenzangu wengine kwa masikitiko

makubwa kutoa rambirambi kwa familia ya Mheshimiwa Margareth Bwana. Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi. *(Amin)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niipongeze Wizara hii kwa kufanya kazi yake vizuri na katika historia ya Wabunge katika Wilaya ya Ludewa mimi nimeweka rekodi kwa barabara ile maarufu kwa jina la Kandamija. Barabara ile imekaa miaka yote na mwaka juzi nilipiga kelele sana, sasa imetengenezwa. Kwa hiyo, tunawashukuru na kuwapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunawapongeza sana, sasa hivi ameniandikia ki-*note* Dr. Luoga jirani zangu pale kwa ajili ya Mto Ruhuhu tulikuwa na kivuko pale cha kuvuta kamba kama enzi za babu zetu. Sasa naona kwenye ukurasa wa sita Mheshimiwa Waziri ameweka kitu pale, ametenga fedha kwa ajili ya kununua kivuko. Kwa kweli tunampongeza Mheshimiwa Waziri kwa Mto ule, maana mwaka jana tulipata taabu sana kiasi kwamba tulivusha pale *grader* moja likadidimiza ile pantoni ambayo tulikuwa tunataka kuvusha. Ilikuwa kazi, Mwenge usingeweza kupita kwenda Ruvuma. Kwa hiyo, tunakupongeza sana. Ingawa unastahili pongezi lakini kuna matatizo madogo madogo.

Pili, labda niipongeze *TANROADS* Mkoa wa Iringa wamefanya kazi nzuri sana. Kulikuwa na mradi wa *RUSIRM* kutoka pantoni ya Mto Ruhuhu kwenda Bandari ya Manda, ulikuwa ni mradi wa *RUSIRM*. Kwa hiyo, *contractors* wa kutoka Ruvuma walitengeneza ovyo ovyo sana ile barabara. Kwa msimu mmoja wa mvua barabara yote ilipotea, sasa hivi mmetenga karibu Shilingi milioni 100 kwa ajili ya kufanya marekebisho. Kwa hiyo, nawapongeza sana watu wa *TANROADS* Iringa. Sasa naamini kwamba utaratibu huu wa kuweka Mameneja katika Mikoa umeanza kufanya kazi.

Lakini pamoja na hayo, kuna matatizo madogo madogo ambayo nataka kuyazungumzia. La kwanza sisi katika Wilaya, kwa mfano ya Ludewa tupo kando kando ya Ziwa Nyasa na tunazungukwa na milima ya Livingstone. Wenzetu upande wa Malawi wamejaribu kutengeneza barabara kutoka Kalonga hadi unafika mwisho wa ziwa. Lakini kwa upande wetu sisi, eneo zima hususan Tarafa ya Mwambao haipitiki. Sisi tulifikiri kwamba ukiwaachia watu wa Halmashauri kutengeneza barabara za namna hii hawawezi, kwa sababu zile barabara zinapita kwenye milima, tunazihitaji fedha na utaalam zaidi. Tulifikiri kwamba sasa kuwepo na mpango mkubwa wa kutengeneza barabara kuanzia Kyela kupitia Kata ya Lumbila, Makonde na Lupingu ili tuweze kupita kwa barabara moja kwa moja.

Mzungu mmoja Padri Alanus alijaribu kufanya hivyo lakini baadaye masikini alifariki. Kwa hiyo, hakuweza kukamilisha zile ndoto zake. Lakini nadhani inawezekana na kama sio hivyo, basi tupate barabara ambazo zinaweza kushuka milima ya Livingstone kwenda Mwambao. Hii *proposal* ya barabara inashindikana kwa sababu tunapewa fedha kidogo sana. Nafikiri uwe mpango mkuu wa Serikali wa ku-*promote* barabara zinazokwenda na kupita kwenye milima ya Livingstone ili na sisi kwa upande wa Tanzania paweze kufikika kwa gari sio kwa meli tu miaka yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilikuwa nafikiri kwamba iko barabara moja ambayo ilipewa msukumo kwa tamko la Rais wa nchi hii. Mheshimiwa Mkapa alipokwenda kufungua daraja moja linaitwa Lyamanzi ya kutoka Lusala kwenda Makete, barabara hii inaweza kuunganisha Ruvuma, Iringa na Mbeya. Lakini alitamka pale kwamba kwa sababu tumeanza kujenga daraja hili, basi ingekuwa barabara aidha ya Mkoa au ya Kitaifa.

Sasa tamko la Mheshimiwa Rais mpaka leo halijatimizwa. Tulipoanza kuhoji kwa nini barabara hiyo haijapandishwa hadhi, tukajibiwa, kwa vile barabara hii haipiti magari mengi, magari mengi yatatoka wapi wakati barabara yenyewe haipo. Tujenge ile barabara ya kutoka Lusala - Makete. Sisi tumekuwa jirani sana na Makete, lakini inabidi uzunguke utoke Makete, uende Njombe, kutoka Njombe ndio uje Ludewa wakati sisi ni majirani tu. Kwa hiyo, tungeomba hii barabara ipewe huo msukumo na nadhani nina swali kesho nitauliza, pengine litapata majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingine tulikuwa tunafikiri ni barabara ile ya Mkiu kwenda Madaba. Barabara hii tunashukuru sana ilikuwa kwenye mpango wa *RUSIRM* lakini mimi nilitoa maelezo hapa kwamba barabara ile watu hawafaidi sana kwa sababu ya mlima wa Gangalanzuki. Gari inayozidi tani tano haiwezi kupita kutoka Mavanga kuja Mundindi na Lugalawa. Kwa hiyo, utakuta kila siku tunavyokuwa na Mradi wa Ujenzi, tunajaribu kuweka kwenye mlima huo huo.

Kwa hiyo, gari linalopita pale ni la Mbunge na Mheshimiwa *DC* na mengine. Lakini sehemu ile ndiyo sehemu *productive* kwa ajili ya kilimo cha mazao yote. Ukisika Ludewa, basi unajua kwamba Mavanga imo, Mundindi imo, wanalima sana mahindi. Mahindi mengi yanayozungumzwa kwamba yanatoka Songea *simply* kwa sababu huna *connection* kati ya Vijiji vya Mavanga na Vijiji vingine vya Ludewa.

Kwa hiyo, wale wa Mavanga wanauzia Songea. Tungeomba pale pachepushwe sisi wenyewe tulifanya juhudi ya kuchepusha na tumeshakubaliana kwenye Bodi ya Mkoa kwamba tuchepushe. Kwa sababu licha ya ule mlima, pana korongo kubwa. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali, maombi ya Mkoa pengine Waziri atazungumza kidogo kuhusu jambo hili. Maana tulileta maombi na mimi nimewahi kuandika hata barua ya kuomba fedha na makisio yalifikia Shilingi milioni 700, lakini tukasema tunaweza kwenda kwa awamu au nusu kwanza tukaendelea halafu baadaye tukapewa nusu, si mbaya tukianza. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali ichukue jukumu hili la kutengeneza hii barabara kwa maana ya kuchepusha kupitia sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ilikuwa ni barabara ya kutoka Njombe hadi Manda kwa maana ya kupitia Ludewa na sehemu nyingine. Ulikuwa ni Mradi wa *RUSIRM*, sasa tatizo tuliloona ni kwamba mwaka huu ulikuwa ni kama mwaka wa mwisho wa mradi, barabara hizi zingetengenezwa, lakini inaonekana kwamba Serikali bado haijachangia sehemu yake. Sasa tulipouliza kwa nini haifanyiwi marekebisho yale, tukaambiwa kwamba kuna tatizo la Serikali kutochangia katika Mradi huu wa *RUSIRM*. Mradi huu ni mkubwa na kwa kweli katika Wilaya zote kwa mfano Wilaya ya Makete, Njombe, Ludewa, Mbinga linategemea sana mradi huu na kwa kweli barabara zetu zote

zimekuwa nzuri kwa sababu ya mradi huu. Lakini mradi wenyewe unaonekana sasa hivi ulikuwa ndio unafikia mwisho, lakini bado haujafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani na wewe barabara zako unazijua hizi. Sehemu ile yote ya Luponde, mle sasa hivi kuna mashimo mengi sana. Kwa hiyo, tungeomba Serikali ichukue jukumu la kutoa mchango wake kama kweli sababu ndiyo hiyo, vinginevyo pengine tuelezwa pametokea nini katika dunia ya leo hii. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ALLY A. KARAVINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi nichangie hoja iliyoko mbele yetu, hoja ya Wizara ya Ujenzi.
Lakini awali ya yote na mimi niungane na wenzangu kwa kutoa salamu za rambirambi kwa wote wale waliofiwa na Mbunge mwenzetu, wananchi wa Rukwa, Marehemu Margaret Bwana, ambaye ametutoka wiki iliyopita. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia moja kwa moja kwanza kwa kuzungumzia juu ya hii *motion* ambayo imekuwa ikizungumzwa kwenye masuala haya hizi barabara hasa *corridor,* kwamba tangu Mkoloni kwa kweli zimekuwa zinajengwa kutoka Magharibi kwenda Mashariki kwa ajili ya ku-*facilitate* Ukoloni. Ni kweli, lakini pia lazima tuji-*adapt* katika hali halisi ya sasa, tuko katika utandawazi. Utandawazi ndio Ukoloni wa leo, soko lake liko Ulaya. Tunazungumza kwenye Soko la Dunia. Kwa hiyo, *corridor* hizi itabidi bado ziondoke Magharibi kwenda Mashariki kama ilivyokuwa wakati wa Ukoloni ili kuweza kutuweka sisi kutu-*facilitate* tuwe na misingi imara ndani ya utandawazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, niseme tu kwamba barabara zetu na *corridor* zetu hizi kubwa zinazotoka Magharibi kwenda Mashariki zitatusaidia sana kupunguza gharama za kwenda kwenye soko la utandawazi la bidhaa zetu. Barabara za kutoka Kaskazini kwenda Kusini na kutoka Kusini kwenda Kaskazini zitatusaidia sana katika kuondoa umaskini. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna moja au nyingine, barabara zote hizi kwa namna zake zina umuhimu wake katika wakati tulionao. Mimi kwa sababu muda najua utakuwa mfupi, basi nianze tu kwanza kuzungumzia juu ya *definition* ya *Central Corridor*. Mimi linanikera kidogo. Kila ninapoiona *Central Corridor* ikielezwa katika nyaraka zetu hii *Central Corridor* ni kama ilivyoelezwa kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri kila inapoondoka Mashariki na kupelekea Magharibi, inapofika kwenye Kilomita 600. Hii *Central Corridor* inaanza kwenda Kaskazini inapotea kwenye u-*central corridor*. Sasa nitaeleza kwa nini linanikera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, linanikera kwa sababu moja tu. Kwa *definition* ya pili niliyotoa ya Kaskazini Kusini, ili kuondoa umaskini, mimi nali-*support* kikamilifu. Kwa tafsiri niliyotoa ya kwanza ya kupambana katika soko la utandawazi ndiyo hapo

linaponikera. Linanikera kwa sababu barabara zote ukiziangalia zinakwenda. Ukifungua kitabu cha Mheshimiwa Waziri ukurasa wa kwanza kwenye ile ramani, inaonyesha wazi kabisa barabara zote zinakwenda mahali ambapo soko la usafirishaji au soko la *transit traffi*c ni *elastic*. Linaacha kwenda mahali ambapo soko la *transit traffic* ni la *in-elastic*. Linakwenda mahali ambapo kuna *competition* tayari.

Ukiiangalia ile *corridor* ya kutoka Mombasa inakwenda moja kwa moja mpaka Uganda, mpaka kwenye mpaka wa Kongo na barabara zetu sisi tunazotoa za *Central Corridor definition* zinakwenda tena kushindana na *corridor* hiyo. Wakati tuna soko la wazi kabisa lisilokuwa na ushindani ukienda moja kwa moja Kigoma. Ndiyo maana umuhimu tunautoa wa *Central Corridor. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo ndiyo pananikera kwa sababu mimi naamini gharama ya kujenga barabara ya lami ni kubwa na ni vizuri katika *priorities* zetu tukaweka gharama kubwa ya kujenga hizi barabara kwenda kule ambapo *return*s zetu za *investments* zitarudi haraka ili tuweze sasa kupata barabara nyingine zitakazojenga barabara nyingine nzuri. Sasa ndio nataka ni-*define Central Corridor* maana yake nini? *Central Corridor* unatoka Bandari ya Dar es Salaam unakwenda kuchukua mzigo wa Maziwa Makuu Kigoma. Kwa maana ya njia fupi kufika Maziwa Makuu na njia fupi kufika kwenye soko kubwa kabisa la Kongo kupitia Bandari ya Kigoma bila ya kupitia Rwanda ambako kwa *definition* ya kiuchumi ile *transit business* yule ata-*retain* asilimia 65 ya mzigo wa kutoka Kongo, faida yake tutabaki tunapitishia *Central Corridor* kupitishia Rwanda.

Ndiyo maana yake na Rwanda sio wajinga. Ndiyo maana wamewahi haraka. Sasa hivi mimi nasema Meneja wa *Central Corridor* namshukuru sana Mheshimiwa Magufuli kwa sababu katika Mawaziri wanaosikiliza mawazo ya Wabunge, huyu kwa kweli ni *second to none,* mimi nafikiri toka uhuru. *(Makofi)*

Ndani ya miaka hii mitano tumezungumza juu ya *corridor* ume-*implement* asilimia 70 ya yale tuliyoyasema na *Central Corridor* sasa jamani ni rasmi na ina Meneja wake. Sasa mimi sitaki ndugu yangu huyu historia imwandike vibaya maana yake historia imeshamwandika vizuri mno kama Waziri wa Miundombinu wakati wa Rais wa miundombinu, awamu ya miundombinu.

Sasa ingekuwa ni vizuri zaidi kwa kweli tukaipeleka ile miundombinu ikatuletea faida *to the maximum*. Ndiyo maana nasema Mheshimiwa Magufuli, naomba marekebisho, *Central Corridor* ni kwenda Kigoma ina *branches* zake za kwenda Mwanza, *Mid-West Corridor* aliyosema ndugu yake pale, inayopita Tabora kwenda Rungwa mpaka Mbeya na inapita Tabora, Urambo, Ukumbi Siganga kupita Mpanda kwenda mpaka Kipili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivyo kwa kweli tuta-*maximize* faida zetu za soko la utandawazi na Mheshimiwa Waziri tuta-*maximize benefit* zitakuwa na *special development initiatives* katika *Central Corridor*. Nilisema hilo niliseme kwa kirefu lakini najua muda haupo. Ninayo mengi zaidi kwenye hilo, lakini nilikuwa nataka hiyo

*definition* kwa maana ya mantiki yake ya kiuchumi ieleweke vizuri, Mheshimiwa Waziri nafikiri amenielewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nizungumzie suala hili la *TANROADS* kwenda kwenye Halmashauri. Barabara zetu za Vijijini, bajeti zake sasa karibu zitazidi kiwango chochote tutakachokuwa tunaweka tunawapa Halmashauri kutujengea barabara za Vijijini katika ule mfumo wa barabara. Kwa sababu gani? Kwasababu tunazijenga za udongo, mvua zetu zikinyesha kila mwaka ni lazima uirudie tena kama unataka iwepo. Kwa hiyo, gharama itakuwa ni kiasi gani? Tutakuwa kila siku tunabajeti barabara zile zile, tunataka tuendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna mojawapo ya kutusaidia kwenda mbele ni kuipeleka *TANROADS* ikafika kabisa kwenye Halmashauri na ndiyo iwe mshauri wa barabara kwenye Halmashauri. Namna nyingine ya kulifanya hilo ni lazima Halmashauri sasa ziwe na vyombo. Zimekomaa! Halmashauri ziwe na vifaa vya ku-*repair* barabara zile tutakazokuwa tumejenga, mvua itakaponyesha mwaka ujao ziwekwe kwenye bajeti, naiweka kwenye Bajeti ya Halmashauri, vifaa vyangu navi-*repair*, vinairekebisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo tutakuwa na barabara nyingi zitaendelea kuongezeka, lakini kwa mfumo huu sasa tunaendelea kwenye *visual cycle*, tunarudi palepale tulipokuwa. Barabara inabidi zile zile uzifungue kila mwaka na fedha ni hiyo hiyo ya Wakandarasi na Wakandarasi sasa Wabunge wenzangu, kama ni Madiwani wanaelewa kabisa Wakandarasi maana yake nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina *point* ndogo nyingine, namwomba Mheshimiwa Waziri, kuna barabara ile ambayo tunajenga sasa, sio ile tunayofikiria ya lami ya C*entral Corridor* kwenda Kigoma, lakini kuna barabara inajengwa kutoka pale darajani kuja Kaliuwa mpaka Urambo ya changarawe na udongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo barabara nimekuwa naisema, imeishia katikati, *traffic density*, kubwa iko kati ya Urambo na Tabora, sio kati ya Darajani na Urambo. Sasa kumekuwa na barabara nzuri sana inayoweza kuchukuwa uzito mkubwa ya *density* kubwa ya *traffic, average daily* ndogo ndiyo pale ambapo kumekuwa na barabara nzuri. *Logical extension* yake ili sasa iweze kuchukua *average daily traffic* kubwa ya kutoka Mjini Tabora kuja kwenye barabara hiyo, kipande kile hakuna barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipata kuzungumza hili na Mheshimiwa Waziri, akanaieleza kwamba lingerekebishwa kwa maana nzima ya kubeba ule mzigo wa tumbaku unaozalishwa pale Urambo uweze kwenda Tabora na mizigo mingine ambayo ni mizito zaidi kutoka pale. Sasa naomba labda anifafanulie, nina wasiwasi isije ikashia pale Wilayani badala ya kufika Mkoani. Maana yake itakapofika Mkoani, ndiyo itakuwa ime-*make economic sense.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado mimi nataka nisisitizie suala la kuziendeleza *corridor* zilizobaki. Sasa tumepata *Mtwara Corridor* na C*entral Corridor*, bado tunahitaji Tanga, Moshi Arusha, *Musoma Corridor*. Ile suda hasi ya *lake* Natron tunamwachia

nani? Tunataka tukamilishe *Corridor* zetu ili tuweze kuvuna uchumi wa jiografia. Suala zima la uchumi wa jiografia linaeleweka, ndiyo maana tunakwenda na *corridor* hii na ndiyo maana tunajitahidi. Mheshimiwa Waziri kwa sababu yeye ndiye Msimamizi wa *Corridor* hizi, basi arekebishe ili tuweze kuvuna uchumi wa jiografia wa kisasa. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi ningemwomba Mheshimiwa Waziri aongeze nguvu tu, Mheshimiwa Waziri wewe unarudi tu wala usiwe na wasiwasi. Kwa hiyo, fanyakazi kama vile huna uchaguzi, wewe endelea tu, anza kufanya shughuli ya kuendeleza hiyo *Corridor* inayofuata sasa ya Tanga, Moshi, Arusha mpaka Musoma. Tunaitaka na yenyewe ikamilike kwa sababu kama mnavyoelewa, nchi yetu hii ni *Maritime Nation* na lazima ivune uchumi wa jiografia kikamilifu, kutoka Kaskazini mpaka Kusini *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ni lazima nikumbushe tu, kwanini mnimeitaja pia *Mid-West Corridor*? Nimeitaja *Mid-West Corridor* kwa sababu kuna kale ka-c*orridor* kakuunga Mpanda ambako kuna reli, kwa kweli sio nzuri sana lakini unaunga Mpanda kwenda kwenye *Central Corridor*. Kwa hiyo, unakuwa umeunga Bandari za Kipili na Kirando kwenye *Central Corridor*. Si cha kusahauliwa, kwa sababu pale katikati, ukikata lile Ziwa Tanganyika kule pembeni yake ndiyo kuna migodi ile ya Kilomoto, yenyewe peke yake inazalisha zaidi ya tani milioni nne za bidhaa zinazotoka Bandarini.

Sasa mimi nasema tu hilo kwa sababu najua tunapojenga hii miundombinu ya bei ghali ni lazima tuwe tumeweka akilini kwamba huko mbele kuna uchumi gani tunataka kuuvuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sasa baada ya kuyasema hayo nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Waziri kwamba mimi nina-*support* Bajeti yake asilimia mia moja na ninamwombea kila la kheri atusaidie sana kurekebisha *Central Corridor,* wajanja wasiingie katikati na kuvuna ile *surplus* yetu ambayo tunataka sisi tuipate katika kuvuna uchumi wa jiografia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE: EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami pia nitoe rambirambi zangu kwa Mbunge mwenzetu aliyetuacha juzi, Mheshimiwa Margaret Bwana. Mungu amweke mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mbeya unakuwa mara nyingine kama una mkosi. Unasifika sana kwa barabara hii ya kwenda Zambia na kwenda Malawi, kuwa imeendelea sana, ni barabara hizo tu, lakini ukiangalia pembeni, ni balaa. Hata hiyo reli ya uhuru tulidhani tumeipata, imekuwa ni balaa kwetu tena. Maana hata Vituo vile tulivyotegemea vingetusaidia kusafirisha hata mizigo na vyakula mbalimbali haifanyi kazi, havipo vimesimama na bahati mbaya sana, kwa kuona hivyo, Mbeya ilivyo imeambukiza na mkosi huu kwa Rukwa tunaopakana nao.

Maana njia fupi sana ya kutoka sehemu za Kalambo kuja Mbeya ni kupitia Kamsamba, lakini njia hiyo haipitiki kabisa na huko ndiko kwenye mifugo na ndiko kwenye uvuvi (Ziwa Rukwa). Yaani sasa njia haipitiki, kwa hiyo, ni ngumu sana kutegemea kwamba Mbeya ingeweza kuchangia uchumi wa nchi hii kama inavyofanya. Wananchi wa Mbeya wana sifa moja ya uzalishaji. Ni wafanyakazi wenye uwezo mkubwa na mbaya hatuna tatizo la njaa. Balaa tu inatupata kwenye sehemu ile ya Mbarali, sijui bonde hili tuligusana na nani mwenye mkosi aliyetuambukiza huko! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya kuishi Mbeya ni ya chini sana, kwa maana kwamba ni rahisi mno. Maana maisha ya binadamu yanategemea chakula na Mbeya fikiria ndizi, viazi mviringo, mpunga na hata matunda kule Kyela hata kule Ileje ni vitu vya bure tu. Mpaka leo tabia iliyopo kule, mtu unaweza kuingia shambani kwa mtu ukapata ndizi imeiva wewe ni kukata na kula unaondoka unaacha maganda pale. Sasa watu wameshindwa hata imani ya kusema uuzem umuuzie nani? Sasa hili nilikuwa ninaomba kwa kweli Wizara ya Ujenzi itufikirie tuzindue hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kunipatia fedha za barabara hii ya kutoka Luanda mpaka Nyimbili ingawa haijafika mwisho, kule ndiko tuliko na Ileje, kule ndiyo sehemu ya uzalishaji na ndiyo sehemu ya kilimo kinachotegemewa cha mpunga na ndiyo mwanzo wa Mto Songwe huu unaoleta matatizo Kyela. Lakini sasa, sehemu hiyo haina usafiri.

Nilikuwa nimwomba sana Mheshimiwa Waziri pamoja na msaada aliotupatia huo, basi ajaribu kutuangalia hata kutuunganisha. Hata usafiri wa kwenda Mbeya kwenda Ileje kwa kweli ni mgumu sana kwa njia iliyopo sasa inayotokea Mbalizi mpaka Ileje. Ni mgumu kwa kweli. Ungetusaidia hata kuunganisha Ileje na Kyela iwe barabara ya kupitika ingetusaidia sana kuibua uchumi wa sehemu zile na kuongeza mapato na kuwezesha nchi kupata chakula cha kutosheleza sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu kwamba leo viazi vya mviringo Mbeya ni Sh.7,000/= kwa gunia mnaloliita la rumbesa, lakini ukija kama Iringa ni kwenye Sh.19,000/=, ukienda kama Mwanza huko ndiyo balaa nyingine, Mtwara ndiyo kabisa kifo. *(Kicheko)*.

Sasa vitu hivi kama barabara zingepitika vizuri, urahisi wa kusambaza vitu kama hivi na kuondoa tatizo la njaa katika nchi ilikuwa ni kazi ndogo sana na ni njema kama ingefanyika hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nishukuru pia kwa Mheshimiwa Waziri, nimeona ziko fedha kiasi cha Shilingi milioni 10 nadhani, ni za kigeni hizi kwa ajili ya barabara ya Mlowo - Kamsamba. Barabara hii imetuletea matatizo sana miaka yote. Ikishanyesha mvua haipitiki na kule bondeni ndiko kwenye uvuvi wa samaki, Ziwa Rukwa na kule ndiko kwenye mifugo na minada mingi iko kule. Kwa hiyo, shughuli hizi haziwezi kufanyika kwa sababu barabara hazipitiki. Haziendi kule na ndicho kilio cha mwenzangu wa Chunya Mheshimiwa Ntwina kule Namkukwe, ndiyo sehemu hizohizo.

Kama barabara hii ingeimarishwa, basi hata Namkukwe ingeimarika vile vile na ingepata maendeleo ya biashara. Lakini sasa kwa kuliona hilo, kwa namna hii itakuwa ni tatizo sana na tutazidi kupata matatizo makubwa ya mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine kinachorudisha nyuma maendeleo ya barabara, pamoja na kujenga barabara hizi, liko tatizo. Zinajengwa barabara nzuri za lami lakini angalia barabara hizi, makaravati mengi madaraja yamegongwa. Hivi kuna nini? Kwanini hawa watu wanagonga makaravati haya na Wizara inachukua hatua gani? Kuna siku swali liliulizwa hapa likajibiwa kwamba, wote watakaogonga madaraja haya wataadhibiwa na kutozwa faini. Wangapi wametozwa faini? Maana sasa yanaendelea, hata ule Mlima wa Kitonga sasa, hata vile vyuma waliyojengea pale na kingo zile zimekwishagongwa. Hivi maana yake nini? Tuanze tena kufukiria kupanga hela nyingine za kwenda kuchimbia vile vyuma vipya na vinagongwa! Sasa mimi nilikuwa ninaomba Wizara hii kama tunataka barabara zidumu, kuwe na ushirikiano mkubwa kati ya mawasiliano kwa reli na barabara. *(Makofi)*

Kwa sababu magari haya makubwa kwa barabara hizi sio rahisi kwenda salama na mizigo mikubwa wanayofunga mpaka Zambia mpaka Kongo sio rahisi. Ukiona barabara zenyewe hata pale Kitonga alipofungua Mheshimiwa Rais, leo tayari ile barabara imekwishaanza kutitia, kwa sababu hakuna mizigo inayosombwa mikubwa kwa namna nyingine yoyote, ni malori haya makubwa. Nenda kutoka pale mpaka Mbeya, barabara ile wanaweka viraka viraka tu, yakipita malori yale na *tonnage* iliyopo unakuta lami yote imekwishayeyuka, imetitia. *(Makofi)*

Ukitoka pale sijui ndiyo wanapaita Mbalizi, kuteremkia Songwe, unapoingia Wilaya ya Mbozi hapapitiki, magari yanaanguka pale kila mara. Lami yote imesagika, haiko kwa sababu ya mizigo mikubwa inayobebwa kupitia sehemu hizo kwenda huko. Sasa basi nilikuwa ninaomba pengine Wizara hii ijaribu kuangalia na kuliona suala hili umuhimu wake na kulisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri tuangalie, tuanze kuangalia hii ni karne ya 21, tulikuwa tunajivuna kwa kutembea kwa mguu sana kwamba watu wengine wanatembea kwa mguu sana. Sasa hiyo ni jadi ya utumwa, lazima tuondokane ni karne ya 21 hii, tuache mawazo ya kutembea kwa miguu. Tujitahidi angalau kuwezesha usafiri. *(Kicheko)*

Leo Dar es salaam vidaladala vimekuwa kama nzige, kwa nini visiende huko tukiwezesha barabara Vijijini huko vikasafiri vikaweka hali ya usafiri uko vyema? Mbona tutapata maendeleo ya kutosha! Sasa wameng'ang'ania wote wanapeleka Dar es salaam kwenye lami na kazi nyingi zinakwenda kwenye lami. Hata hapa Dodoma ukiangalia vidaladala vinagongana humu humu tu kwenye barabara ya hapa iliyonyooka hapa, basi. Ukienda huko kama Ipagala basi huko ni sehemu ya mtu mwingine. Hata hela zinazotolewa za barabara, nyingi utaona ni za kusaidia kuimarisha lami, kurekebisha lami, wapi! *(Kicheko)*

Ipagala ni Mji wa Dodoma. Sasa Wizara ishauri ili mipango iwe inapanua Mji katika uhakika wa kuleta maendeleo. Tusifanye vitu vingine vikabaki katika hali ya kizamani na sisi tunaonekana ni watu wa ajabu. Huwezi ukaenda pamoja na hali hiyo Nairobi. Mimi nilikwenda zamani sehemu zile walikuwa wanaita Kariakoo. Kulikuwa kwa kweli ni kubaya, lakini huwezi ukaona hali hiyo, sasa watu wanajitahidi wanarekebisha. Lakini hapa ikinyesha mvua ni balaa. Isiponyesha, balaa tena la vumbi na mashimo. Sasa tunafanya nini? Tujitahidi angalau kidogo tulichonacho tusaidie kubadilisha hali hii angalau ionekane, hata Ndugu yangu hapa Naibu Waziri akitoka pale Morogoro kwenda kule Kilombero, zile njia zilivyo ni matatizo.

Lazima tuanze kubadili mawazo na kufikiri namna ya kusaidia kuleta mabadiliko. Huko Vijijini ndiko kwenye vyakula. Ni aibu leo kuomba chakula wakati kipo chakula cha kutosha hapa hapa. Watu sasa wanakazana na kujivunia kwenda kusafiri kwa baiskeli; baiskeli ni ujima! Dunia ya leo, baiskeli ni ujima. Lazima tuanze kufikiria. Kwa hiyo, ninaomba sana kwa kweli Wizara hii itusaidie kuleta mapinduzi ya maisha ya watu na maisha ya usafiri na muungane. *(Kicheko)*

Hizi reli tuziimarishe zitusaidie kuleta mabadiliko ya watu. Huko reli ilikopita kama Ifakara huko, hii *TAZARA*-Reli ya Uhuru, haina kitu na watu wanashukuru pengine Reli ilijengwa kwa sababu ya Smith aliyeleta matatizo kule. Sasa mpaka watu wawe na mawazo ya kumshukuru Smith alisaidia reli ijengwe kweli! Watu wamshukuru Smith lami iliwekwa! Yaani sisi hatuoni hilo kama ni ukombozi wetu wenyewe! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba hilo kwa kweli tuliangalie. Nashukuru sana kwa kazi anayoifanya Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na Wizara yake kwa ujumla. Naomba pia hata huku kusema upembuzi, upembuzi, basi wenzetu wakazanie na wao waingie katika kupembua na kukamilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Wizara ya Ndugu yangu, rafiki yangu sana, Mheshimiwa John Pombe Magufuli - Waziri wa Ujenzi.

Ninaomba awali ya yote nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri. Nataka nimwambie Waziri kwamba mimi namchukulia kama mtu *serious* sana na kazi yake na mtu ambaye yuko makini sana. Nimesimama hapa kwa sababu mwaka jana nilimwomba aje katika Jimbo langu la Siha, aje akajionee mwenyewe hali halisi iliyopo katika barabara zangu kule ambazo ziko chini ya Wizara yake. Pamoja na majukumu makubwa aliyonayo, Mheshimiwa Waziri alikubali kuja katika Jimbo langu la Siha.

Napenda nimwambie kwamba wananchi wa Jimbo la Siha wamenituma hapa kutoa shukrani na kusema ahsante sana kwa Serikali na kwa Mheshimiwa Magufuli kwa kufika. Nasema hivi, kwa sababu kuna mambo makubwa yamefanyika, barabara inayotoka Bomang'ombe kwenda *West* Kilimanjaro mpaka Kamwanga kwenda kuunganisha na barabara ya Rongai, ile ambayo inapitia kwa Mheshimiwa Basil Mramba ni barabara ambayo ilikuwa ni mbaya sana. Lakini barabara hii sasa imefanyiwa ukarabati na inakwenda vizuri, nitaizungumzia baadaye. *(Makofi)*

Marehemu Samora Machel wa Msumbiji aliwahi kuzungumzia habari ya *revolution*, akazungumza akasema Mapinduzi maana yake nini? Akajibu, akasema "Mapinduzi ni kitendo chochote kile cha manufaa kinachofanyika kwa haraka na ambacho kinaleta maendeleo." Ndani yake anazungumzia *condition* ya haraka. Kama kitachukua muda mrefu hivi, *according to* Samora Machel, siyo *revolution*. *Revolution* ndani yake lazima iwe na *component* ya uharaka. Ukisema tutakula ubwabwa halafu ubwabwa tutakula miaka kumi ijayo, *don't talk about it*. Usizungumze! Wala usizungumze hapa, haitusaidii sana. Ukisema kwamba watoto watakwenda Shule, halafu unasema baada ya miaka mitano, baada ya miaka kumi, *don't talk about it, according to* Samora Machel. Haikusaidii kwa sababu haileti mabadiliko ya haraka ambayo yanaleta manufaa. *(Makofi/Kicheko)*

Ndivyo alivyosema Samora Machel. Akasema ukitaka kuleta mabadiliko ya haraka, *condition* yake ni lazima uwe tayari kufanya kazi muda wa ziada. Ni kama ile *component* ya *economics.* Ni hiyo hiyo anayoleta hapa, yaani kama wewe ni Daktari unatibu watu mpaka saa 9:30, saa 9:30 unaondoka unachukua begi unakwenda, *there is development, there is no revolution. (Makofi)*

Kama wewe ni mwanafunzi unasoma Shuleni mwenzako analala saa 4.00 na wewe unajua kumbe namba yako ni B, C hukai mpaka saa 6.00 au saa 7.00 ukaingiza miguu kwenye karai, ukakaa pale ukasoma, hutapata mabadiliko. Kuna watu wanaweza wakapata A kwa sababu ya uwezo wao wa kuelewa mambo haraka haraka. Wengine wanapata A kwa sababu ya ku-*struggle*, lakini ni A ile ile. Huyu amepata A kwa sababu uwezo wake ni mkubwa na huyu mwingine anapata A kwa sababu ya *struggle* na ndicho ambacho tumekiona kinatokea katika Wizara ya Ujenzi. Ukikaa ukasikiliza watu wanazungumza hilo, Wizara ya Ujenzi kuna mahali ambapo utaiona *component* ya kuudhiudhi hivi na kama wewe ni kiongozi ukisikia kila kitu unachofanya watu wanafurahi, huyu mtu mzuri na nini, ujue *there is no revolution and therefore no development*. Huwezi kabisa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii kama ningepata nafasi ningeielezea vizuri, najua dakika15 zitakwisha hapa! Ningepata nafasi ningetoa watu wengi waliozungumzia hilo, ukishasikia watu wanasema safi sana, safi sana anza kuiangalia hiyo, ni hatari sana! Ukisikia unafanya halafu unaona unaudhiudhi watu, unajenga nyumba watu wanaudhika, unatengeneza barabara unakaa kule unaweka X watu wanaudhika, songa mbele hapo unapatia na ndicho ambacho amefanya Mheshimiwa John Pombe Magufuli. Leo jina lake linaingia katika *annals of History* katika nchi hii.

Chama cha Mapinduzi kama kuna Wizara ambayo itatuvusha kwa maana ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, Wizara mojawapo ni hii. Nyingi zimefanya kazi nzuri, kuna Mawaziri wengi sana ni *very serious* watakapokuja tutazungumza ya kwao. Sasa tunazungumza habari ya Ujenzi. Huyu Waziri ame-*contribute* na kama wanarudi watu humu ndani, *partly* itakuwa ni kwa sababu ya kazi iliyofanywa na John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nisimame hapa niseme *on behalf of my people from Siha*, *I solute* John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya. Songa mbele. Joseph Stalin alipokuwa anajenga zile *Metro* kule chini watu walikuwa wanapigwa viboko, watu wanasukumwa na nini wakamwita *dictator,* maneno ya ajabuajabu, ikajengwa *Metro* mpaka zikapita. *Metro* zilivyopita, *Metro* ni zile reli zinazopita chini, huko ardhini *underground*. Wakati vita kuu inakuja kupigana, wale Warusi wote walikwenda kujificha kule chini, wakamkumbuka tena Joseph Stalin kwa kazi aliyoifanya. *(Makofi)*

Sasa Mheshimiwa Magufuli mimi sikwambii uwe *dictator,* nchi yetu ni nchi ya *democracy.* Lakini ukiishaamua jambo, kwa mfano unataka kujenga nyumba za wafanyakazi, songa mbele, usikae unarudi nyuma tena unaanza kuangalia huku na huko, *no!* Wewe watu wetu hawa katika *developing countries*, hizi nchi changa ni watu wanaogopa mapinduzi. Mabadiliko kwamba hii inataka kuja hii, itakuwa hatari na nini! *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni lazima sasa ukitaka kuingiza wazo jipya, lazima uwe na *courage* ya kusonga mbele, unakwenda mbele unafanya kazi baadaye watu watakapokuja kujifunza wanasema hivi huyu aliwezaje kufanya hivi? Wewe unasikia pale Zimbabwe! Bora apige kelele pale, yule Mzee yuko pale amesema mimi nataka wananchi wangu wapate ardhi ya kulima watu wanasema huyu mtu wa ajabu sana. Utapataje sasa hiyo kama hutasimama imara ukaenda pale? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba kazi nzuri imefanyika katika Wizara ya Ujenzi. Tumeingia katika utandawazi, nina ndugu yangu Mheshimiwa Karavina amezungumza vizuri sana. Unazungumza habari ya *globalisation*, unazungumza habari ya *independent economy*, unazungumza habari ya *EPZ, how do you get EPZ* kama barabara zako siyo nzuri? *How do you get the strategic investor* kama barabara zako ni za hovyo hovyo? *Strategic Investor* anatakiwa akuletee *capital*, anatakiwa akuletee *technology* ya kisasa, anatakiwa a-*create employment*, anatakiwa afike mahali a-*create Government revenue,* hivyo vitu vyote unavipataje kama wewe huna barabara zinazopitika. Hii kelele inayopigwa hapa ya Mtwara *Corridor,* ya Kigoma nataka nikuambie tusipofanya hivyo Mtwara haitanyanyuka wala Kigoma haitanyanyuka, zitabaki hapohapo! *(Makofi)*

Yaani hiyo ni *science* na ndivyo inavyosema. Ukitaka *investment* ifanyike hapa fanyeni. Sasa tunakwenda kwenye utandawazi, tumezungumza habari ya *EPZ*, songa mbele. *Strategic Investors* sasa hivi baada ya *cold war* hawa-*invest* katika Afrika, wanakwenda kwenye *infrastructure* yenye hali nzuri, yaani *Eastern Europe*, wanakwenda kule kwenye nchi hizi za kijamaa zilizokuwa kule wakati ule ambapo *already infrastructure* yao kwa maana ya barabara, reli zao, simu, *were developed*, hakuna mtu atakuja hapa achukue treni lake alilete hapa. Hakuna mtu atakuja hapa alete malori yale, alete vitu vikubwa vikubwa ambavyo vina pesa nyingi ndani yake aje aka-*invest* katika uchumi huu ambao unasuasua hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilikuwa nazungumza hapa nilipokuwa nazungumza habari ya Mheshimiwa Keenja kwenye kilimo. Nikamwambia hapa kwetu sisi hakuna *program*. Hatuna mipango hapa, tulichonacho katika nchi za kwetu changa hizi duni za kikoloni mamboleo ni shughuli tu, unaziona hapa. *Program* mambo yako anza ku-*fight contradiction* yetu hapa, kati ya *labour* na *the level of the productive forces*, barabara ni moja, ukishaona umefika umetengeneza barabara zako maembe hayataoza kule Mtwara, yatachukuliwa yataletwa Dar es Salaam watu watakula. Fanya hilo. *(Makofi)*

Tunaye kijana ndugu yetu mtoto wa Afrika ambaye amesimama imara anafanya kazi hii na tumeona ya kweli. Sasa nataka kusema kwamba nchi hii watu wa-*invest* na nchi hii ni kubwa na ina uwezo mkubwa. Wenzetu Sumbawanga wanalima vizuri, wenzetu Kusini wanalima vizuri, Mwanza wana samaki huko, ukienda maeneo yote utafikiri ni nchi ile ya ahadi ambayo Musa alikuwa anaambiwa apeleke watu kule. Ina utajari wa kunukia, ina umaskini wa kunuka humo humo, *it is a contradiction!* Haiwezekani *potentiality* kubwa namna hii ipo katika nchi yetu hapo, humo humo kunakuwa na maskini kiasi hiki! Unajiuliza nini? Ondoa tatizo la msingi, *resolve the primary contradiction, the secondary contradiction* itaondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwa na vitendea kazi Mzee Kingunge Ngombale-Mwiru anafahamu habari hii, hapa kwetu hakuna *contradiction* kati ya *labour na capital*. *Contradiction* iliyoko hapa ni kati ya vitendea kazi na kiwango kile cha binadamu na maendeleo yake, ndivyo inaonekana. *Address* hiyo *program,* tengeneza barabara na ndiyo tunaipigia kelele hapa sasa hivi. *(Makofi)*

Ukishafika hapo, unazungumza habari *export promotion zones* kwa sababu watu wata-*invest* kule. Sasa hivi utaona *South Africa* wanapiga hatua kubwa sana kwa sababu wao *infrastructure* ni nzuri. Kwa nini tunakuwa na hiyo *problem*? Tunakuwa na hiyo *problem* kwa sababu sisi kila kitu kinachofanya ukifanya *investment* kwa mfano kwenye *education* itakuchukua miaka mingi sana mpaka u-*realize profit* yake. Elimu inachukua hela nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunafanya hapa kwetu? Tunavuna kahawa, tunavuna korosho, tunavuna samaki, tunavuna kutoka kwenye misitu, tunavuna kutoka kwenye maeneo mbalimbali, lakini hatufanyi kazi ya kurudisha kwenye *production unit* pale tunapozalisha, *How back* unachokipata wewe rudisha kwenye *production unit even classes according to Lenin* zinaanza pale kwenye *production level* pale chini ndipo tunapoanzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitamaliza tu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa nizungumzie barabara yangu ile inayokwenda *West Kilimanjaro* katika Jimbo langu la Siha. Nimekwenda Kenya, nimekuta barabara zote zinakwenda *Mount Kenya*, zinakwenda kwenye mbuga za wanyama. Mheshimiwa Lekule Laizer ameniambia nitoe salamu zake kwako kwa sababu hili ninalolizungumza linatuhusu wote. *(Makofi)*

Mimi nakushukuru kwamba barabara ninayoizungumzia imefanyiwa *rehabilitation,* nimeangalia huku nimekuta bado imeendelea kutengewa hela. Lakini ninachozungumza, nazungumzia sasa barabara inayokwenda Magadini inayotoka pale Sanya Juu kwenda mpaka Ngarenairobi, inatoka Ngarenairobi, inakwenda mpaka Kamwanga inazunguka inakwenda Rongai kwa Mheshimiwa Basil Mramba. Hiyo barabara ukiangalia *cave* yake inafanana na mbalamwezi inapochomoka au ndizi inavyotoka iko hivi, huku kwingine kote kazi inafanyika inamalizika kimebaki hicho kipande. Hapo ndiyo unapopata ngano, hapo ndipo unapopata njegere, hapo ndiyo unapopata viazi, hapa ndipo unapopata miwa, ndipo unapopata maziwa, ndipo unapopata mbao, unapopata kila kitu pale. Lakini cha ajabu hapa tunapozungumza habara hii eneo lile halipatikani. Watalii wanaokwenda Londros *Gate*, hawa watu tunaozungumza Londros *Gate* ni Wasafwa, Wanyaturu na Wanyakyusa. Ni ndugu zenu na dada zenu walioko kule kwenye Jimbo langu la Siha. Kule tunaita *United State of Sih,* ndiyo watu ambao walitoka huku wakapelekwa kule kwa sababu ya historia. Kwa hiyo, hapa mnisaidie mambo haya ili jambo hili liweze kupita.

Mheshimiwa Magufuli, mtu ambaye tumeseme umefanya mambo makubwa kiasi hicho, *investment* ya namna gani unafanya unasahau kupeleka kwenye Mlima Kilimanjaro pale Siha? *(Makofi/Kicheko)*

Barabara ya kutoka pale Sanya Juu kile kipande kinakwenda mpaka pale kuunganisha na Mheshimiwa Mramba. Tunakuomba mimi na Mheshimiwa Lekule Laizer utusaidie barabara ile iwekwe lami. Ndiyo, hiyo ni barabara ya lami! Ndiyo hiyo ni tunazungumza hapa, hatuzungumzi barabara hii ya Moramu, anafanya kila siku, anapeleka watu kule, hiyo nataka nitoe ushuhuda. Lakini barabara ile ndiyo tunayotoa vitu vyote, *West Kilimanjaro*, Mashamba *Janies and Frisian Farm*, Kanamodo yote yale mashamba makubwa, mashamba ya *TBL* anafahamu Mheshimiwa Mwandosya alifika mpaka *West Kilimanjaro,* alikwenda mpaka Londros, kuna *potentially* kubwa pale kama anavyosema Mheshimiwa Karavina. Tusaidieni barabara hii iwekwe lami ipite pale ita-*open up.* Ukitaka kujua kwamba unaanza kubadilisha, angalia, utaanza kuona vibao vya *Cocacola*, utaona vibao vya *Vodacom,* utaona *Mobitel,* utaona Mashirika mbalimbali yanaanza kuonekana kule unaambiwa ndiyo ume-*open up* uchumi. Acha huu uchumi huu mwingine wa ajabu wa kubeba mizigo kichwani, tunakwenda nayo, hiyo ni *primitive* haitusaidii kwa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nirudie kusema tena, kilio chetu nimeiona hapa najua utanijibu, iko kwenye ukurasa wa 145, imetengewa fedha mimi nimeona pale kuna milioni 60 sijui ndiyo huu upembuzi yakinifu, sijui ni nini, mimi sijaelewa. Labda utakaposimama ndugu yangu unisaidie. *(Kicheko)*

Nimalizie hapa nikuulize, lakini Mheshimiwa Magufuli wewe tumesoma wote Chuo Kikuu *degree* ya kwanza na *degree* ya pili, hivi kweli wewe unataka mimi Aggrey Mwanri hapa nisirudi tena kwenye hii nyumba mpya inayojengwa hapo? Unisaidie mzee wangu. Ukisimama hapa useme barabara ile itajengwa mzee wangu uunganishe na ile ya Basil Mramba, sisi na Mheshimiwa Lekule Laizer. Tunakulilia kwa sababu ukienda

ukileta mpaka pale itaishia pale kwa Mzee Mramba, sisi ukatusahau Sanya Juu na wale wa Longido ukawasahau, utakuwa umetusaidia nini? Hunitakii mema! Tulikuwa tunakaa wote, wewe ndiyo ulikuwa *campaign manager* wangu Chuo Kikuu nikawa *President* wa *University* leo tunatupana mzee wangu hapa nisaidie bwana barabara ile ipite pale. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nafikiri na Mramba amesikia. Nitamwita Mheshimiwa Dr. Chegeni. Lakini kwa sababu kwa muda mrefu Kambi ya Upinzani sijawasikia, atamalizia Mheshimiwa Maghoba.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na wenzangu kwa vile nilishachangia mara ya mwisho na nilizungumza suala la msiba, ningependa niungane na wenzangu vile vile kutoa rambirambi kwa mwenzetu Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana. Tunaomba Mwenyezi Mungu ailaza roho yake mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamechangia vizuri sana na hasa Msemaji wa mwisho hapa, mimi nilijua ziende pongezi mpaka mwisho, lakini pale mwisho akaamua kukomelea mambo yake anayotaka. Sasa na mimi sijui nianzie wapi. Nianzie kwenye mambo ninayotaka, nimalizie kwenye pongezi.

Lakini napenda kusema kwamba, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa John Pombe Magufuli, pamoja na Naibu wake Hamza Mwenegoha, Katibu Mkuu *Engineer* Kijazi na Watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi. Kwa kweli katika nchi hii kama ni kuwatendea haki Watumishi wa Mungu, basi ni vyema tukawatendea haki Wizara hii kwa sababu waliyoyafanya hayana kipimo. Ndiyo kila Wizara imeweza kufanya kazi kwa muda wake na kwa nafasi yake, lakini katika karne hii na katika nchi hii toka imeumbwa ni mara ya kwanza kuweza kuona shughuli za ujenzi zimetapakaa katika nchi nzima. *(Makofi/Kicheko)*

Lakini haiishii hapo, Wizara hii huko nyuma ilikuwa imenuka sana kwa rushwa lakini siku hizi Wizara hii ni kati ya Wizara safi. Utaona miradi mingi ya ujenzi inaendeshwa vizuri na mpaka fedha zinabaki kwa baadhi ya makandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakuwa hatuwatendei haki kwa kweli Mheshimiwa Magufuli pamoja na timu yake tusipompa pongezi za dhati kwa kazi nzuri anayoifanya. Kwa kweli hata kurudi hapa Wana-CCM watakaorudi/tutakaorudi hapa kwa kweli ni sehemu kubwa sana ya mchango unaotokana na Wizara hii ya Ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, kama nchi hii tutaamua kuthamini ujenzi na kufufua miundombinu yote ikiwemo barabara na mingineyo, tutakuwa tumefufua mgodi mwingine wa dhahabu kwa sababu tukiimarisha miundombinu pekee nchi yetu ina faida kubwa sana kwa sababu kuna nchi nyingi sana zinategemea Tanzania. Nchi hizo zote zinategemea kupata huduma kutoka kwetu. Tukiweza kuboresha barabara, tunazungumzia barabara ya kutoka Dar es Salaam kwenda mpaka Kigoma, kutoka Dar es

Salaam kwenda mpaka Mwanza, kutoka Arusha kwenda mpaka Kusini huko Songea, kutoka Mtwara *Corridor* sijui *corridor* ya kutoka Mbeya Sumbawanga mpaka Kigoma na chinja chinja zote hizi za kwenda huko Dar es Salaam. Lakini wameshinda kwa sababu wana barabara nzuri, hatuna miundombinu mizuri. Leo hii tungeweza kufungua barabara ya *central corridor* mpaka Kigoma tungekuwa na mapato mengi sana ya fedha na hii itasaidia sana kufufua uchumi wa nchi hii.

Kwa hiyo, ningependa kusema kwamba katika fedha ambazo tumepata msamaha wa kulipa madeni, tuelekeze zaidi huko kwa sababu hatulipi hizi fedha sasa hivi, tutakapowekeza zaidi katika kuboresha miundombinu hii ili leo hii tusije hapa tukaanza kulalamika kwamba barabara zetu ni mbovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la barabara za changarawe limepitwa na wakati, tufikie mahali tuanze kujenga barabara za lami. Kama ni lami, tunajenga lami kwa muda baadaye nchi nzima inakuwa na *connection* ya lami sehemu zote! Hii itasaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa nizungumzie barabara moja ambayo ni ya muhimu sana inatoka Ngorongoro kupita Meatu, Maswa, Bariadi, Mkula, Ramadi, inakuja inaungana na barabara inayotoka Musoma au Sirari, Musoma, Mwanza. Hii itakuwa imesaidia sana kuweza kufungua huu uchumi wa maeneo husika haya na vile vile kuweza kuepusha uharibufu wa wanyamapori wa Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa sana katika majumuisho ya Mheshimiwa Waziri, ajaribu kutueleza japo tu kwamba hii barabara ina mpango gani? Kwa sababu imeshajengwa kutoka Arusha mpaka Ngorongoro. Sasa ni vyema ingeanzia pale Ngorongoro kuja Meatu – Maswa – Bariadi – Lamadi ambao ndiyo Busega huko iungane na barabara inayokwenda Musoma au Sirari kwenda Mwanza. Hii itasaidia wananchi wengi wa maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe tuna hii barabara ya Nyanguge – Musoma, ni barabara ya siku nyingi sana, ina zaidi ya miaka 22 nafikiri toka imekabidhiwa. Lakini barabara hii haifanyiwi matengenezo mazuri ya kutosha, ina mashimo mengi na sehemu nyingi zimekuwa ni mbovu. Nampongeza Meneja wa *TANROAD* wa Mkoa wa Mwanza kwa kazi nzuri anayoifanya. Lakini bado hana fedha za kutosha kuweza kuikarabati barabara hii vizuri. Nimeona zimetengwa kama Shilingi milioni 440 na kitu kwa Kilometa kama saba na nusu. Sasa nikiangalia, kwa kweli barabara hii inahitaji itengenezwe. Leo unaona barabara ya kutoka Morogoro kuja Dodoma inatengenezwa na kila mwenye akili timamu anayepita anasema kwa kweli kazi ni nzuri. Kwa kweli Wizara ya Ujenzi wanafanya kazi nzuri sana, kama ni wakandarasi wanafanya kazi nzuri. Sasa ningependa hii barabara ya Nyanguge – Musoma itengenezwe kwa sababu ni kiungo muhimu sana kati ya Tanzania, nchi za Burundi, Rwanda pamoja na Kenya. Sasa ningependa hii tuweze kuipatia Bajeti ya kutosha. Sijui kama kwa namna ambayo Waziri atafanya, lakini ni vyema ikaongezewa fedha. Imeharibika sana kwa kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hizi barabara ambazo wajenzi wa barabara za Musoma – Nyanguge na barabara ya Mwanza - Misungwi kuja Mji wa Magu, ulipita pembeni na Mji wa Misungwi umepita pembeni. Sasa unakuta ile ni kero wa wananchi wa Halmashauri zinazohusika ya Magu na ya Misungwi. Nilikuwa nashauri hivi kwa sababu tuna teknolojia mpya ya *otter seal,* kwa nini tusiweke fedha angalau ile *by pass* ni kipande kifupi tu, itengenezwe angalau lami ya *otter seal* ili kusudi iweze kuleta mandhari hata ya Mji wa Magu. Ile ni Halmashauri ya Mji wa Magu. Sasa na yenyewe ipatiwe hadhi ya Halmashauri ya Magu siyo vumbi tupu, barabara imepata pembeni. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hili Mheshimiwa Waziri ajaribu kuliangalia. Kuna Wilaya ya Magu na Wilaya ya Misungwi tunahitaji tuweze kupata angalau hiyo teknolojia mpya ya *otter seal*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba katika mfuko wetu wa barabara *(road fund)* kweli fedha ni ndogo ukiangalia na Kilometa zilizopo za barabara za Mikoa ambazo ni kubwa sana na bilioni 63 ukagawa kwa Kilometa zote, bado kazi inakuwa ni ndogo sana. Labda pengine tunaweza kutafuta namna gani tuweze kupata fedha nyingine kuongezea kwenye Mfuko wa Barabara. Hili Mheshimiwa Waziri nadhani hata Wabunge wengi hapa wanavyoelekeza maombi yao, ni kwamba barabara nyingi za Mikoa hazitengenezwi kwa kiwango cha kutosha. Lakini tatizo ni kwamba fedha inayotengwa haitoshi. Sasa ni vyema Wizara ijaribu kutafuta vyanzo vingine vya kuongezea fedha hii ili angalau matengenezo yanayofanyika yawe ya kudumu na ya kutosha. Waheshimiwa Wabunge, wengi kilio chetu ni barabara zetu. Sasa ni vyema zaidi tuweze kuona ni namna gani Wizara hii inaweza kuongeza Mfuko huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Yohana Mbatizaji alisema kwamba mimi siyo, Masiya anakuja, Mheshimiwa Magufuli amefanya kazi nzuri sana. Lakini Watanzania siku zote kuna wale ambao wanaweza kubeza; Magufuli hiki, kafanya hiki, lakini yote haya kwa sababu Watanzania ndiyo tulivyo. Nimesema tunahitaji mapinduzi ya dhati. Nakumbuka wakati Mheshimiwa Waziri anajenga barabara ya kutoka Dar kuja huku Dodoma., Watanzania hawa baadhi yetu walikwenda mpaka *UNHCR* tunasema tunaomba hifadhi kwenye nchi yetu, kisa kwa sababu Magufuli kavunja nyumba zetu. Lakini leo hii Watanzania hao tunasema jamani Tanzania sasa tumeendelea, barabara ni nzuri. Lakini cha ajabu tunagonga taa za barabara, tunagonga madaraja. Sasa hii sijui ni ustaarabu gani tena. Mheshimiwa Magufuli una kazi nyingine hiyo. Sasa sijui utafanyaje, maana yake unakuta tunakuja kwenye ustaarabu lakini sisi Watanzania hao hao tena hatutaki ustaarabu. Mimi naona kuna haja kweli ya kuangalia kwamba hao madereva ambao wanakuwa siyo waangalifu barabarani wachukuliwe hatua za dhati. Sio suala la kumwadhibu mwenye gari, ni dereva mwenyewe aadhibiwe kama dereva ili tuweze kuwa na nidhamu ya kuweza kuheshimu na kutunza mali ya umma na kutunza barabara zetu. Haina maana tunajenga barabara kwa mamilioni mengi sana, lakini matokeo yake tunaharibu. Juzi pale Mikese lile daraja kuna mtu amegonga nguzo ya daraja lile bado jipya hata barabara haijakabidhiwa, amegonga ameliharibu hapo. Sasa Watanzania tufikie mahali na sisi tuanze kubadilika. Serikali inafanya kila linalowezekana kuweza kutupatia miundombinu iliyo bora na safi, Mheshimiwa Magufuli yuko mbele kwa mbele pamoja na kazi zake nzuri sanam hebu tuonyeshe basi na sisi kwamba tunawajibika kutunza

barabara hizi. Kama vipi, basi Serikali itafute namna ya kuwaadhibu hawa madereva ambao hawaheshimu sheria za barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri vile vile kwa kusaidia Taasisi zake. Kwa mfano kuna Taasisi ya Usimamizi wa vifaa, *(National Board of Materials Management),* hii ilikuwa haina hata jengo/Ofisi lakini Mheshimiwa Magufuli amejitahidi amepata Ofisi nzuri sana, inaendelea kusaidia zaidi. Lakini bado ajaribu kuipa msukumo na *support* yake kwa sababu hata katika Idara za Serikali tumekuta kwamba kuna wataalam wengi sana wenye sifa za kuwa maboharia lakini hawana nafasi hizo. Lakini baada ya kupitisha sheria yetu hii, imejaribu kupata msukumo na Bodi imejitahidi sana kuweza kusukuma, angalau sasa Serikali yenyewe imeanza kutambua kwamba kama kuna wataalam. Basi wanapewa haki yao kulingana na taaluma yao. Ningependa Mheshimiwa Waziri ajaribu na azidi kuisaidia Bodi hii ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote haya, nimwombee Mheshimiwa Magufuli, kwamba wananchi wa Biharamulo Mashariki kwa kweli wanamkosa mara kwa mara kwa sababu ana kazi nyingi za nchi nzima hii. Ukienda huko kwa Namkulala huko anatengeneza barabara Nanyamba, kote huko anatengeneza, lakini Biharamulo wanahitaji wamwone kama Mbunge wao, tunaomba watusaidie kwamba huyu Mbunge huyu jamani ikiwezekana wampitishe bila kupingwa. Tunaomba sana wananchi wa Biharamulo Mashariki kama wanatusikia na ningependa vile vile Vyombo vya Habari muwaambie hivi, sisi Wabunge tunamwombea Mheshimiwa Waziri Magufuli mpitishe kwenye uchaguzi bila kupingwa azidi kuwatumikia Watanzania kwa ari, kwa nguvu na kwa kasi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, napenda nishukuru sana na niunge mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. FRANK G. MAGHOBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Kwanza kabla ya hapo nitoe salam za pole kwa familia ya Marehemu Margareth Bwana. Pia, nawapa pole watu wa Rukwa kwa kupotelewa na mchapakazi wao Mheshimiwa Margareth Bwana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niipongeze Wizara ya Ujenzi kupitia Waziri wake Mheshimiwa Magufuli, Naibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hiyo na hasa *TANROAD* kwa kufanya kazi nzuri ambayo kila Mtanzania nadhani anafurahia na hasa mwananchi ambaye anapenda maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuseme tu wazi kwamba kama kuna mapungufu ambayo anayo Mheshimiwa Magufuli, basi tumsaidie ili aweze kufanya kazi yake vizuri. Tunasema hakuna binadamu asiye na mapungufu katika utendaji wa kazi katika maisha yake yote. Mheshimiwa Magufuli, amefanya kazi nzuri ambayo Watanzania wote sasa tunaona mabadiliko makubwa hasa katika shughuli za barabara. Kwa hiyo, nampongeza kwa juhudi hizo na hasa wataalam wake kwa kushirikiana naye kwa kazi zao nzuri ambazo wanazifanya kila wakati bila kuchoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina machache ya kuchangia katika Bajeti hii. Suala kubwa ambalo nitachangia hapa ni sehemu tatu. Kwanza, ni Daraja la Kigamboni na kivuko chake na barabara ya Kilwa na pia suala la usafiri kwa mabasi usiku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kivuko kilichopo sasa hivi kutoka ng'ambo ya Dar es Salaam kwenda Kigamboni, kimechoka kwa sababu kila wakati kinakuwa kinapoteza mwelekeo, wakati mwingine kinazimika katikati ya bahari. Sasa hiyo ni hatari. Mheshimiwa Magufuli, wewe ni rafiki yangu wa siku nyingi, tulishazungumza suala la daraja muda mrefu. Kuna wakati mwaka jana 2005 tulitegemea kwamba daraja lile lingeweza kujengwa kuanzia Oktoba, lakini tukasema kwamba hela zilikuwa hazijapatikana. Nimeshangaa juzi kwamba tunazungumzia kwamba tunafanya kazi ya upembuzi yakinifu kupitia *NSSF*, mimi sikujua kwamba kwa nini tulizungumzia kujenga daraja kipindi cha mwaka jana. Nilikuwa nadhani kwamba kipindi kile suala hili la daraja lilikuwa tayari tulishafanya upembuzi yakinifu, kwa hiyo ilikuwa kazi ya kuanza tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upembuzi yakinifu ambao nilikuwa nafikiria kwamba ungekuwa mgumu ni ule ambao tulikuwa tunatajarajia kwamba daraja lingejengwa kupitia chini ya bahari. Lakini baada ya Serikali kugundua kwamba itakuwa gharama kubwa na kwa sababu sisi Watanzania hatuna umeme wa kuaminika, tukisema lile daraja la kufunguka na kujifunga, haiwezekana. Kwa hiyo, ambacho kilifuata ni kwamba tungetafuta eneo lingine ambalo lingejenga daraja kwa urahisi zaidi na kweli Serikali ikafanya utafiti. Kuna eneo linaitwa Vijibweni pale Kurasini ni karibu, ni maeneo yako karibu mno kiasi hata Kilometa mbili hazifiki. Sasa eneo lile kwanza meli hazipiti, ni mwisho wa meli ambazo zinapita. Sikuona sababu tena ya kutafuta upembuzi yakinifu ambao ungechukua muda mrefu kiasi hicho, nilitegemea sasa Mheshimiwa Magufuli amesema nimepata milioni *so much* kwa kujenga daraja kuanzia mwezi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania walioko Kigamboni wana wasiwasi wa kuvuka na kivuko kile. Kwanza tukubaliane kwamba sasa hivi Kigamboni inakua kwa haraka mno, ina watu wengi mno. Ukienda siku ya Ijumaa, jioni na Jumamosi mpaka Jumapili umati unaokuwepo pale kivukoni ni mkubwa mno. Sasa wale watu wote wanategemea kivuko kile na kivuko hakina uhakika. Namwomba Mheshimiwa Magufuli kwamba suala la daraja lile mimi siku zote nazungumza kwamba tusilichukulie kama ni la kisiasa. Walishapita Wabunge wengi hapa, Mheshimiwa Masoud, Mheshimiwa Kitwana Kondo, wengi walishazungumzia suala hili. Sasa na mimi namaliza muda wangu tunazungumzia daraja hilo hilo, kwa nini? Mimi nilikuwa nategemea kwamba Rais Mkapa anamaliza muda wake, lile daraja lingejengwa na tungelipa na jina kwamba Daraja la Mkapa kama tulivyompa jina daraja lingine kule. Kwa nini sisi inafikia miaka 15 tunazungumza daraja hilo hilo tu? Mimi naamini kwa ukusanyaji wa pesa ambao Serikali sasa imeufanya, sisi wenyewe Watanzania tunaweza kuchangia na pia hawa wafadhili wanaweza kutuchangia katika daraja hilo. Kwa hiyo, namwomba Waziri Mheshimiwa Magufuli, suala la daraja la Kigamboni lisichukuliwe kama ni suala la kisiasa lichukuliwe umuhimu kwa uchumi wa nchi kwa sababu kwanza Kigamboni inabeba watalii wengi kutokana na *beach* zimekuwa nzuri, hoteli zake wanapenda watu kwenda kupumzika siku za Jumamosi na Jumapili, kwa hiyo uchumi unakuwa ni mkubwa. Sasa tusichukulie suala hilo kama ni suala ambalo sasa la kupiga kelele.

Mimi sifikirii kwamba napiga kelele kwa sababu ya kutaka kupata kura za Kigamboni *no,* nazungumzia kwamba mimi ni Mtanzania ambaye nimekuwa kiongozi na mwakilishi wa wananchi wa Kigamboni ambao lazima nizungumzie kwamba wananchi wale ambao wako Kigombani pia walishamchagua Mheshimiwa Rais Mkapa kuwa Rais wao. Sasa wanategemea kwamba Rais wao wamemchagua atawasikiliza matatizo yao. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Magufuli hili suala la daraja tusiliwekee kama suala la kisiasa tuliwekee kama suala ambalo ni la kutukomboa na kuleta uchumi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nihamie katika suala la barabara ya Kilwa. Barabara hii kwenye makabrasha sijaona, labda bahati mbaya nimepitiwa, lakini sikuona kama kuna sehemu ambayo tumezungumzia kwamba tutaanza barabara hii kuijenga lini. Naamini kwamba pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri juzi, nilisikia akisema kwamba tumeshatenga hela tayari kwa kujenga barabara hiyo. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi ni taabu mno baada ya mvua kubwa kunyesha wiki tatu zilizopita, kuna sehemu pale karibu na daraja la Mchina limebomoka kabisa. Sasa pale imebaki sehemu ndogo sana ambayo inapitisha magari. Eneo lile asubuhi kama *traffic* hawafiki mapema pale ukitoka saa 11.00 alfajiri unafika Ofisini saa mbili, sasa hii ni hatari. Tunataka kuinua uchumi wetu kwa misingi hiyo. Hatuwezi kuinua uchumi kwa msingi kwamba mtu anafika ofisini saa 2.00 anakwenda kufanya kazi gani. Tunatarajia Mtanzania anapofika ofisini saa 1.30 kama Serikali ilivyosema aanze kufanya kazi haraka sana. Kikwazo kinakuwa kwenye barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa John Magufuli hata kama suala la kusema kwamba barabara imeshaanza kushughulikiwa basi ianze haraka sana. Ianzie sehemu ambayo kuna utata ili watu waanze kwa haraka haraka. Niliwahi kushauri mwaka jana ikiwezekana hata kama hela haijapatikana basi hiyo barabara ipanuliwe kwa kiwango cha vumbi hivyo hivyo, baadaye Serikali ikipata pesa basi ije kuwekwa lami. Lakini bado hali ni mbaya. Watanzania hasa wanaoishi Mbagala, wana matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja nilikuambia uje kwangu ulale, asubuhi tuamke wote twende kazini, ujionee mwenyewe maana yake inawezekana kwamba Maofisa wako hawakuambii. Ni taabu, ni tatizo. Huwezi kutoka saa 11.00 alfajiri unafika ofisini saa 2.00, sasa ni tatizo, unakwenda Kimbiji, unakwenda wapi huko. Kwa hiyo, mimi naomba hili suala tulititilie mkazo. Tulitilie kwa sababu barabara ni moja ya njia ambayo tunasema ni moja ya njia ya kuinua uchumi haraka haraka katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hiyo pia inaunganisha na daraja la Mheshimiwa Mkapa kule, ndiyo hiyo barabara ya Kilwa. Ningeshauri kwa haraka haraka barabara hii ingeanzia kujengwa pale Mtoni kwa Aziz Ali mpaka *Mbagala Mission* angalau pale tunaweza kusema kwamba tunaweza kupunguza ile ghasia ya katikati hapa. Tatizo lipo kuanzia kuanzia Mtoni, Mtoni Mtongani mpaka *Mbagala Mission* tatizo lipo pale. Barabara imebomoka karibu na daraja la Wachina. Hiyo sasa sielewi kwamba

baadaye mvua ikinyesha zaidi inawezekana lile daraja la Wachina likabomoka, kwa hiyo, itakuwa ni kazi nyingine mpya ambayo nina wasiwasi nayo sana mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana hili suala tulitilie mkazo, tuache kufanya ukarabati ambao hautusaidii. Zile hela ambazo tunafanyia ukarabati sasa hivi tuziache ziingie kwenye kazi ya kujenga barabara yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningeomba kuzungumzia suala la barabara ya kutoka Mji Mwema kwenda Kimbiji, Pemba Mnazi, Yaleyale Puna na maeneo kadhaa. Ile barabara kutoka Mji Mwema kwenda Kimbiji ni barabara ambayo inaweza kutuletea uchumi mkubwa sana katika nchi yetu. Kwa sababu kwanza kule kuna wakulima wengi. Hiyo barabara ni ya Serikali, siyo ya Manispaa. Ni barabara ambayo iko chini ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hiyo ina wakulima wengi na ina maeneo makubwa ambayo Watanzania wengi wanapenda kwenda kupumzika kule. Ndiyo barabara ambayo inapeleka Watalii kwenda kupumzika kule. Kwa hiyo, naomba Wasukuma wapo wengi tu, wengi sana tena wanalima vizuri sana viazi kule, Wasukuma wanalima viazi huwezi ukaamini. Lakini hivi sasa wanakosa soko kwa sababu kuvuka kutoka kule wanatumia baiskeli. Mheshimiwa Edson Halinga, amesema mambo ya kizamani sana ya kutumia baiskeli. Kwa hiyo, ningeshauri kwamba ile barabara kama itaboreshwa kutoka Mji Mwema, Pemba Mnazi, Yaleyale Puna, mimi naamini kabisa kwamba hali itakuwa mzuri sana Watanzania hasa katika uchumi wao.

Naomba sana Mheshimiwa John Magufuli ile barabara uiangalie. Pia kuna barabara kutoka Kibada kwenda *Kisarawe II.* Hiyo iliwahi kutengenezwa mwaka juzi kwa kiwango cha kokoto lakini sasa hivi hali imekuwa mbaya kutokana na mvua inavyoendelea kunyesha, barabara imeshaanza kuharibika na wananchi wa kule walishaanza kukomboka kwa sababu magari yalikuwa yanakwenda, yanawabeba. Sasa hivi kuna tatizo kwa sababu tayari kuna makorongo watu wanaogopa kupeleka magari yao. Ningeomba hili suala pia liangaliwe kwa kuwekwa kiwango cha lami. Kwa sababu barabara za vijijini ndiyo zinazoinua uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Pia nirudi kwenye suala la usafiri wa mabasi, zamani kulikuwa na mabasi yanayosafiri usiku kuanzia saa 11 kwenda Mikoani. Sawa, kulikuwa na ajali nyingi zinatokeza na pia usalama wa raia ulikuwa nadhani ni kidogo. Naamini ili sisi tuweze kwenda kusonga mbele na uchumi wetu uweze kukua kwa haraka, sisi hatupaswi kulala kama Watanzania, hatupaswi kulala hata kidogo. Tunatakiwa tufanye kazi usiku na mchana kuhakikisha kwamba nchi yetu tunainua uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunawapangia kwamba watu walale mpaka asubuhi ndiyo wasafiri. Mchana ndiyo muda wa kufanya kazi, mtu anasafiri. Utaratibu wa zamani urudi wa kusafiri isipokuwa uwepo usalama wa kutosha katika mabasi hayo askari tunao wa kutosha. Haiwezekani sisi tuwe tunasafiri mchana, halafu usiku tunalala tu. Sidhani kama ni sahihi, utaratibu wa zamani wa kusafirisha usiku urudi ili Watanzania wasafiri usiku na mchana wafanye kazi na ndiyo maana nalisema hili kuinua uchumi wa nchi yetu sisi bado hatujawa matajiri kiasi ambacho tunaweza kulala usiku.

Wachina walikuwa maskini na sasa hivi wako mstari wa mbele mno kwa sababu wanafanya kazi usiku na mchana. Hakuna miujiza ni kufanya kazi.

Kwa hiyo, naamini kwamba usafiri wa usiku ukirudi ukiwepo na usalama wa kutosha Watanzania watasafiri usiku na kesho yake watafanya kazi bila matatizo. Kuna watu ambao wanataka kuchukua bidhaa zao Dar es Salaam kupeleka Mikoani ni lazima wasafiri. Leo unaposema usafiri mchana peke yake yule mtu anasafiri mchana peke yake yule mtu ambaye anasafiri mchana anafika Dar es Salaam usiku hawezi kununua na kurudi siku hiyo hiyo. Ushauri wangu ni kwamba usafiri wa usiku uwepo lakini uwe na usalama wa kutosha ili Watanzania waweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Bajeti hii na kwamba naamini kwamba sasa Mheshimiwa John Magufuli, atayafanyia kazi yale niliyoyasema. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Wizara hii tutaendelea nayo kesho na kesho tutaifunga. Kwa hiyo, wale ambao majina yao hayakutajwa wataendelea kesho. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge naahirisha kikao mpaka kesho saa 3 asubuhi.

*(Saa 01.28 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne tarehe 28 Juni, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*